

## **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Ishirini na Tisa - Tarehe 20 Julai, 2004**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla kikao hakijaanza, napenda kumtambulisha Mgeni wa Kimataifa aliyeko kwenye *gallery* ya Bunge leo ni *Managing Director* wa Shirika linaloitwa *Common Fund for Commodities*, ambalo Makao yake Makuu yapo Amsterdam Uhlanzi, anaitwa Balozi Ali Mchumo. (*Makofi/Kicheko*)

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Chuo cha Ushirika Moshi kwa Mwaka 2002/2003 (*The Annual Report and Audited Accounts of the Co-operative College for the Year 2002/2003*).

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

**MHE. SALOME J. MBATIA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA:**

Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 276

### **Fedha za Matunzo na Matumizi ya Kawaida kwa Ofisi za Wabunge**

**MHE. MBARUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa kila mwaka Bunge huidhinisha kasma ya kugharimia matunzo na matumizi ya kawaida ya Ofisi za Waheshimiwa Wabunge kupitia Ofisi za Wakuu wa Mikoa; na kwa kuwa baadhi ya Makatibu Tawala wa Mikoa hawapati fedha hizo na hawapendi kukiri kuwepo kwa fungu hilo:-

(a) Je, Serikali inaweza kulithibitishia Bunge iwapo fedha zinazokasimiwa kwa ajili ya kazi hiyo zinapelekwa Mikoani au la?

(b) Je, ili kuondoa utata uliopo, isingekuwa busara kwa Serikali kulipa fedha hizo moja kwa moja kwa Wabunge kupitia Ofisi ya Bunge?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, fedha za matunzo na matumizi ya kawaida kwa Ofisi za Wabunge limekuwa likiulizwa mara nyingi na Waheshimiwa Wabunge kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Serikali inaelewa umuhimu wa suala hili na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake ya Bajeti ya mwaka 2004/2005, alilifafanua vizuri

Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu inafanya juhudzi za kuhakikisha Waheshimiwa Wabunge wanakuwa na sehemu zao za kutekelezea majukumu yao kwa kuhakikisha wanapatiwa majengo ya Serikali yaliyopo kwenye Majimbo, Wilaya na Makao Makuu ya Mko. Kwa hiyo, kuanzia mwaka 2002/2003 hadi sasa, Serikali imekuwa ikifanya juhudzi za kutengeneza Ofisi za Waheshimiwa Wabunge, kwa viwango mbalimbali kama jedwali lenye taarifa ya fedha na huduma zilizotolewa kwenye Ofisi hizo kwa mwaka 2003/2004, nililolitoa hapa Bungeni wakati ninawasilisha Bajeti ya Ofisi yangu linavyoonesha.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa linalolikabili zoezi hili ni ufinyu wa bajeti kwa upande mmoja na usimamizi mdogo wa fedha hiyo katika baadhi ya maeneo kwa upande mwingine. Ninapenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, walioniletea taarifa mbalimbali kuhusu matengenezo yanayoendelea katika Ofisi hizo. Ofisi yangu imekwishaanza kufuutilia masuala hayo ili kurekebisha kasoro zozote zitakazobainika.

Aidha, Ofisi yangu itazingatia ushauri utakaotolewa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, kufuatia ziara ya Kamati hiyo katika baadhi ya Ofisi hizo.

(b) Mheshimiwa Spika, kulingana na Sheria za Matumizi ya Fedha za Serikali, Afisa Mhasibu wa Mkoa ni Katibu Tawala wa Mkoa. Hivyo, kwa sasa kulingana na mfumo wa Matumizi ya Fedha za Serikali ulivyo, siyo rahisi kwa Serikali kutoa fedha kwa Mheshimiwa Mbunge kwa ajili ya kuendesha Ofisi ya Serikali moja kwa moja. Aidha, Ofisi ya Bunge ina uwezo mdogo wa kuziendesha Ofisi za Wabunge zilizoko Mikoani kwa sasa, kwani yenye haina mtandao katika Mikoa hapa nchini. Hivyo, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, tuendelee kuwa na subira wakati Serikali inatafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili kwa kushirikiana na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kushauri kwamba kuna umuhimu wa kurekebisha masuala haya.

(a) Je, isingekuwa busara kwa Serikali kuagiza Makatibu Tawala wa Mikoa wawahusishe Waheshimiwa Wabunge kikamilifu katika kushughulikia masuala haya pamoja na ununuzi wa vitu mbalimbali vinavyohusika?

(b) Isingekuwa vizuri pakawa na uwazi zaidi kuliko ilivyo hivi sasa na taarifa za hesabu zikatolewa kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusu manunuzi yaliyofanyika? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu rai ya kutaka Waheshimiwa Wabunge wahusishwe katika matengenezo na ununuzi wa vifaa mbalimbali kwa ajili ya Ofisi za Wabunge, ndio hasa nia ya Serikali kwamba, kwa kadri itakavyowezekana, hawa Makatibu Tawala wa Mikoa wanapaswa kushirikiana kwa karibu kabisa na Waheshimiwa Wabunge ili kuweza kujua kinachoendelea nini na kwa utaratibu gani. Pengine niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge, tusaidiane kwa sababu Mikoa hii tunajua vizuri na Makatibu Tawala wa Mikoa tunawajua vizuri. Kwa lengo la kuhakikisha kwamba, jambo hili linakwenda, ni vizuri na nyie mkawabana vilevile moja kwa moja kwa sababu ni sehemu ya uongozi wa Mikoa yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwazi juu ya suala hili, kwa kweli kwa sehemu kubwa ni kama sehemu (a) ya swali la nyongeza linavyosema. Tutajitahidi kutoa maelekezo tena na tena kuhakikisha kwamba, jambo hili linafanyika kwa uwazi kwa kadri itakavyowezekana, ikiwa ni pamoja na kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge, fedha ambazo zimetengwa katika *OC*, lakini *specifically* kwa ajili ya Ofisi za Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Wakuu wa Mikoa

wanapewa fungu linaloitwa *Political Vote* na kwa kuwa fungu hilo limetokana na shinikizo la Bunge hili. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya Waheshimiwa Wabunge kujua fungu hili hasa limetumika vipi hasa kwa mwaka uliopita wa 2003/2004? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Wakuu wa Mikoa wanalo fungu mahsus kwa ajili ya shughuli mbalimbali za Maendeleo katika Mikoa yao na kama mtakavyokumbuka, lilianza na shilingi milioni tano, lakini baadaye zikaongezwa zikafikia milioni kumi. Sasa kuhusu rai hasa ya Mheshimiwa Mbunge kwamba ni vizuri wakajua fedha hizo zinavyotumika, linaloweza kusema hapa Mheshimiwa William Shellukindo ni kwamba, fedha hizi kwa upande mmoja ni kweli zinaidhinishwa na Bunge, lakini kwa upande mwingine ni Rais mwenyewe aliamua kufanya hivyo, kuwapa nafasi hawa Wakuu wa Mikoa ili waweze kutekeleza majukumu yao vizuri.

Kwa hiyo, ambacho tumekuwa tunakiona kinafanyika, Wakuu wa Mikoa wamekuwa wakitoa maelezo kwa lengo la kumwezesha Rais kujua ni nini fedha hizo zimetumika kufanya. Sasa kama rai ni ya kutaka na Bunge lijue, basi inabidi labda baadaye tuwasiliane pengine na Mheshimiwa Waziri Mkuu, tuone kama litakuwa ni jambo zuri au tumwachie Mheshimiwa Rais mwenyewe aendelee kusimamia.

Na. 277

#### **Barabara ya Nduha - Mbarika**

**MHE. JACOB D. SHIBILITI** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Nduha - Kasololo - Mbarika ilifanyiwa matengenezo kwa mara ya mwisho miaka ya 1980 ikiwa chini ya Mkoa:-

- (a) Je, barabara hiyo iko chini ya nani hasa kati ya Mkoa na Halmashauri?
- (b) Je, Mhusika anasema nini juu ya barabara hiyo kwa kutopitika na kufanya wakazi wa maeneo husika kuwa wakiwa?
- (c) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya matengenezo katika mwaka huu wa fedha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Dalali, Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, barabara ya Nduha - Mbarika ni sehemu ya barabara itokayo Manawa mpaka Mbarika yenye urefu wa kilomita 42. Barabara hii iko chini ya

Mkoa na imenorodheshwa katika orodha ya barabara za Mkoa kwa Namba R165 na hivyo wenyewe jukumu la kuikarabati barabara hii ni *TANROADS*.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara hii ni ya Mkoa, ninamshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane moja kwa moja na Wakala a Barabara Mkoa wa Mwanza ili Bodi ya Barabara ya Mkoa iweze kuyazingatia maombi hayo kupitia hiyo *Road Board* na baadaye kwa Waziri wa Ujenzi. Hata hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii kwa Wilaya ya Misungwi, Halmashauri imekuwa ikiifanyia matengenezo ya dharura licha ya kwamba haiko chini yake. Mwaka 2001 Halmashauri ilitenga Sh. 9,000,000/= kwa ajili ya kulifanyia matengenezo daraja la Kasolo, matengenezo sehemu ya Musufini kwa kujenga makalvati, kumwaga changarawe na kufyatua kalvati kwa ajili ya sehemu korofi ya Nduha. Kwa mwaka 2004, Halmashauri imefanya matengenezo ya sehemu korofi ya Nduha kwa kujenga makalvati sehemu saba na kujaza kifusi na changarawe sehemu korofi iliyoharibiwa na mvua kwa jumla ya Sh.9,500,000/=.

(c) Mheshimiwa Spika, barabara itokayo Nduha hadi Mbarika haijatengewa fedha ye yeyote na Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ambazo ni kwa ajili ya kufanya matengenezo madogo madogo tu (*maintenance*), kutokana na ufinyu wa bajeti katika Halmashauri hiyo.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ya leo, tofauti na ya mwanzo ambapo aliwahi kuikubali barabara hii kuwa iko chini yake, lakini kwa leo amesema kwamba, iko chini ya Mkoa. Je, kwa vile haijatengewa fedha yoyote kwake na kwenye *TANROADS*, Mheshimiwa Naibu Waziri anatamka nini na kuwaeleza nini Wananchi wa maeneo hayo ya Nduha - Kasololo mpaka Mbarika jinsi wanavyozidi kuteseka mpaka leo hii? (*Makofu*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ngoja ajibewe na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya barabara hii ilikuwa inababaisha kidogo na ndiyo maana Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI alijibu kwamba, barabara hii ni ya Halmashauri na sasa amejibu kwamba, barabara hii ni ya *TANROADS* Mkoa. Mimi namwomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira, afuatilie msururu aliomshauri Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI ili *TANROADS* wawe na uhakika wa kuipangia fedha kwa sababu fedha katika Mkoa huo wa Mwanza zipo za kuweza kupanga baadaye kutengeneza barabara hiyo.

Na. 278

#### **Upanuzi wa Hifadhi ya Lukwika - Lumesule**

**MHE. ARIDI M. ULEDI** aliuliza:-

Kwa kuwa eneo la chini ya Mto Lumesule lina madini ya kutosha; na kuwa huko nyuma Wananchi walikwishaanza kuchimba madini hayo lakini walisitishwa na Serikali ili kupisha upanuzi wa Hifadha ya Lukwika - Lumesule; na kwa kuwa Wananchi wengi wanaoishi kwenye vijiji vinavyozunguka Hifadhi hiyo hukosa kipato kutokana na mazao yao kushambuliwa na wanyama mara kwa mara:-

- (a) Je, Serikali haioni kuwa uamuzi wake huo umeongeza umaskini kwa Wananchi wa maeneo hayo?
- (b) Je, Serikali itakuwa tayari kulirudisha eneo hilo kwa uchimbaji wa madini?
- (c) Je, Serikali kabla ya uamuzi wake huo ilifanya tathmini yoyote kujua faida itakayopatikana kwa eneo hilo lenye madini kuwemo ndani ya Hifadhi au kuwa la uchimbaji wa madini?

#### **WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Aridi Uledi , Mbunge wa Nanyumbu, naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mchakato wa kutenga maeneo ya hifadhi kisheria hufanyika kwa kushirikiana na Uongozi wa Serikali na Wananchi wa maeneo husika. Pale ambapo kuna mahitaji ya kuanzisha maeneo ya Hifadhi, Serikali katika maeneo husika, huwasiliana na Wananchi kwa kutumia taratibu zilizopo na kisha kufikisha mawazo yao kwa Wizara ya Maliasili na Utalii. Huu ni utaratibu ulioanza siku za karibuni baada ya madaraka Mikoani na kutiliwa mkazo na mabadiliko yanayoendelea ya kiuchumi na kijamii, ambapo pia sera ya nchi zinatilia mkazo masuala ya ushirikishaji jamii katika shughuli mbalimbali za maendeleo na katika kutoa maamuzi yanayowagusa Wananchi.

Sehemu ndogo ya eneo la Lukwika - Lumesule kabla ya kutangazwa rasmi kuwa Pori la Akiba, ilikuwa inatumika kwa shughuli za uchimbaji madini, jambo ambalo lilikuwa linatishia usalama wa rasilimali ya wanyamapori kutokana na uharibifu wa mazingira. Uamuzi wa kulifanya eneo la Lukwika - Lumesule kuwa Pori la Akiba la Uhifadhi Wanyamapori ulifikiwa ili kulinda rasilimali za maliasili na kuwezesha matumizi endelevu ya rasilimali hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swalii la Mheshimiwa Aridi Uledi, Mbunge wa Jimbo la Nanyumbu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Uamuzi wa Serikali wa kuanzisha Pori la Akiba la Lukwika - Lumesule ni wa manufaa kwa Wananchi wengi wa Wilaya ya Masasi, Kitaifa na katika hifadhi ya bioanuwai ya nchi.

Kuanzia mwaka 1997 hadi 2002, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ilipata jumla ya shilingi 10,185,836/= ikiwa ni asilimia 25 ya fedha zilizotokana na uwindaji wa kitalii. Fedha hizo zimetumika katika kusaidia uhifadhi wa miradi ya maendeleo ya Wananchi wanaoishi karibu na maeneo yanayozunguka pori hilo.

Miradi ya Maendeleo ya Wananchi iliyotekelawa ni pamoja na ujenzi wa madarasa ya shule katika kijiji cha Mpombe, ujenzi wa daraja la Mto Lukwamba na ujenzi wa Ofisi ya Kijiji cha Mburusa. Aidha, Kampuni za uwindaji wa kitalii zimetoa michango mbalimbali kwa Wananchi ikiwemo utoaji wa dawa ya *sulphur* kwa ajili ya kuulia wadudu wanaoharibu mikorosho, chakula cha msaada wakati wa njaa na kutoa ajira kwa baadhi ya Wananchi.

(b) Kutokana na manufaa hayo kwa Wananchi, Serikali haikusudii kulirudisha eneo hilo tena kwa shughuli za uchimbaji madini.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya msingi, kabla ya Serikali kufikia uamuzi niliouelezea hapo awali, wadau mbalimbali walishirikishwa kikamilifu. Aidha, tathmini ilifanyika katika eneo hilo na kubaini kuwepo kwa matumizi mabaya ya maliasili pamoja na uharibifu wa mazingira. Kutokana na matokeo ya tathmini hiyo, ilionekana ni busara eneo hilo litengwe kuwa Pori la Akiba la Uhifadhi ili liweze kupata ulinzi wa kutosha na udhibiti wa matumizi ya rasilimali zilizopo kwa manufaa ya Wananchi wote.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa tatizo la wanyamapori limepelekea Wananchi wanaoishi karibu na hifadhi hiyo kukosa mapato kutokana na kilimo na vilevile kutokana na madini; na kwa kuwa Serikali inaruhusu vikundi vyta uvuvi na kurina asili kwenye hifadhi; je, kwa nini sasa Serikalil hiyo hiyo isiruhusu vikundi vyta Wananchi kuchimba madini katika maeneo hayo ili kuweza kujipatia kipato?

(b) Kwa kuwa Wananchi hao sasa wameona kuwa uamuzi wa kuyatua maeneo hayo umewapunguzia kipato hivyo kukaribisha umaskini. Sasa Serikali inasema nini juu ya kuwasaidia Wananchi hao kuondokana na umaskini? (*Makofii*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kwamba, eneo hilo ni eneo ambalo kuna tembo wengi sana. Kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema kwamba ni kweli mara nyingine kunatoka uharibifu kutokana na wanyamapori. Siku zote nimekuwa nikijibu hapa kwamba, utaratibu unafanywa pale ambapo wanyamapori wanaingia katika maeneo ya Wananchi. Lakini niseme kwamba, suala lake Mheshimiwa Mbunge kuhusu uvuvi na urinaji wa asali na jinsi gani ambavyo anafikiri kwamba kwa kufanya hivi kumeleta umaskini zaidi, lakini niseme nafikiri si sahihi kwamba, kumeleta umaskini zaidi pengine umaskini zaidi ungekuwepo pale ambapo uhifadhi ungekuwa haupo katika maeneo haya kwa sababu ya uharibifu wa bioanuwai.

Mheshimiwa Spika, uwindaji katika eneo hili unafanyika katika miezi sita kuanzia mwezi Julai mpaka Desemba, kuanzia Januari mpaka Juni, katika eneo hili kunakuwa hakuna uwindaji. Ukichukua sheria ya misitu pamoja na sheria hii mpya ambayo sasa hivi tunairekebisha ya wanyamapor, itawezekana kabisa kwa Wananchi kuweza kufaidika kwa upande wa asali na upande wa uvuvi. Kwa hiyo, ninasema kwamba, tungoje sheria hiyo ya wanyamapor ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wamehusishwa katika kutoa mawazo ili tuweze kuitipisha na kuona jinsi gani sheria hizi mbili ya Wanyamapor na Sheria ya Misitu, ukizichukua kwa pamoja, zitaweza kusaidia Wananchi.

Na. 279

### **Usambazaji Maji kwa Kutumia mianzi**

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU** aliuliza:-

Kwa kuwa kulikuwa na utafiti wa usambazaji maji kwa kutumia mianzi, utafiti ambao ungepunguza gharama za usambazaji maji katika maeneo ya Milima kama Usambara hususan Lushoto kwa kuepuka matumizi ya mabomba ya chuma na *P.V.C* ambayo yana gharama kubwa. Je, utafiti huo ulifikia wapi na matokeo yake yalikuwaje?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mbunge wa Jimbo la Lushoto, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, zilikuwepo jitihada za kutumia mianzi kwa ajili ya usambazaji wa maji katika maeneo mbalimbali hapa nchini kati ya mwanzoni mwa miaka ya sabini hadi katikati ya miaka ya themanini. Jitihada hizo zilizingatia maoni kuwa mianzi ikitumiwa ipasavyo kwenye mazingira yanayofaa na kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vyta kitaalam, ingeweza kutumika kama ilivyo kwa mabomba ya aina nyingine, kwa mfano, *Polyvinyl Chloride (PVC)* na *Galvanised Steel (GS)*.

Kwa kuzingatia maoni hayo, usambazaji wa maji kwa kutumia mianzi ulifanyika chini ya Mradi wa Mianzi katika Wilaya ya Dodoma Vijijini katika Mkoa wa Dodoma, Wilaya ya Mbinga na Songea Vijijini Mkoani Ruvuma, Wilaya za Makete, Njombe, Mufindi, Iringa Vijijini, Kilolo na Ludewa Mkoani Iringa, Wilaya ya Mbeya Vijijini, Rungwe na Ileje Mkoani Mbeya na Wilaya ya Sumbawanga Mjini na Sumbawanga Vijijini katika Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, kasi ya matumizi ya mianzi ilipungua baada ya kuonekana kuwa mianzi inayo mapungufu mengi ikilinganishwa na teknolojia nyingine zilizopo kwenye soko. Mapungufu hayo yalibainishwa na tafiti mbalimbali zilizofanywa na pia kutokana na uzoefu uliopatikana wakati wa matumizi yake. Baadhi ya mapungufu

hayo yalikuwa ni upatikanaji mdogo wa mianzi ikilinganishwa na mahitaji, kuoza haraka kwa mianzi, uharibifu wa mazingira kutokana na wadudu walioshambulia mianzi hiyo na uwezo mdogo wa mianzi kuhimili nguvu za msukumo wa maji ikilinganishwa na aina nyingine za mabomba.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mapungufu hayo na nguvu ya soko, matumizi ya mianzi kwa ajili ya kusambaza maji yalisimama na teknolojia hiyo kuonekana imepitwa na wakati na haifai tena.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Ni kweli maelezo yake ni mazuri, lakini lipotatizo la taarifa za utafiti kutotolewa kwa Wananchi. Je, Serikali itachukua hatua gani na inakubali kwamba itengwe siku katika nchi yetu ya kutambua tafiti mbalimbali zilizofanyika ili Wananchi wajue matokeo ya tafiti hizo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli inawezekana kwamba, taarifa hizo zinaweza kutowafikia Wananchi, lakini taarifa za utafiti na idadi ya utafiti unaofanyika nchini wakati wowote ule sidhani kama itawezekana kila matokeo ya utafiti yaweze kueleweka kwa Wananchi. Utafiti mwingine unafanyika kwa ajili ya kuendeleza au kutafuta mbinu ambayo baadaye itatumika kwa ajili ya manufaa ya Wananchi. Kwa hiyo, pamoja na wazo zuri la Mheshimiwa Henry Shekiffu, ni vigumu sana taarifa za utafiti kama huo zikatolewa kila wakati. Ni pale tu inapohitajika kama alivyoulima swali Mheshimiwa Mbunge, tunaweza kutoa taarifa hiyo kama leo.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swalii dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu yake ya msingi amesema kwamba, moja ya kikwazo ni upungufu wa mianzi, lakini kwa kuwa mianzi inapatikana sana katika Nyanda za Juu Kusini hata katika maeneo ya mwambao na kwa kuwa mianzi hii ingeweza kuwa *treated*, je, Serikali inatoa msaada gani wa kumsaidia mtafiti huyo ili aweze kurekebisha mfumo huu ambao umeanza? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji wakati ule miaka ya sabini na themanini ndiyo ilioanzisha kwa kupitia mbunifi wake ambaye alikuwa ni mwajiriwa wa Wizara ya Maji, *Engineer Thabiti Lipangile*. Kwa hiyo, ule utafiti ulifanyika kwa *initiative* za Wizara ya Maji na ilichukua miaka kumi na zaidi, nilivyoeleza ni tangu miaka ya sabini hadi ya themanini. Kwa hiyo, inaeleweka kabisa kwamba, maeneo yote ya utafiti, kuangalia *durability* ya mabomba na kuangalia ni dawa gani za wadudu ambazo hazita-*contaminate* tena maji kwa sababu unaposema ku-*treat* hizi *fibre* za mianzi unamaanisha kwamba, hayo madawa yanaweza kuingilia na matumizi ya maji na uka-*poison* maji badala ya kusaidia katika ku-*preserve* bomba lenyewe.

Mheshimiwa Spika, uwezekano wa upatikanaji wa mianzi kwa wingi inawezekana kabisa ni mkubwa, lakini *diameter* zinazohitajika kwa ajili ya kusafirisha maji zinahitajika za aina mbalimbali na mianzi kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge

huko Kusini ina matumizi mengi, ikiwemo pamoja na kutengeneza ulanzi na kadhalika. Kwa hiyo, kuna uwezekano kabisa kwamba, *age* ya mianzi inayohitajika kwa ajili ya matumizi ya bomba inaweza isifikasiwe kwa ajili ya kuongezeka kwa matumizi mengine. (*Makofii*)

Na. 280

### **Mahitaji ya Maji - Mji wa Mhunze**

**MHE. PAUL N. MAKOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Mhunze ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Kishapu unakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa maji ya kunywa na kwa kuwa mtambo wa maji uliopo hautoshelezi mahitaji ya maji kwa wakazi wa Mji huo. Je, Serikali ina mpango gani kutosheleza mahitaji ya maji kwa wakazi wa Mji huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Paul Makolo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Mji wa Mhunze ulifanyiwa ukarabati mara ya mwisho kuanzia mwaka 1992 hadi 1994 kwa ufadhili wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya UNDP na UNICEF. Ukarabati ulipangwa ufanyike katika awamu mbili kutokana na gharama yake kuwa kubwa. Katika awamu ya kwanza utekelezaji wa mradi ulifanyika katika maeneo ya Mhunze, Igaga na sehemu ya Isoso. Mashine ya kutosheleza maji katika maeneo hayo ilifungwa na mfumo wa mabomba na vituo vya kuchotea maji kwenye baadhi ya eneo la mradi ulifanyiwa ukarabati. Kutokana na mpango huu, huduma ya upatikanaji maji iliweza kufika hadi Mhunze kwa kiasi kidogo.

Mheshimiwa Spika, mpango wa awamu ya pili, ulikuwa ni kukarabati maeneo yote ya mradi yaliyokuwa yamebaki na kununua mashine kubwa ya kukidhi mahitaji ya maji kwenye eneo lote la mradi. Hivyo, maji yangetapikana sehemu yote ya Isoso na hata Kishapu. Hata hivyo, awamu ya pili haikutekelezwa kutokana na muda wa mradi kwisha na hivyo kufanya maeneo yaliyolengwa kwenye awamu hii kutopata huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ongezeko la watu kwenye Mji wa Mhunze ambao ni Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Kishapu, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ya Shinyanga na Kishapu, ina mpango wa kujumuisha ukarabati wa mradi huo kwenye bajeti yake ya mwaka wa fedha wa 2004/2005 katika Programu ya Maji Vijiji na Usafi wa Mazingira (*Rural Water Supply and Sanitation Programme*), inayotekelawa kwa msaada wa Serikali ya Uhulanzi Mkoani Shinyanga.

Wananchi wa Mji wa Mhunze wanatakiwa kujiardaa kuchangia sehemu ya gharama ya ujenzi wa mradi huo kama itakavyobainishwa wakati wa usanifu wake. Aidha, ili huduma ya maji iwe endelevu katika Mji wa Mhunze, inashauriwa kianzishwe chombo cha watumiaji maji kitakachosimamia uendeshaji wa shughuli za maji Mjini Mhunze. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na Halmashauri ya Wilaya kama anavyofanya kila mara katika uhamasishaji wa kuanzisha chombo hicho.

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, Wananchi wa hapo wajiandae na kwamba Serikali sasa ina mpango wa kuingiza kwenye bajeti inayofuata.

Kwa kuwa Mhunze ulikuwa ni mji ulioleuliwa kuwa Makao Makuu ya Wilaya Mpya ya Kishapu, hivi mji huo ulianzishwa bila ya kuwa na programu za kuwapatia Wananchi wale maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, huo ni mji umekuwepo miaka mingi sana. Kwa sababu kwanza kuna *ginnery* ya kuchambua pamba. Kwa hiyo, huo mji umekuwepo siku nyingi. Ulianza kama kijiji sasa hivi umebadilika kuwa Mji wa Wilaya. *Water Supply* iliyokuwepo walikuwa wanachota kutoka kwenye mto ambao ndio *source* iliyokuwa *realible* kwa ajili ya Mji wa Mhunze. Hapo awali kwa sababu usimamizi haukuwa mzuri, kumekuwepo matukio mara nyingine mara pampu kuibiwa, wanakamata zinarudishwa zinafungwa tena.

Kwa hiyo, jitihada za kutoa maji kwa ajili ya Mhunze zimekuwepo siku nyingi na tumejitahidi sana kwa wakati mbalimbali Serikali kusaidia. Lakini baada ya hilo tunaomba baada ya kuundwa chombo ni hakika kwamba matatizo haya yatapungua sana. Kwa sababu uzoefu umetuonyesha kwamba, panapokuwepo na chombo cha watumiaji maji kunakuwepo na usimamizi na uwajibikaji. Kwa hiyo nina hakika kwamba matatizo hayo yote yatakwisha.

Na. 281

### **Mpira wa Miguu wa Kulipwa**

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa imedhihirika wazi kuwa kiwango cha mpira wa miguu hapa nchini kimezidi kushuka na hakipandi na kwa kuwa Serikali imeshakubali kimsingi kuanzisha mpira wa miguu wa kulipwa kama njia mojawapo ya kuinua kiwango hicho:-

(a) Je, suala la kuanzishwa kwa mpira wa miguu wa kulipwa (*Professional Football*) limefikia wapi?

(b) Je, Serikali imeandaa mazingira gani mazuri yatakayowezesha kuanzishwa kwa mpira wa miguu wa kulipwa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imesharuhusu uanzishaji wa mpira wa miguu wa kulipwa. Suala la uanzishwaji wa vilabu vya mpira wa kulipwa au kuwa na wachezaji wa kulipwa ni suala la wadau wenyewe wenyе mahitaji ya namna hiyo. Hivyo, hivi sasa milango iko wazi kwa yeote anayetaka kumiliki timu au wachezaji wa kulipwa ili mradi masharti ya sheria nyingine za nchi yanazingatiwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kuridhia uanzishaji wa michezo ya kulipwa ni mazingira tosha ya kuwawezesha Wananchi wake kutekeleza azma yao ya kuwa na wachezaji wa soka ya kulipwa. Kuanzisha michezo ya kulipwa sio suala la mazingira pekee, linahitaji pia mtaji wa kutosha kumudu maendeleo ya timu, miradi endelevu, uongozi thabiti usiroyumba, wachezaji wenyе elimu ya michezo na uwezo wa kuchenza kwa mujibu wa mkataba na chama cha michezo chenye uwezo wa kuendesha mashindano ya michezo ya kulipwa. Hata hivyo, endapo liko tatizo lolote linalokwaza nia hiyo, basi Wizara yangu ipo tayari wakati wowote kusaidia kwa yale yaliyo ndani ya uwezo wetu.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

La kwanza, yapo madai kwamba Serikali imekata tamaa kushughulikia matatizo ya uongozi na uendeshaji wa mpira wa miguu kwa maana kwamba wamezidiwa kete na Ndolanga na *FIFA*. Lakini pia yako madai kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, amepunguza kasi ya kushughulikia matatizo haya kwa sababu ya muafaka kati ya Ndolanga na Wambura. Je, Mheshimiwa Waziri au Serikali inasemaje juu ya madai hayo?

Pili, Kamati ya Utendaji ya Chama cha Mpira ilipokuja hapa Bungeni na kuonana na Kamati inayohusika, Ndolanga alimshutumu Wambura kwamba, ametafuna fedha nyingi za *FAT*. Lakini vile vile Wambura alimshutumu Ndolanga kwamba, ametafuna fedha nyingi za *FAT*. Je, muafaka huu uliofikiwa unaliangalia vipi suala hili au Serikali inasemaje juu ya utafunaji na muafaka uliofikiwa? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Spika, sio siri kuwa kuna matatizo makubwa ya uongozi katika chama chetu cha Soka, ndiyo maana hata Kamati yako ya Kudumu ya Bunge iliwhi hapa kuuita Uongozi mzima wa *FAT*. Lakini tunachofanya sasa hivi sio kuzidiwa kete na Ndolanga au *FIFA*, tunachofanya ni kuweka mbele maslahi ya Watanzania.

Kwa sababu tunao uwezo wa kusema sasa basi, lakini tunaposema sasa basi tunaweza kuwaumiza tunafikiria kwamba unaweza kuwa ni Uongozi wa *FAT* ule wa watu 13, lakini tunafikiria Watanzania wengi ambao watashindwa kabisa kuwa na uhusiano wa masuala ya kisoka katika jamii ya Kimataifa.

Tunawaona wenzetu wa Kenya baada ya Serikali kuchukua msimamo huo hivi sasa Kenya imefungiwa na *FIFA* na hata timu yao ya Taifa ambayo ilituondosha sisi iweze kuendelea *round* ya pili na yenyewe imesimama. Kwa hiyo, kupanga ni kuchagua, sisi turifikiria tuwajali watu wengi zaidi kuliko watu wachache. Hata hivyo, kama kuna ushauri mwingine, inafaa tushirikiane na Wananchi wetu badala ya kufikiria watu wawili au watatu.

Ama hili la kwamba walipokuja hapa walishutumiana kati ya Bwana Wambura na Bwana Ndolanga, ni kweli kila mmoja alimwambia mwenzake ametafuna pesa. Lakini ili warudi walikubaliana kuwa na ndoa ambayo nina hakika sio ya mapenzi, ili waweze kubakia ndani ya Uongozi wa *FAT*.

Ndiyo maana nakuombeni kwa nia njema kabisa Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tunapokwenda kwenye mikoa yetu tuhakikishe kwamba, uchaguzi unaoendelea hivi sasa wa mikoa, tuhakikishe kwamba, tunawaweka watu ambao wanaweza wakaona uchungu wa Watanzania dhidi ya Uongozi uliopo hivi sasa *FAT*. Maana ndio hao hao ambao watairudisha *FAT* mara baada ya Katiba mpya kupita.

Si kweli vile vile kwamba, Bwana Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, amepunguza kasi kwa sababu ya Bwana Wambura kukubaliana na Bwana Ndolanga. Lakini kama tutapata maelezo ya kutosha juu ya hili sio nitamjulisha tu Mheshimiwa Mohamed Missanga, lakini nitalijulisha na Bunge lako vile vile. Ila kwa sasa hatuna taarifa hiyo.

Na. 282

### **Barabara ya Dodoma - Manyara - Arusha**

**MHE. KHALID S. SURU** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Dodoma - Manyara - Arusha ni muhimu sana kijamii, kiuchumi na kihuduma katika maeneo hayo; na kwa kuwa Serikali ilitoa ahadi ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami kutoka Minjingu - Babati - Kondoa - Dodoma hadi Iringa:-

(a) Je, Serikali inatoa maelezo gani kwa Wananchi waliopewa ahadi hiyo ambayo mpaka sasa hakuna chochote kilichofanyika katika barabara hiyo muhimu ambayo inaunganisha Makao Makuu ya Serikali Dodoma na Mkoa wa Arusha yalipo Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki?

(b) Kwa kuwa daraja la Mto Kolo lililokuwa kwenye eneo la Mto Kolo lilivunjika kabisa katika kipindi cha miaka sita iliyopita; na kwa kuwa Serikali ilitoa ahadi ya kulijenga upya daraja hilo ili kurejesha mawasiliano katika pande zote mbili; je, kwa nini Serikali imeacha kabisa kushughulikia ujenzi wa daraja hilo?

(c) Je, kwa nini barabara hiyo imepewa nafasi ya mwisho ikilinganishwa na barabara nyingine na kama sivyo Serikali inaweza kutoa utaratibu unaoelewika, hatua ya kujenga, kuikarabati na kuiboresha barabara hiyo muhimu?

#### **NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Khalid Suru, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa barabara ya Dodoma - Minjingu na Dodoma - Iringa ambazo ni sehemu ya *The Great North Road*, juhudii zimekwishafanyika ambapo barabara hii sasa imejumuishwa katika barabara zitakazojengwa katika mpango wa Jumuiya ya Ushirikiano wa Nchi za Afrika Mashariki. Kwa kuititia mpango huu, barabara ya ukanda wa Tunduma - Iringa - Dodoma - Arusha - Namanga - Nairobi - Isiolo - Moyale imepewa umuhimu namba moja (*Priority No. 1*) katika ratiba ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha wa 2004/2005, barabara ya Minjingu - Babati - Singida (km. 223) itafanyiwa upembuzi yakinifu pamoja na usanifu kwa kutumia fedha za ndani na za wafadhili kwa gharama ya Sh. 984.4 milioni. Vile vile katika mwaka huu wa fedha, barabara ya Babati - Dodoma - Iringa imepangwa kuanza kufanyiwa usanifu kwa kutumia fedha za *IDA* na fedha za Serikali. Jumla ya shilingi bilioni 2.41 zimetengwa kwa kazi hiyo.

Aidha, barabara hii imetengewa katika mwaka huu wa fedha jumla ya shilingi milioni 366.991 kutoka Mfuko wa Barabara. Kati ya fedha hizi, shilingi milioni 288 ni kwa ajili ya matengenezo maalum ya Iringa - Dodoma hadi Bereko na shilingi milioni 78,991ni kwa ajili ya madaraja ya Migoli, Chikora III, Matumburu, Bicha kwa Ntisi na Kagera.

(b) Mheshimiwa Spika, eneo la daraja la Mto Kolo lipo katika Kijiji cha Kolo kilichoko umbali wa kilomita 184 kutoka Dodoma katika barabara kuu ya Dodoma - Bereko. Mara baada ya daraja hilo kuvunjika, Wizara yangu kuititia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Dodoma, ilichukua hatua za dharura za kujenga daraja la mfuto (*Concrete Drift*) pembezoni mwa daraja lililovunjika ili kurejesha upya mawasiliano. Daraja hilo la mfuto liligharimu kiasi cha shilingi 21.34 milioni.

Kwa kuzingatia umuhimu mkubwa wa barabara hii, aliteuliwa Mhandisi Mshauri ili afanye upembuzi yakinifu na kisha kufanya usanifu wa daraja la kudumu litakalojengwa katika eneo hilo. Kampuni ya Uhandisi ushauri ya *M/S Design Partnership* ya Dar es Salaam ilikamilisha kazi hii kwa gharama ya shilingi 28.07 milioni

na kukabidhi taarifa zake mwezi Februari, 2003. Ujenzi wa daraja hili unategemewa kuanza mara baada ya kukamilika usanifu wa barabara yote ya Babati - Dodoma ambao unategemewa kuanza katika bajeti ya mwaka 2004/2005 kama tulivyoonyesha.

Hata hivyo, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara, itahakikisha kuwa sehemu hiyo inaendelea kupitika katika majira yote ya mwaka kwa kulifanyia matengenezo muhimu daraja la mfuto kila itakapohitajika.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu (a) ya jibu, utekelezaji wa matengenezo ya barabara hii umepewa umuhimu namba moja (*Priority No. 1*). Kwa uelewa huo basi, tunaamini kuwa yote yaliyopangwa yatakelezwa kwa mujibu wa ratiba iliyokubalika.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, nauliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo;

(a) Je, kazi ya upembuzi yakinifu ikikamilika kazi ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami itaanza mara moja?

(b) Barabara ya kipande cha Dodoma - Kondo - Bereko ni mbaya sana kwa sababu mwaka 2003/2004, ilitengewa fedha kilomita 15 tu na 2004/2005 wametenga fedha za kilomita 5 tu. Je, Serikali kweli inajali hii barabara, kama inajali barabara itaongeza fedha ili barabara hiyo ipitike mwaka mzima? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu ikikamilika ujenzi utaanza kama tulivyozungumza kwamba, tukipata fedha za kujenga barabara ya lami na lazima tupate fedha. Sisi tuko tayari kujenga isipokuwa tatizo ni ufinyu wa bajeti. Kwa hiyo, tunatafuta fedha kwa sababu ya barabara hii. Tuko tayari kujenga tukipata fedha. Kwa hiyo, sitaki kuahidi hapa kwamba tutajenga upembuzi yakinifu ukimalizika, tukipata fedha za kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Kuhusu swalii la pili, juu ya kuongeza fedha zaidi ya ile iliyopangwa. Mheshimiwa Suru wewe ni shahidi, bajeti tumepitisha wote hapa. Sasa Wizara ya Ujenzi itapata wapi nyongeza! Ni ile fedha tuliyopanga ndiyo hiyo itakayo jitahidi kuhakikisha na barabara hii inapitika wakati wote, lakini si zaidi ya pale.

Na. 283

#### **Daraja la Kuvuka Mto Ruvuma**

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 1996 Serikali ya Uingereza ilitoa msaada wa kujenga daraja kuvuka Mto Ruvuma jirani na Kijiji cha Mitomoni ili kuunganisha Mkoa na hasa Wilaya

ya Songea na Msumbiji na kwa kuwa pia zilitolewa fedha kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Songea - Mitomoni. Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya jambo hilo, kwani tangu msaada huo utolewe hakuna kilichofanyika?

### **NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Simon Mbilinyi, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli wazo la kujengwa daraja kuunganisha nchi ya Tanzania (Mkoa wa Ruvuma) na Msumbiji (Mkoa wa Niassa), eneo la Mitomoni lilikuwepo. Serikali ya Uingereza ilikubali kufadhili ujenzi huo kwa kuleta daraja la chuma ambalo lilikuwa Ngara baada ya daraja la kudumu katika barabara ya kwenda Ngara kukamilika. Aidha, sehemu ya barabara kuelekea darajani upande wa Tanzania pia ingeimarishwa kupitia msaada huo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majadiliano ya muda mrefu na wenzetu wa Msumbiji, wenzetu hawakukubaliana na mradi huo kwa wakati huo. Sababu walizotoa ilikuwa ni pamoja na Serikali ya Msumbiji haikuwa na uwezo wa kugharamia ujenzi wa *connecting road* toka darajani kwa wakati huo na pia Serikali ya Msumbiji ilipendekeza kuwa kwanza lijengwe Daraja la Umoja (*Unit Bridge*) pale Mtambaswala ambapo Serikali hizi zilikuwa zimekubaliana tangu awali.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya kutolewana huku na wenzetu wa Msumbiji wakati huo, Serikali ya Uingereza haikutoa msaada huo. Aidha, daraja la chuma walilokuwa wamelitoa wakati huo waliridhia Serikali kulipeleka Mto Malagarasi ambapo daraja hilo limekwishajengwa.

Mradi huu wa daraja la Mitomoni kwa sasa umeridhiwa na nchi zote mbili na hivyo umejumuishwa katika kabrasha la miradi ya ukanda wa maendeleo wa Mtwara (*Project Profiles*) kama *2nd Unity Bridge*.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi, kupitia Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara (*Mtwara Development Corridor*), itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa daraja la Mitomoni na ukarabati wa barabara ya Songea - Mitomoni. Hivi sasa Wizara yangu inaendelea kuihudumia barabara ya Songea - Mitomoni. Kwa mfano, mwaka huu wa fedha (2004/2005), Wizara yangu imetenga shilingi 49 milioni kwa madhumuni ya kukarabati na kuimarishe madaraja matatu katika barabara hiyo. Madaraja hayo ni Ruvuma, Nakawale na Matanda.

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nafurahi kwa majibu ya Naibu Waziri ni mazuri na nimeelewa. Swali langu moja tu dogo linahusu hasa hiyo kuunganisha kusema kuwa kama itapatikana hiyo fedha wametoa za daraja. Lakini naona huwa zinapatikana kiasi cha shilingi 200 bilioni kwa mwaka huu, lakini sisi tunahitaji labda chini ya shilingi bilioni moja kuimarishe hili.

Sasa hivi utaratibu ni kwamba, wanakarabati ile barabara mpaka mwanzo wa Kijiji cha Muhukulu wanaishia pale bado hawajafika kule darajani.

Je, wanaweza kufanya kazi hiyo ya kukarabati tu hata bila ya daraja?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nisisitize fedha ikipatikana daraja litajengeka. Lakini kwa sasa hivi kero kubwa iliyokuwa kwako ni kwa nini *TANROADS* hawafiki darajani. Nitawasiliana nao nijue kwa nini hawafiki.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniruhusu niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ya Tanzania huwa inaruhusu Wananchi kushirikiana na Serikali yao kutatua matatizo yanayowakabili na hivyo basi Serikali ya Mkao imeanza kuona ni namna gani inaweza kushughulikia ujenzi wa daraja hilo kwa namna moja au nyingine.

Je, Wizara itakuwa tayari kutoa ushirikiano hata kama ni kwa kiufundi ama utaalamu na kadhalika ili kusaidiana na Serikali hii kuanza kutatua tatizo hilo kwa hatua za mwanzo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, mradi wa daraja hili ni mradi mkubwa sana. Lakini kama Mkao unasema unataka kuingia katika kujaribu kujenga daraja hili na wanachotaka ni utaalamu, mimi nafikiri Wizara ya Ujenzi tutawapa wataalamu na tutashukuru sana kama Mkao utaingia kwenye utaratibu wa kujenga daraja hili. (*Makofi*)

Na. 284

### **Mkataba wa Kimataifa wa Kutowatesa Wafungwa na Mahabusu**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali mpaka sasa haijaridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa kutowatesa wafungwa na mahabusu. Je, kwa nini mpaka sasa Serikali haijaridhia Mkataba huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, napenda kutoa maelezo yafuatayo ya utangulizi:-

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Kimataifa wa Kutowatesa Wafungwa (*Prevention Against Torture and Other Inhuman or Degrading Treatment or Punishment*), ulipitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwaka 1984 kwa Azimio Na. 39/46. Azimio hilo liliweka masharti yanayopaswa kutekelezwa na nchi wanachama kabla ya kuridhia Mkataba huu. Masharti hayo ni kwamba, nchi husika inatakiwa itunge sheria au ichukue hatua za kiutawala, kimahakama au kwa njia yoyote ile, kuzuia

matendo ya utesaji wa wafungwa. Pia kwamba, kabla ya kuridhia Mkataba huu matukio yote ya utesaji wafungwa yawe yameingizwa katika sheria za nchi zinazohusu makosa ya jamii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Tanzania ni mionganoni mwa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa ambazo bado hazijaridhia Mkataba wa Kutowatesa Wafungwa. Tanzania hadi sasa haijaridhia Mkataba huu kwa sababu imekuwa inashughulikia kukamilisha utekelezaji wa masharti yaliyowekwa, kabla ya nchi kuridhia Mkataba huu. Masharti hayo tumeyatekeleza kama ifuatavyo:-

(a) Katazo la vitendo vyote vya utesaji wafungwa na mahabusu tayari limeingizwa katika sheria zetu za nchi zinazohusu makosa ya jinai, hasa Sheria ya Kanuni za Makosa ya Jinai (*Criminal Procedure Code*).

(b) Ili kuupa nguvu Mkataba wa Kutowatesa Wafungwa na mahabusu, Serikali imeingiza masuala ya Haki za Bindamu katika Katiba ya Nchi.

(c) Elimu kuhusu haki za binadamu imekuwa inatolewa kwa Wananchi ili wawe na ufahamu wa kutosha kuhusu haki na wajibu wao kwa Serikali. Elimu hii pia imekuwa inatolewa kwa Watendaji wa Serikali, hasa walio katika vyombo vinavyosimamia utoaji haki kwa raia, vikiwemo Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza.

(d) Serikali kupitia Bunge hili, imeanzisha chombo kinachopokea na kuchunguza malalamiko ya Wananchi kuhusu vitendo vyenye kukiuka Haki za Binadamu, ikiwa ni pamoja na utesaji, yaani Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kutekeleza hatua hizi, tayari tumetimiza masharti yaliyowekwa na sasa tunayo sifa ya kuridhia mkataba huu. Hatua za maandalizi ya kuridhia mkataba huu zimeanza kuchukuliwa kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina swal moja la nyongeza. Pamoja na majibu yake yote hayo, ni lini Serikali itaridhia Mkataba huu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba, baada ya kuchukua hatua mbalimbali za kutekeleza matakwa ya Mkataba ule, sasa tayari hatua za maandalizi zimeanza kuchukuliwa na Wizara yangu tukishirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Nataka kuliahidi Bunge lako Tukufu kuwa, baada ya muda si mrefu pengine Bunge la mapema mwakani, Mkataba huu utafikishwa ndani ya Bunge hili ili tuweze kuuridhia.

Na. 285

### **Ujenzi wa Kituo cha Polisi Kibaigwa**

#### **MHE. JOB Y. NDUGAI aliuliza:-**

Kwa kuwa eneo la Kibaigwa Wilayani Kongwa linaandamwa sana na matukio mengi ya ujambazi katika miaka ya hivi karibuni; na kwa kuwa kutokana na hali hiyo Wananchi wa eneo hilo wamejitelea kujenga Kituo cha Polisi ambacho kinahitaji vifaa vya kumalizia ujenzi huo:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia ukamilishaji wa jengo hilo ikiwa ni pamoja na fedha za ujenzi wa nyumba wa Mkuu wa Kituo?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kumpatia gari jipya Kamanda wa Polisi wa Wilaya ya Kongwa ili aweze kupambana na ujambazi kwenye maeneo ya Kibaigwa?

#### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Viongozi na Wananchi wa Kibaigwa Wilayani Kongwa akiwemo Mbunge wao yaani Mheshimiwa Job Ndugai, kwa kuitikia wito unaotolewa na Serikali mara kwa mara kwa Wananchi kwa ujumla juu ya umuhimu wa Wananchi kujitolea kujenga Vituo vya Polisi katika maeneo yao. Kwa kuwaunga mkono Wananchi wa Kibaigwa katika ujenzi wa Kituo cha Polisi, Serikali imechangia Sh. 3,000,000/= na kazi ya ujenzi karibu inakamilika.

Aidha, Serikali inatambua umuhimu wa kumpatia Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Kongwa, gari jipya ili aweze kupambana na ujambazi kwenye maeneo ya Wilaya yake pamoja na maeneo ya Kibaigwa. Mpango wa kununua gari hilo utafanyika pamoja na Wilaya zingine ambazo hazina gari mpya kama ilivyofafanuliwa katika hotuba yetu ya bajeti ya mwaka 2004/2005. (*Makofi*)

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Kwa kuwa Wananchi wa Kibaigwa waliwahi kujenga Kituo cha Polisi siku za nyuma Wizara ikasema ni kidogo, wakajenga jengo lingine limekamilika miezi sita iliyoisha, *Counter* tayari, mahabusu ipo, *strong room* ipo, choo kipo na kila kitu kipo, lakini hakuna askari hadi leo. Je, Wizara itapeleka lini askari?

Pili, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameweka jiwe la msingi juzi kufungua Soko la Kimataifa la aina yake Kibaigwa na wafanyabiashara wa Kenya na nchi nyingine wanafanya biashara ya mamilioni pale. Hivi kweli ni sawa sawa kwamba, biashara kubwa kama ile inaweza kufanyika mahali ambapo hakuna Kituo cha Polisi na Wananchi wamejenga lakini kupeleka askari ni tatizo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Kibaigwa ni Mji unaokua haraka sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi aliweka jiwe la msingi la Soko la Kimataifa na pale sasa hivi iko Benki. Kwa mazingira yote haya tumezingatia na kama alivyojibu juzi hapa Waziri wakati wa Hotuba ya Bajeti kwamba, Kongwa tutapeleka Askari na kufungua kituo kile haraka iwezekanavyo na tunaomba lile jengo la zamani ambalo tulilikataa sasa tushirikiane Wananchi wa Kongwa na sisi Wizara ya Mambo ya Ndani, tulitengeneze iwe ni nyumba ya Mkuu wa Kituo ili tunapopeleka Askari basi nyumba ya kuanzia iwe ni lile jengo la zamani. Kwa hiyo, tuko pamoja na Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Kibaigwa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yote yamejibwa na muda wa maswali umekwisha. Matangazo ya vikao vya leo ni kwamba, kuna Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo Jumanne tarehe 20 Julai, 2004, kuanzia saa 7.00 mchana, chumba namba 231, ghorofa ya pili.

Mheshimiwa Eliachim Simpasa huyo huyo ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati nyingine ya Kilimo na Ardhi, anawaarifu Wajumbe wake kwamba, kulikuwa na msafara wa kuelekea kwenye Shughuli Maalum ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, sasa anawaarifu Wajumbe wake kwamba, msafara huo utaanza saa 5.30 asubuhi hii. Magari ya Bunge yatakuwepo kwenye lango kuu kwa ajili ya kuapeleka Waheshimiwa Wabunge huko wanakokwenda.

Mwenyekiti wa *APNAC Tanzania*, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, anawatangazia Wabunge ambao ni Wanachama wa *APNAC* kwamba, kutakuwa na kikao leo Jumanne tarehe 20 Julai, 2004, vile vile kuanzia saa 7.00 mchana katika chumba... hee, mbona ni chumba kile kile kinatakiwa na Kamati mbili! Namba 231 kimeshachukuliwa na Kamati ya Mheshimiwa Eliachim Simpasa. Kwa hiyo, *APNAC* mtapewa chumba kingine, lakini ni kuanzia saa 7.00 mchana.

Mwisho wa matangazo, tunaendelea na *Order Paper*. Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005 Wizara ya Viwanda na Biashara**

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya

Uwekezaji na Biashara, iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara, naomba sasa kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya Sekta za Viwanda na Biashara kwa kipindi cha 2003/2004, kwa kiasi kikubwa yametokana na hali ya amani na utulivu nchini. Ningependa kutumia fursa hii, kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa uongozi wake thabiti, unaojali shida za Wananchi na unaotilia maanani maslahi ya Taifa. Uhodari wake unathibitishwa na kukubalika kwake katika medani ya Kimataifa alipoombwa na akakubali kuwa Mwenyekiti Mwenza kwenye Tume ya Kimataifa ya Athari za Kijamii za Utandawazi. Taarifa ya Tume hii imeshatolewa na ni rejea muhimu, hasa kwa Viongozi wa Kisiasa (Mawaziri na Wabunge) na Watendaji Serikalini, katika Asasi na Taasisi za Umma, Asasi Zisizo za Kiserikali na Wanataluma wa Vyuo vya Elimu ya Juu. (*Makofi*)

Wizara yangu inawasiliana na Ofisi Binafsi ya Rais, *ESRF* na Kitivo cha Biashara na Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kuona jinsi ya kuongeza uelewa wa yale yote yaliyomo kwenye Taarifa ya Tume ya Kimataifa ya Utandawazi, ambayo Rais wetu ni mmoja wa waandishi wake wakuu. Aidha, umahiri wake umedhihirishwa hivi karibuni alipoombwa kuwa Mjumbe wa Tume ya Afrika iliyoundwa na Waziri Mkuu wa Uingereza. Nampongeza pia Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhud zake na ustadi wake mkubwa anaouonyesha katika kumsaidia Rais katika majukumu mbalimbali ya Kitaifa. (*Makofi*)

Aidha, napenda nimshukuru Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Frederick T. Sumaye, Mbunge wa Hanang, kwa hotuba yake ambayo inajumuisha maelezo fasaha ya utekelezaji wa malengo ya Serikali na usafanuzi wa kina wa mwelekeo wa utendaji wa Sekta mbalimbali, ikiwemo Sekta za Viwanda na Biashara. Namshukuru pia Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda, Mbunge wa Handeni, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Mbunge wa Rombo, Waziri wa Fedha, ambao hotuba zao zimefafanua mwelekeo wa uchumi wetu na malengo ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005. Vile vile, nawashukuru Mawaziri wenzangu wote walionitangulia katika kuwasilisha hapa Bungeni Bajeti za Wizara zao. Hotuba zao zimetuonyesha umakini wa ushirikishwaji katika utendaji, kila Sekta kwa nafasi yake, kwa lengo la kuinua uchumi wa Taifa letu na kupunguza umaskini. (*Makofi*)

Napenda kutumia fursa hii pia kuwashukuru wote ambao michango yao imesaidia sana katika kuandaa Bajeti ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara yangu. Kwa namna ya pekee, naishukuru Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, chini ya uongozi hodari wa Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, kwa michango na nasaha zao nzuri wakati wa kujadili Makadirio ya Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tangu Bunge la Bajeti la mwaka 2003, kumekuwepo na matukio kadhaa yanayoigusa jamii kwa ujumla. Kwanza, mwezi Februari, 2004, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere aliteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge. Pili, tarehe 6 Februari, 2004, ulifanyika uchaguzi wa Wajumbe wa Bunge la Afrika, Wajumbe walioshinda ni Mheshimiwa Balozi Getrude Mongela, Mbunge wa Ukerewe, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mbunge wa Dimani, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Dr. William Shija, Mbunge wa Sengerema na Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini. (*Makofi*)

Tatu, tarehe 19 Februari, 2004, ulifanyika uchaguzi wa Wajumbe wa *SADC Parliamentary Forum*. Katika uchaguzi huo, Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum, alichaguliwa kuliwakilisha Bunge kwenye *Forum* hiyo. Nne, Mheshimiwa Danhi Makanga, alishinda katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Bariadi. Wote hawa nawapongeza sana kwa mafanikio yao. Napenda kuchukua nafasi ya pekee kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Balozi Getrude Mongela kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Afrika. (*Makofi*)

Katika kipindi hiki pia tulipata tukio la kusikitisha pale Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, Mbunge wa Mbeya Vijijini, alipofariki dunia tarehe 24 Juni, 2004. Mwenyezi Mungu, aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amina*.

Mheshimiwa Spika, matukio mengine muhimu yalikuwa, kwanza, kufanyika kwa Mkutano wa Wakuu wa Nchi za *SADC*, ambao ulifanyika Dar es Salaam tarehe 23 - 25 Agosti, 2003. Mkutano huo ulikuwa muhimu katika uendelezaji wa ushirikiano wa kiuchumi na kibiashara mionganoni mwa nchi wanachama. Pili, mwezi Februari, 2004, nchi yetu ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Mawaziri wa Biashara wa *SADC*. Tatu, mnamo Machi, 2004, nchi yetu iliteuliwa kuwa Mratibu wa Nchi Maskini (*Least Developed Countries - LDCs*) katika majadiliano ya kibiashara ya Shirika la Biashara Duniani (*WTO*) na hivyo kuwa Mwenyezekiti Mwenza katika Mkutano wa Tatoo wa Mawaziri wa Biashara wa *LDCs* uliofanyika Dakar, Senegal, tarehe 4 - 5 Mei, 2004, ambao ulitoa Tamko la Dakar kuhusu msimamo wa nchi hizi katika majadiliano ya biashara, maarufu kwa jina la *Agenda* ya Doha ya Maendeleo. Nne, Mkutano huu ulifuatiwa na ule wa Mawaziri wa Biashara wa nchi za Umoja wa Afrika kule Kigali tarehe 27 - 28 Mei, 2004. Mkutano huu ulitoa Tamko la Makubaliano ya Kigali.

Tano, kulikuwa na Mkutano wa Kumi na Moja wa *UNCTAD (UNCTAD XI)*, uliofanyika Sao Paulo tarehe 13 - 18 Juni, 2004. Mkutano huo umesisitiza umuhimu wa *UNCTAD* kuendelea na majukumu ya kuainisha masuala ya biashara na maendeleo kwa pamoja na kuendeleza utafiti katika masuala haya. Aidha, kuendelea kutoa misaada na ushauri wa kiufundi kwa nchi zinazoendelea, hasa zile maskini. Mkutano huu ultanguliwa na mkutano wa Nchi za Kundi la 77 na China tarehe 11 - 12 Juni, 2004 ambao ulikuwa unaadhimisha miaka 40 tangu huo uanzishwe.

Katika mkutano huo, kulitolewa Tamko la G77 ambalo lilikumbusha umuhimu wa kuzingatia kwa bidii zaidi misingi ya umoja na mshikamano wa kundi hili hasa katika nyanja za majadiliano ya sasa ya biashara ambayo bado hayaendeshwi kwa usawa,

ikizingatiwa kwamba sasa umefika wakati mwafaka wa kupanua na kuongeza biashara mionganoni mwa nchi za Kusini. Mkutano huu ukafuatiwa na ule wa nchi 43 za *Global System of Trade Preferences - GSTP*, ambazo ni kati ya zile za G77 na China zikiwemo China yenyewe, India, Brazil na Tanzania. *GSTP* inalenga katika kuanzisha Eneo la Biashara Huru (*Free Trade Area*) kama mkakati wa kuimarisha biashara na shughuli za kiuchumi mionganoni mwa Nchi za Kusini (*South - South Trade*).

Mheshimiwa Spika, sita ni Mkutano wa Baraza la Utawala (*Governing Council*) la Mfuko wa Pamoja wa Kimataifa wa Mazao (*Common Fund for Commodities - CFC*), ambao ulifanyika tarehe 28 - 29 Juni, 2004. Mkutano huo ulikuwa maalum wa kumchagua Mkurugenzi Mwendeshaji wa *CFC*. Napenda kulialifu rasmi Bunge lako Tukufu kwamba, Balozi Ali Said Mchumo, Naibu Katibu Mkuu (Fedha na Utawala wa Jumuiya ya Afrika Mashariki), alichaguliwa kwa kuwashinda wagombea wenzake kutoka Algeria, Urusi na Sweden na hivyo kuipa Afrika na Tanzania heshima ya kuwa Mwfrika wa kwanza kuongoza Shirika hili la Kimataifa chini ya *UNCTAD* linaloshughulikia mazao ya kilimo. Hatua hii ni mwafaka kabisa kwani mazao ya kilimo ni tegemeo kubwa la nchi zinazoendelea, hususan zile masikini zikiwemo zile za Kusini mwa Jangwa la Sahara. Napenda kumpongeza Balozi Mchumo kutoka kwenye sakafu ya moyo wangu kwa ushindi huu ambao umeliletea Taifa letu heshima kubwa. (*Makofii/Kicheko*)

Aidha, nampongeza na kumshukuru Rais Benjamin Mkapa, kwa kuongoza kampeni kubwa ya Balozi Mchumo pamoja na kuwaandikia Viongozi wenzake kadhaa akiwaomba wamuunge mkono mgombea wetu na hivyo kuliwezesha Taifa letu kupata heshima hii. Pia, nawapongeza Maofisa wote walioshiriki katika kampeni hii kule Amsterdam wakiongozwa na Balozi Charles Mutalemwa, Mwakilishi wetu wa Kudumu kule Geneva, Bibi Radhia Msuya wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bi Nyang'anya Hyera na Bwana Zoka kutoka Ubalozi wetu wa Brussels, Ubelgiji.

Napenda pia kumshukuru Mbunge mwenzangu, Mheshimiwa Fatma Said Ali Mchumo, ambaye alishiriki kikamilifu katika kampeni kule Amsterdam akimtia moyo wa kuhimili mpambano Balozi Ali Mchumo na mimi mwenyewe kama Kiongozi wa Ujumbe wa Tanzania katika mkutano huo wa uchaguzi. (*Makofii*)

Mwisho, naishukuru Serikali kwa kunipa fursa ya kuongoza Ujumbe wa Nchi yetu kwenye Mkutano ule. Ushindi wa Balozi Mchumo na kuteuliwa nchi yetu kuwa Mratibu wa *LDCs* katika majadiliano ya *WTO* mara mbili katika muda wa miaka mitatu, kwa tofauti ya miezi minane tu, ni ushahidi tosha unaoonyesha jinsi nchi yetu inavyoheshimiwa Kikanda na Kimataifa chini ya uongozi thabiti wa Rais Mkapa ulivyojikita katika fikra sahihi za Baba wa Taifa letu, Hayati Mwalimu Nyerere. Pengine hapana haja kutaja tena hapa kuwa Rais Mkapa alikuwa Mwenyekiti Mwenza wa Tume ya Kimataifa ya Athari za Kijamii za Utandawazi na sasa ni Mjumbe katika Tume ya Afrika inayoongozwa na Waziri Mkuu wa Uingereza. Fursa hizi za heshima kwa Tanzania katika nyanja za Kimataifa zinatokana na sera nzuri za Chama cha Mapinduzi

na Serikali yake chini ya Rais Mkapa. Ni muhimu kwa Tanzania kutambua hivyo na kujizatiti kuendelea na uzi ule ule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, malengo ya Sekta ya Viwanda katika kipindi cha 2003/2004 yalikuwa ni pamoja na kuandaa mikakati ya kuongeza ufanisi wa Sekta, kuhamasisha uwekezaji ndani ya maeneo ya EPZ, kukamilisha uandaaji wa programu zitokanazo na Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo na uandaaji wa takwimu kuhusu maendeleo ya Sekta ya Viwanda.

Mheshimiwa Spika, utendaji katika Sekta ya Viwanda ulizingatia malengo yaliyokusudiwa. Mikakati na programu mbalimbali zilibuniwa ili kusaidia kusukuma maendeleo ya viwanda. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (*UNIDO*), iliweza kukamilisha uandaaji wa Mpango wa Awamu ya Pili wa Maendeleo ya Viwanda (*Integrated Industrial Development Programme Phase II*). Mpango huu utahusika pamoja na mambo mengine na masuala ya upotevu wa mazao ya kilimo baada ya mavuno (*Post Harvest Losses*) na kuweka mikakati ya kupunguza tatizo hilo ikiwa ni pamoja na kuhamasisha na kuhimiza uanzishaji wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo (*Agro-processing Industries*). Kamati imeundwa ya kusimamia utekelezaji wa mpango huu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mkakati wa kuendeleza Sekta ya Ngozi na Viwanda vya Ngozi unaendelea. Utaratibu wa kusimamia Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Ngozi (*Livestock and Leather Development Fund*) tayari umebainishwa. Azimio la Bunge la uanzishaji wa mfuko huo limekwishaandaliwa na linatarajiwu kufikishwa katika Bunge lako Tukufu ili kutamka rasmi kuundwa kwa mfuko huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatua zilichukuliwa kuhamasisha uwekezaji katika maeneo ya EPZ ambapo hadi sasa viwanda vinne vimeanzishwa kwa ajili ya kutengeneza bidhaa za kuuza nje. Viwanda hivyo ni pamoja na *Nida Textiles, Star Apparel (T) Ltd., Reclaimed Appliances (T) Ltd* na *Africa Pride Textile Mills*. Kuhusu utekelezaji wa Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo, programu nne zimeandaliwa na kuwasilishwa katika warsha iliyojumuisha wadau wote. Programu hizo zinahusu kutenga maeneo maalum ya kufanya kazi, kuendeleza ujasiriamali, kuimarisha huduma za kuendeleza biashara (*Business Development Services*) na programu ya kuimarisha upatikanaji wa mitaji. Mazungumzo yanaendelea na wahisani kuhusu utekelezaji wa programu hizo. Vile vile, ziara viwandani katika Mikoa ya Arusha, Tanga na Dar es Salaam zilifanywa na Viongozi wa Wizara kwa lengo la kuona maendeleo ya viwanda, kuhimiza uzalishaji wa bidhaa bora na kujadili pamoja na Menejimenti husika changamoto zinazokabili maendeleo ya viwanda na mikakati ya kuendeleza viwanda.

Mheshimiwa Spika, ziara katika nchi mbalimbali pia zilifanywa kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kukutana na wawekezaji ili kuwashawishi kuwekeza katika viwanda hapa nchini. Wizara pia ilishiriki katika mikutano mbalimbali ya nje na ya ndani iliyojadili matatizo na maendeleo ya viwanda kwa lengo hilo hilo. Majadiliano na mashauriano kati ya Wizara na Shirikisho la wenye Viwanda (*Confederation of Tanzania Industries - CTI*) na wadau wengine yamefanyika mara kwa mara kwa lengo la kutafuta

mbinu za kuleta maendeleo ya viwanda. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara nyingine, Wizara iliendelea kuweka mazingira mazuri ya uzalishaji ikiwa ni pamoja na kushiriki katika kuweka mfumo wa kodi unaohamasisha maendeleo ya viwanda. Vile vile, viwanda viliendelea kupatiwa mafunzo na ushauri kuhusu njia bora za uzalishaji usiokuwa na athari kwa mazingira (*Cleaner Production*) yanayotolewa na Kituo cha Uzalishaji Bora na Hifadhi ya Mazingira (*Cleaner Production Centre*), ambacho sasa kiko katika Ofisi ya Makamu wa Rais na kina jukumu la kuhamasisha na kuhimiza viwanda kuzingatia mbinu ambazo uzalishaji hauharibu mazingira.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Mei, 2003, Wizara yangu ilitoa agizo la kusimamisha kwa muda wa miaka miwili uuzaaji baadhi ya aina za chuma chakavu nje ya nchi. Kutohana na hatua hii viwanda vyetu vya kuyeyusha chuma chakavu vimeimarika na kuongeza uzalishaji. Hali hii imesababisha mahitaji ya chuma chakavu kuongezeka. Sambamba na ongezeko la matumizi ya chuma chakavu nchini, mahitaji ya chuma hicho yameongezeka pia katika soko la dunia. Pamoja na hatua ya kuzuia uuzaaji nje wa chuma aina ya *iron, steel, alluminium* na *brass*, yamekuwepo malalamiko kutoka kwa wenyewe viwanda kuhusu vyuma vilivyoziwa kuendelea kuuzwa nje kinyume na maagizo ya Serikali. Aidha, yamekuwepo matukio ya kuiba vifaa mbalimbali kama vile mataruma ya reli, mifuniko ya maji machafu, nyaya za simu na kadhalika na kuviuza nje kama chuma chakavu kinyume cha sheria.

Wizara imechukua hatua zaidi za udhibiti ikiwa ni pamoja na kusisitiza kwa Mamlaka ya Mapato (*TRA*) kutoruhusu upitishaji wa aina yoyote ya chuma bila hati iliyosainiwa kwa pamoja na Kamati ya Chuma Chakavu, *CTI* na angalau saini mbili za wenyewe viwanda vinavyoyeyusha chuma. Iwapo amri ya Serikali itaendelea kupuuzwa, Wizara haitasita kupiga marufuku aina zote za chuma chakavu kuuzwa nje ya nchi yetu.

Ningependa kusisitiza kwamba, pamoja na kukuza ajira na mapato, uyeyushaji wa chuma chakavu nchini ni muhimu katika maendeleo ya viwanda kwa sababu ndiyo nguzo ya kuanzisha viwanda vya msingi. Katika kipindi hiki cha mpito cha miaka miwili, Serikali itafanya tathmini ya kina kuhusu kiwango cha uongezekaji wa chuma chakavu, kiasi kilichopo, mahitaji ya ndani kwa sasa na baadaye na takwimu za mauzo nje. Tathmini hii itatuwezesha kuandaa utaratibu wa kudumu kuhusu matumizi ya chuma chakavu hapa nchini. Katika kipindi cha mwaka 2003, Wizara ilifanya uchunguzi wa awali kuhusu upatikanaji na matumizi ya chuma chakavu. Uchunguzi huo umebainisha matatizo yanayogusa biashara ya chuma chakavu na kwamba yale yaliyo ndani ya uwezo wa wadau yameanza kushughulikiwa. Wizara imetafuta mtaalamu nje ya Wizara atakayefanya utafiti wa kina ambaye baadaye atatoa mapendekezo Serikalini jinsi ya kuimarishe matumizi na kuboresha biashara ya chuma chakavu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia inatarajia kufanya utafiti wa kina ili kubaini matatizo yanayokabili bidhaa za mkonge hususan magunia ya katani, lengo ni kuyapatia ufumbuzi ili kufufua viwanda na kuimarishe soko la magunia ya katani nchini ili viwanda husika viweze kutumia uwezo uliopo na kuangalia uwezekano wa kuzalisha bidhaa nyingine za mkonge. Hii inatokana na taarifa za awali za wataalamu wa Wizara kuwa mahitaji ya bidhaa za mkonge katika soko la dunia hivi karibuni yanapanda kwa kasi na

kwa kiwango kikubwa kinyume na hali halisi ilivyo hapa Tanzania, ambapo mazao ya mkonge hayana soko. Uchunguzi wa awali pia umebainisha kuwa matatizo makubwa ni pamoja na uhaba wa mkonge unaofaa kusokotea nyuzi za magunia na uchakavu wa mitambo na mashine katika viwanda. Wizara itaendelea na utafiti huo kwa kuajiri mtaalamu wa kufanya utafiti wa kina na kutoa mapendekezo ya jinsi ya kukabiliana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua zote zilizoelezwa hapo juu, pamoja na utulivu wa mfumo wa sera zetu za uchumi mpana ikiwa ni pamoja na udhibiti wa mfumuko wa bei, tumeshuhudia kuwepo kwa maendeleo mazuri na ya kuridhisha ya ukuaji wa Sekta ya Viwanda. Ukuaji huu umechangiwa pia na sera yetu ya ubinafsishaji ambapo viwanda vingi vimepata wawekezaji wapya wenyewe uwezo na uzoefu wa kuendesha viwanda. Aidha, sera zetu za uwekezaji zimehamasisha pia uanzishaji wa viwanda vipyta kadhaa hasa katika Sekta ya usindikaji wa mbegu za mafuta ya kula, utengenezaji wa nguo, usindikaji wa matunda na bidhaa nyingine za kilimo, usagishaji wa nafaka, bidhaa za ujenzi, kemikali, vinywaji, sabuni, madawa ya binadamu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ongezeko hili linadhihirishwa na takwimu za uzalishaji ambapo kwa mfano, utengenezaji wa nguo uliongezeka kutoka mita mraba 106.3 milioni mwaka 2002 hadi mita mraba 107.4 milioni mwaka 2003, utengenezaji wa kamba za katani kutoka tani 5,901 mwaka 2002 hadi tani 6,839 mwaka 2003, usagishaji wa ngano kutoka tani 219,118 mwaka 2002 hadi tani 355,616 mwaka 2003, uzalishaji wa biskuti na tambi kutoka tani 2,284 mwaka 2002 hadi tani 5,906 mwaka 2003, uzalishaji wa chuma kutoka tani 25,418 mwaka 2002 hadi 31,018 mwaka 2003, mabati tani 31,742 mwaka 2002 hadi tani 41,725 mwaka 2003, utengenezaji wa rangi kutoka lita 13,564,000 mwaka 2002 hadi lita 16,842,000 mwaka 2003, sigara 3,778 milioni mwaka 2002 hadi 3,920 milioni mwaka 2003 na bia kutoka lita 175,870,000 mwaka 2002 hadi lita 194,100,000 mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, kuimarika kwa viwanda na ongezeko la uzalishaji wa bidhaa kumechangia ukuaji wa Sekta kuwa asilimia 8.6 mwaka 2003 ikilinganishwa na asilimia nane mwaka 2002. Mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.7 mwaka 2003 ikilinganishwa na asilimia 8.4 mwaka 2002. Kumekuwepo pia na ongezeko la ajira kutoka watu 180,023 mwaka 2002 hadi 207,571 mwaka 2003, ikiwa ni ongezeko la asilimia 15.2. Mauzo ya bidhaa za viwanda nje ya nchi yameongezeka kutoka Dola za Kimarekani 65.9 milioni mwaka 2002 hadi Dola za Kimarekani 99.9 milioni mwaka 2003. Uwekezaji kwenye miradi ya viwanda umeongezeka kutoka Shilingi 195.072 bilioni mwaka 2002 hadi Shilingi 239.622 bilioni mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya, Sekta ya Viwanda iliendelea kukabiliwa na changamoto hasa kuhusiana na gharama kubwa za uzalishaji wakati huu ambao pia unashuhudia ushindani mkubwa katika soko la nje na hata soko la ndani. Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kutafuta ufumbuzi wa matatizo haya ili kuwezesha viwanda vyetu kuzalisha kwa ufanisi mkubwa zaidi na hivyo kuhimili ushindani. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na uimarishaji wa miundombinu hasa barabara, mawasiliano

(simu, barua pepe na tovuti), urekebishaji wa mfumo wa kodi na ukaguzi wa ubora wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje. Aidha, baadhi ya wenyewe viwanda wamejitalidi kuwekeza katika teknolojia mpya ya kisasa ili kuongeza na kuzalisha bidhaa zenyenye ubora wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara itaendelea kutekeleza programu mbalimbali na kubuni mikakati zaidi ya kuimarisha Sekta ya Viwanda ili iweze kuchangia kwa kiwango kikubwa zaidi katika uchumi wa Taifa letu. Kipaumbele kitatolewa katika kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika Sekta za kipaumbele, yaani Sekta za Nguo, ngozi na usindikaji wa mazao ya kilimo na chakula. Katika kufikia azma hii, Wizara ina mipango mahsusini itakayohusu kuimarisha Sekta ya Ngozi, Sekta ya Usindikaji wa Vyakula, kuanzisha *database* ya takwimu za Sekta, kuboresha hali ya viwanda vya katani na biashara ya vyuma chakavu. Aidha, tutarekebisha sheria za Asasi zilizo chini ya Wizara ili kuzipa majukumu mapya yanayokidhi mahitaji halisi ya maendeleo ya uchumi wa soko na kuhamasisha uwekezaji katika Kanda za Maendeleo (*Development Corridors*).

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi mbalimbali kuboresha zaidi mazingira ya uzalishaji viwandani ikiwa ni pamoja na miundombinu, sera za fedha na kodi na kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya Sekta ya Viwanda vidogo. Lengo la hatua zote hizo ni kuhamasisha ufufuaji wa viwanda vingi zaidi, kukuza uwekezaji, kuongeza uzalishaji na tija ili kuifanya Sekta hii iweze kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya uchumi wa nchi yetu. Kwa hali hii, inakadiriwa kuwa ukuaji wa Sekta ya Viwanda utafikia asilimia 9.3 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, shughuli za Sekta ya Biashara zimebadilika sana siku za karibuni kutokana na mifumo na maingiliano mbalimbali ya kiuchumi ikiwemo biashara inayosababishwa na utandawazi. Kwa hiyo, ningependa sasa kuzungumzia kwa kifupi changamoto itokanayo na dunia ya leo ya utandawazi. Utandawazi ni matokeo ya mabadiliko ya kasi katika teknolojia, upashanaji habari na mawasiliano miongoni mwa jamii ya Kimataifa. Aidha, utandawazi unatokana na mfumo wa biashara ya dunia ambao umeleta ushindani mkubwa wa kibashara ndani ya nchi na baina ya nchi. Wakati mfumo wa zamani ulikuwa ni wa soko kutafuta bidhaa (*Sellers' Market*), mfumo wa sasa ni bidhaa kutafuta soko (*Buyers' Market*). Bidhaa sasa zinazalishwa kulingana na matakwa ya soko.

Utafiti wa soko unatangulia utafiti wa uzalishaji. Ni dhahiri utandawazi unatoa fursa kwa nchi kukuza biashara na uchumi wake kutokana na soko la Kimataifa kuwa wazi zaidi. Lakini ni dhahiri pia kuwa utandawazi una athari kubwa kwa nchi changa na hasa zenyenye teknolojia duni na ambazo sehemu kubwa ya biashara yake inategemea mazao ghafi ya kilimo. Utandawazi unazisukuma nchi hizi pembezoni mwa uchumi wa Kimataifa (*Economic Marginalisation*). Pamoja na ukweli huu, Tanzania au nchi nyingine yoyote ile, haiwezi kujijengua na kujijengea ukuta dhidi ya utandawazi. Ni lazima, kama Taifa, tujizatiti kushindana katika soko la Kimataifa tukitambua kuwa hata soko letu la ndani ni sehemu ya soko la Kimataifa kutokana na ukweli kwamba bidhaa

zinazozalishwa hapa nchini kwa soko la ndani zinashindanishwa pia na bidhaa za kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, tutaweza kuhimili changamoto itokanayo na utandawazi kwa kufanya mambo matatu ya msingi. Kwanza, ni kuendeleza sera zetu za jumla za uchumi zinazohamasisha uwekezaji. Pili, ni kuimarisha taratibu za ushirikiano wa karibu kati ya Serikali na Sekta Binafsi (*Public-Private Sector Smart Partnership*), ambapo misingi yake tayari tumeiweka. Taratibu hizi zinaiwezesha Serikali na Sekta binafsi kubaini vikwazo vyta kisera na kiutendaji vinavyoweza kudumaza maendeleo ya uchumi wa Taifa na kuafikiana njia sahihi za kuchukua. Tatu, ni kwa Sekta binafsi yenyewe kutumia fursa zitokanazo na sera na vivutio mbalimbali vinavyotolewa na Serikali kuzalisha bidhaa bora na kwa bei za ushindani.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Sekta ya Biashara ilikuwa na malengo yafuatayo: Kutekeleza Sera ya Biashara, uandaaji na utekelezaji wa Mikataba ya Biashara ya Kimataifa na ushirikiano na nchi mbalimbali, usimamiaji wa Sheria za Wakala, urekebishaji wa Sheria ya Leseni za Biashara, utekelezaji wa Sheria ya Wakala wa Meli na maandalizi ya Sheria ya *Anti-Dumping*.

Mheshimiwa Spika, utendaji katika Sekta ya Biashara ulizingatia malengo yaliyokusudiwa kufanywa katika kipindi cha mwaka 2003/2004, kama yalivyoanishwa hapo juu. Lengo kuu na mahsusililikuwa ni kuanza utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Biashara. Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba katika hotuba yangu ya mwaka jana, niliwa fahamisha kwamba Sera ya Taifa ya Biashara ilikuwa tayari kwa uzinduzi. Sera hii imeishazinduliwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali. Utekelezaji wake umeanza kwa warsha za wadau za kuandaa mikakati ya kufanikisha malengo ya Sera hii.

Sera hii, mbali na kuwa na lengo la kujenga uwezo wa ushindani katika biashara, inabainisha nyenzo kuu za kukuza biashara kwa kuzingatia misingi ya uendelezaji tija na ushindani katika Sekta za uzalishaji mali na utoaji huduma. Nyenzo hizo ni pamoja na mfumo wa kodi unaohamasisha biashara, taratibu za kuondoa vikwazo vyta biashara, ujenzi wa mila na desturi ya kuthamini viwango vyta ubora katika mfumo wa uzalishaji na kuwa na vivutio maalum katika kuendeleza biashara. Aidha, nyenzo nyingine ni uandaaji na uwekaji wa mikakati ya makusudi ya kulinda viwanda vyta ndani ambayo haipingani na mikataba, masharti na taratibu za *WTO*.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekuwa ikishiriki katika majadiliano na nchi tulizoingia nazo mikataba ya biashara kwa lengo la kuangalia namna ya kurekebisha mikataba hiyo kwa kuzingatia maslahi ya Taifa na mwelekeo wa dunia wa biashara na maendeleo. Mikataba ya biashara kati ya nchi na nchi ni mbinu madhubuti ya kupanua na kukuza uwekezaji na biashara. Wizara imeweka mikakati ya kuendeleza biashara baina ya Tanzania na nchi za nje (*Bilateral Trade Arrangements*). Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara imekuwa ikishirikisha wadau katika majadiliano ya mikataba na nchi za nje ili kupata ushauri na mawazo mbalimbali. Kwa lengo hili, Wizara itaendelea kuandaa na kuingia katika mikataba mipyta ya biashara na nchi za Afrika, Asia, Mashariki

ya Kati, Marekani na Ulaya. Wakati huo huo itachukua hatua za kuimarisha ile iliyopo, lengo likiwa ni kukuza biashara yenye uwiano mzuri baina ya Tanzania na nchi husika. Biashara ya aina hii itatusaidia kuinua kiwango cha ukuaji wa uchumi na hatimaye kupunguza umasikini. Katika kuhakikisha lengo hilo linafanikiwa, Sekta zote za kiuchumi hazina budi kuzingatia na kutilia mkazo suala la kukuza na kuongeza uzalishaji, kupanua biashara na kuingia katika masoko mapya ili kukidhi malengo yanayobainishwa katika mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara na Serikali kwa ujumla imefanya kila jitihada kupata wawekezaji ambao wanafufua na kupanua viwanda vya nguo na viwanda vingine nchini ili viweze kutumia fursa zilizopo kutokana na mikataba ya *AGOA*, *EBA*, *Canadian Initiative* na ule wa *GSP* wa Japan na masoko mengine ya upendeleo (*Preferential Markets*) nje ya nchi. Ubora wa viwango vya bidhaa za nguo kutoka viwandani umeongezeka kukidhi matakwa na mahitaji ya masoko ya nje tofauti na miaka iliyopita. Pia, Wizara imechukua hatua za kuelimisha jamii ya Watanzania ili kuitumia ipasavyo fursa ya soko linalotokana na *AGOA*. Kwa mfano, fursa hii imeiwezesha Tanzania kuongeza mauzo nchi za nje. Katika mwaka 2003, thamani ya bidhaa tulizouza katika soko la Marekani ilikuwa Dola za Marekani 24,234,000, kati ya hizo tuliiza nguo na bidhaa zingine zenye thamani ya Dola za Kimarekani 1,110,000 chini ya Mkataba wa *AGOA* ikilinganishwa na Dola za Marekani 638,000 mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, majadiliano kuhusu Itifaki ya Mkataba wa kuanzisha Umoja wa Forodha baina ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (*Customs Union Protocol - EAC*) yamekamilika. Itifaki ya Mkataba huo imetiwa saini na Wakuu wa Nchi za Afrika Mashariki tarehe 2 Machi, 2004 huko Arusha. Serikali za Nchi Wanachama wa Jumuiya hii ikiwemo Tanzania zinakamilisha maandalizi pamoja na kupata ridhaa za mamlaka zinazohusika na zinajiaandaa kutangaza hivi karibuni kuanza rasmi kwa utekelezaji wa Itifaki ya Mkataba huo hapo ifikapo tarehe 1 Januari, 2005.

Kufuatana na Itifaki ya Mkataba huo, uanzishwaji wa Umoja wa Forodha katika nchi za Afrika ya Mashariki umejumuisha ulegezaji wa masharti ya biashara kwa kuondosha au kupunguza vikwazo vyote vya biashara ikiwa ni pamoja na ushuru wa forodha na vikwazo visivyo vya kiushuru (*tariff and non-tariff barriers*). Kuhusu ushuru wa forodha, makubaliano ni kwamba, kuanzia tarehe 1 Januari, 2005, Tanzania na Uganda watauza bidhaa zao katika nchi ya Kenya bila ushuru. Kwa upande wake, Kenya itauza bidhaa zake Tanzania na Uganda kwa kutozwa ushuru wa forodha utakaokuwa unapungua mwaka hadi mwaka kwa muda wa miaka mitano. Mwaka wa sita ushuru huo utamalizika hivyo biashara ya bidhaa kutoka nchi zote wanachama itafanyika bila kutozana ushuru wa forodha.

Pamoja na ulegezaji wa masharti ya biashara, nchi wanachama zimekubaliana kuweka wigo wa pamoja wa ushuru wa forodha (*Common External Tariff*), kwa bidhaa zinazotoka nje ya Jumuiya. Wigo huo utaruhusu malighafi na vifaa vya uwekezaji (*Raw Materials and Capital Goods*) kuingia bure (0%), bidhaa zilizosindikwa kidogo (*Intermediate Goods*) kutozwa asilimia 10 na bidhaa za watumiaji ambazo ni tayari kwa matumizi yaani zilizokamilika kutengenezwa (*Consumer Goods*) zitatozwa asilimia 25.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa mara nyingine, kutoa rai kuwa, kipindi hiki, ambacho Serikali za nchi wanachama zinajiandaa kutangaza tarehe ya kuanza utekelezaji wa Itifaki ya Mkataba huu, kiwe ni kipindi cha changamoto kwa Jumuiya ya wenge viwanda, wafanyabiashara na Watanzania wote kwa ujumla kuijandaa kutumia kikamilifu fursa inayotolewa na Itifaki hii kwa kutafuta masoko katika nchi za Afrika Mashariki. Lengo liwe ni kuuza bidhaa nyingi, bora na za aina mbalimbali zinazotengenezwa viwandani, mazao ya mashambani, ufügaji, uvuvi, misitu na kadhalika ili ifikapo tarehe 1 Januari, 2005 wawe tayari wanayo masoko kwa bidhaa zao na wawze mara moja kuanza kuuza. Wafanyabiashara wetu wasisubiri tangazo la Serikali la kuanza rasmi utekelezaji wa Itifaki hiyo ndipo waanze kutafuta soko. Watakuwa wamechelewa. Bila wafanyabiashara wetu kuitikia wito huu, Tanzania itaendelea kuwa soko la bidhaa za wengine bila bidhaa zetu nazo kupanya katika masoko hayo na hivyo kushindwa kunufaika na Jumuiya.

Mheshimiwa Spika, Umoja wa Nchi za Ulaya (*EU*) na kundi la Nchi za Afrika, Caribbean na Pacific (*ACP*) zilikamilisha awamu ya kwanza ya majadiliano mwezi Septemba 2003, ambayo kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya mwaka 2003/2004, yalikuwa yameandaliwa kwa lengo la kuanzisha muundo mpya wa Ushirikiano wa Kiuchumi baina ya pande hizo mbili (*Economic Partnership Agreement - EPA*), ambao utazingatia sheria, misingi na taratibu za kibiashara za Shirika la Biashara la Dunia (*Compatible to World Trade Organization rules, Procedures and Trading Arrangements*).

Awamu ya kwanza ya majadiliano yalikuwa ni kati ya kundi zima la nchi za *ACP* na *EU* kuhusu masuala mtambuka (*cross cutting issues*). Awamu ya pili ambayo itakuwa ya majadiliano kati ya nchi moja moja ya *ACP* au kikundi cha kikanda cha *ACP* na *EU* yako katika hatua za maandalizi baada ya kuzinduliwa mwezi Septemba, 2003. Katika awamu hii ya pili, nchi za *ACP* zimejiunga katika makundi ya kikanda zilizoyachagua kwa kuzingatia vigezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na maslahi ya nchi husika kwa ajili ya kuanza majadiliano na *EU*. Tanzania kwa upande wake imechagua kujadiliana na *EU* chini ya kundi la *SADC-EPA* ambalo ni la nchi saba. Nchi hizo ni Angola, Botswana, Lesotho, Mozambique, Namibia na Swaziland. Maandalizi kwa ajili ya uzinduzi wa majadiliano ya *SADC-EPA* na *EU* yanaendelea na yanatarajiwu kuzinduliwa rasmi mwezi Julai, 2004. Awamu hii ya majadiliano ya *EPA* imepangwa kumalizika mwezi Desemba, 2007 ili mikataba ya *EPA* na vikundi mbalimbali vya *ACP* na *EU* kuanza kutekelezwa mwezi Januari, 2008.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imepangiwa jukumu la kuwa mratibu (*Coordinator*) wa kikundi chake katika majadiliano na *EU* katika maeneo ya biashara ya huduma (*Trade in Services*) na sera za uwekezaji na ushindani (*Investment and Competition Policies*). Kamati ya Mawaziri wa Biashara wa *SADC-EPA* (*SADC Committee of Ministers of Trade-CMT*), ndiyo itakayosimamia na kuongoza majadiliano hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza maaazimio ya Mkutano wa Nne wa Mawaziri wa Biashara wa Nchi Wanachama wa *WTO* uliofanyika Doha, Qatar, Novemba, 2001, Tanzania iliendelea kushirikiana na nchi nyingine zinazoendelea ili kuweza kuwa na msimamo wa pamoja utakaoziwezesha kupata manufaa, hasa katika mambo muhimu yaliyokubaliwa kushughulikiwa katika majadiliano ya Shirika la Biashara Duniani (*WTO*). Mambo hayo yanajumuisha makubaliano ya kupunguza ushuru, kuondoa vikwazo vya ruzuku katika bidhaa za kilimo na hasa katika nchi zilizoendelea, ulegezaji wa masharti ya uwekezaji kati ya nchi wanachama, sera bora za ushindani wa biashara, masuala ya hakimiliki na masuala ya ubora wa bidhaa.

Katika Mkutano wa Tano wa Mawaziri wa Biashara wa Shirika hilo uliofanyika Cancun, Mexico, Septemba, 2003, haukufikiwa muafaka uliokusudiwa kwa kuwa nchi zinazoendelea zilitaka mazungumzo yanayozingatia masuala ya maendeleo ya nchi changa kama yaliivyokubalika Doha na kuwa utekelezaji wa matakwa hayo yazingatiwe katika mkutano huo. Kwa kuwa nchi zilizoendelea hazikukubaliana na hayo, mkutano ulimalizika bila maafikiano yoyote. Hivi karibuni pamekuwa na juhudi mbalimbali za kufufua mazungumzo kuhusu Maazimio ya Mkutano wa Doha, ili kuzungumzia masuala manne ambayo yanahu kili, pamba, masoko ya bidhaa zisizo za kilimo na masuala yaliyotokana na mkutano wa *WTO* uliofanyika Singapore mwaka 1996, yanayojulikana kama Singapore *Issues (Trade and Investment, Trade and Competition Policy, Transparency in Government Procurement and Trade Facilitation)*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mazingira ya biashara, lengo ni kuwa na mfumo wa biashara unaohamasisha ukuaji wa Sekta ya Biashara. Katika misingi hii, Wizara imeandaa mapendekezo mahsusii ya kuboresha mfumo wetu wa biashara. Misingi ya mfumo unaotarajiwa kutekelezwa mara kazi inayoendelea itakapokamilika ni pamoja na:-

(i) Kuanzisha utaratibu mpya wa kusajili biashara na wa utoaji wa leseni za udhibiti badala ya mfumo wa leseni unaotokana na Sheria ya Leseni za Biashara ya mwaka 1972;

(ii) Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa zitapewa mamlaka kisheria ya kusajili (*registration*) biashara katika maeneo yao isipokuwa biashara ambazo zitasajiliwa na Wizara ya Viwanda na Biashara;

(iii) Ada za usajili zipangwe na Serikali Kuu na kujumuishwa ndani ya misingi ya sheria ili kuondoa tofauti baina ya Halmashauri na pia kuondoa uwezekano wa kutumia mfumo wa kusajili biashara kama njia ya ukusanyaji kodi;

(iv) Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na TAMISEMI iandae mwongozo wa kusajili biashara kwa Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa zote. Waziri wa Viwanda na Biashara akasimu madaraka ya Mamlaka ya Usajili Biashara husika kwa Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa na Jiji;

(v) Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara na Asasi zinazosimamia sheria za udhibiti wa biashara, iandae

mkakati wa kuwianisha utoaji wa leseni za udhibiti (*Regulatory Licensing*) kwa biashara zinazopaswa kudhibitiwa kwa mujibu wa sheria zinazohusu afya, usalama, mazingira na kadhalika. Biashara zinazopewa leseni za udhibiti zitapaswa pia kusajiliwa katika Serikali za Mitaa za maeneo husika na

(vi) Wizara ya Viwanda na Biashara na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zishirikiane na Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji katika kutekeleza mapendekezo haya.

Ili kuhakikisha mfumo huu unaeleweka na kurahisisha utekelezaji wake, Wizara iliandaa kikao cha wadau wa Sekta hii kilichofanyika Morogoro tarehe 28 - 29 Mei, 2004. Kikao kiliwashirikisha Maafisa Biashara ngazi ya Mikoa na Wilaya, Maafisa Vipimo na Mizani na Mameneja wa *SIDO* wa Mikoa. Kutokana na majadiliano ya kikao hiki, Wizara sasa inakamilisha mfumo utakaotumika katika kuhamasisha ukuaji wa Sekta ya Biashara. Mkakati huu ambao pia unanufaika na matokeo ya tafiti za kina, kimsingi utekelezwa katika ngazi za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji chini ya usimamizi wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza hatua zinazopendekezwa, itabidi kufuta sheria ya Biashara Na. 25 ya 1972 na kutunga sheria mpya ya usimamiaji wa Sekta ya Biashara nchini. Katika misingi hii, hatua zinazohusu leseni za biashara kama zilivvyotangazwa wakati wa uwasilishaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha 2004/2005, zitatekelezwa baada ya kufuta sheria ya sasa ya biashara ili hatua hizo zisipingane na matakwa na masharti ya sheria inayotumika sasa. Wizara yangu inakusudia kuwasilisha Muswada wa Sheria mpya ya Biashara mapema iwezekanavyo ili kupata idhini ya Bunge kuwezesha utekelezaji wa yanayokusudiwa katika kuboresha utendaji wa Sekta ya Biashara katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mafanikio ya kuridhisha katika utekelezaji wa Malengo ya Biashara kama nilivyoeleza hivi punde. Yamekuwepo pia mafanikio ya kuridhisha katika utekelezaji wa malengo yanayohusu usimamiaji wa Sheria za Wakala, Sheria ya Wakala wa Meli na ukamilishaji wa Sheria ya *Anti-Dumping* kama nitakavyoeleza baadaye katika hotuba hii.

Pamoja na mafanikio haya, Sekta ya Biashara iliendelea kukabiliana na changamoto hasa kuhusiana na ubora wa bidhaa pamoja na ukosefu wa bidhaa za kutosha kuuza nje ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje (*Supply Constraints*). Aidha, Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kutafuta ufumbuzi ili kuiwezesha Sekta Binafsi iweze kuzalisha bidhaa nyingi na zenyе ubora zaidi ili kukidhi masoko ya nje. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuwashirikisha wadau katika misafara ya biashara ili waweze kujifunza na kujionea wenyewe mambo ya biashara yanayoendeshwa ili hatimaye kujenga uwezo wa kuzalisha bidhaa nyingi na bora kutokana na kuona mbinu ambazo wanatumia wenzao na namna wanavyofanya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya juhudhi hizi za Serikali ni ongezeko la mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi kutoka Dola za Kimarekani 1,568.3 milioni mwaka 2002

hadi Dola za Kimarekani 1,827.6 milioni mwaka 2003. Katika kipindi hicho, mauzo ya bidhaa peke yake yaliongezeka kutoka Dola za Marekani 902.5 milioni hadi Dola za Marekani 1,142.4 milioni sawa na asilimia 26.6. Kuimarika kwa Sekta ya Biashara kunaashiria mwelekeo mzuri wenyewe matumaini katika kipindi kijacho. Aidha, mchango wa Sekta ya Biashara katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 16.8 mwaka 2003 ikilinganishwa na asilimia 16.5 mwaka 2002. Hata hivyo, nakisi katika biashara haijaonyesha kubadili mwelekeo wake ambapo kwa miaka kadhaa sasa, thamani ya bidhaa tunazonunua toka nje imeendelea kuwa kubwa ikilinganishwa na thamani ya bidhaa tunazouza nje. Thamani ya mauzo inaweza kulipia nusu tu ya manunuzi yetu nje.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara ilitoa jumla ya leseni za biashara 96,767 ukilinganisha na leseni 96,172 zilizotolewa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2002/2003. Idadi ya leseni iliongezeka kwa asilimia 4.8. Katika kipindi cha 2003/2004, mapato yanayotokana na leseni yalifikia Shilingi 8,879 milioni ikilinganishwa na Shilingi 8,127 milioni zilizokusanywa kipindi cha 2002/2003, sawa na ongezeko la asilimia 9.25. Aidha, kiasi cha Shilingi 460 milioni zilikusanywa kutokana na adhabu na faini kwa makosa mbalimbali ya ukiukaji wa sheria ya leseni za biashara katika kipindi hicho cha fedha, ukilinganisha na shilingi 301.7 milioni zilizotozwa katika kipindi cha 2002/2003. Hili ni ongezeko la asilimia 34.5.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, lengo la Wizara katika Sekta ya Biashara ni kuweka mikakati itakayotuwezesha kama Taifa, kuhimili ushindani wa biashara kimataifa na kutupa uwezo wa kushiriki na kufaidika na mfumo wa biashara ya Kimataifa katika zama hizi za utandawazi. Aidha, lengo ni kujenga uwezo kwa wazalishaji na wafanyabishara ili waweze kufaidika na masoko mbalimbali kama vile *EAC, SADC, AGOA, EBA, PACT* (Canada) na kadhalika. Ili kutimiza lengo hili, Wizara itatilia mkazo kujenga uwezo wa Taifa katika kushiriki kwenye Majadiliano ya Kimataifa na kuongeza uwezo wa ushindani wa bidhaa zetu katika Soko la Kimataifa, kushughulikia matatizo yanayosababisha uhaba wa bidhaa za kuuza nje na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Biashara ya 2003.

Lengo la sera hizi ni kufikia kiwango cha juu cha ukuzaji wa uchumi. Aidha, katika hatua za utekelezaji wa Sera ya Biashara, sisi kama Taifa tutakabiliana na changamoto za kutatua matatizo ya msingi yanayosababisha uchumi na biashara kudumaa. Zipo nyenzo za kukabiliana na changamoto hizi zilizoanishwa katika sera ambazo zitatumwiwa na Wizara, Asasi na wadau wanaohusika. Nyenzo husika ni kodi na ushuru wa forodha, mbinu za kujihami kibiashara, vikwazo visivyo vyta kodi wala ushuru wa forodha, makubaliano mbalimbali ya kibiashara ya Kikanda na Kimataifa na sheria kama vile Sheria ya *Anti Dumping*. Kutokana na mikakati hii Sekta ya Biashara inakadiria kukua kwa asilimia 8.5 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, ubinafsishaji wa Makampuni ya Umma yaliyo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara katika kipindi cha 2003/2004, uliendelea. Katika kipindi hiki Makampuni tisa yalibinafsishwa yakiwemo yale ambayo ubinafsishaji wake umechukua muda mrefu. Makampuni haya ni pamoja na Kiwanda cha Karatasi Mgololo (*SPM*), Kiwanda cha Zana za Kilimo Ubungo (*UFI*) na Kiwanda cha Nguo cha

*Morogoro Polyester.* Kukamilika kwa ubinafsishaji wa kiwanda cha *SPM* ambao umechukua zaidi ya miaka kumi umeondoa mzigo mkubwa kwa Serikali wa gharama za uendeshaji kwa ajili ya kutunza mitambo ili kuепusha athari za uchafuzi wa mazingira. Aidha, katika kipindi hiki Makampuni sita ya Biashara ya *HOSCO, BCS, S&O, Dar es Salaam RTC, Arusha RTC* na *Mwanza RTC* yaliuzwa kwa wafanyakazi kwa utaratibu wa *MEBO*, hii ikiwa ni njia mojawapo ya kutekeleza azma ya Serikali ya kushirikisha na kuwezesha Wananchi katika kumiliki baadhi ya viwanda na makampuni madogo. Hii inafanya jumla ya Makampuni yaliyo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara yaliyouzwa kwa wafanyakazi kupitia *MEBO* kuwa kumi na moja. Taratibu za kukamilisha ubinafsishaji wa Shirika la Vyuma la Taifa (*NSC*) na Makampuni ya *Tanzania Express* na *Tanzania Publishing House* kwa njia ya *MEBO* zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, hatua za kuhitimisha shughuli za Mashirika Mama yaliyo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara ambayo Kampuni tanzu zake zimebinafsishwa zinaendelea. Katika kipindi hiki shughuli za Shirika la Karatasi zilihitimishwa na kufanya jumla ya Mashirika Mama yaliyokwishahitimisha shughuli zake kuwa sita. Aidha, taratibu za kuhitimisha shughuli za Kampuni ya Wakala wa Meli (*NASACO*), pamoja na Kampuni zake tanzu zinaendelea. Kuhitimishwa kwa shughuli za *NASACO* kunatokana na ukweli kuwa hata baada ya kutunga Sheria ya Uwakala wa Meli, Kampuni hizi hazikuweza kuhimili ushindani kutokana na Makampuni ya Meli kuwa mawakala pia wa Makampuni yao na hivyo *NASACO* na kampuni zake tanzu kukosa biashara.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuiendeleza Sekta hii, Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo iliidhinishwa na Serikali mwezi Februari, 2003 na kuzinduliwa rasmi mwezi Agosti, 2003. Malengo makubwa ya sera hiyo, kama nilivyolieza Bunge lako Tukufu mwaka 2003, ni kuchocha uanzishaji wa miradi mipya na pia kuiimarisha miradi iliyopo. Ili kufikia lengo hilo, mikakati kadhaa itatumika, ikiwa ni pamoja na kujenga mazingira mazuri ya kisheria, upatikanaji na uboreshaji wa maeneo ya kufanya kazi, kuimarisha upatikanaji wa huduma za kuendeleza Sekta katika nyanja za teknolojia, masoko, upatikanaji wa taarifa na uendelezaji ujasiriamali, kuboresha upatikanaji wa mitaji, kuimarisha mfumo wa taasisi wa kuiendeleza Sekta na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo yanategemea utekelezaji mzuri wa sera hii ili kuwawezesha Wananchi wengi zaidi kushiriki katika shughuli za kiuchumi. Baada ya uzinduzi wa sera hii, mambo ya msingi yafuatayo yamefanyika: -

(i) Sera imetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili na pia maandalizi yanafanyika ya kuchapishwa sera katika picha na michoro (*popular version*) ili kuwafikia watu wengi zaidi.

(ii) Wizara imefanya warsha ya siku moja Mjini Dar es Salaam ambayo imewahusisha wadau mbalimbali kujadili mikakati ya kutekeleza sera. Aidha, zimeandaliwa warsha zitakazofanyika katika kanda nchini ili kuweka bayana majukumu ya wadau wote katika utekelezaji wa sera.

(iii) Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*), imechukua hatua za kuhakikisha kuwa masuala ya jinsia yanazingatiwa katika utekelezaji wa sera husika. Mafunzo yamefanyika kwa Taasisi kadhaa kuhusu utoaji wa huduma kwa kuzingatia mahitaji ya jinsia zote. Aidha, utafiti ulifanyika kubaini matatizo yanayozuia miradi mdingi ya wanawake kupata manufaa na kupanuka badala yake kudumaa na kubakia midogo. Utafiti huu uliohusisha pia nchi za Kenya na Ethiopia, utatuwezesha kuandaa mikakati maalum ya kuboresha ujasiriamali mionganoni mwa wanawake.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo imeendelea kutoa mchango mkubwa katika kukuza na kuboresha uchumi wetu ikiwa ni pamoja na kuchangia katika vita dhidi ya umaskini. Sekta hii imechangia pia katika upatikanaji wa ajira, uzalishaji wa bidhaa kwa matumizi ya soko la ndani na nje na kutoa fursa ya kuendeleza teknolojia na ujasiriamali. Aidha, Sekta hii imeendelea kujenga utamaduni na kutoa uzoefu wa uendelezaji wa viwanda nchini kwa Watanzania Wazalendo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Wizara itaendelea na utekelezaji wa programu zitokanazo na Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo kwa kuboresha maeneo ya kufanya kazi za viwanda na biashara (*industrial clusters and business premises*), kuimarisha huduma zinazotolewa na Sekta ikiwa ni pamoja na utaalamu wa masoko, kuboresha upatikanaji wa taarifa, uimarishaji wa teknolojia na elimu ya biashara, kujenga uwezo wa Taasisi zinazohudumia viwanda vidogo na biashara ndogo kwa kujenga uwezo wa kuratibu shughuli za Sekta, kuimarisha upatikanaji wa mitaji na kutekeleza mikakati inayohamasisha ujasiriamali katika jamii.

Mheshimiwa Spika, tarehe 12 Machi, 2004 Waziri wa Viwanda na Biashara aliteuliwa kuwa ndiye mwenye dhamana ya Sheria ya Ushindani katika Shughuli za Kiuchumi (*The Fair Competition Act, No.8 of 2003*). Sheria hii imeanza kutumika tarehe 12 Mei, 2004 baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali kwa Tangazo Namba 150 (*GN. 150*), la mwaka 2004. Kusudio letu ni kuwa ushindani baina ya wafanyabiashara katika shughuli za uchumi utaimarika na maslahi ya mlaji katika mazingira ya uchumi wa soko yatalindwa. Ni muhimu Wananchi sasa wakatumia Tume hii katika kutanzua matatizo na malalamiko yao kuhusu uendeshaji wa biashara hapa nchini. Wizara yangu au Serikali kwa ujumla haitaweza tena kujiingiza moja kwa moja katika masuala haya ya ushindani wa biashara. Hatua za kuwapata Watendaji Wakuu wa Tume ya Ushindani zinaendelea kuchukuliwa ili Tume iweze kuwa na watumishi wake wote kama inavyohitajika. Katika muundo wa Tume hii, kutakuwa na Makamishina watano ambao ndio watakuwa na maamuzi yote makuu juu ya masuala yatakayokuwa yanajitokeza na kuhitaji uamuzi. Tume itakuwa na mamlaka ya kutenda kazi zake kwa uhuru mkubwa bila kuingiliwa. Utaratibu huu ndio unaonekana kukidhi matakwa ya Kimataifa juu ya uendeshaji bora wa Taasisi za namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, uendeshaji wa uchumi wa soko katika nchi yetu bado ni dhana mpya ambayo haijazoleka. Mionganoni mwa kazi ambazo Tume itajikita zaidi kuzifanya ni kuelimisha umma na wadau mbalimbali juu ya uchumi wa soko unavyohitaji

kusimamiwa na matakwa ya sheria na utekelezaji wake. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Serikali itaendelea kujenga uwezo wa Tume ili iweze kutekeleza majukumu yake mengi kikamilifu kama ambavyo yameanza kujitokeza. Pamoja na kuanzishwa kwa Tume ya Ushindani, taratibu za kuanzisha Baraza la Ushindani katika uchumi ambalo litakuwa Baraza la Rufaa kwa maamuzi yatakayotolewa na Tume ya Ushindani na Mamlaka za Udhibiti za Kisekta kwa mfano *SUMATRA, EWURA* na kadhalika zimeanza na tunategemea kukamilisha mwaka huu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Ofisi ya Jaji mkuu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Kikanda kuhusu Sheria za Ushindani na Uwekezaji katika Uchumi wa Kimataifa (*Regional Conference on Competition Policy, Competitiveness and Investment in the Global Economy*) uliofanyika Dar es Salaam tarehe 10 - 12 Mei, 2004. Lengo la mkutano huo lilikuwa kuhamasisha nchi ambazo hazina sera na sheria ya ushindani kuzianzisha na zile ambazo zinaendeleza utekelezaji wake, kujenga na kuimarishe uhusiano miongoni mwao. Mkutano huo ulihisaniwa na Benki ya Dunia, *UNCTAD* na Jumuiya ya Uchumi ya Ulaya (*EU*).

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea na jukumu lake la kuhakikisha kuwa nchi yetu haigeuzwi jalala la kutupia bidhaa toka njie zinazouzwa kwa bei chini kuliko gharama za uzalishaji wake. Aidha, napenda kulishukuru Bunge lako kwa kupitisha Sheria ya *Anti-Dumping and Countervailing Measures*, ambayo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa alitia saini tarehe 14 Aprili, 2004 kuwa sheria. Wizara inashirikiana na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, kukamilisha kanuni za utekelezaji wa sheria hiyo ili ianze kutumika mara moja.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni za Viwanda aliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuimarishe uwezo wake wa kutoa huduma bora. Katika kuimarishe utoaji huduma bora, mkakati uliwekwa katika kuwaelimisha Wananchi juu ya huduma zitolewazo na wakala na kupunguza muda wa utoaji wa huduma hizi kwa kuondoa vipengele ambavyo si vya lazima kisheria. Kutokana na mabadiliko ambayo yanaendelea kufanywa na wakala kama kujijengea uwezo wa utendaji kazi, ufanisi wa utekelezaji kazi umeongezeka. Katika kikao kilichopita nilielezea hatua ambazo Wakala ilikuwa imechukua kutekeleza azma hii katika kutoa elimu kwa Wananchi kwa nia ya kuwarahisishia usajili.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, nililieleza Bunge lako Tukufu kuwa Wakala atafanya uchambuzi wa kuona uwezekano wa kupeleka huduma zake karibu zaidi na Wananchi kwa kufungua Ofisi za Kanda na kutumia Ofisi za Biashara za Mikoa kutoa huduma husika. Kupeleka huduma mikoani ni moja ya malengo ya Wakala ili kuwapunguzia Wananchi gharama za kuja na kusajili Kampuni, jina la biashara, alama za biashara, hata na leseni za viwanda Dar es Salaam. Kwa sasa Wakala inajenga uwezo wa ndani (*Internal Capacity Building*) ili kuweza kumudu majukumu haya mapya.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wakala anakusudia kutekeleza majukumu aliyopanga kwenye mpango wa muda mrefu kikamilifu. Pamoja na azma ya kupeleka huduma karibu na Wananchi, Wakala itaendelea kuboresha sheria mbalimbali

inazosimamia kwa nia ya kurahisisha utoaji huduma, kujenga na kutumia mbinu za kisasa katika utendaji kazi na kuhamasisha watumiaji wa huduma za Wakala ili kupanua wigo na hivyo kuboresha mapato.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kilichopita, Wakala wa Mizani na Vipimo, amekuwa akiendelea na uboreshaji wa huduma zake kwa kufanya yafuatayo: -

(i) Kukagua na kusimamia usahihi wa vipimo vinavyotumika katika biashara ili kuwahakikishia Wananchi kutendewa haki na usawa;

(ii) Kuhamasisha watengenezaji na waundaji wa vipimo wa hapa nchini ili wabuni vipimo bora na kuwajengea uwezo kwa lengo la kuwarahisishia Wananchi upatikanaji wa vipimo hivyo na kwa bei nafuu;

(iii) Kuhamasisha na kushirikisha umma katika kukuza uelewa wake kuhusu umuhimu wa matumizi sahihi ya vipimo; na

(iv) Kushirikiana na Taasisi na Asasi nyingine za Kitaifa na Kimataifa kwa lengo la kukuza ufanisi na tija ya watumishi wa Wakala na hatimaye kuongeza ari ya kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu yaliyotajwa, Wakala anategemea mapato yanayotokana na ada kwa huduma zake kwa umma. Makadirio ya mwaka 2004/2005 ni kupata Sh.562,367,000/= ikilinganishwa na kiasi cha Sh.498,612,643/= kilichotegemewa kupatikana katika mwaka 2003/2004. Ingawa kiasi hiki kinaonyesha mwelekeo wa kukua, bado hakitoshelezi mahitaji ya Wakala. Wakala wa Mizani na Vipimo inapambana na vikwazo vingi. Baadhi ya vikwazo hivyo ni upungufu wa vitendea kazi. Hata hivyo, upungufu huo wa vitendea kazi ni changamoto kwa Wakala kupanga mikakati ya kutafuta fedha zaidi.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Wakala inayo mashirikiano ambayo itayaendeleza baina yake na Taasisi mbalimbali za Kikanda na za Kimataifa. Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*), Wakala itaendelea kushirikiana na Idara za Vipimo na Mizani za Kenya na Uganda kuainisha maeneo yanayoweza kusaidiwa chini ya mradi mpya wa *PTB-EAC*. Aidha, kwa kuititia Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*), Wakala itasimamia ukusanyaji wa maoni ya Wananchi juu ya rasimu iliyokamilishwa na nchi hizo kuhusu bidhaa zinazouzwa zikiwa zimefungwa (*pre-packed goods*).

Mheshimiwa Spika, Chama cha Kutetea Wasanii (*Copyright Society of Tanzania - COSOTA*), katika kipindi cha mwaka 2003/2004 kiliendelea kutekeleza jukumu lake la kuwaelimisha na kuwahamasisha wasanii na watunzi juu ya Sheria ya Hakimiliki Na. 7 ya mwaka 1999. Aidha, idadi ya Wanachama imeongezeka kutoka 402 hadi 798 mwaka 2003/2004. Wanachama hao wamesajili jumla ya kazi 3001 za utunzi na sanaa ili zilindwe. Nyingi ya kazi hizo ni nyimbo za muziki, maigizo na vitabu. *COSOTA* hadi tarehe 16 Aprili, 2004 ilikusanya mirabaha (*royalties*) yenye thamani ya jumla

Sh.2,434,136/=.*COSOTA* inaendelea na juhudzi zake za kuelimisha na kuhamasisha wadau wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003, *COSOTA* ikishirikiana na Wataalam wa Wizara ya Sheria na Baraza la Kiswahili la Tanzania (BAKITA), ilifanikiwa kutafsiri Sheria yote ya Hakimiliki katika lugha ya Kiswahili. Kwa kuwa sheria inayohusu hakimiliki ni muhimu sana kwa kutetea maslahi ya kazi zote za usanii na watanzi na kwa kuwa kazi hizo ni chanzo muhimu cha kuliingizia Taifa fedha za kigeni na kuondoa umaskini, ninawashauri Waheshimiwa Wabunge wawahamasishe wasanii na wahusika wengine katika majimbo na maeneo yao ili wajipatie nakala za Kiswahili za sheria hiyo. Aidha, natoa wito kwa watu au Makampuni yenye uwezo wawekeze katika studio zenye miundombinu na mitambo ya kisasa inayoweza kutoa santuri na kanda zenye ubora wa Kimataifa. Vile vile, pamoja na kuwekeza katika miundombinu na mitambo, kuna haja kuendeleza taaluma zinazohusiana na utengenezaji wa kazi za sanaa zikiwemo filamu, santuri za muziki na kanda.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*), liliendelea na majukumu ya uwekaji viwango vya ubora wa bidhaa na usimamiaji wa utekelezaji wa viwango hivyo. Pamoja na viwango vinavyohusu Sekta mbalimbali, Shirika lilikamilisha viwango 47 vya ubora wa vyakula, saruji na nguzo za umeme na simu ili kulinda afya na usalama wa Wananchi na kukuza na kuendeleza Sekta za ujenzi, nishati na mawasiliano. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2003, Shirika lilikuwa limetayarisha viwango vya Taifa 798 katika Sekta mbalimbali zikiwemo za kilimo na chakula, nguo, kemikali, uhandisi, mazingira na kadhalika. Shirika pia liliendelea kusimamia utekelezaji wa viwango vya Taifa kwa kutumia mifumo iliyopo ya uhakiki bora (*Certification Schemes*). Hadi kufikia mwezi Desemba, 2003, Shirika lilikuwa limetoa jumla ya leseni 504 za ubora wa bidhaa mbalimbali katika viwanda 396. Leseni hizi hutolewa kwa wazalishaji wanaotimiza masharti ya ubora wa bidhaa hasa zile zinazogusa afya na usalama wa walaji na uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka kwa umuhimu wa majukumu ya Shirika katika mazingira ya uchumi wa soko na utandawazi, Shirika lilibuni na kuanza kutekeleza mkakati wa kudhibiti bidhaa duni kutoka nje ya nchi kuanzia mwaka 1999. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2003, Shirika lilikuwa limetoa jumla ya leseni 7,069 za ubora wa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje. Mkakati huo unatekelezwa kwa ushirikiano wa karibu na Mamlaka ya Mapato (*TRA*), katika Bandari ya Dar es Salaam na Tanga na vituo vingine vya mipakani mwa nchi kama Namanga, Horohoro, Holili na Kyaka. Baadaye juhudzi hizi zitahusisha vituo vyote vilivyobaki kama vile Tunduma, Kasumulu na Sirari.

Mheshimiwa Spika, kuanzia Januari 15, 2004 Shirika lilianza kudhibiti ubora wa mitumba inayoagizwa kutoka nchi za nje kuzuia Tanzania kuwa dampo la mitumba isiyofaa. Aidha, kuanzia tarehe 1 Machi, 2004, Shirika limeanza kudhibiti ubora wa mafuta ya petroli na bidhaa nyingine zinazotokana na mafuta hayo ili kuhakikisha kuwa mafuta yanayoingizwa nchini yana ubora unaotakiwa. Hatua hii ilichukuliwa kufuatia kudhihirika kuwapo kwa mafuta ya petroli yasiokidhi kiwango cha Taifa cha bidhaa hiyo.

Katika mwaka 2005, Shirika litaendelea kuimarisha juhudini zake za kudhibiti ubora wa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na zile zinazotoka nje ya nchi zikiwemo vyakula, magari yaliyotumika, petroli na mitumba.

Mheshimiwa Spika, Wizara ina jukumu la kuratibu utendaji katika Taasisi zinazotoa huduma mbalimbali zinazohusiana na maendeleo ya viwanda na biashara hususan kutangaza biashara nje, mafunzo, ushauri, maendeleo ya teknolojia na utafiti. Taasisi hizi ni pamoja na Halmashauri ya Biashara ya Nje (*BET*), Kituo cha Biashara cha London (*LTC*), Shirika la Maendeleo ya Utafiti wa Viwanda (*TIRDO*), Kituo cha Kuendeleza na Kueneza Teknolojia rahisi Vijijini (*CAMARTEC*), Shirika la Ubunifu wa Mitambo (*TEMDO*), Shirika la Taifa la Maendeleo (*NDC*), Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO*) na Chuo cha Elimu ya Biashara (*CBE*).

Mheshimiwa Spika, Shirika la *TIRDO* katika kipindi cha 2003/2004, lilikamilisha utafiti wa kupunguza sumu ya *Ochratoxin A*, kwenye mbegu za kahawa. Utafiti umekamilika katika kuchanganua ili kutambua sehemu zinazoweza kuathiriwa na sumu ya *Ochratoxin A* na namna ya kuzuia. Utafiti unafanywa katika mashamba ili kuzalisha kahawa bora.

Aidha, katika kipindi cha 2003/2004, Shirika lilizalisha na kusambaza mbegu bora za uyoga kwa wakulima wa uyoga. Katika kipindi hicho hicho, Shirika pia lilikamilisha utafiti na utengenezaji wa mashine za kukamulia machungwa kwa kutumia vifaa vya hapa nchini. Zoezi la kusambaza teknolojia hiyo mpya na kutoa mafunzo kwa wakulima wa michungwa linaendelea vizuri. Vile vile, Shirika katika kipindi hicho, lilifanya uchunguzi wa madini ya bauxite katika Kijiji cha Magamba Wilaya ya Lushoto na kupendekeza kuwa uamuzi wa kuruhusu au kutoruhusu kuchimba madini ya bauxite ufanyike baada ya kufanya tathmini juu ya athari kwa mazingira kuhusu mradi huo (*Environmental Impact Assessment*). Ripoti yao inaonyesha kuwa katika kila sampuli waliyopima, madini aina ya *Alumina* ndiyo yanaonekana kuwa mengi. Kiwango cha chini ni asilimia 26 na kiwango cha juu ni asilimia 62. Imethibitishwa kuwa sampuli zote hizo zina madini ya *Alumina* mengi ambayo yanaweza kuchimbwa kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Shirika pia limetoea mafunzo kwa Taasisi na Kampuni za Ujenzi namna ya upimaji wa zege, ujuzi ambaa hutumika pia kupima ubora wa madaraja, barabara, nyumba za ghorofa na mabomba makubwa. Shirika pia limeongeza ujuzi wa mafundi chuma kwa wazalishaji wadogo na katika katika uchomeaji wa chuma cha pua, chuma cha kawaida na uungaji wa vyuma. Vile vile, Shirika limetoea mafunzo katika kuboresha kazi za samani na vifaa viliviyotengenezwa kwa mbao kwa lengo la kuzalisha bidhaa za samani ambazo ni imara na bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya utaalamu wa kusindika takataka ili zitumike tena kuzalisha bidhaa (*recycling*), yanaendelea kwa lengo la kupunguza uchafuzi wa mazingira. Shirika limetoea teknolojia ya kusindika mahindi na mboga, kutengeneza unga wa chaki na chaki zisizo na vumbi, kupima uchafuzi wa mazingira na matumizi bora ya nishati.

Mheshimiwa Spika, malengo ya *TIRDO* kwa mwaka 2004/2005 ni kukamilisha tafiti zilizokwishaanza, kuanzisha tafiti mpya, kutoa huduma kwa viwanda vingi zaidi kwa lengo la kufikisha utaalam na teknolojia kwa walengwa. Nguvu zaidi itawekwa katika kuisaidia Sekta Isiyo Rasmi na Viwanda Vidogo kwenye maeneo mbalimbali kwa nia ya kuongeza ubora wa bidhaa zinazozalishwa viwandani. Lengo kuu ni kujenga uwezo katika kuthibiti ubora wa miundombinu ya kihandisi na kuongeza usalama wa vifaa vya kihandisi.

Mheshimiwa Spika, kituo cha *CAMARTEC* katika kipindi cha 2003/2004, kiliendelea na jukumu lake la kubaini mahitaji ya zana rahisi za kilimo vijiji, kuunda zana husika, kuzisambaza na kutoa elimu kwa walengwa. Katika kipindi hicho hicho, kituo kilibuni na kuendeleza teknolojia za nishati mbadala kama kuunda majiko na mitambo inayotumia nishati ya jua, utengenezaji wa majiko sanifu yanayotumia mkaa au kuni kidogo na kueneza matumizi ya gesi ya samadi katika kuchangia juhudzi za Serikali za kulinda na kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, *TEMDO*, ambayo jukumu lake kubwa ni uhandisi na usanifu wa mitambo, iliendelea na shughuli za kubuni mitambo na teknolojia mbalimbali zinazolenga kusaidia uendelezaji wa Sekta binafsi kwa kutumia mashine na teknolojia sahihi. Mashine zilizobuniwa na kuundwa na *TEMDO* ni pamoja na za kukamua mafuta ya mawese, mashine ya kuongeza uhifadhi wa maji ya matunda na mashine ya kukamua asali. Aidha, viwanda na karakana mbalimbali zilihamasishwa kutengeneza na kusambaza kwa wingi mashine hizo. Katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Asasi hiyo itaendelea kutoa huduma za kihandisi kwa viwanda ili kuongeza mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa (*PLT*).

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo ya Taifa (*NDC*), ni Chombo cha Serikali cha kuchochea, kuhamasisha na kuratibu shughuli za kiuchumi katika Sekta ya Viwanda. Kutokana na hali hiyo, *NDC* itaendelea kuimarishwa katika muundo na utendaji wake wa kazi katika kipindi hiki cha 2004/2005. Hii ni pamoja na kutunga sheria mpya itakayoipa *NDC* uhai na nguvu mpya ya utekelezaji wa majukumu yake mapya na yaliyopanuka likiwemo lile la uwezeshaji Wananchi kiuchumi.

*NDC*, licha ya kuwa na jukumu la kuendeleza programu ya *EPZ*, pia inasimamia Maendeleo ya Kikanda (*Spatial Development Initiatives - SDI*), yakiwemo yale ya *Mtwarra Development Corridor*, ambayo miradi yake mikubwa na ya msingi ni mradi wa mkaa wa mawe wa Mchuchuma na Mradi wa Chuma wa Liganga.

Mradi wa magadi ya Ziwa Natron nao ni mradi mkubwa unaosimamiwa na Shirika hili ingawaje haumo katika Ukanda wa Mtware. Aidha, Mameneja wa Miradi ya Mtware na Kati wameshatikana na kuanza kazi katika Makao Makuu ya *NDC*. Mameneja hawa wamepatikana kutokana na hisani ya Serikali ya Afrika kusini kupitia Benki yao ya Maendeleo (*Development Bank of South Africa*).

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kuliimarisha Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO*) ili kuliwezesha kuhudumia Sekta ya Viwanda Vidogo na

Biashara Ndogo kikamilifu. Hatua hizo ni pamoja na kuipa *SIDO* vitendea kazi yakiwemo magari. Katika kipindi cha 2003/2004, *SIDO* ilifanya utafiti wa awali ili kuweza kutambua mahitaji halisi ya kiufundi ya wanaviwanda na wafanyabiashara wadogo. Kutokana na utafiti huo, jumla ya mashine 170 za kubangua korosho zimetengenezwa ambazo zimesambazwa kwenye maeneo yanayozalisha korosho. Ubunifu wa teknolojia zinazohusu kuhifadhi kwa muda mrefu maziwa, kusindika pilipili na kukamua mawese umefanyika na mashine hizo kutengenezwa, kufanyiwa majaribio na kuonyesha mafanikio. Aidha, katika kipindi cha miezi sita ya mwanzo wa mwaka 2003/2004, jumla ya kozi 48 zilizowashirikisha wajasiriamali 982 ziliandaliwa na kuendeshwa na *SIDO*. Kozi 16 maalum kwa ajili ya kutoa ujuzi wa usindikaji wa vyakula ziliendeshwa na kuhusisha wajasiriamali 277. Katika mwaka huo jumla ya wajasiriamali 2,680 kutoka Mikoa yote walipatiwa ushauri wa masuala mbalimbali yanayohusu shughuli wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, vile vile, *SIDO* iliendesa maonyesho ya biashara katika Mikoa mbalimbali nchini yaliyoshirikisha wajasiriamali 923 ambao walifanya mauzo ya bidhaa zenye thamani ya Shilingi 66.5 milioni fedha taslimu na Shilingi 104.8 milioni kwa miadi. Pia katika kipindi hicho, Shirika liliwawezesha wajasiriamali 37 kushiriki maonyesho ya biashara ndogo ya Nairobi na Kampala.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, *SIDO* imetoa mitaji kwa jumla ya wajasiriamali 2,301 yenye thamani ya Shilingi 1,248.3 milioni kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza miradi ya aina mbalimbali kwa kutumia Mfuko wa Kuendeleza Wafanyabiashara Wadogo (*NEDF*). Mitaji hiyo imewezesha kuanzisha na kudumisha ajira zipatazo 15,594. Tangu ulipoanzishwa na hadi kufikia mwezi Desemba, 2003 mfuko huo ulikuwa umetoa mitaji kwa wajasiriamali 17,840 yenye thamani ya Shilingi 6.58 bilioni kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao za kiuchumi mbalimbali. Mchango huo uliwezesha upatikanaji wa ajira kwa Wananchi 24,056. Bado mahitaji ya mitaji kwa wafanyabiashara wadogo ni makubwa ukilinganisha na uwezo wa mfuko. Jumla ya maombi ya mitaji yaliyopokelewa hadi kufikia Desemba 2003 ni 72,993 yenye thamani jumla ya Shilingi 29.32 bilioni. Mitaji iliyotolewa ni asilimia 24 tu kwa idadi na asilimia 22 tu kwa thamani ya jumla ya maombi yote yaliyopokelewa katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya programu zitakazotekelezwa na *SIDO* katika mwaka 2004/2005 ni pamoja na kutafiti na kuwezesha upatikanaji wa teknolojia mpya 20, kuanzisha viatamizi (*incubators*) 20, kusaidia upatikanaji wa maeneo 20 ya biashara, kuandaa maonyesho manane ya biashara kikanda na kusaidia uanzishaji wa Vyama Mama vinne nchini (*Apex Organisations*) kwa ajili ya wadau wa Sekta. Aidha, shughuli nyingine za *SIDO* zitaendelea kuboreshwa kadri hali itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Biashara ya Nje (*BET*), katika kipindi cha 2003/2004, iliendesa Maonyesho ya Kibiashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam ambayo yameendelea kuwa moja ya kichocheo cha ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini katika Taifa letu. Katika Maonyesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam, bidhaa mbalimbali za Tanzania zimeweza kupata soko la nje. Mauzo na maulizo kwa mwaka 2003 yalikuwa na thamani ya Dola za Kimarekani 22.39 milioni. Halmashauri pia, kwa

kipindi cha 2003/2004, imeboresha miundombinu ndani ya Uwanja wa Maonyesho wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Barabara ya Kilwa, Jijini Dar es salaam ikiwa ni pamoja na kuchimba visima vya maji ya kutosheleza mahitaji ya uwanja mzima na kuweka lami upya barabara zote za uwanja, pamoja na ukarabati wa baadhi ya mabanda likiwemo *Dome* ambalo hutumika kwa ufunguzi rasmi wa maonyesho na lile la Sheikh Abeid Amani Karume.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Kituo chake cha Biashara kilichoko London (*Tanzania Trade Centre*), imeweza kuitangaza Tanzania nchi za nje, kwa kutangaza biashara ya Tanzania, vivutio mbalimbali vya uwekezaji na utalii. Kutokana na jitihada hizo, Taifa limeweza kushiriki katika vikao mbalimbali vya Asasi za Kimataifa za kahawa na sukari. Aidha, kituo kwa kushirikiana na Jumuiya ya Madola, kilitoa mchango wake wa uhamasishaji wakati wa maandalizi ya mikutano ya wawekezaji iliyofanyika Dar es Salaam na Zanzibar mwaka 2003. Kituo kitaendelea kushirikiana na Makampuni ya Uingereza yanayotangaza vivutio vya utalii ili kuendelea kuitangaza na kuikuza Sekta ya utalii na fursa za uwekezaji katika Sekta za viwanda, biashara, ujenzi, madini, mawasiliano na uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Elimu ya Biashara ni moja ya Taasisi muhimu kwa Wizara ya Viwanda na Biashara katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Biashara ya mwaka 2003 na Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ya mwaka 2003. Katika Kipindi cha mwaka 2003/2004, Chuo cha Elimu ya Biashara (*CBE*) kiliweza kutekeleza malengo waliojiwekea kwa mwaka 2003/2004, katika kuboresha mitaala yake ya Elimu ya Biashara. Maeneo yaliyotiliwa msisitizo kwenye mitaala ya Chuo ni pamoja na kuingiza somo la ujasiriamali katika kila programu inayofundishwa chuongi. Katika kipindi cha 2003/2004, Kitengo cha chuo cha kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara wadogo (*Small Business Development Centre - SBDC*) kiliweza kuendesha mafunzo ya ujasiriamali kwa Wilaya za Temeke na Ilala.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo limetiliwa umuhimu wa juu ni kurekebisha mitaala ya mafunzo ya miaka mitatu ya *Diploma* ya Juu ya Mizani na Vipimo (*Advanced Diploma in Legal, Industrial and Scientific Metrology*) ili yawewe kwenda na mabadiliko ya kiuchumi na kiteknolojia duniani. Kwa kipindi cha mwaka 2003/2004, Chuo kilishiriki katika vikao vilivyoandaliwa na kushirikisha wawakilishi toka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nia ya vikao hivyo ilikuwa ni kutengeneza vigezo (*criteria*) au sifa zinazotakiwa Chuo kuwa nazo, ili kiweze kuendesha kozi za mizani na vipimo kwa niaba ya nchi zote tatu za Jumuia (*Centre of Excellence*). Vigezo hivyo bado vinafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, malengo ya Chuo katika kipindi kijacho ni pamoja na kuwezesha Taifa kupata utaalamu wa masuala ya biashara na hasa katika ujasiriamali na uendelezaji wa biashara. Ili kuweza kufikia malengo haya, masomo yatakayopewa nafasi kubwa kutekelezwa kwa kipindi cha mwaka 2004/2005, yatalenga zaidi katika kufundisha Ujasiriamali, Masoko ya mitaji, Biashara kupitia mtandao wa *internet (E-Commerce)* na Fursa za Teknolojia ya Upashanaji Habari na Mawasiliano (*Information and Communication Technology - ICT*), uendeshaji wa Biashara za Kimataifa

(*International Business Management*), Mbinu za Mawasiliano ya Kibiashara (*Business Communication Skills*) na Taaluma ya Teknolojia ya Kisasa ya Mizani, Vipimo na Mambo yanayohusu Viwango. Pamoja na kutoa mafunzo, Chuo kimejipangia kuimarisha masuala ya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika masuala yanayohusu uendelezaji na ukuzaji wa Viwanda na Biashara hapa nchini. Ili kuweza kufanikisha malengo yote yaliyotajwa Chuo kitakeleza jukumu la kuwaendeleza wakufunzi na wafanyakazi ili kufikia viwango vya juu vya kitaaluma, tija na kimaslahi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kuandaa mkakati wa kuendeleza Sekta binafsi nchini. Jukumu hili ambalo linasimamiwa na Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji linashirikisha Asasi na Taasisi mbalimbali za Serikali ikiwemo Wizara ya Viwanda na Biashara na Sekta Binafsi yenewe. Wizara yangu imejizatiti kutoa ushirikiano wa karibu kufanikisha azma hii ya kuendeleza Sekta binafsi hapa nchini. Tunaamini kwamba mkakati huu utakapokamilika na kuanza kutekelezwa kwa nguvu na kasi mpya utaleta mabadiliko makubwa katika uwezo wa ushindani wa Sekta binafsi ya nchi yetu. Katika zama hizi za uchumi wa soko na utandawazi, Sekta binafsi siyo injini tu ya ukuaji wa uchumi bali pia ni kiongozi wa shughuli zote za uchumi wa Taifa. Wizara yangu inalitambua hili na tutakeleza majukumu kwa namna na dhamira inayodhihirisha uelewa wetu wa uchumi wa soko katika mazingira ya utandawazi ambao aliyetangulia katangulia tu na aliyechelewa ndiyo kachelewa na kumfikia aliyetangulia inataka kiwango kikubwa cha juhud, maarifa na bidii iliyojikita katika sayansi na teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Kuwawezesha Wananchi Kushiriki Kikamilifu katika Shughuli za Uchumi imeshaandaliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na tayari imezinduliwa tarehe 19 Juni, 2004 wakati wa Mkutano huu wa Bunge la Bajeti. Nia hasa ya sera hii ni kuwawezesha Wananchi kwa kuwapatia mitaji kwa kutumia vyombo vya fedha vilivyopo na vingine vitakavyoanzishwa ili Wananchi waweze kuanzisha miradi mbalimbali ikiwemo ya viwanda na biashara ndogo na kati. Miradi hiyo inaweza kuanzishwa na Wananchi wenewe au kwa ubia na watu kutoka nje ya nchi. Wizara yangu imojiandaa, kupitia *NDC* na *SIDO*, kutoa ushauri wa kitaalamu na upembuzi yakinifu ya baadhi ya miradi ya wahusika ili kuwawezesha kupata mikopo kutoka katika Asasi za Kifedha.

Mheshimiwa Spika, zoezi la utekelezaji wa muundo mpya wa Wizara kama sehemu ya kuimarisha uwezo wake katika utendaji kazi linaendelea. Nafasi zilizoainishwa katika muundo zimekamilishwa na kujazwa hadi ngazi ya Wakuu wa Sehemu au Wakurugenzi Wasaidizi. Aidha, taratibu zinaendelea kuchukuliwa za kuajiri, kuwateua rasmi Maofisa waliopendekezwa kujaza nafasi mbalimbali katika muundo kwa kushirikiana na Idara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya mpango mahsus (*Strategic Plan*), unaojumuisha malengo ya uboreshaji utendaji, uwajibikaji na usimamizi wa raslimali na utumishi na utoaji wa huduma kwa umma yamekwisha kamilika. Hatua za utekelezaji zimeanza ikiwa ni pamoja na maandalizi ya uzinduzi rasmi wa Mkataba wa Wizara wa Huduma kwa Umma (*Client Service Charter*). Aidha, ukamilishaji wa zoezi la kuboresha utendaji kazi wa masijala ili kuimarisha mawasiliano ndani ya Wizara na kat

ya Wizara na Asasi nyingine za umma na Wananchi yamefikia hatua nzuri. Tayari mtandao wa kompyuta umekwisha kamilika kufungwa ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo ya matumizi yake kwa watumishi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Wizara itaendelea kushirikiana na Asasi mbalimbali kuboresha zaidi mazingira ya uzalishaji viwandani ikiwa ni pamoja na miundombinu, sera za fedha na kodi na kutenga maeneo maalum kwa ajili ya Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Lengo la hatua zote hizo ni kuhamasisha ufuluaji wa viwanda vingi zaidi, kukuza uwekezaji, kuongeza uzalishaji na tija ili kuifanya Sekta hii iweze kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele kitatolewa katika kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika Sekta za kipaumbele yaani sekta ndogo za nguo, ngozi na usindikaji wa mazao ya kilimo na vyakula. Mipango husika ni pamoja na: -

- (i) Kuendelea kutekeleza mkakati wa kuimarisha Sekta ndogo ya ngozi na viwanda vya ngozi kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo;
- (ii) Kuendelea na utekelezaji wa awamu ya pili ya *Intergrated Industrial Development Programme* kwa kushirikiana na *UNIDO*, inayolenga katika kuimarisha usindikaji wa mazao ya kilimo na chakula;
- (iii) Kuendelea na zoezi la ukusanyaji wa takwimu za viwanda kuwezesha uanzishaji mahsus wa Benki ya Takwimu ya Sekta (*Sectoral Data Bank*);
- (iv) Kutekeleza maamuzi yatakayofikiwa na Serikali baada ya kupokea ripoti za Sekta ndogo ya Viwanda vya Katani na hali ya biashara ya chuma chakavu;
- (v) Kufanya utafiti katika maeneo mengine yenyе matatizo yanayokwamisha maendeleo ya viwanda kwa kushirikiana na wadau husika;
- (vi) Kufuatilia utayarishaji wa sheria mpya za Taasisi za Huduma kama itabidi ili kuziwezesha kutekeleza majukumu mapya;
- (vii) Kufuatilia uwekezaji katika maeneo ya *Development Corridors* za Mtwara na Kati ikiwa ni pamoja na miradi ya mkaa wa mawe wa Mchuchuma na Chuma cha Liganga;
- (viii) Kuendelea kuhamasisha uanzishwaji wa maeneo ya *EPZ* na uwekezaji ndani ya maeneo hayo; na
- (ix) Kuongeza kasi ya kutekeleza Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, lengo la Wizara katika Sekta ya Biashara ni kuwa na mikakati itakayotuwezesha kama Taifa, kuhimili ushindani wa biashara Kimataifa na kutupa uwezo wa kushiriki na kufaidika na mfumo wa biashara ya Kimataifa katika zama hizi za utandawazi. Aidha, Wizara itaendelea kujenga uwezo kwa wazalishaji na wafanyabishara ili waweze kufaidika na masoko mbalimbali kama vile *EAC, SADC, AGOA, EBA, PACT* na kadhalika. Ili kutimiza lengo hili, Wizara katika mwaka 2004/2005 itajielekeza katika maeneo yafuatayo: -

- (i) Kuendelea kutekeleza Programu ya *Joint Intergrated Technical Assistance (JITAP)* na Programu ya *Intergrated Framework (IF)*, kwa lengo la kujenga uwezo wa Taifa katika kushiriki kwa manufaa zaidi katika majadiliano yanayofanyika sasa na kuongeza uwezo wa ushindani wa bidhaa zetu katika Soko la Kimataifa;
- (ii) Kuendeleza ushirikiano na Asasi za Kimataifa hasa *WTO, ITC, UNCTAD* na *UNIDO* kwa lengo la kudumisha mafanikio yaliyopatikana katika *JITAP* na *IF* awamu ya kwanza ili kutufikisha katika hali ya kujitegemea;
- (iii) Kushughulikia matatizo yanayosababisha tushindwe kunufaika na fursa za masoko ya nje (*Supply Constraints*);
- (iv) Kuongeza kasi ya kutekeleza Sera ya Taifa ya Biashara ya mwaka 2003; na
- (v) Kushiriki katika vikao vya *SADC* na *EAC* kwa lengo la kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi Kikanda;

Mheshimiwa Spika, lengo ni kufikia kiwango cha juu cha ukuzaji wa uchumi. Aidha, katika hatua za utekelezaji wa Sera ya Biashara sisi kama Taifa tutakutana na changamoto za kutatua matatizo ya msingi yanayosababisha uchumi na biashara kudumaa. Sera hiyo imebainisha nyenzo za kukabiliana na changamoto hizi hasa kodi na ushuru wa forodha, mbinu za kujihami kibiashara, vikwazo visivyo vya kodi wala ushuru wa forodha, makubaliano mbalimbali ya kibiashara ya Kikanda na Kimataifa na sheria kama vile Sheria ya *Anti -Dumping*.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara yangu yanapanuka kadri hali ya uchumi na biashara duniani inavyobadilika. Kwa mfano, Wizara yangu inatakiwa kuanzisha na kuendeleza maeneo maalum ya kutengeneza bidhaa za kuuza nje (*EPZ*). Katika utaratibu wa *EPZ*, Serikali inatakiwa kujenga na kuendeleza miundombinu katika maeneo hayo ili kuwavutia wawekezaji. Shughuli hizi zinahitaji pesa nyingi. Mathalan, *Millenium Bussiness Park* iliyoko Ubungo, Dar es Salaam ambayo imejengwa na wawekezaji binafsi inatakiwa inunuliwe na Serikali kwa Shilingi 16.3 bilioni ili kuwapa wawekezaji wengine fursa ya kuingia na kuwekeza ndani ya eneo hilo. Kwa upande wa *NDC*, wanahitaji Shilingi 691.2 milioni kwa ajili ya kuanza kujenga eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya asasi na taasisi zilizoko chini ya Wizara yangu pia ni makubwa na kwa kipindi kirefu sasa hazijaweza kupewa fedha za kutekeleza

majukumu yaliyokusudiwa ikiwa ni pamoja na kuendeleza teknolojia, kusimamia viwango, kuendeleza nishati mbadala na tafiti nyingine mbalimbali ambazo ni muhimu katika zama hizi za utandawazi. Maeneo mengine yanayohitaji fedha nyingi ni ushiriki wa Tanzania katika majadiliano (*negotiations*) mbalimbali yanayohusu masuala ya biashara na ushirikiano wa Kimataifa.

Kwa mfano, majadiliano ya *WTO*, *EU - ACP (EPA)*, *SADC*, *EAC* na kadhalika. Kwa hali hii, ni dhahiri kuwa ceiling ya Bajeti ya Wizara kama ilivyo katika Mwongozo wa Bajeti haiwezi kukidhi mahitaji haya. Ni matumaini yangu kwamba, fedha za kutosha zitapatikana kadri hali ya uchumi inavyozidi kuimarka na mapato ya Serikali kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuzishukuru nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa ambayo yamekuwa yakitoa misaada iliyoiongezea uwezo Wizara yangu wa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na tija zaidi. Napenda kuzishukuru nchi za Austria, Canada, China, Denmark, Finland, India, Japan, Marekani, Sweden, Uhlanzi, Uingereza, Ujerumanu na nchi nyingine ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara. Aidha, napenda kuyashukuru Mashirika ya *Sida*, *UNIDO*, *DANIDA*, *DFID*, *GTZ*, *NORAD*, *WTO*, *UNCTAD*, *USAID*, *UNDP*, *OPEC Fund*, *JICA*, *WIPO*, *ARIPO* na *ITC*. Nazishukuru pia Taasisi za Kimataifa za Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*) na *Commonwealth Fund for Technical Cooperation*, kwa misaada na michango yao ya fedha na utaalam katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hoja hii ni matokeo ya kazi nzuri na ushirikiano wa karibu nilioupati kutoka kwa wenzangu katika Wizara, Mashirika, Asasi, Taasisi na Makampuni yaliyo chini ya Wizara. Naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rita Mlaki Mbunge wa Kawe, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Katibu Mkuu, Bwana Ahmada Ngemera na watumishi wote wa Wizara, Mashirika, Makampuni na Taasisi zilizo chini ya Wizara, ambao wamehusika kwa namna moja au nyingine na maandalizi ya bajeti ninayoiwasilisha leo. (*Makof*)

Nazishukuru pia Jumuiya na Taasisi za Sekta binafsi, ikiwemo Jumuiya ya Wenye Viwanda (*CTI*), Jumuiya ya Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo (*TCCIA*) na *Tanzania Private Sector Foundation*.

Aidha, nazishukuru Taasisi zinazoshughulikia utafiti, hasa Kituo cha Utafiti wa Masuala ya Jamii na Uchumi (*ESRF*), Idara ya Utafiti wa Uchumi (*ERB*) na Kitivo cha Biashara na Menejimenti cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Sokoine na Chuo Kikuu cha Mzumbe kwa michango yao ya mawazo wakati wa mikutano, warsha, semina na makongamano mbalimbali kuhusu Sekta za Viwanda na Biashara hapa nchini. Ushirikiano huu ni muhimu katika kuendeleza na kuimarisha Sekta za Viwanda na Biashara. Natoa pia shukrani za dhati kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, kwa huduma muhimu ya kuchapa hotuba hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005, Wizara inaomba Sh.1,562,649,000/= kwa ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo ya viwanda na biashara. Kati ya fedha hizi, Sh.200,000,000/= ni fedha za ndani ambazo zitatumika katika shughuli za maendeleo katika Taasisi zilizo chini ya Wizara na Sh.1,362,649,000/= ni fedha za nje kutoka kwa wafadhili ambazo zitatumika kulipia tafiti za kitaalam na vifaa kwa miradi mbalimbali itakayotekelezwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza malengo na majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Wizara inaomba Sh.7,352,870,400/= kwa matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizi, kiasi cha Sh.3,015,809,400/= ni matumizi ya Wizara yenye na Sh.4,337,061,000/= ni ruzuku kwa Mashirika ya Umma yanayosimamiwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Wasemaji wanne wa mwanzo baada ya taarifa za Kamati na Kambi ya Upinzani kutolewa, watakuwa ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Abdullatif Hussein Esmail, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Mohamed Missanga na Mheshimiwa Halima Kimbau, wajiandae. Sasa namwita Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, atoe maoni ya Kamati yake. (*Makofî*)

**MHE. SALOME J. MBATIA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA:** Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Viwanda na Biashara katika mwaka wa fedha uliopita pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya Matumizi na Mapato ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Mwaka 2003/2004 na kutoa ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutimiza Masharti ya Kanuni ya 81(1), Toleo la 2004, naomba kumshukuru Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara na Wajumbe wa Kamati kwa ujumla, kwa kunipa heshima ya kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti, Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Omar Chubi, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Stephen Masaba Kazi, Mheshimiwa Margareth Bwana, Mheshimiwa Freeman Mboge, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Ali Sheha Mussa, Mheshimiwa Aisha Philipo Magina, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mheshimiwa Sumri A. S. Mohamed, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Nazir Karamagi na Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Uwekezaji na Biashara (*INTRA*), ilikutana Dar es Salaam tarehe 1 Juni, 2004 na tarehe 3 Juni, 2004 kuitia na kuchambua Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha wa 2004/2005. Katika kutekeleza jukumu hili, Kamati ilizingatia maeneo muhimu yafuatayo: Utekelezaji wa ushauri wa Kamati katika bajeti ya 2003/2004, Kamati ya Uwekezaji na Biashara ilitoa ushauri ufuatao kwa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004: Wizara iratibu na kusimamia Viwanda vilivyobinafsishwa, Wizara iweke Mikakati ya kukuza mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi, Soko la bidhaa za Viwanda Nchini liimarishwe, Wizara iimarishe taasisi zake za utafiti, hatua zichukuliwe kukuza ushirikiano kati ya Taasisi za Wizara na Taasisi nyingine za utafiti ndani ya nchi, Sheria na programu zinazolenga kuongeza mauzo ya bidhaa zetu nchi za nje zitekelezwe ipasavyo, Wizara iimarishe udhibiti wa ubora wa bidhaa, Sheria ya ajira viwandani isimamiwe na kutekelezwa na Wizara iipitie upya Sheia ya Biashara ya Mwaka 1972. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Uwekezaji na Biashara, imesikitishwa na utekelezaji usioridhisha wa ushauri wake kutokana na Wizara hii kupewa fedha kidogo ukilinganisha na majukumu yake pamoja na taasisi zake. Aidha, Kamati imebaini kuwa kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya kuendeleza Taasisi za Utafiti za Wizara pamoja na Programu Maalum za kukuza mauzo ya bidhaa zetu nchi za nje kama vile *Export Processing Zones (EPZ)*, kimebaki kama ilivyokuwa mwaka wa fedha uliopita. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, maelezo kuhusu mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2003/2004. Kamati ilielezwa kuwa katika Mwaka wa Fedha 2003/2004, Serikali ilitarajiwa kupata jumla ya Sh.3,000,000,000/= kutokana na utoaji wa leseni za biashara zinazosimamiwa na Wizara. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2004, kiasi cha Sh.2,627,434,000/= kilikuwa kimekusanywa sawa na asilimia 87.6 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi ya Wizara katika kipindi cha 2003/2004, Wizara ilitengewa jumla ya Sh.6, 607,176,600/= kwa matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo Sh. 2,401,545,040/= ni matumizi ya kawaida kwa Wizara, Sh.3, 863,152,948/= ni ruzuku kwa Mashirika ya Umma yanayosimamiwa na Wizara na Sh.342, 458,612/= ni mishahara ya Wafanyakazi. Aidha, hadi kufikia mwezi Aprili,

2004 ,Wizara ilikuwa imepokea na kutumia Sh.5,460,940,640/= sawa na asilimia 82.6 ya fedha zilizotengwa katika Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za Matumizi ya Maendeleo, katika Mwaka wa Fedha 2003/2004, Wizara ilitengewa jumla ya Sh.200, 000,000/= fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, kati ya hizo Sh.150,000,000/= zilitengwa kwa ajili ya Shughuli za Maendeleo katika taasisi zinazosimamiwa na Wizara na Sh.50, 000,000/= zilitengwa kwa ajili ya kuendeleza Programu ya EPZ. Hadi kufikia Aprili, 2004 kiasi chote cha fedha kilichotengwa kilikuwa kimetolewa kwa shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2004/2005, kwa mara nyingine tena Wizara imetengewa kiasi cha Sh.200,000,000/=fedha za ndani kama ilivyokuwa mwaka 2003 kwa ajili ya Maendeleo. Aidha, Sh. 50,000,000/= zimetengewa NDC kwa ajili ya kuendeleza Programu ya EPZ na Sh.150,000,000/= zimetengewa Taasisi za Wizara kama vile TEMDO, CAMARTEC, TIRDO, BET, TBS na kadhalika ambazo kimsingi kazi zake ni utafiti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Viwanda na Biashara ndiyo Sekta pekee yenye fursa nzuri ya kuinua na kujenga uchumi imara na wa kisasa katika zama hizi za utandawazi na soko huria. Bajeti ya maendeleo inayotengewa Wizara ya Viwanda na Biashara, haitoi matumaini na inapingana na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya kufikia maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha kati (*Semi-industrialized Economy*) ifikapo 2025. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mafanikio na matatizo yaliyojitekeza katika utekelezaji wa malengo ya Wizara katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Kamati ilielezwa kuwa Wizara ilipata mafanikio yafuatayo kwa mwaka wa 2003/2004:-

- Utekelezaji wa Sera Endelevu ya Viwanda (*Sustainable Industrial Development Programme - SIDP*) kuanzia mwaka 1996-2020.
- Kukamilika kwa uandaaji wa Sera ya Viwanda na Biashara ndogo ndogo (*Small and Medium Enterprise Policy*).
- Kuongezeka kwa Uwekezaji katika Sekta ya Viwanda chini ya Mpango maalum wa kuzalisha kwa ajili ya mauzo Nje (EPZ). Viwanda vilivyoanishwa chini ya Mpango wa EPZ kuanza kazi ni pamoja na *NIDA Textiles Mills Ltd.*, *Star Apparel (T) Ltd.*, *Reclaimed Appliances (T) Ltd* na *African Pride Textile Mills Ltd.*
- Uimarishaji wa Taasisi za Huduma za Teknolojia na Utafiti kwa Sekta ya Viwanda kama vile TIRDO, CAMARTEC na TEMDO.
- Utekelezaji wa mkakati wa kuongeza Mauzo Nje (*Export Development Strategy*) ikiwa ni pamoja na kuanzisha Maeneo Huru ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje unaosimamiwa na Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Wizara inakabiliwa na matatizo ya Ufinyu wa Bajeti ya Serikali, uwezo mdogo wa kiutendaji na uchache wa Watendaji na Serikali kutotoa fedha za Matumizi ya Kawaida kwa Taasisi za Utafiti.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia na kuchambua kwa makini Mpango na Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2004/2005, Kamati inatoa ushauri ufuatao ili kuboresha utendaji wa Wizara. Fedha kidogo zinazotengwa na Serikali kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo ya Taasisi za Wizara.

Kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo, Serikali imekuwa ikitenga fedha kidogo sana kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo ya Taasisi za Wizara. Aidha, Serikali imetenga Sh.150,000,000/= tu fedha za ndani kwa ajili ya kugharamia shughuli za Taasisi za Wizara. Vile vile, Serikali imetenga Sh.50,000,000/= tu kwa *NDC* kwa ajili ya kugharamia shughuli za uanzishaji wa *Export Processing Zones - (EPZ)*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, fedha hizi ni kidogo sana hasa ukizingatia kuwa Taasisi za Wizara hii zinajihuisha na utafiti ambao huhitaji fedha za kutosha na kuchukua muda mrefu. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha wa 2004/2005, Kituo cha Uenezaji wa Teknolojia Rahisi Vijijini (*CAMARTEC*), kimetengewa Sh.10,000,000=, Shirika la Maendeleo na Utafiti wa Viwanda (*TIRDO*), limetengewa Sh.20,000,000= na Shirika la Ubunifu wa Mitambo (*TEMDO*), limetengewa Sh.10,000,000= tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kiasi hiki kidogo cha fedha kinazifanya taasisi hizi kushindwa kutekeleza majukumu yao na hivyo kuviza taaluma za Wataalam wa Mashirika hayo. Kwa mantiki hiyo, Kamati inashauri Serikali kuyapatia fedha za kutosha Mashirika hayo ili yatekeleze majukumu yao. Aidha, Serikali iangalie uwezekano wa kuunganisha shughuli za mashirika hayo ili kuyaongezea nguvu kifedha, kitaalam na kinyenzo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, utafiti, ni mojawapo ya majukumu ya msingi ya Serikali. Hii inatokana na ukweli kuwa, hakuna mfadhili yeoyote atakayekuwa tayari kugharamia utafiti. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa utafiti katika kuleta maendeleo kwenye sekta zote, Kamati inashauri Serikali kushughulikia suala hili kisera ili taasisi mbalimbali zinazojihuisha na utafiti ziweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyopo kwenye Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara (*Mtwara Development Corridor*) unaosimamiwa na *NDC* unakwenda kwa kasi ya kusuasua. Hii inatokana na ukweli kuwa, Kamati za Mashauriano mionganoni mwa Nchi Wanachama, zimekuwa hazikutani kwa muda mrefu sasa. Kwa mfano, Mkutano wa Kamati ya Mashauriano ya Kitaifa (*National Consultative Committee Meeting*), ulifanyika mara ya mwisho tarehe 5 Agosti, 2000. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuanzisha Tume ili kuleta uwajibikaji wa karibu katika usimamizi wa utekelezaji wa miradi iliyopo katika Ukanda

wa Maendeleo wa Mtwara na Ukanda wa Maendeleo wa Kati (*Central Development Corridor*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Biashara cha London kikiimariswa kitasaidia kutangaza bidhaa za Tanzania nchi za Ulaya na kuvutia Wawekezaji. Hata hivyo, kituo hicho kimekuwa kikitengewa fedha kidogo, hali inayosababisha kisitekeleze majukumu yake ipasavyo. Kwa mfano, katika Mwaka huu wa Fedha, kituo hiki kimetengewa Sh.226,800,000/=.

Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kukipa fedha za kutosha ili kiweze kutangaza bidhaa za Tanzania na kuvutia wawekezaji. Aidha, Wizara zinazohusika na kituo hicho, yaani Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Utalii na Maliasili, Ushirika na Masoko na Kilimo na Chakula, zichangie fedha ili kuimarisha kituo hicho. Vilevile, Serikali irudishe utaratibu wa *Foreign Exchange Rate Equalization* ili Hazina iweze kufidia hasara inayotokana na kushuka kwa thamani ya shilingi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Uwekezaji na Biashara ilipata fursa ya kutembelea Kituo cha Ubungo cha kutengeneza bidhaa kwa ajili ya kuziwa kwenye soko la Amerika chini ya Mpango wa *AGOA*. Kituo hicho ambacho kimejengwa kwa gharama ya Sh.14 bilioni, ni fursa muhimu katika mkakati wa kukuza mauzo ya bidhaa zetu chini ya *EPZ* na *AGOA*. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kukinunua kituo hicho ili mwekezaji aendelee na ujenzi wa vituo kama hivyo katika sehemu nyingine. Aidha, Serikali ichukue hatua za dhati kupunguza matatizo ya upatikanaji wa umeme, maji na miundombinu ya kiuchumi ili kuvutia wawekezaji wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, uimarisaji wa asasi za udhibiti na uangalizi wa Biashara, hivi karibuni Bunge lako Tukufu limepitisha sheria kadhaa zinazolenga kudhibiti na kuweka uangalizi kwenye Biashara hapa nchini. Baadhi ya Sheria hizo ni Sheria ya Ushindani wa haki ya mwaka 2002 (*Fair Competition Act, 2002*) na Sheria ya kukabiliana na bidhaa kutoka nje ya nchi zinazouzwa kwa bei ya chini kwa makusudi ya mwaka 2003 (*The Anti-Dumping Act, 2003*).

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa vyombo vya udhibiti na uangalizi vilivyoundwa chini ya Sheria hizo vinawezeshwa ili vitekeleze majukumu yake ipasavyo. Aidha, Serikali iwahamasishe na kuwaelimisha wadau na Wananchi kwa ujumla, juu ya maudhui ya sheria hizo ili washiriki katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Viwanda na Biashara ni kichocheo cha kukuza maendeleo ya uchumi wa kisasa hususan katika kipindi hiki cha ushindani wa kibashara na soko huria. Aidha, Sekta hii ikiimariswa mchango wake katika Pato la Taifa, utaongezeka na hivyo kuchangia uboreshaji wa Sekta za Jamii kama Elimu, Afya, Maji na kadhalika, ambazo tayari ziko katika Sekta za kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, Kamati inaishauri Serikali kujumuisha Sekta ya Viwanda na Biashara kwenye awamu ya pili ya mkakati wa Taifa wa kuondoa umaskini (*PRSP II*), unaoandaliwa hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, usimamizi na uratibu wa viwanda vilivyobinafsishwa, kazi ya kubinafsisha Mashirika ya Umma na Viwanda iliyoanza mwanzoni mwa miaka ya 1990, imeleta mafanikio ya kuridhisha. Hata hivyo, baadhi ya viwanda vimetelekezwa na waliovinunua. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuongezea Wizara ya Viwanda na Biashara, jukumu la kuwanyang'anya Wawekezaji Wababaishaji Viwanda hivyo mbali na kazi ya usimamizi ambayo tayari Wizara hii ilishapewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Uwekezaji na Biashara ilitembelea Maonesho ya 28 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam yaliyofanyika Mwezi Julai, 2003. Kamati inapongeza mwitikio wa Wafanyabiashara na ubora wa bidhaa kwenye maonesho hayo. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa Maonesho hayo yasiwe sehemu ya kufanya biashara na kuuza bidhaa tu, bali yalenge kuvutia na kuhamasisha uwekezaji halisi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara na Wajumbe wa Kamati hii, naomba kuchukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Waziri wa Viwanda na Biashara na Mheshimiwa Rita Louise Mlaki, Naibu Waziri wake, kwa ushirikiano walioipa Kamati hii wakati inachambua Bajeti ya Fungu 44, Wizara ya Viwanda na Biashara. Aidha, nawapongeza Watendaji wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Ahamada Ngemera, kwa kazi nzuri ya kuandaa mpango wa Bajeti hii. (*Makofi*)

Naomba pia kwa namna ya pekee, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, kwa ushirikiano na umakini wao wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara hii. (*Makofi*)

Mwisho, namshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Kipenka Mussa na Katibu wa Kamati hii, Ndugu Daniel Eliufoo, kwa kuhudumia Kamati hii ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi uliofanywa na ushauri uliotolewa na Kamati, Kamati imekubaliana na Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha wa 2004/2005. Kiasi cha fedha kinachoombwa na Wizara chini ya Fungu 44 ni Matumizi ya Kawaida, Sh.7,352,870,400/=, Matumizi ya Maendeleo Sh.1,562,649,000/=, Jumla Sh.8,915,519,400/=.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. ADELASTELA E. MKILINDI (k.n.y. MHE. FREEMAN A. MBOWE - MSEMADI MKUU KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA):** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani,

kuhusu Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5) (b) (c) na 81(1), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuungana na wenzangu kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo langu la Hai, kutoa rambirambi zetu za dhati kabisa kwa Wananchi na familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, kwa msiba mkubwa wa kuondokewa na aliyekuwa mpendwa Mbunge wao. Mwenyezi Mungu, amlaze Marehemu mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, pamoja na Naibu wake, Mheshima Rita Mlaki, pamoja na watumishi wote walioshiriki kufanya kazi hii ya kuandaa bajeti ya Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kiasi cha jumla ya Tshs. 8,915,519,400/= ambazo Wizara imeomba katika kipindi cha bajeti ya 2004/2005 ni kidogo mno ukilinganisha na majukumu ambayo Wizara hii inapaswa kuyatekeleza. Haitoshi kwa Serikali kuendelea kuimba tu kuhusu umuhimu wa sekta ya Biashara na Viwanda katika kukuza Pato la Taifa bila ya kutoa nyenzo na uwezo wa kufanya kazi. (*Makofi*)

Kambi ya Upinzani inadhani kuwa, Serikali imejitoa katika sekta hii ya viwanda labda ndio sababu kubwa ya kutotenga fedha za kutosha katika Wizara hii. Hili ni kosa kubwa sana ambalo Serikali inalifanya, kwani kama Taifa letu lina nia kweli ya kuendelea, basi kilimo na viwanda ndizo sekta za kuleta mabadiliko na hususan *vision* ya Taifa ya 2025 ya kuondoa umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Viwanda katika nchi yetu bado hajafanikiwa kukidhi lengo kama ambalo Mwasisi wa nchi hii, alivyokuwa amekusudia kwa manufaa ya Watanzania wote. Tunasema hivi kwa kuangalia takwimu za uchangiaji kwenye Pato la Taifa (*GDP*), kisekta kama ilivyo oneshwa kwenye jedwali la I ukurasa wa 9 kwenye kitabu cha hali ya uchumi, kipindi cha miaka kumi iliopita tangu nchi yetu iingie kwenye utandawazi na ubinafsishaji. Sekta hii ya viwanda imekuwa haikui, *percentage change after conversion into US\$* inaonesha mwaka 1995 kulikuwa na asilimia 17.9, mwaka 1996 kulikuwa na 17.2%, mwaka 1997 ilikuwa 10.7%, mwaka 1998 ilikuwa ni 21.9%, mwaka 1999 kulikuwa na 0.8%, mwaka 2000 kulikuwa na 7.4%, mwaka 2001 kulikuwa na 3.2%, mwaka 2002 kulikuwa na 2.5% na 2003 kulikuwa na 3.6%.

Mheshimiwa Spika, kutokukua kwa sekta hii ya viwanda kunatokana na dhana au fikra ya Serikali ya kuamini kuwa mtu anaye fungua kiwanda basi ni tajiri na anajitosheleza kwa kila kitu. Kufungua au kuwa na kiwanda ni jambo moja na kukifanya kikidhi lengo la kuanzishwa kwake ni jambo lingine ambalo Serikali inatakiwa iwepo na iweke mkono wake wa kuhakikisha linafanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kujitoa kwa Serikali katika sekta ya viwanda kiundeshaji ni jambo la muhimu na Kambi ya Upinzani, tunalikubali lakini kuhakikisha kuwa sekta hii inafanya kazi kwenye mazingira yatakayoifanya itimize lengo la uanzishwaji wake

ndicho kitu ambacho Serikali inatakiwa ikifanye, kama vile kuhakikisha upatikanaji wa mali ghafi nchini unakuwa kwa manufaa ya mzalishaji na mnunuzi, kutenga maeneo maalum ya uzalishaji bidhaa kwa ajili ya masoko ya nchi za nje ni bora yangefanyiwa utafiti ili yawekwe sehemu ambazo upatikanaji wa malighafi zake ni rahisi, kitu ambacho kingewahamasisha wazalishaji kuongeza uzalishaji wake kwani bei zingenufaisha pande zote mbili. Mfano, viwanda vya nguo kwa ajili ya soko la nje ni vizuri vingejengwa maeneo ambayo pamba inazalishwa kwa wingi hapa nchini badala ya kujengwa Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka huu wa 2004/2005, Wizara imetenga kiasi cha Sh.1,440,649,000/= kati ya hiyo pesa za ndani ni Sh.200,000,000/= kwa ajili ya shughuli za Maendeleo. Fedha za ndani zilizotengwa ni kwa ajili ya Taasisi za Utafiti za *TIRDO*, *TEMDO*, *CAMARTEC*, *TBS* na kadhalika. Vile vile kwa ajili ya *NDC*. Hapa inaonesha kuwa fedha nyingi kwa ajili ya utafiti na maendeleo tunategemea kuzipata kutoka kwa Wafadhili wa nje. Ni kweli hali ya sasa, mfumo wa biashara ni tofauti na mfumo wa zamani ambapo soko lilitua linatafuta bidhaa. Kwa sababu ya utandawazi hivi sasa mfumo unaotawala ni wa bidhaa kutafuta soko (*Sellers Market*). Katika hali hiyo bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu lazima ziwe na ubora wa kushindana na bidhaa zinazozalishwa na Mataifa mengine, ili bidhaa ziweze kushindana kwenye soko lazima ziwe zimefanyiwa utafiti wa kutosha. Ndiyo maana tunaitaka Serikali iwekeze kiasi kikubwa cha fedha kwenye taasisi zetu za utafiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hali ya kawaida, mtu ambaye anashindana na mwenzake sijui kama anaweza kumpa mbinu za kumwezesha kumshinda, tusitegemee wafadhili waendeleze tafiti nchini ambazo zitasababisha kuboresha bidhaa zetu na kushindana na za kwao. Tafiti watakazopendelea kuzipatia fedha ni zile zenye manufaa kwa ajili ya mambo yao tu waliyoyalenga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuangalia umuhimu wa taasisi hizi kwa maendeleo ya sekta ya viwanda na biashara, bado bajeti hii ni ndogo mno kwa ufanisi wa sekta nzima. Kazi ya utafiti na uendelezaji (*research and development*), ni kazi nzito na ni ya umuhimu kama kweli tuko makini na maendeleo ya nchi yetu.

Kambi ya Upinzani ina wasiwasi mkubwa kuwa, kutokana na kutokuzingatiwa na kupewa umuhimu kwa taasisi hizo, ndio sababu baadhi ya viwanda vyetu vilivyobinafsishwa vinaacha kuzalisha bidhaa zilizokuwa zikizalishwa awali na kuanza kufanya biashara nyingine tofauti na pengine kuanza kukodisha maghala yake kwa makampuni mengine. Mfano ni Kiwanda kilichokuwa kinatengeneza Viatu cha Bora. Uuzwaji wake umesababisha kuua Shirika la Viwanda vya Ngozi na viwanda vingine vya ngozi. Wazalishaji wa ngozi wameendelea kukosa soko la ndani la bidhaa hiyo kwani Kiwanda cha Bora tangu kiuzwe hakijawahi kutengeneza chochote mpaka sasa zaidi ya *rubber products*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaishauri na kuikumbusha Serikali kuwa, hakuna nchi hata moja duniani ambayo imeendelea kiuchumi, kibiashara, kwa kilimo na viwanda, bila

kutumia vizuri na kuboresha taasisi zake za utafiti na maendeleo (*Research and Development Agencies*), Serikali haina budi kufanya kila iwezalo kuimarisha taasisi hizi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa, *TIRDO* ambayo iliundwa na Sheria ya Bunge Na. 5 ya 1979 na kuanza kazi rasmi tarehe 1 Aprili, 1979, ilikuwa na lengo la kufanya utafiti ambao ungesaidia viwanda vyetu kutumia malighafi zipatikanazo hapa nchini, aidha teknolojia na utaalum utakaosaidia viwanda hivyo kuzalisha bidhaa zenyne uwezo wa kushindana hapa na kwenye masoko ya nje. Kwa sababu hizi tunaona na tunaishauri Serikali kuwa, *TIRDO* ndio wapewe jukumu la kufanya utafiti na kupendekeza uanzishaji wa maeneo huru ya uzalishaji kwa mauzo ya nje (*EPZ*). Hivyo, wangeongezewa nguvu kifedha kuhakikisha wanakuwa na wataalam wa kutosha kufanya utafiti kulingana na ukubwa wa nchi yetu na malighafi zipatikanazo hapa nchini. Bado nchi yetu ina rasilimali kubwa sana na nyingi ambazo bado hazijawa *exploited*. Umaskini wetu bado unasababishwa na kutopanga mipango yetu vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa, Tanzania ina wafanyabiashara wengi wazuri na ambao kutoptera na utandawazi, wanawenza kufanya biashara nje ya nchi. Kitu ambacho kinasumbua ni sheria na kanuni zetu zinazohusu biashara ya nje, hivyo tunaiomba Serikali iangalie sheria na kanuni hizo upya ili Watanzania waweze kunufaika na utandawazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, itabidi tukubaliane kuwa Watanzania huko nyuma hatukukuzwa kwenye maadili na hulka ya kibiashara, hivi sasa tumeingia na inatulazimu kushindana kwenye Jumuiya za watu ambao wao ni wafanyabiashara wa miaka mingi, wamelelewa na kukulia kwenye biashara. Wanachama waliomo kwenye ushirikiano wa Jumuiya ya nchi za Afrika ya Mashariki, utakuta Viongozi wake na Watendaji Wakuu Serikalini wote ni wafanyabiashara. Hapa ndipo wanapotuzidi kete na kuchukua nafasi kubwa zaidi kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi. (*Makofî*)

Hapa kwetu watendaji wengi Serikalini hawana *background* ya biashara, wengi ni wakiritimba, kitu kinachosababisha ukwamishaji wa kutoa maamuzi ya haraka kwenye masuala yahusuyo biashara. Mfano, wenzetu wa Uganda, Soko la *AGOA* wamelitumia vizuri sana na wengi limewanufaisha, kwa nini Tanzania bado wafanyabiashara wetu hawajanufaika nalo ingawa nchi yetu ina bidhaa nyingi za kuuza kuliko wenzetu?

Katika biashara wa kwanza kulikamata soko ndio wanaonufaika zaidi, hivyo, *timing* kwenye maamuzi ni muhimu sana, vinginevyo Tanzania itaendelea kupewa sifa kubwa ya kuwa mabingwa wa kutengeneza sera nyingi nzuri, zisizokuwa na misingi ya utekelezaji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa miezi ya karibuni tumekuwa tukisoma na kuona kwenye vyombo vyaya habari, ujio wa wafanyabiashara toka Mataifa kama, Denmark, German, Uingereza kuititia Balozi zao wanakuja kuangalia na kutafuta masoko ya bidhaa zao hapa kwetu. Tunamtaka Waziri alieleze Bunge, ni wafanyabiashara wangapi wameishakwenda

nje kuitia utaratibu wa Mabalozi wetu au ofisi zetu za Kibalozi na kati ya hao ni wangapi na kwa kiwango gani wamefanikiwa kufanya biashara na nchi hizo?

Tunaitaka Serikali chini ya Sera mpya ya Mambo ya Nje iliyozinduliwa hivi karibuni, iweke malengo kwa wawakilishi wetu walioko nchi za nje kuhusu biashara wanazopaswa kuzifutilia na Ubalozi unatakiwa kufanya nini ili kuhakikisha wafanyabiashara wa Tanzania wanajipenyeza kwenye nchi walizomo.

Suala la nchi yetu kuingia mikataba chungu nzima halitasaidia chochote endapo Mikataba hiyo haimletei Mtanzania mapato. Itabakia ni hadithi ile ile ya “kufunga mwatufunga lakini chenga twawala”. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Balozi zetu huko nje ni mara chache sana zimeandaa wafanyabiashara wetu kufanya ziara za makusudi kwenye nchi za nje kutangaza na kukutana na wanunuzi mbalimbali wa bidhaa za Tanzania. Imeshatokea mara chache, msafara wa Rais nje ya nchi umeondoka na Wafanyabiashara wa ndani. Lakini kinachoonekana, ni Balozi zetu huko nje hazifahamu ni bidhaa gani zinatengenezwa au kupatikana nchini na kwamba ni zippi zingeweza kuuzwa katika nchi wanazoziwakilisha. Tunazitaka Balozi zetu ziwe na ufahamu thabiti wa bidhaa tunazozalisha na wazifanyie *marketing* huko waliko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kazi za Balozi zetu kwa kiasi kikubwa ziwe ni pamoja na kufanya *marketing* ya bidhaa zetu. Balozi atakayefaulu katika hili apewe tuzo na kupongezwa. Kama Balozi atashindwa kufanya kazi ya kuwaunganisha wafanyabiashara wa Tanzania ili watumie soko la nchi aliyopo, basi hiyo ni dhahiri atakuwa ameshindwa kuiwakilisha Tanzania nchi za nje na ni vyema akarejeshwa nyumbani haraka. Ukiangalia biashara kati ya Tanzania na Kenya au Afrika ya Kusini, utaona Kenya wanaauza zaidi bidhaa zao hapa nchini kuliko tunavyouza kwao. Hii inatokana na Balozi za nchi hizo kuwasaidia wafanyabiashara wao kutangaza zaidi bidhaa zao, pia kutokana na kuweka wazi anwani na mahali kunakopatikana bidhaa hizo, yaani *contacts*.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumekuwa tukielezwa, kilimo kinatoa mchango mkubwa katika Pato la Taifa. Ni mara nyingi huwa kuna maonesho na makongamano ya biashara ya mazao ya kilimo kwenye nchi zilizoendelea na Tanzania huwa inashiriki. Cha ajabu ushiriki wa Tanzania huwa kwa kiasi kikubwa ni wa watunga sera! Wafanyabiashara katika Sekta hiyo ya mazao ya kilimo wataipata wapi *Exposure* na *Contacts* za watu wanaojihusisha na biashara hiyo kwenye Soko la Dunia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali ijaribu kudhibiti watendaji wake waache kuhudhuria maonesho na makongamano yahusuyo biashara na kuwaacha wahusika nyuma, hiyo ni kuwapotezea *opportunities* wafanyabiashara na nchi kwa ujumla kwa ajili ya ubinafsi usio na faida. Mara kunapotokea makongamano na maonesho kama haya, Serikali itoe nafasi zaidi na msaada kwa wafanyabiashara na viongozi wa vyama vyao kama *TCCIA*, *CTI* na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, biashara katika sekta isiyo rasmi au machingira, kama itapewa umuhimu na kuwekewa mazingira ambayo wafanyabiashara hao watajiona na wao ni sehemu ya uchumi wa Taifa lao, inaweza kuwanufaisha wahusika na Serikali pia, tofauti na ilivyo sasa ambapo wengi wamekuwa na uadui mkubwa na Serikali kutokana na kutokuwa na utaratibu unaoeleweka. Uwekaji na utekelezaji wa mipango inayowahusu huwa ni ya upande mmoja wa Serikali na wao amba ni wahusika hawapewi nafasi ya kutoa mawazo yao ni jinsi gani wangependa biashara zao ziendeshwe na katika mazingira ya namna gani.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuiangalia upya na kuweka motisha zaidi kwenye sekta hii isiyo rasmi kwani idadi kubwa ya Watanzania wafanyao biashara wako kwenye sekta hii na kama mapato yao yatakusanywa vizuri, basi umuhimu na mchango wao utajionyesha wazi katika maendeleo ya Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, uimarishaji soko la bidhaa za viwandani nchini, hapa ndipo sehemu mwafaka kwa Serikali kuingilia kati na kutoa mwongozo kwani bidhaa zinazozalishwa hapa nchini zinakuwa na bei kubwa kuliko zinazotoka nchi za nje. Viwanda vyetu mara zote hulalamikia ughali wa malighafi pamoja na kutoaminika kwa maji na umeme. Malighafi huwa ghali ingawa zinazalishwa hapa kwetu lakini tukiangalia bei wazipatazo wazalishaji wa bidhaa hizo ni ndogo, sasa Serikali ndio watueleze huo ughali wa bidhaa hizo unatokea wapi na kwa nini malighafi zinatozwa kodi nyingi na hivyo kuzifanya ziwe ghali? Kama ndiyo hivyo kuna mpango gani wa kupunguza au kufuta kabisa kodi hizo? Mfano, pamba inaonekana kuwa na kodi nyingi mno, kodi ya elimu asilimia tano, *District*, pembejeo na kadhalika. Hizi kodi zinafanya pamba kama malighafi ziwe ghali bila sababu. (*Makof*)

Kambi ya Upinzani inaamini kabisa, Serikali ikishaangalia kwa makini na kuondoa matatizo yanayosababisha viwanda vyetu kuzalisha bidhaa kwa gharama za juu, bei ya bidhaa hizo haitakua juu ukilinganisha na bidhaa zitokazo nje. Hapo soko la ndani litaimarishwa kwani soko lipo na bado kabisa linahitaji bidhaa isipokuwa bei ya bidhaa zenyewe ndio inalifanya lishindwe kukua.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya jumla, wafanyabiashara wengi wamepokea kwa furaha uamuzi wa Serikali wa kufuta au kupunguza ada za leseni za biashara na pia kuweka utaratibu mpya wa kukata leseni. Kambi ya Upinzani inaipongeza Serikali kwa hatua hizo lakini tungemwomba Mheshimiwa Waziri, atufafanulie mambo yafuatayo kwa misingi ya kutafuta kuelewa:-

(i) Kwa vile leseni ya biashara itakuwa ikitolewa mara moja (*once and for all*), utaratibu wa udhibiti utakuwa wa namna gani, wafanyabiashara wasio raia si wataweza kufanya biashara wasizoruhusiwa na wengine kufanya biashara haramu? Je, utaratibu huu utajumuisha na leseni nyingine zitolewazo na kuwa *renewable* kila mwaka au kwa kipindi fulani, mfano, Leseni za Magari, *Driving Licence*, Leseni za Kuuza Dawa nakadhalika, kama sio, ni kwanini zitofautishwe? (*Kicheko*)

(ii) Kwa vile *turnover* ya mfanyabiasha mpya asiye na leseni inakuwa haijajulikana, ni kwa vipi *turnover* yake itajulikana hata kama imefikia au kuzidi shilingi milioni 20? (*Makofi*)

(iii) Kwa vile leseni huwa ni *Non-Transferable*, Serikali katika utaratibu wa kukata leseni moja kwa moja imetayarisha utaratibu gani wa kuepusha tatizo la kurithishana leseni kati ya mtu na mtu?

(iv) Kwa vile leseni za vileo ziko chini ya Sheria tofauti, je, nazo zinaingia katika utaratibu huo huo mpya?

(v) Kwa vile Sheria ya Leseni ya Mwaka 1972 inaonekana kukabiliwa na mabadiliko makubwa, ni vyema Serikali ikaifanyia marekebisho ya jumla badala ya kupachika viraka ambavyo vinaji-*contradict* sehemu nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa vile Serikali imenuia kuwasaidia wafanyabiashara na kuwaondolea urasimu usiokuwa wa lazima, ni vyema Serikali ikawaruhusu *exporters* na wale wazalishaji wakubwa waliopo mikoani kuruhusiwa kukata leseni zao katika Mikoa au Wilaya wanakotoka ili kupunguza gharama ya mwananchi kufuata leseni Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mwisho, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa kwa vile kumekuwepo mabadiliko makubwa ya Sera na taratibu za biashara ni vyema kukawepo mpango wa maksudi wa kuyafikisha mabadiliko hayo kwa Wananchi ili wayaelewe na kuyatekeleza.

Wizara iziwezeshe Halmashauri katika suala zima la kutoa elimu na ufahamu wa mabadiliko hayo na kuhamasisha Wananchi hasa katika uanzishaji wa viwanda vidogo vya kusindika mazao. Ni kwa njia hiyo pekee, hata huo utafiti unaofanywa na Taasisi mbalimbali utakuwa ni wa manufaa kwa Wananchi wetu. Kwa vile hivi sasa Sekta ya Biashara inatoa ajira kwa vijana wengi wa elimu ya chini, ni wakati muafaka hata mitaala ya Elimu ya Msingi ikawekewa somo la ufahamu wa jumla wa Elimu na mbinu za kibashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. ABDULLATIF H. ESMAIL:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa, nampongeza Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Juma Ngasongwa, pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Rita Mlaki na vile vile Watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Ahmad Ngemera, kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kutuletea Bajeti hii, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kuhusu EPZ. NDC imepewa shilingi milioni 50 mwaka 2003 na mwaka huu wa 2004 itapewa shilingi milioni 50. Labda imemaliza kazi nyingi, imebakiza kazi kidogo, lakini ukiangalia EPZ bado kuna viwanda

kama vinne tu vilivyosajiliwa pale. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa *NDC* isaidiwe zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ningependa Mheshimiwa Waziri, anifahamishe kwa nini Viwanda vilivyosajiliwa *EPZ* ni vya *Textile*? Kwa nini viwanda vikubwa kwa mfano vya kubangua korosho au mazao mengine ya kusindika, havisajiliwi katika *EPZ*? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuongeza ajira kwa juhudzi zake kwa asilimia 15.2 mwaka huu. Naipongeza sana. Pia naipongeza kuhusu mauzo ya bidhaa za nje kutoka Dola milioni 66 mpaka Dola milioni 100. Hizi ni bidii za Wizara yenyewe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna gharama kubwa za uzalishaji hasa umeme na Wizara imeahidi kwamba, inashughulikia tatizo hili, ni matarajio yangu kwamba, Wizara itajitahidi kuhakikisha kwamba, umeme unapungua gharama zake ukilinganisha na nchi za jirani ambao watakuwa mbele sana kama tutaendelea na gharama hizi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushindani wa soko la nje na ndani, mimi nasema, bila ya mashindano huwezi kuendelea. *Competition is the only thing that make two parts, one of the part grow up and one remain behind* na yule aliyekuwa nyuma atajitahidi afike mbele. Utandawazi una athari kubwa kama Mheshimiwa Waziri alivyotueleza. Mimi namnukuu Rais Benjamin William Mkapa, juzi alipokwenda Ethiopia alisema: "Wakoloni wametutenganisha kwa mipaka ya kijinga kabisa. Amesema kwamba Afrika ndio mnyonge wa dunia ya utandawazi. *Globalization* ni treni ambayo sisi kasi yake hatuwezi". Lakini kama alivyo sema Mheshimiwa Waziri kwamba, tumeshajijengea ukuta hatuwezi kutoka.

Ukiangalia katika Maonysho ya Kimataifa ya 28 yaliyofanyika hivi karibuni Dar es Salaam, biashara iliyofanywa ya uagizaji ni kubwa mara mbili au mara tatu na biashara iliyofanywa na wauzaji wa ndani, yaani *export* imekuwa *40 billion recorded* na *import 96 billion*. Sasa hapa inabidi lazima tujiulize tujue kwamba, *imbalance of trade* ipo na tunahitajika tutengeneze bidhaa ambazo zinakubalika nje. *WTO* leo inakwambia provide things that are accepted by us. Provide what market wants, tuhakikisha kwamba, bidhaa zetu zinakuwa nzuri na *imbalance* hii ya biashara iondoke.

Mheshimiwa Spika, *infrastructure* ni muhimu sana, kwa mfano, barabara nzuri, mawasiliano, maji, urahisi wa umeme, Wizara ijtihadi kuhakikisha kwamba, haya yanafanyika ikishirikiana na Wizara zinazohusika.

Lingine ukuaji wa asilimia 5.6 mpaka asilimia nane mwaka huu, mimi naipongeza sana Wizara ya biashara. Lingine, uwezeshwaji wa Wananchi hasa akina mama. Mikopo iwe rahisi kupatikana, lakini tatizo la Wanawake katika biashara ni kwamba, ukimchukulia kama mwanamume anakasirika na ukimchukulia kama mwanamke nyumbani mke wako anakukasirikia. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuwa maskini sio ghali, kuwa maskini ni rahisi sana. Tatizo la maendeleo yako pengine ni wewe mwenyewe kama hujitumi wala hufanyi kazi. Kujituma zaidi ndio ujasirimali wenyewe. *Hardwork is a soundest investment we can have. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inachunguza bei kubwa za bidhaa zinazouzwa kwenye *Supermarkets* kwa sababu inakerwa kwa nini wenyewe *Supermarket* wanazipata hizo fedha kabla wao hawajazipata kwa njia za kodi na kadhalika. Tuwe Watanzania na tununue bidhaa za Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Biashara ya Viwanda ni kichocheo kikubwa cha kukuza uchumi wetu. Kule Marekani kuna msemo wanasema kwamba, *if you can not develop the country by industrialization, create market*, ikiwa huwezi kuiendeleza nchi kwa kujenga viwanda vingi, fanya nchi yako iwe soko zuri la biashara na bidhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwezo sio kitu bila ya fursa, tuwape fursa Wananchi wetu ya kujiendeleza. Waingereza wanasema *well done is better than well said*. Tutoe ahadi nzuri kwa Wawekezaji ambazo zitawavutia kuja kuwekeza nchini mwetu. Wataalam wamsaidie Waziri, japokuwa Waingereza wanasema *expert is the one who knows more and more about less and less. (Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, mimi naunga mkono hoja na ninasema Mheshimiwa Waziri apewe hizo shilingi bilioni tisa, ni kidogo sana lakini apewe bila kufikiriwa mara ya pili. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na Watendaji wote katika Wizara, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika mazingira magumu ya ukosefu wa pesa za kutosha. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kulipongeza Shirika la *SIDO* kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wanaifanya. Mimi nimebahatika kuwa Mwenyekiti wa *SIDO* Mkoa wa Kigoma kwa muda na nilikuwa naona kazi tunayoifanya katika mazingira magumu sana. Ninachoomba ni kwamba, sasa Wizara iweze kuliongezea uwezo Shirika hili la *SIDO* lipate nyenzo zaidi ili isiendelee kujikita Mjini na badala yake ielekeze nguvu zake Vijijini ambako ndiko inaweza kuondoa umaskini kwa Wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuhusu *SIDO*, ni vyema ikazingatia *vision* yake kwamba, ni Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo Vidogo na sio Shirika la kutoa *working capital* kwa ajili ya maduka ya mijini, hapa tutakuwa tumepoteza mwelekeo wa *SIDO*. Leo *SIDO* inashughulikia maduka, batiki, kutoa mikopo kwa watengeneza *ice cream!* Inawezekana ikaonekana ni jambo zuri, lakini lile lengo la *SIDO* la kuhudumia viwanda litakuwa limepotea, cha msingi ni viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni suala la ubinafsishaji wa viwanda vyetu. Nakubaliana kabisa na Kamati kwamba, wale ambaao wameshindwa kutekeleza mikataba ya ubinafsishaji, wanyang'anywe vile viwanda ambavyo walipewa. Mikataba ifuatwe, kwa sababu kama kiwanda kilitakiwa kuzalisha viatu, leo kinazalisha vifaa vya *plastic* maana yake kinatukosea haki sisi Watanzania ambaao kiwanda kile tuliamua mwanzoni kwamba, kizalishe viatu na mkataba ni wa kuzalisha viatu, sio bidhaa za *plastic*.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri sisi nchi yetu wakati inaaniszisha hivi viwanda, ilikuwa ina *linkage* kubwa ya uchumi. Kiwanda cha Viatu kilikuwa ndio soko la bidhaa za ngozi, Kiwanda cha Bia kilikuwa ndio soko la shayiri inayolimwa Hanang, kilikuwa ndio soko la Kiwanda cha *Crown Corks* kilichokuwa Dar es Salaam, kilikuwa ndio soko la Kiwanda cha *Kioo Limited* cha Mbagala. Leo tumebinafsisha, hakuna shayiri ya kutoka Hanang, hakuna kioo kutoka Mbagala, wala hakuna *Crown Corks*, wanunuwa kutoka *South Africa*. Sasa hapa lazima tuangalie, kama hatutakuwa tunafuata ile Mikataba na kuwalazimisha hawa watu kufuata jinsi tulivyokusudia sisi awali. Maana ya ubinafsishaji itakuwa haipo kwa uchumi wa Taifa. *Intention* yetu itakuwa haipo na viwanda vitakuwa vina-serve purpose ya watu wengine badala ya uchumi wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini cha kusikitisha zaidi ni kwamba, hata hiyo ajira yenewe katika viwanda hata hivi ambavyo tumeviweka kwenye *EPZ*, kwa kiwango kikubwa hakuna Watanzania ambaao wamejiriwa katika hivi viwanda. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, achukue uamuzi atembelee hivi viwanda akishirikiana na watu wa Mambo ya Ndani na watu wa Wizara ya Kazi, aone jinsi ambavyo Wazalendo wamekosa kazi hasa katika viwanda vya nguo (*Textile Sector*), atakuta jinsi Wapakistan walivyojaa mle na wengine hawana hata vibali vya kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri hii Wizara ina Taasisi nyingi sana za Utafiti na uvumbuzi. Juzi tulikuwa na Semina na tumeona maonesho ya *CAMARTEC*, *TIRDO*, *TISCO*, *TATEDO* na kadhalika. Bahati mbaya kubwa iliyopo ni kwamba, zile sheria zilizoanzisha hizi Taasisi zimezibana mno kwamba, hawawezi kuendelea zaidi. Lakini jambo la pili ni kwamba, Wizara yenewe haikutoa pesa za kutosha kuweza kuwawezesha wafanyakazi ili wawe wavumbuzi kweli na watafiti wa kweli. Shilingi milioni kumi kwa Taasisi ya Utafiti ni sawa na bure. Naiomba Wizara kwa makusudi, iziwezeshe kabisa hizi Taasisi ili ziweze kufanya kazi zake zilizokusudiwa na sheria zilizozianzisha. (*Makofi*)

Lakini cha msingi ni kwamba, Taasisi hizi zenewe zinatakiwa kutengeneza *prototypes*, zikishamaliza *prototypes* wauze zile *prototypes* kuwe na namna ya mtu mwingine kuzalisha na kuuza. Mimi sitegemei kwamba, kama ikivumbua plau ndio itatengeneza na ku-market hii. *There should be another organization*, ambayo itafanya uzalishaji wa ile *tractor*, inunue ile *prototype* ya *CAMARTEC* izalishe kwa wingi halafu ipeleke yale matokeo Vijiji ambapo ilikubaliwa. Sasa hii haipo! (*Makofi*)

Lakini pia ukiangalia kazi za hizi Taasisi, zina-overlap mno kiasi kwamba, unakuta zina ushindani sasa. Badala ya kuwa *complimentary*, zinashindana. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, aangalie hizi Sheria zilizoanzishwa ili tutengeneze Taasisi moja kubwa ya Utafiti na uvumbuzi. Tuipe nyenzo za kutosha ili wao watengeneze *prototypes* za kutosha na tuitumie Taasisi kama *SIDO* ili sasa izalishe na kusambaza badala ya kung'angania, mwisho wake hizi Taasisi zitaishia kutengeneza *prototype* na hawawezi kuzalisha zaidi ya ile waliyotengeneza.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Wizara kuptitia *NDC* kwa kutambua *potential* iliyopo Kigoma na kuiweka kwenye *EPZ* programu. Lengo mimi najua ni zuri, lakini Mheshimiwa Waziri bila shaka anafahamu, pamoja na utashi wanaoweza kuwa nao, bado utashi wa kisiasa haujakuwepo hasa kwa kupeleka miundombinu ya umeme, barabara na hatimaye Uwanja wa Ndege wa kuweza kusafirisha hizo bidhaa. Kwa hakika sisi Mkoa wa Kigoma tuna matatizo yanayotokana na Wakimbizi na *geographical setting* yake. Lakini tunaweza kabisa kutoa haya matatizo, tukabdalisha haya matatizo ya Kigoma yakawa ni fursa kwetu kuweza kuuza kwa nchi zilizo jirani. (*Makofi*)

Namwomba Mheshimiwa Waziri katika hili, kwa kuwa ameanzisha *EPZ*, Wizara yake iwe ndio *coordinator* sasa wa kushirikiana na Wizara nyingine ili kuhakikisha kwamba, miundombinu inayotakiwa katika kuboresha *EPZ* imeanzishwa katika Mkoa wa Kigoma. Kwa sababu hakuna anayeweza kwenda kuwekeza mahali ambapo hakuna umeme. Hakuna anayekwenda kuwekeza mahali ambapo hakuna barabara ya uhakika. Soko tunalo la uhakika katika nchi ya Kongo, Rwanda na Burundi na Mikoa ya jirani ya Tabora, Shinyanga, Mwanza na Kagera. Lakini kama Kigoma haijafunguka, ile dhana ya kuwa na *EPZ* itakuwa haiwezi kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, niseme tena kwamba, biashara sio maduka ya nguo wala maduka ya vipodozi, ni zaidi ya maduka tunapozungumzia biashara. Nimemaliza suala la viwanda. Sasa mimi naishauri Wizara kwa sababu Wizara hii sasa imeshika biashara mtambuka. Basi Wizara hii ndio iunganishe nguvu za Vyama vya Ushirika ambavyo vinafanya uuzaaji wa mazao. Bodi zinazofanya uuzaaji wa mazao nje Wizara ndio izisimamie badala ya kubaki kule ambapo hakuna biashara kwa sababu *cooperative* inapojiingiza kwenye biashara, lazima tukubali kwamba, imetoka kwenye Wizara ya Kilimo sasa. Wizara ya Kilimo sio mtaalam wa biashara. Kwa hiyo, itoke kule *cooperative* sasa iingie chini ya Wizara ya Biashara ili Wizara ya Biashara iweze kuwashauri hawa wafanye biashara namna gani. Hapo ndipo tunapoweza kufika.

Lakini pia tuna *opportunities* za *AGOA*, *EPA* na nyinginezo, tunategemea viwanda binafsi na watu binafsi ndio *wa-take advantage* ya hizi nafasi ambazo zipo. Basi viwanda hivi binafsi vitakavyokuwa vimeanzishwa, ni vyema *TBS* ivisaidie kufikia viwango vinavyotakiwa na sio kuwa kikwazo katika kufikia hivyo viwango. *TBS* ni wagumu sana kutoa vile viwango vinavyotakiwa hata kwa *local products* za hapa nchini. Naomba iwasaidie badala ya kuwa kikwazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na maonesho ya biashara hivi karibuni. Ni jambo zuri, lakini Mheshimiwa Waziri naomba anisaidie. Hivi tunakwenda kuonyesha biashara

pale au tunakwenda kuuza biashara? Maana yake lazima tulenge jambo moja na tulifikirie tulifikishe mwisho. Kama tunakwenda kuonyesha kwa minajili ya kwamba watu wajue tulichonacho, watoe *orders*, wavutike halafu ndio watoe *orders* wanunue, *then* utaratibu unaotumika pale kwa kweli haujafikia *standard* inayotakiwa. Ni vurugu tupu mle ndani. Kama tunakwenda kuuza, *then* suala kwamba sasa maonesho yamegeuka ni duka, tunaweza kuendelea na utaratibu uliopo kwa sababu itakuwa ni vurugu ya kupishana tu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Abdullatif Hussein Esmai, amezungumza kwamba, tuwe Watanzania, tununue bidhaa za Tanzania. Mimi nakubaliana naye kabisa. Lakini katika hali ya soko huria, sio rahisi kung'ang'ania vitu vya Tanzania wakati havijakidhi ubora tunaoutaka. Sasa naishauri Wizara itusaidie, zile bidhaa ambazo zinaletwa za Kitanzania ziwe kweli zimefikia *standard* inayotakiwa *ku-compete* na bidhaa zinazotoka nje. Nakubali kuna watu wana ugonjwa wa kununua vilivytoka nje, nakubali hilo lipo. Sasa nina hakika Wizara inaweza kuanzisha wiki ya *Buy Tanzanian Products Campaign* ili tuweze kufikia huko. Lakini pia lazima iendane na ubora unaotakiwa. Lazima *packaging* yake iweze kuvutia na isiwe ni *imitation* tu ya bidhaa ambazo zinatoka nje. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho, hizi *Supermarkets* ambazo tunazo, ni vyema tukaziwekea sera za kununua bidhaa zinazotoka Tanganyika. Sioni kwa nini *apples* zitoke *South Africa* wakati tuna *apples* Mlalo. Sioni kwa nini *tuuze juices* za kutoka Arabuni wakati *juices* zinaweza kutengenezwa hapa Tanganyika na sioni kwa nini tununue nyama kutoka Kenya wakati Kongwa tuna nyama nzuri zaidi? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa ni *information* ya biashara. *Market Development Bureau* ambayo iko chini ya Wizara ya Kilimo, ningeshauri kabisa ihamie chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Hapa ndio mahali pake ambapo Wananchi wanaweza kupata taarifa sahihi na ambazo zimechujwa na wataalam wa biashara hasa kwa masoko ya nje. Masoko ya ndani tunaweza kufanya mchezo, lakini tunapokuwa tunataka *ku-compete on a global level*, lazima tukubaliane kwamba, *information* wafanyabiashara wanayoipata ilingane na ukweli halisi uliopo. Sio kusema kwamba, gunia la mahindi Kibaigwa lilikuwa kati ya Sh.28,000/= na Sh.30,000/=, hiyo sio *information* itakayomsaidia mfanyabiashara. *Information* lazima iwe sahihi na *to the point*.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, nakushukuru tena na ninaunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia asubuhi hii ya leo kuwa mtu wa tatu katika Waheshimiwa Wabunge ambao watachangia, nakushukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kushukuru, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Ngasongwa kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye Wizara hii. Vile vile nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Rita Mlaki kwa kazi nzuri anayofanya.

Lakini yuko ndugu yangu Sheikh Ahmed Ngemera, Katibu Mkuu wa Wizara naye nampongeza sana pamoja na Watendaji wake wote wanaomsaidia yeye na kuwasaidia Waheshimiwa Mawaziri kwa kuifanya kazi hii kubwa walionayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha niungane na wenzangu kutoa rambirambi kwa kifo cha Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Hayati Yeti Mwalyego, ambaye ametutoka, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwenda kuwakilisha Bunge kwenye mazishi yale.

Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa mambo ambayo yatakumbukwa yaliyofanywa na mwasisi wa Taifa hili, Mheshimiwa Mwalimu Nyerere ni pamoja na kazi ya kuanzisha viwanda katika nchi hii. Mzee wetu huyu kama ilivyo kawaida yake aliona mbele na kwa makusudi kabisa alianzisha viwanda vingi tu, vikiwepo viwanda vya nguo. Faida ambazo zilionekana mpaka kuanzishwa na mpaka kuona umuhimu wa kuanzisha viwanda ni nydingi na wataalam wanazijua nina hakika Mheshimiwa Waziri na wenzake wanafahamu.

Mheshimiwa Spika, kati ya hizo, ni kutumia mali ghafi yetu au mazao tunayozalisha hapa nchini ili kuyapa soko zaidi. Kwa mfano, pamba kuitumia kwenye viwanda vyetu vya nguo na kadhalika na kadhalika. Hiyo ni moja ya faida ya kuwa na viwanda. Vile vile Mwalimu alifikiria suala zima la ajira kwa wananchi. Utakumbuka kwamba viwanda vingi kwa kweli vilikuwa vina ajira ya kutosha au ya kuridhisha kwa Watanzania kulikoni ilivyo sasa ambapo wafanya kazi au wananchi wengi wameachishwa na wanazurura hovyo huku na kule. Licha ya kwamba viwanda pia vinatuongezea pato la Taifa kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ili mradi faida ziko nydingi na ndiyo maana mwasisi wa Taifa hili Mwalimu Nyerere aliamua kwa makusudi kabisa kuanzisha viwanda. Historia tu kwamba ni bahati mbaya kwamba dhana nzuri na mtazamo nzuri wa viwanda hivi havikuweza kuendeshwa katika utaratibu unaofaa. Lakini inawezekana kabisa sera zetu za wakati ule zilikuwa ni moja ya sababu ambazo zilisababisha viwanda vikafariki au kufa au vikawa havifanyi kazi vizuri. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa si vizuri sana saa nydingine kuwalaumu wale amba walikuwa wanaendesha, lakini tunadhani kabisa ya kwamba kama tulivyojisahihisha kwamba sera zetu tulizokuwa nazo zilichangia sana katika kufanya viwanda hivi vifilie mbali. Sasa kama ilivyo Chama Cha Mapinduzi na Serikali yake tunajisahihisha pale ambapo tunaona tunakwama na tumejisahihisha sasa kwa Serikali ya Awamu ya Tatu chini ya kiongozi wake mahiri Mheshimiwa Mkapa ya kuleta Sera nydingine ya binafsishaji ili kuhakikisha kwamba viwanda vyetu tunawakabidhi wenzetu wenye uwezo, wenye taaluma mbalimbali waweze kutusaidia na sasa tunavyo viwanda vingi tu vimeanza kufanya kazi vizuri. Vingine vilivyo kufa vimefufuliwa na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda niipongeze Serikali ya Awamu ya Tatu na hasa Mheshimiwa Mkapa kwa kweli kwa hii Sera nzuri na zoezi hili zuri ambalo linaendelea, ingawa limekwenda kwa mawimbi ya hapa na pale. Siku zote safari ndefu

lazima utapambana na mawimbi ya hapa na pele. Zoezi la ubinafsishaji ni kweli kabisa limetusaidia. Lakini pia zoezi la ubinafsishaji ni kweli pia limeleta matatizo mengi, mtafaruku mwingi, kama nilivyosema hapo awali, wenzetu amba walikuwa wanafanya kazi katika viwanda vile sasa hawapo. Maisha wanayoishi sasa ya tabu. Vipato vyenyewe walivyokuwa wanapata tatizo, pensheni walizopewa ni kidogo sana. Ahadi ambazo tulipewa na Serikali kwamba wale amba wataachishwa watapewa fedha za kutosha ili waende wakaanzie maisha haikutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo haya ni baadhi ya mawimbi ambayo yametokea katika hali hiyo. Sasa nasema hayo yataendelea kurekebishiwa lakini kubwa zaidi kwa kweli nadhani nchi imefanikiwa kwa kuwa na zoezi hili la ubinafsishaji. Niwaombe wenzetu amba wanasmamia zoezi hili, Wizara zote au Serikali kwa ujumla isikilize sana mawazo ya Waheshimiwa Wabunge amba tumekuwa tukiyatoa mara kwa mara kwa nia ya kuboresha ili kuona kwamba tunafaidika na kuondoa matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, tatizo langu ni kwamba viwanda vingi vilijengwa Dar es Salaam na kiasi fulani vikajengwa Morogoro. Ndiyo tatizo langu mimi, kwamba *concentration* kwa kweli ya viwanda vyote hivi ukiacha sijui kama Mwanza kuna kiwandani gani, labda cha minofu ya samaki sasa hivi. Lakini nasema Dar es Salaam na Morogoro ndiyo viwanda vyote vikapelekwa huko. Matokeo yake ni kwamba vijana wetu huko vijijini amba tunawatazamia ndiyo nguvu kazi ya kule vijijini wasaidie wazee wetu waweze kulima, wote wanakimbilia Dar es Salaam kwa sababu huku Mikoani, Wilayani na vijijini hakuna ajira. Ajira iko Dar es Salaam kwa maana viwanda vyote viko Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi katika zoezi hilo la ubinafsishaji au Sera hii mpya tunaendelea huko huko kwamba vinafuliwa vile viwanda ambavyo vilikufa Dar es Salaam na vinajengwa vingine vile vile Dar es Salaam kana kwamba Tanzania ni Dar es Salaam peke yake.

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani hayo ni makosa. Kwa kweli ipo haja sasa ya kuangalia kutawanya viwanda hivi katika maeneo mengi. Zipo sababu nyngi tu za kufanya hivyo. Kuendelea kuwekeza Dar es Salaam peke yake mimi nadhani ni vizuri Serikali ikaliangalia upya jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi siamini kwamba Serikali ya Tanzania na umahiri wake chini Rais shupavu kama Mzee wetu, Mzee Mkapa ishindwe kumshawishi muwekezaji kwa hoja, kumwambia hapana bwana, kama unataka kuwekeza katika kiwanda cha *Cement* Dar es Salaam kuna kiwanda, Tanga kuna kiwanda. Twende sasa Dodoma, twende Shinyanga. Serikali ya CCM na uongozi wake nina hakika wana nguvu ya hoja ya kuweza kuwashawishi wenzetu hawa wawekeze. Hii lugha ambayo tunapewa kwamba wawekezaji wanachagua wenyewe, mimi nadhani hiyo haipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini sisi tusitumie nguvu na ushawishi wetu tulio nao. Sisi tuna sifa, tumeshawishi mambo mengi katika ulimwengu huu. Kwa nini tusitumie nafasi hiyo tukashawishi na hawa wawekezaji wanaokuja tukawaambia bwana, kama

unataka kuwekeza katika kiwanda cha *Cement*, nazungumzia *Cement* kwa mfano, nenda Dodoma. *Gypsum* iko hapa Itigi, Manyoni hapa, iko nyingi tu, wala ile *argument* ya kwamba eti mazao ghafi hakuna siyo kweli. Manyoni pana *gypsum* nzuri na iko nyingi inaweza kabisa Kiwanda cha *Cement* kikajengwa Dodoma, inaweza kabisa kiwanda cha *Cement* kikajengwa Singida.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba Serikali iangalie upya na lugha hii ya kusema kwamba wahisani, au wawekezaji wanachagua naomba tusiendelee kupewa isipokuwa tuitume, tuiombe Serikali shupavu au maaskari miamvuli shupavu chini ya ushupavu wa jemedari wetu Mheshimiwa Mkapa iwashawishi wawekezaji wawekeze katika Mikoa mingine. Hii habari ya kuonekana Dar es Salaam pekee nadhani haifai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo lake ndiyo hilo sasa mnamwachia Mheshimiwa Makamba anapigizana kelele na vijana kila siku kukicha, wenzetu Wamachinga. Lakini inawezekana vijana wa Singida wako chungu mzima pale. Waende wapi sasa Singida hakuna kitu, hakuna kiwanda hata kimoja. Lazima watakwenda Dar es Salaam, ndugu yangu Makamba atafukuzana nao, mara awafukuze huku, mara awapeleke huku. Haya yote yangeondoka kama mngetawanya viwanda hivi vikaenda Dodoma, Shinyanga, Arusha, Mwanza na vijana hawa wasingeckimbia huko, kwa mfano tulipoanzisha Makao Makuu Dodoma mimi nilitegemea kwamba Dodoma angalau kutakuwa na viwanda, hata vile viwanda ambavyo vilikuwa vimeanzishwa vimeondolewa. Kulikuwa na kiwanda cha Soda hapa kimeondolewa. Kulikuwa na kiwanda cha magodoro kimeondolewa, hakuna sababu za msingi, ningependa Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja atueleze ni sababu zipi za msingi zilizopelekea viwanda vya Magodoro na Soda kuondolewa hapa Dodoma na kupelekwa huko huko.

Mheshimiwa Spika, lakini magodoro yale mpaka leo ukienda kununua unaambiwa ni magodoro ya Dodoma. Sasa mimi sielewi. Hebu atueleze ni sababu zipi, ili atueleze atakapokuwa anahitimiza hoja yake. Tatizo lililopo ukiacha tatizo la ajira kwamba wanajazana kule Dar es Salaam ni bei kubwa. Juzi Mheshimiwa Mussati alipokuwa akitoa kilio chake hapa, amesema mfuko wa *Cement* kule Kigoma unauzwa sh.15,000/=. Jirani yangu hapa Mheshimiwa Buzuka anasema kule Shinyanga mfuko wa *Cement* unauzwa sh.11,000/=. Nina hakika na Mwanza hivyo hivyo 12,000/= na kadhalika na kadhalika. Lakini hii ni kwa sababu *Cement* inatoka mbali ama itoke Tanga au itoke Mbeya kwenda Mwanza na Kigoma *definitely* itauzwa hivyo. Lakini kama Kiwanda cha *Cement* kingejengwa hapa katikati Shinyanga, Dodoma bei isingekuwa hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hilo ndiyo ombi langu ambalo nadhani ni vizuri likawekwa. Bati hivyo hivyo, wenzetu wananchi jengeni nyumba za kisasa, jengeni na *cement* hivi mwanakijiji kweli wa Singida kule Ihanja, Ikungi, atawea wapi kupata mfuko wa *cement* shilingi elfu kumi na kitu ajenge nyumba nzuri, atajenga wapi. Ni dhana ambayo inakuwa *contradiction* wakati tunataka wajenge nyumba nzuri, hatuwasaki hawa watu wa vijiji wajenge nyumba nzuri kwa kuwapelekea huduma huko tunakotaka wapeleke.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ombi langu ni kwamba kwa hili suala habari iangaliwe, kama *Cocacola*, Bia, wale wanywaji, wako Waheshimiwa Wabunge wanapiga vitu/pamba.

**MBUNGE FULANI:** Tupo!!

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Bei ya Mwanza na Dar es Salaam haitofautiani sana. Bei ya Singida ya soda na Dar es Salaam haitofautiani sana, wale wanafanya nini? Kwa nini mfano wa soda na mfano wa bia usiwe katika *cement* usiwe katika mabati. Kwa sababu huyu pia anasafirisha kutoka Dar es Salaam anapeleka Mwanza na Singida. Sasa na huyu wa *cement* kwa nini asisafirishe asitumie utaratibu huo ambao unatumiwa na *Cocacola* na bia ili wananchi wanunue vitu hivi katika bei ambayo ni nafuu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Serikali naomba waliangalie hilo, vinginevyo sisi tunaokaa mikoani tunakuwa *penalized* kwa sababu ya kukaa Mikoani tu. Tuambieni kama wote tuje Dar es Salaam. Tulime pamba, tumbaku, lakini kufaidi wafaidi watu wa Dar es Salaam sisi watu wa huko hatufaidi. Haiwezekani uchumi namna hiyo, hilo ni jambo ambalo linafaa kuliangalia. (*Makofi*)

Mazao tulime sisi, wanaofaidi wakae Dar es Salaam, sisi tununue *cement* sh.15,000/= huo ni uungwana kweli? Hebu uliangalie, ushauri wangu ni kwamba moja, viwanda hivi wafuate mfano wa Cocacola na Bia, viwanda *vifungue Zonal Depots* kama ilivyokuwa zamani, pawe na *Depot* kwenye Kanda, hapa pana *depot* ya mabati *depot* ya *cement* angalau mtu wa Singida, mtu wa Tabora, mtu wa Shinyanga anaweza akapata urahisi wa kuchukua kuliko ilivyo hivi sasa. Au vinginevyo pawe *territorial prices* ambayo inaweza ikasaidia kama nilivyozungumza huko nyuma, lakini la msingi ni kwamba Serikali isambaze viwanda katika maeneo mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nigusie kidogo tu suala la soko huria. Tumekubaliana kweli, lakini mbona *monopoly* inarudi tena. Wafanya biashara wa pamba, pamba ilikuwa sh.350/=, sh.300/= sasa wamekaa wamefanya *cartel* ambao ni *conspiracy* kwa kweli hiyo. Sasa wanataka pamba inunuliwe kwa sh.250/= Singida tunalima pamba. Wanauliza wale walimaji wetu imekuwaje tena sh.250/= wakati tulikuwa tunategemea 300/= na sh.350/= na tulipita kuwahamasisha na mwaka huu kwa kweli Singida wamelima sana pamba. Lakini katika hali kama hii, hii *cartel conspiracy* inatoka wapi, mimi nashangaa. Niombe Wizara waliangalie hili kwani tumeondoa *monopoly* na sasa tumerudisha *monopoly* tena kwa mlango mwagine kwa hawa jamaa kukaa mahala pamoa na kuanzisha *monopoly*. Nadhani hiyo itakuwa ni *contradiction* katika mambo yetu haya.

Mwisho, niseme tu Serikali idhibiti uingiaji wa bidhaa, tumeambiwa juzi na watu wa *TTCL* kwamba simu mbovu hizi za mikononi zimezagaa Dar es Salaam zinapita wapi? Kwa nini vyombo vinavyohusika havifanyi kazi ya kuchunguza. Kwa nini

Tanzania iendelee kuwa *dampo* la bidhaa mbovu? Hayo naomba sana wenzetu waweze kuangalia ili tuondokane na kuwa *dampo* na ziangaliwe bidhaa nzuri zinazofaa kuingia.

Mwisho kabisa ni suala la wafanyakazi. Huku nyuma kulikuwa na matatizo makubwa sana katika masuala ya wafanyakazi hasa pale ambapo pamebinafsishwa. Lakini nashukuru sasa angalau Serikali imeanza kuona. Sitaki tujenge *impression* kwamba haki za mfanyakazi hazitoki mpaka waandamane, mpaka wapige kelele, mpaka umfungie mtu mlango. Tukijenga dhana hiyo ndugu zangu itakuwa vibaya, tuachane na dhana hiyo. Naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Lakini pia napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kuongelea zaidi kwenye mambo mawili tu. Kwanza suala zima la maonyesho ya biashara. Kwa kweli napenda kumshukuru sana Mama Ana Mkapa kwa jinsi anavyotusaidia akina mama kuweza kuonyesha bidhaa zetu kwenye maonyesho haya. (*Makofî*)

Na kwa uhakika tumeweza kupiga hatua kubwa kwenye dhana mzima ya kufanya vitu bora zaidi lakini bado kwenye suala la kuchukua ubora na bei hapo kidogo mambo yanakuwa yanatofautiana. Wengi wa baadhi ya wafanyakabiashara akina mama ambao wanatengeneza bidhaa nzuri sana sasa hivi bei zao ni kubwa mno. Sasa naomba sana wakati wanapopewa semina hizi kabla ya maonyesho basi waelekezwe jinsi gani ya kuweza kufanya mahesabu mazuri kuona kwamba kiasi gani wanatumia kwenye uzalishaji na baada ya hapo waweke *percent* ngapi ili bidhaa zao ziende kupata soko la uhakika kwani wengi tutaweza kuvinunua na kuweza kuvisambaza na kuvitangaza vitu vyetu ambavyo tunatengeneza akina mama.

Lakini lingine kwenye suala zima la maonyesho ya biashara kama baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walivyosema, unakuta wengi wanauzu, wala si suala la kuonyesha mazao yanayotengenezwa. Unakuta ni biashara tu. Vitu vile vile ambayo maduka yako mjini ndiyo yamehamishiwa pale. Ni maduka ambayo tunayafahamu, lakini kule matokeo yake yanaongezeka bei. Vitu vinaongezeka bei, kwa kuona labda wanunu ni wengi. Sasa hili nalo linapoteza lengo zima la kuonyesha maendeleo yetu ya uzalishaji na biashara tunayoifanya katika nchi yetu na kutaka biashara za nje nazo waweze kuleta vitu vyao kuweza kuona na kuweza kufanya vitu hivyo viweze kupata soko.

Mheshimiwa Spika, lakini baya zaidi ambalo ningependa niliongelee pamoja na kuhamasisha wananchi na kuona umuhimu wa kuweza kwenda kwenye maonyesho hayo. Mambo ambayo yametokea mwaka huu tusiyakalie kimya na kuona kwamba tuiswashauri wenzetu nini cha kufanya. Hali iliyotokea mpaka baadhi ya wananchi kuzimia, wakitaka kuingia ndani kuona maonyesho haya. Kwa kweli haya mambo yanasiskitisha.

Sasa wenzetu wanaohusika na viwanja hivi hebu walione hili na waweze kuchukua hatua mwakani, nina hakika mwakani wengi tutataka kwenda kuona maonyesho haya, kwa hiyo, kuona kwamba mambo haya hayatokei tena. Mimi ningeshauri waongeze maeneo ya kukatisha tiketi na maeneo ya kuweza kuingia ndani, milango. Milango ni michache na ni finyu mno. Ukiachilia mbali na usimamizi mimi nafikiri hilo watu wapo tu. Wanaweza wakaongeza maaskari, *FFU* kama walivyofanya kipindi hiki cha Saba Saba hii. Lakini bado milango na maeneo ya ukataji wa tiketi ni michache mno.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba sana wenzetu wanaoshughulikia uwanja huu waweze kuona njia gani ya kuweza kuondoa hili tatizo la wanaoweza kuingia na kuweza kutoka kwa raha kwa bila kupata usumbufu. Baadhi yetu sisi kwenye Saba Saba tulishindwa kuingia ikabidi turudi nyumbani na tiketi mikononi. Sasa hii inaonyesha wazi kwamba mahitaji ya watu kuona vitu hivi yamekuwa. Pia baada ya mapato ya wenzetu wanaokusanya hizo fedha za kiingilio wameyakosa kwa sababu watu wameona aah! Ya nini kwenda kutafuta kubanwa na watoto. Kwa hiyo, hili jambo nimeona niliongelee mapema ili mwakani yasitokee tena haya ambayo yametokea.

Mheshimiwa Spika, lingine katika suala zima la maonyesho upangaji wa mabanda. Mimi ningeomba mwakani au hata baada ya miaka miwili mitatu kwa sababu mengine yameishajengwa, yaweze kupangwa katika hali tofauti. Tusichanganyechanganye, mwingine amepanga vitu nje barabarani, hapa unakuta kuna hali nzuri tu inaonyesha jinsi ya kutengeneza bidhaa, kwa mfano *SIDO* lakini hapo hapo kati kati kuna mtu mwingine tena anauza bia. Vitu ambavyo havifanani fanani. Tutenge maeneo kuona kwamba eneo hili ni kwa ajili ya kula na kunywa. Eneo hili ni kwa ajili ya kuonyesha tu. Eneo hili ni kwa ajili ya kuuza tu. Ili mtu anapokwenda ndani ajue kabisa niende wapi kwa mahitaji yangu. Maana yake sisi wengine hatuendi kununua, tunakwenda kuona nini ambacho kimeongezeka katika masuala mazima ya maendeleo ya nchi yetu. Kwa hiyo, na hili pia wakati wanaongeza milango waangalie pia na upangaji wa mabanda yetu ndani ya uwanja huu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuongelea masuala mazima ya *SIDO*. Kwa kweli napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza sana *SIDO*. *SIDO* walikuwa wanafanya kazi nzuri, wanaendelea kufanya kazi nzuri na kwa kweli sisi wa Mafia tutakuwa wezi wa fadhila kama tukisema *SIDO* haijafanya chochote Mafia na tunaomba leo waende. Katika kumbukumbu zangu, kwa miaka ya nyuma, tangu wakati akiwa Mheshimiwa Basil Mramba, Mkurugenzi wa *SIDO* ameweza kuchukua baadhi ya vijana kuwapeleka Sirilanka kuititia *SIDO* kwenda kujifunza kutengeneza vifaa vya kutumia zao la mnazi. Kuititia Shirika letu la *MAFIDECO*, Shirika la Maendeleo la Wilaya.

Sasa matokeo *MAFIDECO* kufa isiwe kwamba *SIDO* hawakutusaidia. *MAFIDECO* baada ya kufa hawa vijana bado wapo Mafia na wanaendelea kutengeneza vifaa hivi vya minazi. Sema tu ambalo nitaliomba kwa *SIDO* waendelee kuwa karibu nao hawa vijana ambao wamepata huu utaalam waendelee kuwasaidia kuweza vitu

vyao vieleweke na viwe bora zaidi kama wanavyofanya wengine lakini pia waweze kulipanua soko la vifaa hivyo.

Lakini pia napenda kukumbuka tu kwamba wakati wa ndugu Epa Toroka pia *SIDO* waliweza kuchukua vijana na akina mama kuwapeleka mpaka *Gotiland* kwa kutafuta kuweza kuweka uhusiano *Gotiland* na Mafia katika masuala mazima ya Viwanda vidogo vidogo. Labda tu kwa haraka haraka Ndugu Laizer nafikiri atakumbuka hivyo viwanda mpaka leo vipo. Tunavyo viwanda vya kutengeneza magari viwili ambavyo ndiyo viwanda vinatusaidia sasa hivi kutengeneza magari yetu hata ya Serikali hata ya wananchi Mafia. Lakini haya chanzo chake ni *SIDO* kuwapeleka hawa watu wawili wa ushirika kwenda kujifunza jinsi ya kutengeneza magari na kupewa vifaa kwa mkopo wa kutengeneza magari. Lakini kipo kiwanda kikubwa tu mambo ya Useremala ambacho mwanzo wake pia ni kati ya *Gotiland* na Mafia. Lakini sasa unakuta uhusiano wa karibu wa *SIDO* na viwanda hivi tu ndiyo unaokosekana. Wana vifaa vizuri tu, wamepata mikopo mizuri ya kufanya hivi vitu lakini basi tujitahidi kuwafuatilia na kuzidi kuwaona kwamba haya wanayoyafanya kweli yako kwa manufaa ya nchi yetu na Wilaya ya Mafia kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, lakini tusiishie kusema kwamba miaka hiyo tumefanyiwa hili na lile. Mimi nasema tu niliona hili niliweke kwenye rekodi kwamba *SIDO* wamefanya na kweli bado wanaendelea kufanya. Sasa tunakumbusha tu, kwamba bado Wana Mafia wanaendelea kuwahitaji kuweza kushirikiana nao na tungeomba sana sana sana kupitia Wizara yako uhusiano wa *Gotiland* na Mafia ufufuliwe, ulisinzia sababu ni nini kwa kweli mimi sijui. Lakini kama sababu ipo basi itafutwe ifanyiwe kazi na tuufufue uhusiano wetu wa Visiwa vya *Gotiland Sweden* na Mafia. Mimi nafikiri hii itasaidia kuwapa ajira Wana Mafia amba si wengi wanaokimbilia Dar es Salaam. Lakini bado wanahitaji kazi vijana wetu wa Mafia.

Mheshimiwa Spika, lakini hali kadhalika wenzetu wa *SIDO* waone kwamba mazingira ya Mafia ni tofauti na Wilaya nyingine. Mimi nawashukuru kwamba wamepitia kwa akina mama wengi kuwafundisha jinsi ya kusindika mazao. Na husuan katika Mkoa wangu, nina hakika Mkuranga wamekwenda, Kisarawe, Kibaha na juzi tu wamekwenda Bagamoyo. Lakini Mafia sijui wanaiona iko wapi? Mimi napenda kuwakumbusha kwamba Mafia ni moja katika Wilaya za Mkoa wa Pwani. Na ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa akijibu swalí alisema kwamba atanunua magari, lakini si rahisi Mafia kununua boti, lakini atawaongezea uwezo wa kuweza kufika Mafia. Sasa naomba basi tukitoka kuitisha hii Bajeti ambayo nina hakika uwezo wa *SIDO* utaongezeka, waende wakawaelekeze akina mama jinsi ya kuhifadhi mazao, jinsi ya kuweza kuzalisha tui la nazi lililokaushwa, ambayo minazi ipo mingi tu na kama tunavyojuwa kwamba mara zote tunajaribu kupeleka viwanda pale ambapo malighafi ipo.

Mheshimiwa Spika, sasa unapoongea machicha ya nazi na tui la nazi kama huendi Mafia unaenda wapi? Kama unaongelea habari ya kukoboa korosho kama huendi Mafia utaenda wapi? Kwa sababu malighafi ipo. Kama unaongelea habari ya kutengeneza mikeka ambapo ukindu mwingi tu umezagaa Mafia kama huendi kuongesha

jinsi ya kutengeneza mikeka bora, kama hutaenda Mafia utaenda wapi? Kwa hiyo, naomba sana *SIDO* waone kwamba Mafia bado tupo, tunawahitaji kwa ushirikiano wetu ulikuwa nzuri tu huko nyuma, sasa Wasitusahau warudi waone kwamba haya ambayo tulianza na *Gotiland* yanaendelezwa. Yale ambayo tulianza na *MAFIDEKO* na Sirilanka yanaendelezwa na haya mapya basi yanayokuja na Wana Mafia nao waweze kufaidika nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ningeomba sana na mimi niungane na Mheshimiwa Waziri kwa kumpongeza Balozi Ali Mchumo na Mheshimiwa Fatma Said Ali. Kwa kweli mimi ningeshangaa kama asingemsifia Mheshimiwa Fatma Said Ali kwa kamsaidia Mheshimiwa Balozi. Nasema ametimiza wajibu wake na tunampongeza mwenzetu kwa kuona kwamba ni wajibu wetu kuwasaidia wenzetu wanapokuwa kwenye shughuli za kutafuta maisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kwamba na sisi wote akina mama tutaiga mfano huu. Lakini pia na Mheshimiwa Balozi Ali Mchumo kama kawaida yake ataonyesha umahiri wa kufanya jukumu baki alilopewa ili kuweka jina zuri la Tanzania na lake yeche mwenyewe binafsi na familia yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo narudia kuwapongeza sana Wizara ya Viwanda na Biashara, kwa kazi nzuri wanayotufanyia, kwa uhusiano nzuri, kwa sababu wao wanahusiana na wana vijiji ambao ndiyo wengi katika nchi hii lakini basi uwezo nao uongezeka na waweze kufika kwenye yale maeneo ambayo wanaona ni magumu bado kule wana vijiji wapo na wananchi wapo wanahitaji msaada wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa natoa shukrani kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hii na kabla sijaendelea noamba nitamke kwamba naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dr. Ngasongwa na Mheshimiwa Naibu wake, dada yangu Mheshimiwa Rita Mlaki na Watendaji wake katika Wizara pamoja na Wakurugenzi wengine wote ambao wako katika Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Nawapongeza sana kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile natoa pongezi nyingi sana kwa Serikali kwa kuandaa Sera nyingi zikiwemo Sera ya Maendeleo ya Viwanda vidogo vidogo na biashara ndogo ndogo, Sera ya Taifa ya Biashara, Sera ya Taifa ya Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi na hii kwa kweli ni kwa sababu Tanzania katika dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 ina makusudio makubwa kabisa ambayo imedhamiria kufuta umaskini mionganii mwa jamii. (*Makofi*)

Lengo la maendeleo ni kutoa fursa ili kuwepo na utandawazi na ulegezaji wa masharti ya biashara ili kuipa msukumo mpya na wale wafanya biashara waweze kuongeza ukuaji wa uchumi, maendeleo ya teknolojia ambayo yatapunguza gharama na vile vile kuwaweka katika hali ya kuweza kushindana katika soko la dunia ukichanganya utawala bora.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupongeza hivyo, naipongeza Serikali kwani hii yote ni katika kuangalia kwamba inapunguza umaskini kwa wananchi. Lakini pamoja na hayo naomba nigosie machache kama ifuatavyo:- Nitazungumzia kidogo kuhusu sera na mikakati ya maendeleo ya Sekta ya Viwanda na Biashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Spika, kama ile sera ilivyoelezea ni kwamba bado mfumo wa kisheria ni mgumu sana kuna mlolongo mkubwa sana na gharama nyingi sana ambazo mfanyakishashara au mwekezaji mwingine anatozwu ili hatimaye aweze kuanzisha biashara yake. Hapa Serikali imekiri hili na imeliona na imeweka katika mikakati yake kuangalia jinsi gani itaweza kushughulikia tatizo hili. Naomba ifanye haraka kwa sababu kweli kabisa gharama zikiwepo, gharama za kisheria vile vile ukiangalia na wale wanaotoza kodi kwa mfano *TRA* mlolongo ni mkubwa sana wale wenye biashara ndogo ndogo huwa wanashindwa kufikia yale masharti kwa hiyo wanapata matatizo makubwa sana. Namwomba Waziri kwa kweli hii iwe ni mojawapo ya kazi ambayo wangefanya haraka kidogo.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba kulipongeza sana Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo (*SIDO*) kwa kazi kubwa wanayofanya hapa nchini kwetu kwa kuzingatia kwamba *SIDO* imezagaa Mikoa yote ya Tanzania ukiondoa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, vile vile naipongeza Serikali kwa kuifanya *SIDO* kuwa wakala wa viwanda vidogo vidogo na biashara ndogo ndogo kama vile tulivyoona wakati tunazindua zile sera wakati ule tulipokuwa na semina hapa nafikiri Waheshimiwa Wabunge wanakumbuka.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iiwezeshe *SIDO* ili iweze kukidhi azma yake ya uwakala huu waliopewa kwa sababu bado tunaona katika mwaka huu wa fedha na katika miaka ya miwili ya nyuma iliyopita sikumbuki vizuri kila unapoangalia kiasi cha pesa ambacho *SIDO* wanapewa kinazidi kupungua. Nafikiri hii inapunguza ule uwezo mkubwa ambao sisi wananchi tunahitaji *SIDO* iweze kutusaidia kwa sababu mpaka sasa hivi licha ya kwamba kila Mkoa una ofisi yake lakini kazi zake zinaenda mpaka Wilayani na vijijini na kwa kweli zinasaidia sana akina mama na vikundi vidogo vidogo kule vijijini. Ni vizuri basi Serikali ikaiangalia kwa jicho sio la huruma kwa jicho kamilifu ili iweze kufanya kazi zake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba nizipongeze zile taasisi za ubunifu ambazo zinashirikiana na *SIDO*. Kama tunavyofahamu research ni muhimu sana ili kuweza kuleta maendeleo hapa nchini kwetu. Sasa hivi tumeona hapo nje ambapo maonyesho yanaendelea taasisi kama hizi *CARMATEC*, *TILDO*, *TEMDO* na kadhalika lakini ukweli ni kwamba kama walivyozungumza wenzangu Serikali imezitupa mkono.

Mheshimiwa Spika, *CAMARTEC* walitufanyia semina wiki iliyopita na wamekuwa wakilalamika lakini sio *CAMARTEC* peke yake hata wale *TEMDO* na wengineo wanatakiwa wasaidiwe. Hii pesa ambayo wametengewa ni ndogo sana milioni 10 kwa mfano ukimpa mtu wengine ni biashara yake ya wiki moja tu sasa milioni 10 unampa mtu kwa mwaka mmoja unafikiri ataifanyia nini? (*Makofî*)

Mheshimiwa Waziri labda kutokana na wengi kugusia hapa, namshauri yeye Waziri na Hazina watafute pesa mahali popote pale ili waweze kuongeza bajeti ya hizi taasisi za *research* na *SIDO* vinginevyo tutakuwa tunapiga kelele tu ya *research* lakini sioni kitakachoendelea.

Mheshimiwa Spika, nikirudi upande wa *research* ninashauri wale wanaofanya utafiti wajaribu kwenda kule vijijini ili wasibuni tu vitu ambavyo kule vijijini haviuziki. Waende kule wazungumze na wananchi kwanza waone miundombinu ikoje, hali ya hewa, mahitaji ambayo wananchi wanahitaji ili waweze kubuni vitu na hatimaye waweze kuvitengeneza.

Mheshimiwa Spika, vile vile ninashauri kuwa iwepo basi katika hawa wabunifu au katika hawa wanaofanya *research* taasisi moja iwe kama mama ambayo wote hawa wanaangukia kwenye *umbrella* moja. Huyu anabuni hiki hiki anapeleka kwa yule mama yule mama ndio anafanya kazi ya kutafuta jinsi gani ya kutengeneza vile vifaa ambapo vitawafikia wananchi badala ya kila mmoja anatengeneza kitu chake kimoja ukitaka kokinunua wanakuambia hiki hapa ni kwa sababu ya maonyesho mpaka uweke *order*. Mimi nafikiri baada ya wao kufanya utafiti ile taasisi mama iwezeshe kutengeneza vile vitu wakati wowote ukishakiona pale anaambiwa nenda mahali fulani utakikuta. Huo ni ushauri napenda kutoa.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho napenda niongelee ni udhibiti wa bidhaa zinazoingia hapa nchini. Napenda kulipongeza Bunge lako Tukufu kwamba limepitisha Sheria ya *Anti-dumping and Countervailing Measure* na bahati nzuri Mheshimiwa Rais amesaini tarehe 14/4/2004 kama ilivyosemwa katika taarifa ya mtoa hoja. Katika suala zima la kuendesha viwanda vidogo vidogo bado ubora unakuwa ni tatizo na hii inafahamika.

Mheshimiwa Spika, nina tatizo moja naomba Mheshimiwa Waziri anipe jibu. Ukienda pale Dar es Salaam sehemu za Kariakoo, mtaa wa Kongo na Kipata kuna bidhaa pale zinauzwa kama mitumba yaani inasikitisha. Kuna vikombe vingine havina mkono, vingine vina mapengo, vijiko vinauzwa katika ule mtaa na hivi vimeingia nchini kama *ku-dump* na bila shaka wamelipa ushuru.

Sasa ni kwa nini vifaa vyetu tunavyotengeneza hapa wanasema havina ubora hivi kweli vile vikombe vyenye mapengo vina ubora gani na kwa nini viuzwe pale wakati sisi tunavyo viwanda vidogo vidogo vinavyoweza kutengeneza vitu kama hivi? Vingine vimefungwa lakini bado wengine wanaleta hapa wanakuja *ku-dump* wakati sheria tumepitisha. Naomba Waziri hili angenipa maelezo. Hivi alishawahi kutembelea katika

mtaa ule na kama hajawahi kutembelea basi mimi niko tayari kwenda kumwonyesha mwenyewe akaone. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza *SIDO* kwa juhudi zake inazofanya kwa kuwasaidia wananchi. Lakini pia nina suala moja ambalo labda Wizara ingenieleza. *SIDO* inaonekana imetandaa katika Mikoa hii ya Bara lakini kule Zanzibar bado hajaenda. Hivi karibuni Waziri aliulizwa swali ni sababu zipi ambazo zinaifanya *SIDO* kutotandaa kule Zanzibar, akasema atalifanya kazi. Kwa vile leo ni siku yake anawenza kutuambia ni lini basi *SIDO* na yenyewe itaenda kule Zanzibar ili iweze kuwahudumia akina mama walioko kule kwa sababu na wenyewe kama Serikali ya Muungano wana haki sawa kupata huduma hizi kama sisi tunavyozipata huku. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii mimi binafsi kwa kuipongeza *SIDO* kwa kuwa imenisaidia sana katika Mkoa wangu wa Tanga. Akina mama wengi wamepata mafunzo katika usindikaji na hii ilikuwa hajawahi kutokea katika kipindi kirefu sana. Nawapongeza katika Mkoa wa Tanga wana ushirikiano mzuri nataka nitamke hapa ili viongozi wao wafahamu kwamba Tanga kwa kweli wana mshikamano na ningeshauri Mikoa mingine wafanye hivi ili waweze kuwasaidia akina mama wengine. Vile vile ningependa Waheshimiwa Wabunge wanapopita katika Majimbo yao wasisahau kuwaambia wananchi kwamba *SIDO* ipo na inaweza kuwasaidia akina mama sio lazima wapate mikopo mikubwa kwa sababu *SIDO* hata mikopo midogo wanatoa na akina mama wana uwezo mdogo lakini kila mtu mwenye kikubwa alianzia na kitu kidogo. Kwa hiyo tujaribu kuwaelimisha akina mama wenzetu na sio akina mama peke yao kwa sababu hata akina baba pia wanakopeshwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na naipongeza Wizara na naiombea kila la kheri wao na watendaji wao na naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakifanya na hasa Mheshimiwa Waziri katika kuwakilisha nchi yetu katika vikao mbalimbali vyta Kimataifa vizito vyta masuala ya biashara ambavyo hivi sasa vimechukua nafasi kubwa. Kwa ujumla Afrika tumekuwa tukifanya vizuri kwa kuanza kuingiza *agenda* zetu katika chombo hiki kikubwa cha biashara duniani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika masuala ya maendeleo ambayo tunayatekeleza hapa kupitia bajeti hii lazima tukubaliane kwamba mambo makuu yote ya kimsingi ni yale yale kwa maana ya kinachosimamiwa na nchi kama *vision*. Kwa mfano nia ni hali nzuri ya kiuchumi kwa kila mwananchi sidhani kama kesho Wapinzani watakuja na sera tofauti na hiyo, afya bora kwa wananchi, elimu bora kwa kila mtu tutakachotofautiana ni mikakati, sera, mwelekeo wa namna ya kutekeleza hayo. Sasa ili tufikie hapo kuna vitu vitatu katika wakati huu wa bajeti ambavyo lazima tuviwianishe navyo ni sera, mipango na bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, nikianza na masuala ya mipango mbalimbali kwa mfano hivi sasa hali ya hewa ya biashara imechafuka sana kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta ambayo hata haieleweki inatupeleka wapi. Mafuta yamepanda sana na hivi majuzi Waziri wa Nishati na Madini amekubali hapa kwamba ziko dalili za baadhi ya watu kula njama ya kuharibu soko hili la mafuta ziko dalili hizo, wana *collude*. Sasa sheria yetu ya *Fair Trade* iko wapi? Kamishna wetu wa *Fair Trade* yuko wapi? *Fairness* katika biashara hii ya mafuta iko wapi? Unajua ukishagusa mafuta mambo mengi sana yanavurugika. Hilo naongelea katika mipango. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tukija katika bajeti yenye ukurasa 30 wa kitabu chake, kifungu cha 40, naomba ninukuu anasema hivi: "Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza hatua zinazopendekezwa itabidi kufuta Sheria ya Biashara Na.25 ya mwaka 1972 na kutunga Sheria Mpya ya Usimamiaji wa Sekta ya Biashara Nchini. Katika misingi hii, hatua zinazohusu leseni za biashara kama zilivyotangazwa wakati wa uwasilishaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha 2004/2005 zitatekelezwa baada ya kufuta sheria ya sasa ya biashara ili hatua hizo zisipingane na matakwa na masharti ya sheria inayotumika sasa. Wizara yangu inakusudia kuwasilisha Muswada wa Sheria mpya ya Biashara mapema iwezekanavyo ili kupata idhini ya Bunge kuwezesha utekelezaji wa yanayokusudiwa katika kuboresha utendaji wa sekta ya biashara katika nchi yetu". Mwisho wa kunukuu. Vema.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa mwananchi wa kawaida Waziri wa Fedha amesimama hapa akafanya mabadiliko makubwa sana katika masuala ya leseni. Wananchi hawatakiwi kulipa leseni ya biashara ambazo ziko chini milioni 20, imeshatangazwa hapa kwenye Bajeti. Mheshimiwa Waziri anakuja anasema kwamba, sawa kabisa kwamba iko Sheria Na.25 lazima ije irekebishwe kwanza ndio leseni zisikatwe sasa na mwananchi wa kawaida yuko sawa pia lakini sasa mwananchi wa kawaida tunampeleka wapi, tunamchanganya.

Maana hivi sasa huko Wilayani Maafisa Biashara wanataka kukata leseni wananchi wanasema ninyi ni matapeli, wababaishaji kwa sababu tumesikia sisi kwenye bajeti hakuna leseni kwa biashara za aina hii, ni migongano. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba mambo haya tuwe tunayazungumza huko, yanakuja mapema zaidi. Tunetafuta muda hata baada ya ile bajeti ya Wizara ya Fedha japo hili ni Bunge la Bajeti basi tukafanya kitu fulani hapa maana sasa hivi huko Wilayani ni mkanganyiko mkubwa sana kuhusiana na suala la hotuba ya Bajeti ilichosema na masuala ya sheria za biashara kama zinavyosimama sasa. Nashauri jambo hili litafutiwe ufumbuzi kabla ya kipindi hiki cha bajeti kwisha ili yale yote yaliyosemwa kwenye hotuba ya bajeti sasa yatekelezeke vinginevyo tutawachanganya sana wananchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kuendelea na sera yetu na utekelezaji wa masuala ya viwanda na biashara na ninapozungumzia viwanda hapa nazungumzia *industry* kwa ile tasfiri unasema *agricultural industry*, *coffee industry* sio *industry* ya viwanda tu machuma yale, *industry* kwa ujumla ambayo ina-cover biashara mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mbunge wa Kongwa ninashauri sana kuwepo kwa *systems approach* ya mambo sio tu sera kama hizi ulizotupa leo sera ya biashara na nini lakini sera mbalimbali ambazo zinawiana kuweza kufanya kazi kwa pamoja sera za fedha, kilimo, viwanda, nishati, ulinzi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano leo asubuhi niliuliza swalii kuhusu Kibaigwa. Tunajenga mazingira ya kuweka soko zuri pale. Tunashukuru Wizara ya Ardhi wamekuwa wakipima viwanja pale na vinaendelea kupimwa sasa hili jambo ni *positive* kwa biashara pale. Nishati wamepeleka umeme pale, Wizara ya Maji wanao mpango mkubwa, mwaka huu tumepata msaada wa Serikali ya Ufaransa wa kuboresha huduma za maji pale wa zaidi ya milioni 200, Wizara ya Masoko imewezesha soko kujengwa lakini sasa pamoja na yote hayo kufanyika unakuta biashara kubwa inafanyika pale ya mamilioni ulinzi wake haueleweki. Ndio nasema *systems approach* lazima kila mmoja a-*play party* yake ili kuwezesha mazingira ya biashara kuwepo. Ulinzi ndio jambo la kwanza maana mahali ambapo sio salama hapawezi kuwa na biashara, hata siku moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ameyatoa. Ni matarajio yangu kwamba kwa kweli jambo hili watalipa kipaumbele cha hali ya juu kwa kufungua Kituo kile cha Polisi ambacho wananchi wamekijenga. Tukumbuke wananchi walijenga Kituo cha Polisi mara ya kwanza hakuna Polisi aliyepelekwa pale wakasema ni kidogo, kama miaka mitano iliyopita na alikizindua Waziri Mkuu kituo hicho cha Polisi kidogo. Waliposema kidogo tumejihamasisha tena tumejenga kingine kikubwa zaidi kimeisha kama miezi saba, nane iliyopita kila kitu kiko pale lakin hakuna Askari wanategemewa Askari wa kutoka Kongwa mjini kilometra 40 kwenda kulinda kule.

Askari hawa na silaha zao wanadandia magari, mabasi au vigari vyatia abiria vyatia kawa hawana usafiri. Gari la *OCD* wa Kongwa ni bovu kweli kweli matokeo yake biashara pale Kibaigwa ni vurugu mechii tupu tumeachia wahuni na majambazi wanafanya wanavyotaka pale. Kwa nini basi tusiwe na *systems approach* kila mtu aweze kuweka mazingira yake kuhakikisha kwamba biashara inafanyika?

Mheshimiwa Spika, Askari wanaotegemewa kwenda kulinda kule tuliwahi kupata majibu hapa kwamba nauli ya kwenda na kurudi kila siku imewekwa kwenye mishahara. Hivi watakuwa na mshahara unaofananaje wa kila siku na silaha yake ajilipie nauli kwenda na kurudi? Hivi kweli tunajenga *systems approach* ya kuweza kuboresha mambo haya? Kwa hiyo, kituo kile kipo nawaomba sana Wizara ya Mambo ya Ndani wapeleke Askari ili kuweza kuweka ulinzi pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukiacha Mambo ya Ndani, Wizara ya Kilimo kwa mfano katika eneo kama lile kwa nini tuweke soko la mahindi ya kwenda sehemu nyingine zote na nje ya nchi yetu lakini tunashindwa hata kujenga ma-*godown* ya *SGR* pale? Tujenge ma-*godown* ya *SGR* pale ili baadhi ya mahindi yanunuliwe kwa ajili ya akiba ya chakula cha Taifa zima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini sisi tuendelee kuuza mahindi kila siku, narudi kwako Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda, kwa nini sisi tuisisindike tukauza unga wa mahindi huko Kenya, Malawi na kwingine? Mambo kama hayo mtuwezeshe kama tatizo ni EPZ si mje mtubatize EPZ na sisi tupate hivyo viwanda tuweze kuuza nje? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunahitaji matrekta ili kuboresha kilimo ili kuweza *ku-feed* lile soko mahindi. Tusiachie Wizara ya Kilimo peke yake, Wizara ya Viwanda na Biashara na ninyi ni jukumu lenu kuhakikisha matrekta ya bei nafuu yanapatikana ili kubadilisha kilimo chetu ili sasa hayo masuala ya viwanda na biashara, viwanda vinavyofanana na mazao ya kilimo viweze kupata nafasi yake. Utaona ile *systems approach* ninayoisema mimi ndio ambayo itatusaidia kutoka hapa tulipo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mfano mwengine rahisi. Kuna sehemu mmeanzisha EPZ kwa mfano mnaweza kuwa na viwanda 4,5,6 lakini mnahitaji lami kama ya nusu kilometa tu kuweza kuboresha njia ya kuweza kuingia kwenye viwanda vile lakini kwa sababu barabara sio ya kwenu ninyi, ninyi ni viwanda na biashara inashindikana. Sasa *systems approach* ndio itakayoweza kuboresha mambo haya mme-*allocate* mahali kuwa na kiwanda maji yatakwendaje, umeme utakwendaje pale, barabara itaboreshwa vipi ndio hiyo *systems approach* siyo sera moja moja ni sera hizi ziwe na mwengiliano wa pamoja, hili litatusogeza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vile vile katika eneo hili la biashara ambalo ndio mtazamo mkubwa wa dunia kwa maendeleo yetu na ndio njia ambayo itatusaidia kupambana na umaskini tunategemea sana maendeleo ya upashanaji habari (*information technology*). Tulikuwa kwenye *industrial age* sasa hivi tuko kwenye *technological age* hasa *information technology*. Bila habari za hakika na haraka hawezu ku-compete katika dunia ya sasa, huwezi kushindana hata kidogo. Lazima ujue soko liko wapi, ni bei gani na kwa namna gani uweze kuwasiliana haraka kabisa. Kwa hiyo, anayewasiliana haraka ndiye anayepata soko, ndiye anayeuzua. Kwa hiyo Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Sayansi na Teknolojia tupate *computer*, simu hizi na vifaa vingine vinavyohitajika na Wizara ya Nishati lazima umeme usambae nchini, mbinu hizo ndizo zitakazosaidia kibiashara tuweze kushindana.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana Serikali hii imejitahidi sana upande wa mawasiliano sehemu nyingi sasa zina simu za uhakika hizi za mkononi zinatusaidia sana kimawasiliano. Lakini naomba sana ikazanie kutoa mwelekeo maalum katika kuboresha masuala ya *information technology* bila hivyo hatuwezi kushindana hata kidogo. Wenzetu Malyasia wameweka lengo wanasema katika miaka 10 ijayo wanataka wawe ni nchi iliyoendelea kama Japan lakini kwa sababu wamewekeza sana hapa kwenye *information technology*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nadhani litakuwa la mwisho katika eneo hili hili la kuboresha biashara ni eneo la watumishi wa Serikali (*civil service*) yenyewe. Lazima watumishi wa Serikali sasa wabadilike wasaidie sekta binafsi kuweza kupata

nafasi ya kufanya kazi kwa kufuata sheria na taratibu zilizopo badala ya kuwa na taratibu na sheria ambazo ni kikwazo kwenye biashara.

Mheshimiwa Waziri ametuambia hapa *January* mwaka ujao tunaanza *Customs Union* na Kenya na Uganda. Ili tuweze kwenda speed inayopaswa lazima watumishi wetu ndani ya Serikali wawe na *speed* ambayo inahitajika katika kufanikisha masuala haya ya kibiashara. Mtu ana *order* yake tarehe fulani anatakiwa aifikishe mahali fulani, hivi na hivi lazima *procedure* zile ziwe za haraka, uhakika, hazina ubabaishaji, hazina rushwa. Lazima utamaduni huu tuujenge, *corporal governance* tusipojenga uharaka huo hatuwezi kushindana katika ulingo huu tu wa Afrika Mashariki lakini zaidi hatuwezi kushindana huko nje.

Mheshimiwa Spika, lakini watumishi hawa wa Serikali hawawezi kujenga hiyo kama mazingira yao hayataboreshwa, kama sheria zilizopo haziwapi kujisukuma na kujituma. Kwa mfano kuna upunguzaji wa watumishi ambao umefanyika juzi (*retrenchment*). Mtu anapunguzwa anaambiwa kwa sababu una miaka inayozidi 50 kwa hiyo hatalipwa kiunua mgongo chako. Sheria kama hizi tunazo za nini? Bado zipo za kazi gani? Umeamua kumpunguza mtu kwa nini usimlipa haki yake huyu mwenye miaka 5 kazini unamlipa huyu unasema kwa sababu una miaka 50 na kuendelea hatukulipi, kajipunguza mwenywewe? Kwa nini katika dunia ya leo tunakuwa na sheria za aina hiyo?

Lazima tuzitazame sheria zetu hizi ziwatие moyo watumishi wa Serikali kuweza kuitumikia Serikali yao kwa uadilifu, uaminifu na kwa haki kama tunavyotaka iwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia, ahsante. (*Makofii*)

**MHE. SALOME J. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyomezani ikiwa ni hotuba ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Ali Mchumo, pamoja na Mama Fatma Said Ali Mchumo, kwa *post* ya Ukarugenzi wa *Common Fund for Commodities (CFC)* ushindi waliouputa hivi majuzi. Nampongeza Mheshimiwa Balozi huyu ambaye tunajua zamani alikuwa ni Waziri wa Wizara hii ya Viwanda na Biashara na mchapakazi mzuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Waziri Ngasongwa na Naibu Waziri Mama Rita Mlaki, pamoja na timu yao kwa kazi nzuri sana waliyofanya katika kipindi kilichopita lakini pia kwa mipango mizuri sana ambayo wameipanga kwa kipindi kijacho.

Mheshimiwa Spika, naomba nitambue kazi nzuri inayofanywa na Waziri Ngasongwa. Waziri Ngasongwa anafanya kazi kama sisimizi. Ninaposema sisimizi nina maana nzuri sana. Sisimizi mara zote unamwona anakimbia huku na kule, mara

anachukua hiki analeta huko mara anachukua cha huku anapeleka kule ili mradi kufanikisha kazi. Ninaipongeza sana Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza, nikiwa kama Mbunge wa Kamati, nina machache tu ya kuchangia. Ninaomba nianze na suala la *Open Market* au *Sunday Market*. Suala la *Sunday Market* limeanza Mkoa wa Dar es Salaam na naomba nimpongeze sana Mheshimiwa RC, nina hakika ame-coordinate na Wizara hii.

Wafanyabiashara wadogo wadogo mara nyingi walikuwa wanakimbizana na Askari wa Jiji na walikuwa hawana mahali ambapo ni halali pa kufanya biashara. Utaratibu huu wa *Sunday Market* ni utaratibu mzuri kwa sababu utakuwa umekidhi kiu ya wafanyabiashara hawa wadogo kwa kuweza kufanya biashara kwa amani na utulivu bila kukimbizwakimbizwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ninaomba suala hili la *Sunday Market* lihamie katika kitu kinaitwa mitaa ya biashara. Mitaa ya biashara ni kitu *permanent* maeneo fulani, mitaa fulani, *blocks* fulani zinatengwa ili wafanyabiashara wadogo wadogo wakiwemo akina mama waweze kufanya biashara *permanently* katika maeneo hayo.

Ni matumaini yangu utaratibu huu wa *Sunday Market* utaendelezwa kuwa mitaa ya biashara na hivyo kuleta amani kwa kiasi fulani kwa wafanyabiashara ndogo ndogo na hasa sekta isiyokuwa rasmi katika Mkoa wa Dar es Salaam na Mikoa mingine nchini Tanzania.

Katika hili mifano iko mingi ukienda katika nchi za wenzetu Misri, Bangkok, Uchina kote wana utaratibu huu na ni utaratibu mzuri sana na mara nyingi maeneo haya yanakuwa katikati ya Mji au Jiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba niongelee juu ya Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam. Kwanza niipongeze Wizara hii kwa maandalizi mazuri na namna walivyojituma hadi nchi nyingi zimeweza kushiriki. Niki *zero in* kwa akina mama naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mama Anna Mkapa kwa juhudzi zake ambazo amefanya tangu mumewe aingie madarakani katika kufanikisha akina mama kushiriki katika maonyesho haya.

Akinamama hawa mbali na kupata *exposure* wanajua vile vile namna ya kufanya biashara kwa namna iliyo bora zaidi, kujua *standards, packaging*, namna ya *finishing* ya *products* na kadhalika na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lakini ningewomba Mheshimiwa Waziri suala hili aliangalie vizuri kwa sababu mwaka huu ushiriki wa akinamama kutoka Mikoani ulipungua kiasi na ndiyo maana katika mabanda mengi ya banda hili la akinamama walionekana wengi ni makampuni au *NGOs* za akinamama wa Dar es Salalam.

Kwa hiyo ina maana kwamba akinamama kutoka Mikoani walipungua. Mimi nilipofuutilia niliambiwa kwamba safari hii ufadhili haukuwepo, kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri kama anaweza kushirikiana au aka-coordinate na Wizara ya

akinamama kuhakikisha kwamba akinamama hawa wanafadhiliwa na Mikoa yao ili waweze kushiriki katika maonyesho haya kikamilifu.

Kwa kweli kama tunavyojuu akinamama wengi hawana uwezo hasa wa Mikoani, kama tutawaacha wajitegemee basi banda lile la akinamama litajaa watu wa Dar es Salaam. Namwomba Mheshimiwa Waziri aweze kulichukua hili na kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba niongee juu ya *Internet centers*. Mimi nafikiri umefika wakati pamoja na umaskini wetu, pamoja na sisi kuwa katika dunia ya tatu tuwe na *internet centers* katika kila Makao Makuu ya Wilaya. Napendekeza hivyo kwa sababu tumewahamasisha sana wananchi wetu na hasa akinamama kushiriki katika biashara ya Kimataifa.

Sasa wakiwa Vijijini kwao sidhani kama wanaweza kujua kinachotokea ulimwenguni endapo hatutakuwa na *internet centers*. Napendekeza tuteue *agent* kila Wilaya, wawe *trained* katika masuala haya ya *ku-surf* na kutafuta market, bei, kutafuta vitu gani vinatakiwa wapi ili kutoa *information* hizo kwa hawa wajasiriamali wanaojitokeza katika maeneo yetu ya Wilaya mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba nigusie kidogo juu ya suala la *Supermarket* ambazo zimezuka sana hasa katika Miji mikuu na hasa katika Jiji la Dar es Salaam. Naungana sana na wale waliochangia kwamba maduka haya yanauzu bidhaa nyingi tu kutoka nchi za nje wakati wanaacha bidhaa zetu solemba.

Mheshimiwa Spika, mimi huwa najiuliza, sawa, tunataka *standardization of products* labda machungwa yetu hayana size inayotakiwa, labda mapapai yetu makubwa mno au labda mananasi yetu ni makubwa mno. Lakini ni bidhaa hizi hizi ambazo soko la ndani linahitaji. Sasa kwa nini tusiwe na *categorization* ya soko la ndani na soko la nje. Soko la ndani wauze *size* za matunda ambazo sisi tunataka. Sisi tunataka matunda makubwa labda soko la nje linataka matunda madogo, kwa nini kusiwe na *categorization*. Kwa hiyo, nafikiri ni kazi yetu sisi sote Serikali na Wizara hii kuweza kushauri na *ku-intervene* kwa kweli kama alivyozungumza Mheshimiwa nafikiri Mbunge wa Singida pale kwamba ni lazima *at one point or the other* Serikali iweze *ku-intervene* katika masuala ya *investors* walio katika nchi hii, tusiache waende holela tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nigusie vile vile suala la *Export Processing Zone*. Sijui tuongee kwa uchungu gani, *NDC* imekabidhiwa jukumu hili lakini wanapata sh. 50m/= tu kufanya kazi hii kubwa katika Mikoa iliyoteuliwa ya kuanzisha *Export Processing Zones*. Sijui tumshauri Mheshimiwa Waziri Ngasongwa aombe vipi na yeye aweze kupatiwa hela nyingi ili aweze kuzipatia taasisi zilizo chini ya Wizara yake fedha za kutosha. Sijui wenzake huwa wanaombaje fedha mpaka wanapata nyingi.

Lakini ni vema ikafahamika kwamba pamoja na kuendeleza barabara, kutoa wanafunzi wengi mashulenii kwetu, pamoja na kuendeleza sekta za kilimo na kadhalika tutahitaji viwanda na biashara kuendeleza yote hayo. Ni lazima kuwe na *forward and backward linkages*, sasa kukiwa na barabara nzuri mkulima amelima, amepata mazao

mazuri, anasafirisha anapeleka kwenye kiwanda gani kama Wizara hii haiangaliwi. Wizara hii inapata takriban shilingi 9bn/= tu lakini kuna Wizara nyingine zimepata zaidi ya 100bn=/. Sasa mimi nafikiri pamoja na ku-*identify sectors* ambazo tunafikiri ni muhimu kwa mfano barabara, mashule na kadhalika, lakini sekta ya viwanda na biashara ndio itakayotuvusha katika ku-*process* na kufanya *exports* na namna hiyo kupata *foreign exchange* ambayo mara nyingi tuna *deficit* katika hesabu zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niongee juu ya *Fair Competition Commission* (Kitengo cha Udhibiti wa Biashara). Katika biashara ya ushindani ni lazima faulo nyingi zinatokea, lakini ni lazima kuwe na refa wa kupuliza kipenga pale inapohitajika. Mimi nikiri kwamba kitengo hiki pamoja na kwamba najua kipo lakini sijakiona kinafurukuta, sijakisikia kikipiga filimbi hata siku moja. Nitoe mfano mdogo tu ni hivi majuzi daladala ziligoma Dar es Salaam, lakini tulisikia filimbi ikipigwa na RC Mheshimiwa Makamba, hatukusikia kitengo hiki kikifurukuta. Naomba kitengo hiki kwa kweli kiamke zaidi kwa sababu sasa hivi kuna mashindano ambayo si *fair*. Kwa mfano, viwanda vya nguo kuibiana *designs* za khanga au nguo mbalimbali lakini hatujasikia wanapiga kelele. Kuna suala la *Kibo Breweries*, labda limepita ni la zamani, lakini hatukusikia kikipiga kelele na kadhalika. Mimi naomba kitengo hiki cha *Fair Competition* kifanye kazi yake kwa sababu kimeingia katika uchumi huru ambaa una *competition* kubwa na namna hiyo wengi wanakiuka taratibu na hivyo ni lazima wawe tayari kupiga kipenga.

Mheshimiwa Spika, nikikaa bila kuisifu *SIDO* nitakuwa sikujitendea haki. Naomba nichukue nafasi hii kuipongeza sana *Management* mpya ya *SIDO*. Kazi ni nzuri, naomba waendelee na moyo huo. Watu hawa wana utayari na ukarimu, ukienda pale wanakupokea vizuri, wanakusikiliza shida zako na wanakusaidia. Naomba Wizara isiiache *SIDO*, iendelee kuipa kila *support* inayohitajika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuzungumza juu ya sekta isiyo rasmi. Sekta isiyo rasmi kwa hesabu nilizo nazo mimi inachangiwa kwa kiwango cha asilimia themanini hivi na akinamama. Sasa ningependa kujua Wizara hii inaisaidiaje sekta isiyo rasmi katika masuala ya ku-*coordinate* shughuli zao, kuwasiliana na Wizara mbalimbali ili mradi sekta hii ipewe *position* yake inayostahili.

Mheshimiwa Spika, vile vile ningependa Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* atuambie ni namna gani uchambuzi na *quantification* ya *value* ya mchango wa sekta hii unavyoingizwa katika pato la Taifa. Kwa sababu mimi nina wasiwasi mbali na kwamba sekta hii inachangia kwa kiasi kikubwa sana katika uchumi wa pato la Taifa, sina hakika *significance* yake katika kufanyiwa hesabu ni namna gani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na kwa kuwa nilianza kwa kusema kwamba nina machache naomba nimalizie hapo. Napenda kumpongeza tena Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na timu yake pamoja na watendaji wote wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hii kwa kuendelea kufanya kazi nzuri

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie katika hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Kwanza utaratibu ambao umeupanga kwa mujibu wa kanuni ya Bunge kuanzia Ibara ya 89 mpaka Ibara ya 103(b) kwa kuzipanga zile kanuni za kisekta ambazo mimi nimo katika Kamati ya Biashara na Uwekezaji.

Kwa hiyo, nilipata muda mrefu sana kwenda kwa kina kurasa kwa kurasa, kwa hiyo *figures* na majedwali ambayo yamo humu tuliyapitisha sisi hapa. Kwa hiyo, nashukuru sana kwa hayo. Hapa ninazungumza ya kisera tu. Nimesema Wabunge tuhoji sera na hela, kuhoji kudra ni kufuru. Sasa hapa nahoji mambo ya sera. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza napenda kufanya masahihisho kidogo, sijui kama nitakuwa sahihi mimi au vipi. Kwa sababu hii imeingia kwenye *Hansard* kule, wakati akisoma mwakilishi wa upande wa Upinzani, ukurasa wa 13 kwenye hitimisho kuna Kiingereza kimeandikwa pale *once and forever*. Sasa kwa Kiingereza nadhani kama cha Makerere ambako Mheshimiwa Spika ulipita kule, mimi nimeweka maneno fulani yanasema *once and for all*, nadhani hiyo itakuwa sahihi zaidi kuliko *once and forever*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nimesema Wizara hii inaitwa Wizara ya Viwanda na Biashara. Naomba nichukue nafasi hii kukubaliana nilipobisha vikali sana, niliposema kwamba sekta ya viwanda nchini iwe ni sekta kiongozi, mimi nilibisha kwa nguvu zote, nilisema sekta kiongozi ni kilimo. Kumbe kilimo ni uti wa mgongo wa nchi hii, hakiwezi kubeba wananchi kwa utaratibu huu ambao tunakwenda. Nimekwenda kwenye *internet* nikacheki idadi ya Mawaziri toka uhuru, nikamkabidhi Waziri Mkuu, Mawaziri ishirini na nne.

Majina ya Wizara ya Kilimo yakabadilishwa toka *Mereleck Brison* ilikuwa Wizara ya Kilimo na Misitu, ikaja ikabadilishwa mpaka sasa hivi Wizara ya Kilimo na Chakula. Nashukuru sasa nataka nitangaze kwa sababu ambazo nitazitoa kwamba Wizara hii ya Viwanda na Biashara iwe sekta kiongozi ili kusudi baada ya kujaza mafuta gari yako muda mrefu, baada ya kubadilisha madereva ishirini na nne, ukafanya *over whole engine* halafu gari haiendi unakusudia nini? La msingi unachukua hela unajaza mafuta kwenye *brake down* ili ibebe gari liende.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuanzia leo kwamba *brake down* iwe Wizara ya Viwanda na Biashara ili ibebe kilimo na sekta zingine mtambuka ambazo zimo mle ndani. Hilo ni tangazo dhahiri kabisa, natangaza kwamba Wizara ya Viwanda na Biashara, lakini pamoja inaitwa Wizara ya Viwanda na Biashara ipo kama Kawizara fulani, kama Kawizara kadogo ambako kanaonekana kwa pembeni ambacho hakioneckani kama ni *pseudo Ministry*. Kuna hii inayoitwa biashara ya viwanda nayo ni *PSRC*. Kwa hiyo Wizara ya Viwanda na Biashara na Biashara ya Viwanda zinapambana, kaeni pamoja ili kusudi mwende pamoja. Naona hii Wizara ingeitwa Wizara ya Biashara au Viwanda vya Biashara, hivi viwanda vinavyouzwa au iitwe biashara ya viwanda ili tuuze viwanda vyetu tubaki bila kitu. Lakini kwa sababu mnasimamia sera hamtaki viwanda na

Serikali imejitoa katika biashara mnafanya kusimamia na kudhibiti matokeo. Mnafanya kazi nzuri tu na tunawapongeza kwa hilo na ndio haya mafanikio ambayo mmeyatoa na mmeyaleta mbele yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bada ya kusema hayo nilitaka kusema kabisa kwamba kuna vyombo veya udhibiti na vyombo veya utafiti. Vyombo veya utafiti tuliviona jana. Nimefurahiwa sana na ule mradi wa Chaki ambao unawezekana kabisa kwa wananchi, mimi tayari nimeshamwambia Mkurugenzi pale wa mradi wa Chaki wa *TIRDO* kwamba nitachukua walimu karibu 200 kutoka Vijiji veya Jimbo langu kwenda kufanya kozi ya kutengeneza chaki kutokana na *gypsum* kwa utaratibu wa kutumia mwanga wa juu tu. Hii ndiyo teknolojia nyepesi na sahihi ya kuwapelekea Watanzania. Tositengeneze teknolojia ya kisasa ambayo ni sahihi lakini haiendi Vijijini, inaelekeza mpango wa Mijini, kwa mfano, mitambo ambayo yenyе umeme tutengeneze teknolojia inayoshughulikia *physical* ya kutumia vitu ambavyo vinatumika kwa mitulinga au kwa hewa na vidogo vidogo vinavyomlenga Mtanzania wa kawaida ama sivyo tunaingiza nchi yetu kugundua viwanda vikubwa badala ya viwanda vidogo vidogo ili Watanzania waweze kushiriki katika kujikwamua kwa umaskini. Nimesema Tanzania ni nchi maskini siyo nchi changa kwa sababu tumepata uhuru miaka arobaini iliyopita na kama tukijaji kwa umri wa mtu, basi tuite ni kijeba, lakini siyo neno zuri, kwa sababu hatukui kiuchumi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hii inatokana kwa sababu moja, Tanzania inakua kiuchumi, aidha, Tanzania inakua kweli kiuchumi, lakini kuna wenzetu ambao ni walafi wanakula kwa kutumia makoleo badala ya kutumia vijiko veya kawaida. Hivyo huchota vyakula veya wenzao pamoja na vijiko veya wenzao. Hili lipo ndani ya uwezo wa Serikali tutatafutana, kutazamana wenyewe kwa wenyewe ili kuambizana kwamba wewe mwenzetu acha koleo tumia kijiko cha kawaida. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, au ndani ya sera zenyewe utekelezaji wake hatuuelekezi kwa walengwa. Kwa hiyo tuna siasa ya makengeza kuangalia tusikokwenda au kwenda tusikoangalia. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu huu basi katika Wizara ya Viwanda na Biashara nimependekeza sasa baada ya kuwa na idara ya viwanda na biashara, *Fair Competition, mipango, accounts and technology*, kwa hiyo tungependekeza kuwepo na kitengo kinaitwa *monitoring* na kuunda dawati la biashara la kila Wizara ambalo ni kama utaratibu wa jinsia waliouweka kwamba kuweka dawati kila Wizara ili kuweza kusimamia masuala ya jinsia. Sasa napendekeza Wizara ya Viwanda na Biashara lakini siyo kwa fedha hii, lazima kuwepo na mchango na nimesema michango midogo midogo haisaidii kwa sababu ingekuwa inasaidia basi Matonya angekuwa na maghorofa sasa hivi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuujenga uchumi wa nchi yetu kwa kuwapa wawekezaji mapromota ambao wana-beep uchumi wa nchi yetu, wale tutawaangalia kwa macho ambayo si ya husuda bali ni ya ukali zaidi ili waweze kama wana uwezo wa kutaka kuendeleza, anachukua kiwanda miaka kumi hakifanyi kazi kipo tu,

wanakichungulia tu kama mzimu, hauendelei. Kwa hiyo, watu kama wale tunawaambia ole wenu, mchezo wenu ni mauti kwetu, tutaamua sasa hivi, magolikipa wazuri wapo kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara tukaunyang'anya mpira huo tukaudaka tukaurudisha tena uwanjani, ni kuwanyang'anya viwanda hivi na kuweza kuvisambaza kwa watu wengine wenyewe uwezo wa kuviedeleza viwanda hivyo badala ya kubaki na watu hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyombo vya udhibiti *TBS*. Nashukuru sana kwa utaratibu mnaoufanya nimeona sampuli ambazo mlikuwa mnazi-*analyze* kwa kutumia mitambo ya sasa hivi lakini wanawazidi kete. Zipo bidhaa ambazo ni hafifu na zimepitwa na wakati wake zipo katika *Supermarket*, muwe na ukaguzi wa kustukiza. Kwa bidhaa ambazo zinapimwa kabisa unakuta zimeshafungashwa, zimeandikwa kilo mbili, una uhakika kweli ni kilo mbili, ukishaiba kwa mfano robo kilo au asilimia kidogo tu kwa mifuko mia mbili, tayari ishaibiwa Tanzania kwa ujumla. Kwa hiyo pimeni upya vile vitu vilivyofungwa kabisa kama ni kilo mbili kweli au kilo moja kweli. Hiyo ni kazi ya Kitengo cha Mizani na Udhibiti wa Bidhaa, mfanye kazi hiyo kwa usimamizi wa vitu kama hivi.

Mheshimiwa Spika, pengine bidhaa ambazo zinakaa muda mrefu, vingine havinunuliwi kwa mfano vitu kama juice na aina za vyakula ambavyo vinakuja muda mrefu lakini bado vipo, vimekaa, havinunuliwi. Sasa vile haviandikwi *expiring date* na ama *expiring date* inaandikwa kwa kugongwa na mhuri. Sasa mhuri mtu anaweza kuchongesha akagonga. Sasa kuwepo na ukaguzi wa mara kwa mara wasije kuwaathiri Watanzania kwa vitu kama hivi. Vile havina haja ya kuangalia kwa kwenda kutumia *atom scope* au kucheki *gloma doglos* au vitu vingine bali ni kuangalia tu rangi, wajihii na harufu na vile vite na kuangalia kama hivi vitu vimeingia tarehe ngapi pale kiwandani Kitengo cha Forodha kuangalia pale kwamba vimekuja lini, utakuta bado *mango pico* zipo pengine miaka mitano ndani ya duka.

Kwa hiyo Serikali itangaze, wenyewe *mango pico* ambazo zina muda mrefu na kuitwa na wakati waya-*surrender* wenye, wayatupe kabla Wizara ya Viwanda haijafanya hivyo. Tunadhani watu wazuri wataweza kufanya hayo. Sasa hivi walikuwa wanasema kizuri chajiuza kibaya chajitembeza, niliwaambia wakati nabadilisha sheria kwamba vizuri sasa hivi ndio vinajitembeza, kwa hiyo vipo vingi lakini kibaya kinatupwa. Hicho kibaya kinajitembeza ili kifanye nini, kikanunuliwe? Vibaya hutupwa, narudia tena vibaya vinatupwa, Watanzania tuangalieni. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu taasisi na zana ambazo zinafanya utafiti. Wale waliofanikisha katika upande wa utafiti hongera andikeni *papers*, toeni *model*, halafu pelekeni katika idara ambayo inatengeneza ili ianze kusambaza teknolojia nyepesi na sahihi, isiwe teknolojia sahihi tu ambayo si nyepesi na haitumiki. Nilisema wakati mmoja hapa kwamba mtu mmoja alitengeneza teknolojia, akawa ghorofa ya kumi na mbili. Sasa chini pale kulikuwa na mtu anapita na maji, akataka maji. Teknolojia sahihi pale ilikuwa ni simu lakini wakati ule ilikuwa hakuna, teknolojia sahihi ilikuwa *loudspeaker*, amwite bwana mwenye maji nipo ghorofa ya kumi na mbili, niletee hapa, angesikia. Lakini alichokifanya akachukua teknolojia ya kisasa, akachukua *binocular*

akamvuta karibu akamwambia, nipo ghorofa ya kumi na mbili niletee maji, hawezi kusikia pamoja yupo karibu yako. Ni teknolojia ya kisasa lakini imetumika vibaya. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Watanzania tunapowaogopa wale wawekezaji ambao wamechukua viwanda vyetu wala hawaguswi, sawasawa na mtu ambaye amepewa adhabu ya dunia. Ukioma mwanaume mfupi jeuri jeuri tu wewe mwozeshe kwa mwanamke mrefu. Mwanamke mrefu atakuja nyumbani, kwetu kuna tabia moja, unakuja na mtungi halafu lazima mumeo akutue. Sasa anakuja kwa mfano mtu amebinafsisha kabeba mzigo wake, anakuja anakwambia haya nitue, halafu anasimama vile vile, sasa hufiki itabidi upande kwenye matofali uende ukamtue. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, yaani vyombo vyenyewe ambavyo vinabinafsisha vitu vyetu hapo mnawaogopa kwa kuwaambia kama vile watu ambao ni warefu, sasa wewe mfupi unapata adhabu hapa katika nchi yako mwenyewe, iliyopata uhuru miaka arobaini, tunashindwa kauli. Tuwaambie bila kuogopa na kama tunaona aibu, tuvae miwani ya juu. Halafu umwambie bwana sasa naomba, tafadhali sana, rudisha kile kiwanda. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hii kwa sababu hakuna mahusiano na ushirikiano mzuri kati ya sekta mtambuka ambazo Wizara zinazohusika na kitengo ambacho nilichokitangaza cha *PSRC*, unastukia tu kwamba sera tayari, kiwanda cha magunia kimeuzwa.

Watanzania wanataka magunia, kwa mfano kipindi kama hiki cha mazao wananchi wa kule Vijiini wameshavuna mahindi yao, sasa wanahitaji magunia. Nilikuwa napiga simu katika Vijiini kwa mfano kule Mkuyuni tunayo tayari ile simu ya siwaya, nilitaka kuongea na Katibu Tarafa sikumpata, nikaongea na mwenye simu, akasema kwamba sasa hivi tunahitaji magunia. Sasa hatuwezi kutumia magunia ya plastiki kwa kuhifadhia mahindi, kuna kitu kinaitwa *humidity*, yanaweza kuvunda kwa kupata *afratoxies* na yakasababisha sumu kwa wananchi.

Kwa hiyo Mheshimiwa Spika, tunaomba viwanda vya magunia viibuke. Tupewe *time frame* ya muda ambao magunia yanashindikwa hapa nchini, ndiyo hicho tu. Wananchi wa kule Luholole, Changa, Kibwaya, Mfumbwe, Logo, Uponda, Mifurwe, Heba, Bagilo mpaka Mkulazi kule wale wanavuna sasa hivi. Moja ya masikitiko ni kwamba wakati wa kilimo vyombo vya kulimia kwa mfano majembe yalikuwa yanakatika katika ovyo. Kwa mfano, dawa ya kuhifadhia nafaka unapoweka baada ya miezi mitatu wadudu wanashangilia mle ndani, hizi ndio dawa za *ku-beep*. Naomba nazo kama zime-expire, tafadhali sana, kabla ya kufanya *checking*, naomba Mkemia Mkuu wa Serikali, *PSRC* hivi ni vyombo tulivyokuwa tumeviacha kama *SP* yetu, *Andrews, Binalography* ambazo zimeharibika, hebu pimeni halafu toeni taarifa Serikalini na msitangaze tangaze kwenye magazeti au kwenye *TV*. Si vizuri sana huo udhibiti ukawa unasema kwamba dawa zimekamatwa halafu unakwenda kwenye *TV*, unafanya kazi kimya kimya, Serikali inafanya kazi kimya kimya siyo kutangaza kila kitu. Unastukia tu hivi vitu vimeshatupwa ili wananchi wawze kufurahia miaka arobaini ya uhuru ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nimesema nilikuwa katika Kamati hii, nimetoa mwelekeo tu na msimamo wa Kamati tuliyokuwa tunasema, lakini mengine niliyokuwa nimeyasema yalikuwa yanatoka kabisa ndani ya moyo wangu na nimeyasema haya kwa huzuni kabisa ili kusudi nchi ambayo iliyokuwa huru, inakuwa na demokrasia yenyeharama ingawa haina vipuri, kwa sababu kama haina vipuri basi inaleta vurugu baridi, kashfa za kina, maisha ya kusigana katika nchi zao. Kwa nchi ambayo inalinda watu wake basi inasimamia haya niliyoyasema.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ndiyo tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi. Kama nilivyokwishakueleza siku za nyuma kwamba, Wizara hizi zenyehiki moja moja mjadala wa jumla unaendelea mpaka saa kumi na mbili.

Kwa hiyo, ni nafasi ya kutosha kwa wachangiaji wengine wanenye wa dakika kumi na tano, kumi na tano. Hao wanenye watakaochangia mchana ni Mheshimiwa Ali Karavina, Mheshimiwa Khamis Awesu, Mheshimiwa Edson Halinga na Mheshimiwa Profesa Mbilinyi, wajiandae kwa kipindi cha jioni kabla watoa hoja hawajaanza kuhitimisha hoja yao.

Baada ya maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(*Saa 6.52 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. ALLY A. KARAVINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe shukrani zangu kwa kuniona tena leo mara ya tatu; na kwa kuwa nilishatoa utangulizi na kuwatakia kheri wale waliochaguliwa na kuwapa pole wale waliopata mikasa na maafa mbalimbali. Naomba leo niende moja kwa moja katika hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kusema kwamba mimi ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Sababu zangu za kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja nianze tu na hongera kwa Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwa ambavyo amekuwa anashughulikia kwa kweli masuala ya biashara na utetezi wa biashara ya nchi yetu dhidi ya athari hasa za utandawazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia pongezi sana kwa Mheshimiwa Rais kwa kuwa Mwenyekiti mwenza wa Tume ya Kimataifa ya Athari za Utandawazi kwa Jamii na pia kwa kuwa Mjumbe wa Tume ya Afrika iliyoundwa na Waziri Mkuu wa Uingereza. Lakini pia pongezi sana kwake Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwa kuteuliwa kuwa mratibu wa nchi maskini katika majadiliano hayo ya WTO na kwake kuwa Mwenyekiti

mwenza katika Mkutano wa Nchi maskini uliofanyika huko Dakar na baadaye mkutano wa Kigali na baadaye kushughulikia pia mkutano ule wa *Accra* na *Sao Paulo*. Hii yote inaonyesha jinsi gani nchi yetu ilivyo mstari wa mbele na Mheshimiwa Waziri ameshika hilo jukumu katika kuhakikisha kwamba majadiliano ya biashara ya Kimataifa ambayo hayaendeshwi kwa usawa hata kidogo nchi yetu inakuwa mstari mbele katika mapambano hayo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuwa mbele sana katika Mkutano ule wa *GSPT* unaolenga kuanzishwa kwa soko huru la biashara kwa ajili ya nchi za Kusini yaani *South South Trade*. Kwa sababu kwa kweli katika mazingira ya utandawazi hili ndilo eneo moja ambalo angalau na sisi tunaweza tukapata nafuu sana ya kuwa na msimamo wa kuweza kuendeleza nchi yetu kibiashara na kiviwanda. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mkutano wa Baraza la Utawala wa Mfuko wa Pamoja ambao mimi niwape pongezi tu Mheshimiwa Waziri, lakini sana kwa Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo mlivyofanya kampeni nzuri iliyohakikisha kwamba Mtanzania yule anachukua wadhifa huo kwa niaba ya wananchi wa Tanzania. Naomba muendelea hivyo kwa sababu kuna Watanzania wengi wenye uwezo na tunaamini wakati huu wa utandawazi ni muhimu kwa kweli wakashika nyadhifa katika Asasi nyingi za Kimataifa ili waweze kutusaidia kutetea maslahi ya nchi yetu. (*Makofî*)

Utandawazi kwa wakati tulionao sasa hivi hauepukiki na kwa kweli kwa hapa tulipo usiporatibwa vizuri unaweza ukaleta mvurugano ndani ya nchi vibaya sana. Lakini hii yote inakuja kwa sababu utandawazi unaambatana na kupunguza sana majukumu ya Serikali katika kuratibu utawala wa uchumi hasa katika sehemu kuu tatu za Taifa na sisi Watanzania kwa kweli mfumo wetu ulikuwa ulivyo. Sasa sehemu hizi tatu ni:- Moja, kulegeza masharti ya biashara ambayo inafanya nchi inaondoa zile *trade barriers* na kuijunga na biashara ya Kimataifa.

Pili, kulegeza masharti ya sera za fedha na *ku-adopt ile free float currency mechanism* ambayo kwa kweli kwa nchi ambazo zinaendelea kama zetu inachangia sana kufanya *exchange rate* iwe mbaya kweli kweli kama ilivyo ya kwetu, thamani ya fedha inashuka kila leo na matokeo yake mnajua. Chochote kile utakacho-*import* sasa ni aghali na chochote kile tutakachojitahidi sisi kuzalisha na kuuza nje, kwa sababu sasa tunalazimishwa katika utandawazi lazima tuuze nje tunakuza kwa bei ndogo kabisa. Masharti hayo hayo ndiyo yanasaki uwekezaji, *investors* wanakuja tu direct kuja kuwekeza, na kwa sababu unakuwa una masharti ambayo unalazimishwa kufuata basi wana-*invest* wakati mwingine kwa masharti yao wenyewe.

La tatu, ni ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma. Matokeo yake ni nini? Matokeo ni kwamba sasa *trans-national co-operations* ambazo zinaendeshwa Kimataifa zinakuwa na nguvu ndani ya mahusiano ya kiuchumi na ya kijamii katika nchi yetu. Jukumu ambalo kwa kawaida lilikuwa linaendeshwa zamani na Serikali na kwa nchi changa kwa kweli lilikuwa linasimamiwa na Serikali. Mwishoni kabisa nchi inakuwa haina nguvu kabisa katika kudhibiti uchumi wake na inaweza tusipoangalia, ikabaki

kuwa soko tu na chanzo cha malighafi basi na tatizo lake ni kwamba mnakuwa sasa *dumping ground* tu na maendeleo kunakuwa hakuna kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunakubali kwamba nchi yetu inategemea sana kilimo kama uti wa mgongo basi Wizara hii ya Viwanda na Biashara lazima sasa ijielekeze katika kusaidia kilimo. Viwanda ambavyo kwa kweli vinatakiwa vipewe kipaumbele sasa ni vile vya *Agro Processing* ambavyo sisi ndiyo tuna *advantage* kubwa. Maana yake *advancement* kidogo tu itakayopatikana katika *Agro Processing* ina-effect zaidi ya asilimia 80 kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo njia hasa sasa ya kuondoa umaskini ni kwa Wizara ya Viwanda na Biashara itusaidie katika kuanzisha viwanda vinavyotegemea malighafi ya kilimo. Lakini huwezi ukapata malighafi ya kuingia kwenye *Agro Processing* kama haujafanya matayarisho yafuatayo:- Viwanda vya zana za kilimo sasa hivi tumekuwa hata majembe tunaagiza kutoka nje, lakini tulikuwa na viwanda vyetu vya zana za kilimo. Kile kiwanda Mheshimiwa Waziri cha Mbeya vipi? Hivi hatuwezi tukaingia katika ubia na mtu binafsi ye yote yule ambapo Serikali ikawa na *share* kidogo ili tuweze kuhakikisha kwamba zana za kilimo zinapatikana hapa hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na kiwanda cha mbolea Tanga. Sasa utaendeshaje kilimo kwa mbolea nyingi kama hii inayotakikana katika nchi hii yote kuagiza kutoka nchi za nje. Utazalisha fedha kiasi gani kwa *exchange rate* hii ambayo tunauza rahisi na *ku-import* ghali, utaleta mbolea kiasi gani ya kutosha ili uweze kujikombua kwa kweli katika kilimo, si rahisi. Njia rahisi Mheshimiwa Waziri ni lazima turudishe kiwanda chetu cha mbolea hata kama kilikuwa na athari za mazingira Tanga basi kwa nini tusikijenge kule Minjingu kwenye malighafi yenye kuna tatizo gani? Kwa nini *tu-import* mbolea wakati tuna malighafi ya mbolea. (*Makofi*)

Pia nishati katika viwanda hivi vya kilimo ni muhimu sana. Mimi sielewi mbadala wa *Tipper* ni nini mpaka sasa ni mafuta haya ya kuagiza kutoka nje katika hali hii? Kweli tutaendelea katika mapinduzi tunayotaka ya kilimo kwa mfumo huu, kwa mafuta ambayo wakati wowote yanaweza kupanda bei kwa matakwa tu ya wafanyabiashara binafsi! Mheshimiwa Waziri ushauri wetu ni kwamba hayo mafuta yanauzwa siyo katika soko huria yanauzwa katika *cartel* mojawapo ndiyo maana unaona yote yanapanda bei kwa wakati mmoja na yote mkiyalazimisha yanafuata vile yanavyofuata kwa namna moja, kwa sababu ni *cartel* hakuna soko huria kuna soko holela tu kwenye mafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda sasa kuzalisha ule umeme wa makaa ya mawe Mchuchuma lazima kile kiwanda kianze Mheshimiwa Waziri sababu hakuna. Sababu ya kuambiwa kwamba wazalishe chini ya megawati 400 zile wanazozitaka kuzizalisha pole pole kwa sababu mahali pa kuuza ni tatizo si kwa kweli wazo la busara kwa Wizara ile inayohusika. Hawa waacheni wazalishe *TANESCO* atanunua kama mtu mwingine utakaobaki waacheni wafanye *marketing* wao wenye. Lakini umeme ule usiingizwe kwenye ughali wa umeme wa *TANESCO* uachwe tu angalau tuwe na *source* moja ya umeme wa bei nafuu nchini ili iwe *attraction* kwa viwanda kule. Pia

Mheshimiwa Waziri sasa nafikiri imefika wakati kwa kutumia ule umeme wa Mchuchuma na kwa sababu tunataka *Agro Processing Industries* zirudi kutakuwa na mahitaji ya chuma mengi kwa nini sasa Liganga isianze pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini wakati wa kuanzisha Kiwanda cha Chuma umefika. Tusingojee mpaka tukajikuta tunauza ile chuma tena kama malighafi, kwa sababu tu tuna masharti ya kuonekana lazima tubaki ghafi ghafi. Mheshimiwa Waziri nafikiri hili ni la muhimu sana ni lazima lizingatiwe kwa kweli na lazima kiwanda hiki kianze. Sababu zenyewe ni nini kama tutakuwa na umeme wa kutoka Mchuchuma na umeme ule ni megawati 400 na Wizara husika ilikuwa inalalamika kwamba umeme utakuwa mwingi. Hivi ukitumika pale kwenye Liganga kweli utakuwa ni umeme mwingi huu au ndiyo utatosheleza tena kwa bei nafuu. Tunataka chuma itakayozalishwa iwe ya bei nafuu na nishati itakayotumika iwe ya bei nafuu ili iwe malighafi sasa katika ujenzi wa viwanda vyetu hapa hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Wizara hii kuitia *NDC* ina uelewa mzuri sana wa uchumi wa jiografia wa nchi hii na uelewa mzuri sana wa namna ambavyo kanda zile za maendeleo zinavyofanya kazi, hususan *spatial development initiatives*. Wizara ya Viwanda na Biashara basi ikishauriana na Wizara ya Ujenzi hebu Watutengenezee tafsiri sahihi kwa uharaka na ghamra na faida ya biashara hii ya uchumi wa jiografia ili angalau sasa iweze kuwa ndiyo njia rahisi ya *accumulation*, tuweze ku-*accumulate* sasa kiwango cha fedha cha kuweza kujenega viwanda vingine. *Source* ya kuweza kufanya *accumulation* ya kujenga viwanda ipo na ndiyo huo uchumi wa jiografia wenzetu huko Kenya na Uganda sasa hivi wanashirikiana na wanataka kubinafsisha mambo yao kwa pamoja ili kupambana na sisi katika *competition* ya huu uchumi wa jiografia kwa soko la Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri ili tuumudu utandawazi Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii yeye ana umuhimu wa pekee katika kuhakikisha kwamba biashara hii inafanikiwa na biashara hii inafanyika. Kwa kweli pengine akisaidiana na wenzake awaonyeshe namna gani basi biashara inayotokana na uchumi wa jiografia inaweza kutumika ku-*integrate* uchumi *local* na kuuinua kwa haraka haraka ili uweze ku-*play part* yake katika utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ya muhimu niliyotaka kusema ni hayo. Lakini pia ningeomba labda kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge wenzangu na kuieleza Serikali kwa kweli kwamba jamani Wizara hii kama tunataka kupambana na athari ya utandawazi basi Wizara hii. Hizi fedha zinazotengwa kwa ajili ya Wizara hii hazitoshi kabisa. Mimi nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri maana yake kafanya kazi ya kutosha kupambana kule kwenye *WTO* na kwenye mikutano mingine yote kwenda kutetea biashara yetu.

Lakini kwa kiwango cha fedha ambacho tunakiidhinisha kwa Wizara ya Viwanda na Biashara kama tunataka kweli tupambane na athari za utandawazi basi fedha hizi hazitoshi na nafikiri katika mwelekeo wa bajeti zinazokuja ingekuwa ni vizuri basi Wizara ya Viwanda na Biashara ikapewa umuhimu wa pili tu kwa kilimo. Tukielewa fika

kwamba utandawazi sasa hivi hauepukiki na ni lazima sisi wote tuogelee humo ndani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi nataka nirudie tena kwamba nina-*support* bajeti kwa asilimia mia moja. Namtakia Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wote kheri na utekelezaji mwema katika shughuli zote walizotueleza katika hotuba yao hii. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie machache katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kabla sichangia nachukua nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri Dr. Juma Ngasongwa, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Maafisa wote wa Wizara hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nafasi ya pekee ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri ni kwa sababu amefanya kazi kubwa hasa wakati tulipokuwa tunatembelea Viwanda vya biashara mbalimbali. Mimi kwanza ni Mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara tulikuwa tunazunguka naye Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kama vile siyo Mawaziri katika Wizara hii, walikuwa wanaonekana tu kama ni Wajumbe wa kawaida, lakini kwa vile wao wanajali kazi zao tulikuwa tunafuatana nao kwa pamoja mpaka tukamaliza ziara hiyo basi nawapongeza sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine mimi mchango wangu nataka niuelekeze katika Kiwanda cha *Tipper* kile kilichopo pale Kigamboni Dar es Salaam. Ongezeko la kupanda kwa bei ya mafuta Tanzania kwa mawazo yangu limesababishwa na kufa kwa Kiwanda cha *Tipper* cha kusafishia mafuta.

Kiwanda kile ninavyokumbuka kilikuwa kinafanya kazi nzuri tu na tulikuwa tunaagiza mafuta ghafi kutoka nchi za nje tunayapeleka pale Kigamboni yale mafuta yanasa fishwa, gharama ya usafishaji ilikuwa ni ndogo tulikuwa tunapata mafuta ya taa, dizeli na petroli. Sasa hivi ninavyoongea mafuta ya petroli hapa Dodoma lita moja ni shilingi 910, dizeli shilingi 850/=, mafuta ya taa 800/= naamini kama kiwanda kile kingekuwepo bei hii isingelikifa hivi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nataka niulize sisi huku tunahangaika na kufanya kazi ya kuimarisha nchi yetu na kuimarisha Mashirika ni sababu zipi zilizosababisha kufa hiki Kiwanda cha *Tipper*. Sasa nafikiri Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho si vibaya akaliambia Bunge hili kwamba kuna sababu zipi zilizosababisha kiwanda cha *Tipper* kikafa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi naishauri Wizara kiwanda kile wakitupie jicho la huruma ili tuondokane na huu mzigo mzito wa mafuta. Ongezeko la kupanda kwa bei ya mafuta sasa hivi limetuletea janga kubwa.

Mafuta yakinapanda bei kila kitu kinapanda bei. Bei ya nauli ya daladala pale Dar es Salaam kutoka shilingi 150 mpaka shilingi 250, bei ya nauli ya meli kutoka Unguja na Pemba kuja Dar es Salaam mwaka uliopita tu pale zile *speed boat* ilikuwa shilingi 13, 500 lakini sasa hivi nauli ni shilingi 14,500 na kama bei ya mafuta itapanda zaidi je, hao wanyonge waliokuwa hawana uwezo wa kusafiri mara kwa mara itabidi wawasiliane kwa barua kwa sababu kupigiana simu pia hawawezi. Kwa hiyo mimi naomba tuangalie suala la kiwanda cha *Tipper* ili tuokoe hili jahazi la kupanda kwa bei ya mafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kero nyine ambayo nimeiona mimi ni kiwanda cha kutengeneza zana za kilimo cha *UFI* pale Dar es Salaam kama alivyo sema Mheshimiwa Ally Karavina. Pamoja na kuwa kuna Waheshimiwa Wabunge wenzangu wanapiga vita majembe ya mkono lakini tupende tusipende lazima majembe hayo tutakuwa nayo tu. Kwa sababu huwezi ukalichukua trekta ukalipeleka juu ya Mlima pale Bumbuli haiwezekani hata kidogo.

Kwa hiyo, majembe ya mkono na zana zingine za kilimo ambazo tulikuwa tunazipata pale *UFI* ni vizuri kile Kiwanda kifanyiwe ukarabati ili kifanyiwe kazi kama kawaida. Katika ukurasa wa 35 kwenye hotuba yake Mheshimiwa Waziri ameeleza tu hapo kwamba kiwanda cha *UFI* kimebinafsishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi wakati mwingine huwa najiuliza tu hivi hawa wanaochukua dhamana ya hivi viwanda vilivyobinafsishwa, hivi wanafanya kazi kweli au wanavichukua tu ili Serikali ya Tanzania ipate hasara! Mimi naomba tuangalie vizuri vinginevyo tukiendelea kuvibinafsisha tu hapa matajiri wanaweza wakachukua viwanda baadaye wakaviua sisi tuking'ang'ania kuvibinafsisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka niseme kwamba wale wote ambao tumewakabidhi viwanda kwa nia nzuri lakini utekelezaji wao haujulikani basi naomba wanyang'anywe wasiibebe mzigo Serikali yetu. Kwa hiyo, naomba wanyang'anywe na watafutwe watu wenye uwezo wa kuviedesha hivi viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka nilizungumzie, mimi mara nyangi huwa nakaa pale Dar es Salaam na sisi Wabunge ndiyo tunaopata matatizo mengi au maneno mengi kutoka kwa wafanyabiashara wadogo wadogo. Pana kero pale Dar es Salaam naamini si Dar es Salaam tu hawa wafanyabiashara wadogo wadogo pengine wanauza nguo, wanatembeza masufuria mkononi wakati mwingine wananyanyaswa tu.

Sasa mimi naomba tungewatafutia utaratibu maalum ili na wao wajisikie vizuri kwa sababu na hawa ndiyo ajira yao. Serikali imeshasema kwamba haina uwezo wa kuajiri watu wote wakapata kazi Serikali. Sasa hawa wanaofanya biashara ndogo ndogo ni vizuri tungewatafutia njia maalum ya kuwaondolea kunyanyaswa ili na wao wawezekiti riziki kwa kazi zao wanazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa kweli mchango wangu nilitaka niuelekeze katika maeneo hayo. Sasa bila kupoteza muda naomba niseme tu kwamba ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo maneno machache kuhusu hoja iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na wataalam wao katika Wizara kwa kutengeneza hotuba fupi, lakini yenyenye kuchukua kila kitu na kutaja yote yaliyohitajika kutajwa kwa Sekta hii Viwanda na Biashara.

Halafu nitoe pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwa miezi hii miwili nadhani ameishi masaa mengi ndani ya ndege kuliko nyumbani kwake na alikuwa *cross country*. Mara yuko *West Africa*, yuko *Latin America*, yuko *Europe*, yuko kila mahali na *mission* zake zote zimeelekea kuwa *successful* kwa upande wetu sisi, basi nampa pongezi nyingi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitaongelea machache tu kuhusu Viwanda na Biashara. Kuhusu Viwanda nadhani niongelee vitu kama viwili. La kwanza kabisa ni uwiano kati ya umeme na viwanda, kwa umeme ndiyo malighafi au muundombinu mkuu wa viwanda bila umeme ni vigumu mtu kuanza kujenga viwanda maana havitaendeshwa kwa ufasaha.

Lakini ukiwa na umeme unaweza kuweka viwanda. Sasa umeme wa kwetu hapa Tanzania una magonjwa yote ya Kimataifa na yote yamekuja hapa. Kwanza, ni mdogo hautoshi, unatosha nadhani asilimia 10 ya *population*. Halafu pili ni aghali wengi wameishasema kwamba ni wa aghali sana. Halafu tatu, hatuna uhakika tunataka tupate msaada gani, tunakimbilia nchi jirani mara Msumbiji *connector*, mara tunaenda Uganda wote hawa wataishiwa umeme miaka miwili, mitatu inayokuja. Sisi wenyewe tunayo *resource* ya umeme.

Kwa hiyo tuna haja ya kuweka miguu yetu chini tutengeneze umeme wa uhakika ili viwanda viweze kuenea mpaka hata kule kwetu kunakoitwa *Peramiho Constituency* yangu. Leo wengi tunabeba mahindi kwenda mpaka kwa *Mohamed Enterprise Dar es Salaam* wakomboe na wasage tubebe tena unga tipeleke Songea kwa kuwa umeme tu haupo.

Lakini ungekuwepo tungekomboa mahindi na kusaga na kusambaza unga kote hapa nchini na nchi jirani. Lakini mengi hayo aliyasema Mheshimiwa Beatus Magayane, kwa hiyo kwa kumalizia niseme namuunga mkono yote aliyoongea Mheshimiwa Beatus Magayane asubuhi. (*Makofii*)

La pili, ni kuwa tuna miradi na miradi, tuna miradi ya *SIDO* ambayo ni *size* ndogo, kuna miradi *medium size* tuna miradi *large scale*. Sasa hizo zote za *SIDO* naunga mkono tu maana wengi wameongelea *SIDO*.

Lakini mimi nasema kuwa miradi mikubwa iwe *push* ya nchi nzima. Nchi nzima tukiweka miradi mikubwa *tui-support* na tuifanyie nguvu zote siyo Serikali peke yake iwe Serikali, *cabinet* yenyewe kama Serikali, Mheshimiwa Rais ndiyo dereva wa *cabinet* na sisi *back benchers* tuwepo tuna-*support* hiyo na nchi nzima tu-*support* miradi hiyo mikubwa kwa pamoja tukigawanyika tu hatuwezi kutekeleza mradi mkubwa.

Hata wale wa Msumbiji wameishaweka pale za kutengeneza chuma na sasa hivi nimesoma jana wana-*spent two point eight billion dollars* ku-*develop* ile gesi yao kupeleka *South Africa* na wao wenyewe kutumia katika viwanda vyao na kutengeneza umeme *two point eight billion dollars* siyo shilingi ni *dollars U\$*. Hiyo tuweka pamoja tunaweza kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa miradi miwili mikubwa ninayoiona hapa tulioianzisha miaka mitano, sita iliyopita ni hiyo *Mtware Development Corridor* pamoja ya *Central Development Corridor*. Sasa Mtware ndani yake kuna miradi mingi, lakini nataka kuongelea mmoja tu mkubwa ule wa Mchuchuma wa kutengeneza umeme, lakini Mchuchuma iko kilomita 80 tu na chuma cha Liganga na hiyo iko kilomita 25 kutoka kijiji jirani kinacho-*dolomite*.

Kwa hiyo, hivi vitu vitatu vinaweza kutengeneza kitu kikubwa sana cha viwanda *complex* kubwa inayoweza kuzalisha umeme mwangi wote ukatumika katika kuyeyusha chuma, kuyeyusha ile *iron ore* katika *iron ore* tukapata *steel* na ile *steel* kwa kuwa pale kuna madini mengine mawili *titanium* na *vanadium* tungeweza kupata ile *vanadium steel* na *titanium steel* na *manganese* iko pale Rukwa jirani tu zote hizo katika *Mtware Corridor* tukawa na *manganese steel*. Yote hiyo labda *investment* yake ingekuwa zaidi bilioni 2.3 *dollars* kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Kwa hiyo, *growth* ya uchumi hatungeongelea *six and seven percent* tungengelea habari ya *fourteen percent growth rate* yake. (*Makofii*)

Kwa hiyo, hayo nilidhani kuwa ukichukua ule mkaa wa mawe wa Mchuchuma, *Liganga Iron* pamoja na *dolomite* tunataka *steel mills* na tukipata *steel mills* kunakuwa na *a lot of other industries connected* na *steel mills* inakuwa kama ndiyo *Ruah*, kule Ujerumani wana *Ruah Industrial Area*, ndiyo kitovu cha maendeleo ya Ujerumani na sisi kule tuna mto unaitwa Ruhuhu.

Kwa hiyo, tungeweza kusema na sisi tunatengeneza Ruhuhu ambayo ni sawa na *Ruah* ya Ujerumani. Hao wenzetu wa *South Africa* wana kitu wanaita *GAUTANG*, ni *center* ya viwanda. Kwa hiyo, nadhani tungeweza kufanya hilo na tukawa kama wale wenzetu wa Brazil au wale wa upande *far East*.

Sasa hii yote itahitaji kuwa lazima tufanye kazi kwa ushirikiano wa hali ya juu. Wizara zote ziwe kitu kimoja katika hiyo na sisi *back benchers* tuwe kitu kimoja kwenda *ku-support* hao wenzetu wa Serikalini na hayo tutaweza kuyatimiza kwa urahisi zaidi. Lakini kama kule mbele wako *divided* sisi *back benchers* tunakuwa *lost* huku nyuma

hatujui tu-back kitu gani *which bench* na tulitaka iwe moja tu. Hiyo ni kuhusu upande wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa madini na upande wa biashara nilidhani nitaongelea kitu kimoja kikubwa kwa ufupi tu ni *orientation* yetu kuwa siku zote tunaangalia tukifanya biashara, tukifanya nini tunaangalia Ulaya, Amerika. Ndio na wao sasa hivi nadhani wako hoi, sidhani kama wana hali kama ya zamani waliyokuwa nayo. Waliweza kutudanganya sasa wanasisitika wanaona kuwa nchi ya Afrika imeanza *to diversify friendship*. Wanakwenda *North Eastern Europe* ingawa na wao wanajizatiti kuwa *developed* lakini wana nafasi ya kutufikia *comfortably*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi kwa upande wangu uchumi wetu sasa hasa biashara tuanze kutazama Mashariki. Tuanze kutazama China, India, *Asian Tigers* wale wazito wako saba pale *the Pacific ream*, wengine wanaita. Kule sasa ndiko kwenye mali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nadhani China inahitaji tani karibu 100 milioni ya *steel*. Hiyo ni *steel* nyangi sana sisi tukipata hata milioni 5 au 7 katika hiso tutajiona tuna *market* kubwa tu ya *steel* hiyo. Lakini tukienda kule *European Union* hawatutaki. Amerika ndio kabisa wala usiguse habari za *steel* wanakuwa *fully protected, they protect themselves*. Lakini *Far East*, kuanzia India watu wengi hata wale tuliokuwa sisi tunawategemea *North* nao pia wanakatisha kule juu kwenda China na India. Huko ndio kwenye fedha na huko ndio kwenye *market*. Watu bilioni mbili, China bilioni moja na India ni bilioni tatu. Watu bilioni tatu hata wakitumia kilo moja ya chuma inakuwa bilioni tatu na bila shaka watatumia kilo nyangi tu.

Halafu licha ya madini hayo niliyyoyasema ya *iron* ambayo yako kwa wingi kule Ludewa *over billions tones* na *coal belt* yoyote ni ya *coal* kuna *over also one billions tones* tunaweza kuanza na miaka 10, 15 tunaweza kuwa mbali sana tukawa na sisi a *big tiger* kwa Afrika ambayo tutakuwa *full tiger* labda kwa muda mfupi tu. Lakini ushirikiano uanze sasa hivi.

La mwisho ningependa kuongea kuwa kuna madini mengi hapa kwetu. Sasa madini tulioanza nayo sio mabaya, mazuri tu ni Dhahabu na Almasi. Hiso zaidi ni madini ya wakubwa ya *first world*. Lakini kwa maendeleo ya uchumi wa kwetu ni madini haya tulionayo ni mengi kama nilivyo sema *iron* na *coal* ni mojawapo lakini kuna madini mengine tena ambayo kama ni *nickel, copper, cobalt, tin, soda ash* hapa ipo, *manganese* nilishasema ipo na tunaweza kuwa na msululu mkubwa. Lakini yapo madini mengi na yote tukiweza kuya-*develop* na kuya-*orient toward the eastern market*, nadhani tutakwenda haraka zaidi kuliko tukiya-*orient* kwa upande wa Kaskazini pamoja na *traditional markets* zetu hawa nadhani hawana nafasi kama hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani niachie hapo na niunge mkono hoja mia kwa mia. Nawatakia kila la kheri na tutaendelea katika kuendesha Wizara hiso. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya mwisho na afagiae mwisho huona uchafu zaidi uliosalia. Nadhani akifagia anaweza kufagia vizuri zaidi. (*Makofi*)

Napenda nimpongeze Waziri wa Viwanda na Biashara, Naibu wake, Katibu Mkuu, wafanyakazi wote na watafiti kwa kazi waliyoionyesha na kutudhihirishia kwamba bado tuna uwezo wa kubadili maisha yetu tukitaka. Lakini kwa kweli liko tatizo nadhani sisi wenyewe hatujataka.

Kwanza nilikuwa naomba hawa wenzetu wanaofanya utafiti wa vifaa hivi vipyta kama *CAMARTEC, TEMDO* na vikundi vingine wamejifunza matatizo yaliyotokea huko nyuma na kuua viwanda vyetu. Mimi nadhani iko haja ya utaalamu wetu kujifunza matatizo yaliyotokea huko nyuma. Leo tunazungumza juu ya chakula cha njaa (mahindi).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ulimwengu wa leo kuzungumzia kugawa mahindi kwa chakula cha njaa ni kuzungumzia masuala yaliyokwisha kufa. Tulipaswa kugawa unga, sasa unga huu tuusagishe kwa mawe au tutwange kwa vinu? Tulikuwa na viwanda vya *National Milling* viko wapi na kwa nini vimekufa? Sasa nadhani kazi hii moja ya Wizara hii ya Viwanda na Biashara ifanye utafiti wa kina kuona matatizo yaliyojitokeza. *Polyester* haipo, kwa nini haipo? Sasa mafuta tulisema hapa jamani haya mafuta msibinafsische kwa watu, wakasema hii ndiyo itakuwa sawa sawa. Sasa ni sawa sawa? Sasa ni mambo ya kujiuliza haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vitu vingine tunajiletea kwa utashi tu. Sasa tunashindwa hata wa kumlilia. Sasa iko haja kwa kweli ya Wizara hii kufanya utafiti wa kina kabla hawajaruhusu kiwanda chochote kile kuwa mikononi mwa mtu asiyeleweka. Ni lazima tujue kwamba tunao watu, shule tunazo tumesomesha watu. Hivi kweli hawa wanaoshika viwanda hivi kuvia tumeshindwa kupata Watanzania wanaoweza wakawa *counterparts* katika viwanda hivyo wakasimamia viwanda vyetu vikazalisha. Hivi tuna tatizo la watu hawajasomea shughuli za viwanda hivi kweli? Hata ukichukua watu wa *VETA* wenye juhudhi na nia watasimamia tu na uzalishaji utafana tu. Lakini sasa hili ndilo tatizo.

Mimi naunga mkono sana utafiti unaofanywa na *CAMARTEC, TEMDO* na vikundi vingine vyote. Mimi naona tafiti hizi zinatukumbusha kuwa tunao uwezo wa kugundua mashine mbalimbali kwa maendeleo yetu. Lakini mashine hizi bado tusije tukazisifu sana kwa sababu kuna mwaka sisi tuliletewa matrekta ya *Swaraj*, sijui yanatoka Uchina ?

**MBUNGE FULANI:** India.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Yakapigwa moto pale jembe lilibaki kuruka juu ilibidi sote tukimbie. Maana ardhi ni ngumu kuliko nguvu ya trekta, *power* ya trekta kulima pale, lakini lilikuwa linakwenda. Sasa hivi vitu mnavyotuonyesha hapa ni vizuri lakini mmevifanyia majaribio? Kwa nini msifanyi *sample* kila mahali. Nendeni hata

kule Usambaa tengenezeni vifaa ambavyo vinaweza vikakokotwa na ng'ombe. Sehemu nyingine matrekta hayawezi kufanya kazi. Muwe na *samples* kwa kila mahali. Halafu *samples* hizo zikifaa kule mkifanya majoribio kule viwanda vitengeneze vifaa vya kutosha viende kwenye *samples* zilikofana ili watu watumie wazalishie.

Lakini leo tukisema kwamba watu wazalishie, watazalisha vipi? Kwa namna hii *CAMARTEC* itabaki ni suala la kuona tulivyoona sisi hapa lakini wananchi na wakulima hawatahusika wala hawataona maana ya kuwa na shughuli hizi za ufundi huu tuliouona. Hivi vitu vitumike ndipo tuseme kweli tumefanikiwa. Nilikuwa naangalia jembe moja hapa nikawa namwuliza mtaalamu kwamba jembe hili yaliyokuwa yanatengenezwa kule Zana za Kilimo Mbeya, mimi binafsi niliridhika ni bora zaidi kuliko haya mnayotengeneza. Akasema tumeweka chuma hili kubwa refu ili mtu aweze kushika hata kwa mkono mmoja akalima. Lakini Ndugu zangu kulima kwa namna hiyo hakuna uhakika sana labda kwa Wasukuma ambao hawajali suala hilo wao ni kutwanga ardhi na ng'ombe tu bila kuona. Lakini ukitaka ulime na ufanye *harrow* kwa kweli jembe hili lina matatizo yake. (*Makofi*)

Sasa nilikuwa naomba m jitahidi yale matanki ya kuchemshia maji kwa kweli yale ni matanki kwa ajili ya *elites* tu, watu wa ngazi za juu, huwezi ukalipeleka Kijijini pale. Nikauliza bei kiasi gani wakasema kwenye shilingi milioni moja na kiasi kidogo. Hivi tutakwenda kweli, nani watakaonunua? Labda sisi tujikamue wenyewe na tutajenga tabaka la watu wenyewe uwezo Vijijini na hatutaelewana. Tujitahidi kuweka vitu ambavyo vitakubalika na wananchi wetu na vitaleta maana na maendeleo tunayoyatarajia. Tujitahidi kuwa na vitu ambavyo vina hali nafuu. Vile vile tukumbuke hakuna nchi duniani imepata kuendelea kwa viwanda vikubwa bila viwanda vidogo. Tukizungumza viwanda vikubwa bila *SIDO* tunapoteza muda wetu. Tutarudi hapa hapa tukumbushane tena ubovu tuliuopata, *SIDO* ndiyo njia pekee. Kile Kiwanda kidogo cha *SIDO* Mbeya, mimi ni mdau wao wamenitengeneza hata mashine ya kupukuchua mahindi pale. Ni nzuri wametengeneza wenyewe wiki moja tu. Hayo ndiyo tunayoyataka kulingana na maendeleo ya mahali hapo. Lakini kama hizi zingine za kukamua mafuta hizi mashine *manual work* unaskuma mpaka unatoa jasho ndiyo ikamue robo lita, hatuendi mbali hii ni fatiki kwa watu. Wala hakuna sababu ya kutangaza vitu kama hivyo ambavyo havina mabadiliko ya maana na ya msingi hata kidogo. Ile kubwa ya umeme mimi nakubali tushawishi watu wenyewe uwezo wakamue mafuta maana mbegu tunazo tunaweza kulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vidogo tusipotilia nguvu hatuendi mahali. Viwanda vidogo ndivyo vitatuwezesha tupate hali, kule nyumbani wamefika hawa *SIDO* wameonyesha namna ya kutengeneza majembe ya mkono wakati maduka yalipokosa vifaa vya Zana za Kilimo sasa wanatumia majembe ya nchini. Sasa viko viwanda vidogo wananchi wanatengeneza majembe ya mkono kwa msaada wa *SIDO* Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hili ndilo ninaloliomba liendelee na tubadili kwa kulingana na hali na utaratibu. Tuweze kurekebisha na kuendeleza maendeleo na taasisi zetu zifae. Tukitegemea tupate viwanda vikubwa mimi nina hakika tutaendelea kudumaa, hatutakwenda mahali popote. Naomba hawa *CAMARTEC* waende Vijijini, waone matatizo, wajifunze matatizo ya kila mahali, watengeneze vifaa vya mahali hapo

walipokwenda kuona na umuhimu wa kitu kile na watu vile vile wana mifano hata ya ufundi uhunzi wa asili wa vitu mahali pale wao wakavione wajifunze, warekebishe, waviweke katika hali inayofaa ya kisasa, hapo tutakwenda. Tutakwenda kama alivyosema Waziri juzi huyu mmoja aliyetangaza anatengeneza ungo wa kutusafirisha Mbeya, tusikatae, inawezekana waende wamuone pengine unahitaji tu kuweka vijiti pembeni au viwaya watu wakiruka juu ikiyumba wasianguke.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kuna uwezo huo. Waoneni watu *mu-improve* kutokana na mwanzo waliouanza na wao, tutakwenda. Lakini hii ya kukaa kukisia tutabaki na *ma-book* makubwa yako ofisini na hapa walisema juzi hatusomi, muda wa kusoma utaupata saa ngapi. Maana na matatizo yanazidi, hali ya maisha ni ngumu maana hali ya kiduni kabisa. Huna hata umeme utasoma saa ngapi, usiku ndio wakati wa kusoma huna umeme, utasoma saa ngapi. Kwa hiyo, nadhani iko haja kwa kweli ya watafiti wetu kwenda Vijiji na kushughulikia hilo kuungana na wananchi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna sababu ya kusema kwamba eti *UFI* na Zana za Kilimo haiko kwa nini? Kama tunaweza tukatoa majengo haya kwa watu wengine haya ya *TANESCO* pale Morogoro, kwa nini wasipewe watu kama wa *CAMARTEC* wakashughulikia pale, wakaendeleza? Sasa si suala la kuwaambia aliyekuharibia si wa kubembeleza. Hatuwezi kwenda nchi hii kwa kubembelezana na watu wanaotudhulumu. Hatuwezi kwenda mahali. Wako watu tumejifunza, wataalam wako hapa tuwakabidhi waendeshe waishi kwa jasho lao na fikra yao na matakwa yao ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kusema kwamba tunachowenza tukitengeneze kwa makini na kiuzike hapa hapa nchini. Lakini mnatengeneza vitu, akinamama wanatengeneza sijui *juice* ya mananasi ya wapi lakini iko wapi? Maana wauzaji wako, hawa Wamachinga hawa ndio kazi yao wangepeewa watembeze humo, wauze. Lakini wanauza haya ya kujisugulia, madodoki. Tuwakusanye hawa tuwaambie kazi iko hapa vijana. Fanyeni hivi, uzeni mle hapa, watumie viwanda vyetu viwasaidie, wabadilike, wapate kuishi vizuri. Lakini tunawasukuma watu wauze tu vitu ambavyo hata vilikotoka hatujui. Hatuwezi kuleta mabadiliko hata kidogo.

Kwa hiyo, kwa hali hii nisingependa nigongewe kengele, naomba sana tujitahidi hivyo. Kuiba ufundi kwa aliye fundi zaidi si mbaya maana hata Wachina, Wajapani, Warusi wameiba. Tunachokatazwa ni *partern*, lakini kama ni bunduki ukapiga ukaweka uzito wa chuma zaidi inchi mbili kuliko yule aliywewka moja ya kumi ni bunduki mradi inafyatulika pale. Mtu hawezi kukushtaki akikuona umechukua *partern* yake wewe umeanza ya kwako ya uzito huo. Tufanye hivyo. Urusi walitengeneza trekta Rais akawaambia mtengeneze trekta la kulimia, wakatengeneza kuliwasha likaenda nyuma badala ya kwenda mbele. Walifanya akawaambia nendeni mlirekebishe. Leo ndio wanaotoa matrekta. Sasa sisi tutafanyaje, tutangoja tugundue vyetu lini na Chuma cha Liganga bado hatujawaza kukichimbua. Tutapata wapi chuma na hayo yaliyokufa humu magari na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na ninamwombea Waziri aendelee kufanya juhudhi hiyo. Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Waziri, Mheshimiwa Rita Mlaki, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hoja ya Waziri wa Viwanda na Biashara, ningependa kupitia suala la uanzishaji wa *EPZ* katika sehemu mbalimbali. Mtwara ni sehemu mojawapo iliyopendekezwa na Wizara toka Bajeti iliyopita ya mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa sijaona juhudini zilizofanywa na Wizara hii katika kufanikisha lengo la Mtwara kuwa na *EPZ*. Mtwara ina raslimali zinazoweza kuanzhishwa kwa *EPZ*, kama utengenezaji wa bidhaa za matunda mfano, huisi ya maembe, machungwa, ndizi na kadhalika, pia ubanguaji wa korosho, suala ambalo ni nyeti kwa mikoa yote inayolima korosho. Waziri atueleze kuna matumaini yoyote kwa Mtwara kuanzhisha *EPZ* hivi karibuni?

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la *CAMARTEC* ambalo Wizara yake ndiyo mzalishaji mkubwa katika viwanda nchini na hapo hapo Wizara hiyo ndiyo wanaosimamia masoko. Inasikitisha kuona kuwa *CAMARTEC* haina maendeleo yoyote mazuri hasa kutokana na *undercapitalization* ambayo kiini chake ni Wizara yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ihakikishe kuwa *CAMARTEC* wanapatiwa fedha za kutosha ili kujiendesha. Wizara haiwezi kukwepa jukumu hili. Huu ndio msingi wa Wizara hii. Ni lazima ivilee viwanda vyake na hasa hivi vya wanyonge wakulima, hatuna budi kuhakikisha tunavilinda na kuvipa misaada. Nategemea kuona mabadiliko makubwa katika uwezeshaji wa *CAMARTEC* kifedha kwani Wizara ina vifungi vingi inavyoweza kuvihamishia huko ili Taasisi isife.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka Mheshimiwa Waziri atueleze kwa nini katika kitabu cha hotuba yake hakuna hata kipengele kimoja alichoelezea kuhusu korosho?

Kuhusu Kiwanda cha Ubanguaji Korosho cha Vingunguti, amewanyima nafasi *EPZ* na kufungwa kiwanda hicho na kukosesha ajira kwa akinamama 2,500 na hata hakuna mpango wa wabanguaji Korosho wadogo wadogo kuhusu tatizo la soko. La sivyo, atangaze kwamba wananchi waishio Mtwara sasa waende Msumbiji. Ahsante.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kuunga mkono hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri. Hotuba hiyo ni nzuri na ina kila sababu ya kuungwa mkono. Jambo ambalo ningependa kupata maelezo ni kuhusu Kiwanda cha *Premier Cashewnut* kilichopu kule Vingunguti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi, nilibahatika kufanya ziara kwenye kiwanda hicho cha Watanzania na niliona jinsi kiwanda hicho kilivyoweza kuajiri zaidi ya akinamama 2,500 kwa wakati huo na kulikuwa kunajengwa *godown* lingine na tuliambiwa ya kwamba pindi *godown* hilo litakapomalizika kujengwa, kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuajiri kiasi cha akinamama 4,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hilo tu, pia kiwanda kilikuwa kinatumia mikasi ya kukobolea korosho ya idadi kama hiyo ya akinamama. Mikasi hiyo inatengenezwa hapa hapa nchini na hii inamaanisha ya kwamba hata wahanzi wetu wa Kitanzania wamepata ajira ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa ziara hiyo niliyoitaja hapo awali, kilio kikubwa cha kiwanda hicho kilikuwa kujiunga na *EPZ*. Hilo suala, Kamati yetu ilipokea na iliahidiwa ya kwamba litafanyiwa kazi. Baada ya kufuutilia sana, nimegundua kwamba kiwanda hicho kilishindwa kuingia kwenye mfumo wa *EPZ* na hivi sasa kiwanda hicho kimefungwa. Hii inasikitisha sana na ningeomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ya kina na mazuri kuhusu kukosekana kwa Kiwanda hicho cha Vingunguti kujiunga katika mfumo huo wa *EPZ*.

Nampongeza tena Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Wataalam wote na nawatakia kila la kheri.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Rita Mlaki, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wataalam mbalimbali wa Taasisi za Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba kilimo kitakua iwapo Serikali itaongeza ujenzi wa viwanda katika maeneo mbalimbali nchini. Hiyo ndiyo njia pekee ya kuwakomboa na umaskini wananchi wetu. Ni vizuri Wizara ikajitahidi kila eneo hasa katika Mikoa na Wilaya zetu, kama wananchi wanalima zao fulani, juhudzi zikawepo za Serikali, aidha, wao wenyewe kujenga viwanda au kutafuta wawekezaji. Hii itasaidia sana kuwawezesha wananchi kuuza mazao hayo kwenye viwanda hivyo na hatimaye kujikwamua na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano ni kifo cha Kiwanda cha *TANGOLD*, Korogwe. Naomba sana Wizara hii ikifufue kiwanda hiki. Mwekezaji aliyepewa kukiendesha ni zaidi ya miaka 12 sasa ameshindwa kukiendesha. Matokeo yake ni kwamba maembe, nyanya, pilipili, *passions* na matunda mengine yanaoza tu. Wananchi wengi wamekuwa maskini. Aidha, hata upandaji wa nyanya sasa umepungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi rasmi ni kwamba namwomba sana Mheshimiwa Waziri, Kiwanda cha *TANGOLD*, Korogwe kifufuliwe kwa juhudzi zote. Majengo bado yapo na yanaharibika. Pia nashauri sana juhudzi za kuwatafuta wawekezaji wenye uwezo,

watafutwe. Nashauri sana juhudhi hizo zifanyike ili kuokoa matunda ya Korogwe yanayooza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri sana juhudhi za makusudi ziendelezwe ili teknolojia ya zana za kilimo za kisasa zinazotengenezwa humu nchini ziwafikie wakulima wetu vijijini. Jembe la mkono sasa halitatuifikisha popote. Bidhaa za *SIDO*, *CAMARTEC* na kadhalika, zizaliwe kwa wingi na ziuzwe kwa bei nafuu ili ziwafikie wadau ambao ni wananchi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudhi zifanyike za makusudi kwa Watanzania kutumia bidhaa za nchi yetu. Soko la ndani ni muhimu sana katika kuviimarisha viwanda vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazao ya Mkonge yaimarishwe kwa kuwa na kiwanda katika Mkoa wa Tanga, ambapo ndipo Mkonge mwingi unalimwa. *Final products* za Mkonge zina soko zuri sana nje. Kwa sababu Mkonge upo na majengo yapo. Naomba Wizara isimamie hili kwa nguvu zake zote. Hiyo itasaidia sana kupata ajira na kutumia Mkonge ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla naunga mkono hotuba ya Waziri wa Viwanda na Biashara kwa asilimia 100.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima, upendo na unyenyekevu mkubwa, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Naibu Waziri, Watendaji wote na Wafanyakazi wa Wizara hii kwa juhudhi na uongozi wao imara katika kuisimamia Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya uchumi wa viwanda katika Taifa letu hili la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ambazo zimeendelea kiuchumi duniani, msingi wake mkubwa umetokana na viwanda ambapo inadhihirishwa na misingi mikuu ya Elimu ya Juu ya Nchi hizo ambapo mhimili wake mkuu ni suala zima la Sayansi na Teknolojia. Kwa hiyo, Serikali yetu ijenge uwezo wa elimu ya kiwango cha juu kwa wananchi wake, ili uchumi wetu katika sekta ya viwanda, uimarike zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni nzuri sana ambayo imetuonyesha juhudhi za Serikali yetu katika kujenga uchumi na maendeleo ya kweli kwa Taifa letu na wananchi wake kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoptaka na haya ambayo yameelezwa katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri ni imani yangu kuwa Taifa letu litafika katika maendeleo makubwa ya kiuchumi katika miaka michache ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara hii kuongeza juhudni katika uendeshaji na usimamizi wa majukumu yake iliyopangiwa na Serikali Kuu na kuangalia yale maeneo ambayo katika kipindi kilichopita yalikuwa na kasoro ndogo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 15 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameeleza juu ya hali ya uchumi wa sekta ambapo ameelezea juu ya kuimarika kwa viwanda na kuwepo ongezeko la uzalishaji wa bidhaa ambao umechangia ukuaji wa sekta kwa 8.6% kwa mwaka 2003, ikilinganishwa na 8% kwa mwaka 2002.

Pia katika ukurasa huo huo ameelezea kuwa mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa, ulikuwa 8.7% mwaka 2003. Pia tumeelezwa katika hotuba hii kuwa kumekuwepo na ongezeko la ajira kutoka watu 180,023 mwaka 2002 hadi kufikia watu 207,571 kwa mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa huo huo tumeona mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika kusimamia na kuongoza Wizara hii vizuri sana kunakofanywa na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Watendaji na Wafanyakazi wote wa Wizara chini ya misingi imara na sera madhubuti za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kuipongeza Wizara hii kwa juhudni zake za kiuundaji na usimamizi mzuri. Nawatakia kazi njema na usimamizi mzuri wenye mafanikio makubwa

Mheshimiwa Naibu Spika, nikinukuu kitabu cha Sera ya Taifa ya Biashara katika ukurasa wa 10, kinatueleza kuhusu mazingira ya Kimataifa. Katika ukurasa huu, unasema kuwa mazingira ya biashara duniani yamebadilika kwa kiasi kikubwa kutokana na maendeleo ya kiteknolojia na mkazo uliowekwa katika kuhimiza utawala bora wa kisiasa na kiasasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali yetu kuyaona mabadiliko hayo ya biashara yaliyobadilika, yasije yakapunguza nguvu na juhudni za nchi yetu kujenga uchumi na maendeleo ya Taifa na wananchi wake kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia haya mabadiliko yaliyotokea kutokana na maendeleo ya kiteknolojia ni vizuri tukayaangalia na kuyafuatilia vizuri sana ili nchi yetu iende sambamba na hali ya mwenendo wa uchumi duniani katika maendeleo ya viwanda na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naisisitizia Wizara yetu hii ya Viwanda na Biashara, iongeze juhudni zake katika uendeshaji na usimamizi mzuri na wa mafanikio ya Wizara katika sekta hii ya Viwanda na Biashara nchini kwetu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Watendaji na Wafanyakazi wote na nawatakia usimamizi mzuri na wa mafanikio katika Wizara wanayoiongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kuiptata nafasi hii ili nami niweze kuchangia taarifa ya Waziri kuhusu bajeti ya kipindi hiki. Natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na Watumishi wa Wizara, kwa jinsi wanavyojitahidi kuandaa mipango yenyewe mwelekeo wa kuwainua wananchi katika kuleta maendeleo Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mama Anna Mkapa, kwa jinsi anavyojitahidi kuandaa mipango mizuri ya kuwaunganisha wanawake wa Tanzania kwa kuwaleta kwenye maonyesho ambayo akinamama wengi sasa wamepata mwamko wa kutengeneza na kuonyesha bidhaa hizo. Nashauri pale penye uwezekano, aungwe mkono kwa jitihada hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Maonyesho ya Sabasaba, akinamama wamepata mwamko sana, lakini wanapata tabu katika kusafirisha bidhaa zao toka Mikooani kwenda Dar es Salaam. Lakini Wilaya na Mikoa mingine wanawapatia usafiri na huduma za chakula na kadhalika. Elimu itolewe kwa Mikoa yote kuthamini michango ya akinamama wanayoitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa jinsi sikukuu ya Sabasaba ilivyoandaliwa vizuri mwaka huu, kwani kila aliyeona maonyesho amesifia. Hivyo, nashauri Serikali iendelee kuandaa vyema na sikukuu zijazo, kwa sababu sifa inayopatikana ni ya Tanzania ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itimize azma zake za kuhakikisha barabara zinapitika ili kuwezesha wakulima kusafirisha mazao yao kwa wakati na kupata masoko mijini, kwani Wilaya nyingine kusafirisha bidhaa toka shambani kwenda mijini, inakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO* inafanya kazi nzuri nchini, kwa sababu huduma zao zinamlenga mwananchi aliyeo kijijini na ndiye tunayemlenga. *SIDO* iimarishe katika kufufua majengo ambayo yako Mikooani na yalifanya kazi huko nyuma na hapa katikati yakaachwa. Ni taratibu ambazo zilikuwa nzuri, kwa sababu ukiwhitaji, ilikuwa rahisi uwapate wapi na ikipendeza kwa taratibu zake ambazo zimeachwa. Fufueni haraka iwezekanavyo na endeleza pale walipotuachia, waliotutangulia na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa viwanda kunamhakikishia kila aliye karibu na kiwanda, uhakika wa maisha kwa sababu atapata ajira au kuuza bidhaa zake kwa uhakika na kupata pesa. Je, Wizara ina taratibu gani za kufufua viwanda ambavyo vimesimama kwa muda mrefu kama Viwanda vya Kubangua Korosho? Kitendo cha kuvifufua viwanda kutatupatia heshima kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wengi wamejitokeza kujiunga katika vikundi mbalimbali, vikiwemo vya ubanguaji wa korosho. Ni jitihada gani zinafanywa

za uhakika kuwapatia utaalam wa ubanguaji kwa kutumia teknolojia ya kisasa? Nashauri Serikali iwe makini kwa kuinua shughuli za wanawake kuwapatia soko, uandaaji wa bidhaa na wahisani waende vijijini. Waachane na mijini ambako wamejizatiti kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Mtwara Development Corridor*, mbona Serikali haisemi lolote kwa nini mambo hayaendi? Kwani utekelezaji wa miradi chini ya Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara, mimi sioni kinachofanyika kwa vitendo. Nashauri kuacha kabisa maneno na mipango mizuri ambayo yamo kwenye makaratasi. Tatizo ni nini wataalam wasimamizi Tanzania hatuna? Miaka mingi imepita tangu taratibu zianze na zinakwenda pole pole au kwa kusuasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri mipango yote iliyoandaliwa ianze utekelezaji wake mara moja. Endapo walioeteuliwa, Serikali iwaone kama wameshindwa na wengine wateuliwe wazalendo ambao wataona uchungu na maendeleo ya Mkoa wa Mtwara na nchi nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iagize maonyesho ya bidhaa yawe yanafanyika kila Wilaya kwa kipindi kile kile ambacho maonyesho yanapoonyeshw Kitaifa ili kumwezesha mwanakijiji wa kawaida naye kwenda na wakati kwa kuangalia vitu, atapata nafasi ya kuuza biashara yake. Sababu wengi wao wanapenda sana kwenda Dar es Salaam, lakini wanashindwa uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia kila la kheri Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote kusimamia vyema mipango katika utekelezaji wake ili kuipa heshima Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Waziri na Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rambirambi zangu kwa Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Ngemera, kwa kufiwa na mpendwa mke wake. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri na mchango wangu kwa Wizara hii ni katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Export Processing Zones (EPZ)*, utaratibu unaotumika sasa na juhudzi zilizopo katika ujenzi wa *Export Processing Zones*, havitoshi wala kukidhi haja. Tunahitaji hasa Serikali yenyewe iwekeze kwa nguvu nyingi katika miundombinu ili kuvutia wawekezaji katika kanda hizo za *export*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwekeze katika barabara, umeme, maji na kadhalika katika maeneo yanayotarajiwa kuendesha shughuli za *export processing*. Maeneo mapya katika kanda husika, utaratibu wa sasa kujenga *processing zones* mijini ambako kuna miundombinu ya barabara, umeme na maji, ni kuweka makambi tu ya kuiibia Serikali, kodi kutoweza kudhibitiwa kikamilifu. Serikali ikubali kuwekeza, siyo lelemama. Matokeo yake yataonekana baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wafanyabiashara wazalendo, Wizara isione soo kutangaza biashara ambazo haziruhusiwi wageni kuzifanya. Duniani kote, Serikali huweka sheria na kanuni za kulinda wananchi wake katika maeneo fulani fulani ya kibiashara. Kwa mfano, biashara ya rejareja, vinyozi na kadhalika. Je, Wizara leo inajua kwamba Kariakoo wako Wachina na Wakorea wanauzu maua na bidhaa mbalimbali, jumla na rejareja?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ubinafsishaji, kama ilivyotamkwa na Kamati ya Bunge ya Biashara na Uwekezaji, kuna umuhimu wa kufuatilia viwanda vilivyobinafsishwa. Mikataba iliyokubaliwa wakati wa ubinafsishaji, haitekelezwi. Viwanda vingi havifanyi kazi kwa programu zilizopangwa wakati wa ubinafsishaji. Wizara ifuatilie mikataba na programu zilizokubaliwa. Taarifa zitolewe Bungeni kupitia Kamati ya Bunge ya Biashara na Uwekezaji. Uchambuzi wa kina ufanyike. Ahsante.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, napenda nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kuandaa hotuba hii kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa mchango wangu, naomba kuunga mkono hoja hii. Hata hivyo, kwa lengo la kuboresha, napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ombi maalum, Serikali ichukue hatua za haraka kuhalalisha biashara isiyo rasmi kati ya Msumbiji na Tanzania na Malawi na Tanzania. Ni muhimu eneo hili likatambuliwa kama EPZ.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atembelee Mbinga kabla ya Bunge hili kumaliza muda wake.

**MHE.AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa hotuba yake nzuri ambayo ameitoa asubuhi ya leo. Nampongeza pia Naibu wake, Mheshimiwa Rita Mlaki, ambaye amekuwa msaada mkubwa wa Waziri wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba hii. Naomba kukumbushia umuhimu wa kuendeleza na kuanzisha viwanda vidogo vidogo hasa katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABDILAH O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kuunga mkono hoja. Lakini niboreshe sehemu tatu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu. Hivyo, pembejeo za kilimo ni muhimu sana kupatikana bila vikwazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la korosho linatumia hasa pembejeo iitwayo *Sulphur*, bila *Sulphur*, hakuna korosho. Lakini sisi wakulima wa korosho, tunateseka na upatikanaji wa pembejeo hiyo maana *agent* wa kuagiza *sulphur* ni mmoja tu. Hivyo, huamua kuleta kwa wakati au la, kupandisha bei bila mpangilio maana hana mshindani.

Kwa sasa ni Abasi tu hapa nchini. Tunaomba ma-*agent* wa uagizaji *sulphur* waongezeko ili kuwe na ushindani wa bei na uagizaji na upatikanaji wa *sulphur* kwa wakati. Tutoe huu Umungu Mtu katika uchumi wa Kusini.

Pili, biashara ya mafuta katika Mikoa ya Mtwara na Lindi, kila msimu wa mauzo ya korosho, lakini katikati ya msimu wakati bei ya korosho imepanda, wanunuzi (Wahindi) huchenza mchezo haramu na wafanyabiashara wa mafuta Mtwara hivyo kuzorotesha harakati za ununuzi wa korosho. Hivyo, baadhi ya wanunuzi ikupungua nguvu hatimaye bei kuteremka sana na hili la bei ikiwa ni lengo lao na kutudhulumu korosho zetu kwa bei ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba hili pia Serikali iliangalie na kutusaidia viwanda vidogo vidogo vya ubanguaji korosho Mtwara na Lindi, ni muhimu sana. Korosho zetu zikitakiwa kwa bei ya chini ya uzalishaji, tutapeleka katika viwanda vyetu vidogo vidogo na kubangua ili kuuza korosho zilizobanguliwa ambazo soko lake ni zuri nje na ndani ya nchi. Hii ni pamoja na kuboresha viwanda vikubwa vyote.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa ya kuchangia hoja ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa mchango wangu, naomba uniruhusu kutoa rambirambi zangu za dhati kwa viongozi na watumishi wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Halmashauri ya Biashara ya Nje (*BET*) pamoja na familia na jamaa husika kwa msiba mkubwa wa kufiwa na aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa *BET*, Ndugu yetu mpendwa Marehemu Emmanuel Buliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Marehemu Buliki alikuwa mtu rahimu, mpenda watu, mfanyakazi na kiongozi mahiri, shupavu, mbunifu, mhamasishaji mzuri na ambaye daima alijitolea mhanga katika kuchapa kazi bila kujali saa, ili kuhakikisha maendeleo endelevu ya *BET* na mchango wake thabiti katika ukuzaji wa uendelezaji wa biashara ya nje ya Tanzania na uchumi wa Taifa kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifo chake kimeacha pengo kubwa katika nyanja za uendelezaji na ukuzaji wa Biashara ya Nje Tanzania katika Kanda ya Afrika Mashariki na Kati na pia nchi nyingi duniani tunazoshirikiana nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sana naomba pia kutoa rambirambi kwa Katibu Mkuu wa Wizara hii, Ndugu Ahmada Ngemera na familia yake kwa kufiwa na mke wake mpendwa. Nawaombea Mwenyezi Mungu awalaze marehemu hawa mahali pema peponi, awape viongozi na wafanyakazi wa Wizara na *BET* pamoja na familia za marehemu hawa subira na awape nguvu za kuendeleza yale mema yote ambayo marehemu hawa walikuwa wakiyasimamia na kutrajia. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwenye hoja iliyo mbele yetu, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Waziri wa Viwanda na Biashara, Naibu wake, Mheshimiwa Rita Mlaki, Katibu Mkuu Ndugu Ahmada Ngemera pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa hotuba hii nzuri na kwa kazi nzuri wanayoifanya katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha sana kwamba Wizara hii na Taasisi zake, inatengewa bajeti finyu sana eti kwa sababu za kihistoria au fikra zisizo sahihi kwamba kazi zake ni za *advocacy, promotion, facilitation* ambazo hazina gharama kubwa. Fikra hizi siyo sahihi, hasa katika zama hizi za utandawazi ambapo mashindano ni makali zaidi na kazi za Wizara hii zinahitaji kufanywa kwa kiwango kikubwa zaidi, kwa ufasaha zaidi na kwa gharama kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu ikazingatiwa kwamba hata nchi zilizoendelea sana kama vile Marekani, Japan, Ujerumanu na kadhalika, Serikali zina Wizara, Idara au Vitengo maalum kwa ajili ya shughuli za uhimili wa kukuza uwekezaji, viwanda na uuzaji nje na hutengea fedha nyingi sana Wizara/Idara/Tasisi hizo. Mfano mzuri ni jinsi ambavyo Serikali ya Japan inavyotoa kipaumbele cha kwanza kwa Wizara ya Biashara ya Kimataifa na Viwanda (*MITI*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli usiopingika ni kwamba nchi zote zilizoendelea, sehemu kubwa ya maendeleo imetokana na mkazo kuwekwa kwenye maendeleo ya viwanda na biashara ya Kimataifa, hususan uuzaji nje wa bidhaa na huduma. Ukweli huo umedhihirika zaidi katika maendeleo ya kiuchumi yaliyopatikana katika nchi za Mashariki ya Mbali, *Tigers* na sasa Uchina.

Mheshimiwa Naibu Spika, isichukuliwe kwamba kuelekeza maendeleo katika huduma za jamii na sekta za uzalishaji wa msingi (*primary production*) hakuna maana. Lakini tutadumaa kama si kurudi nyuma kimaendeleo iwapo hatutatoa uzito unaostahili katika kuweka kipaumbele cha juu zaidi katika uwekezaji katika maendeleo ya viwanda vidogo, vyakati na vikubwa. Uongezaji wa thamani kwa tija au kuunda bidhaa kwa tija, siyo tu kunaongeza ajira, mapato ya Serikali katika kodi na fedha za kigeni bali pia mapato makubwa zaidi ya kuwezesha uwekezaji zaidi, uboreshaji zaidi wa bidhaa na uendelezaji wa raslimali nguvukazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutangaza sera na kuunda taasisi peke yake bila kuwezesha taasisi hizo kutekeleza yale yanayotarajiwa, si hoja. Kwa kiwango cha bajeti iliyotengewa Wizara hii na Taasisi zake, si Wizara wala Taasisi zake zitawezza kutekeleza matarajio mengi yanayokusudiwa, licha ya kuwepo sera nzuri za biashara ya nje, viwanda vidogo na kati, diplomasia ya uchumi pamoja na Taasisi kama vile *NDC (EPZ), SIDO, BET, Tanzania Trade Centre (London na kadhalika), TBS, TIRDO, CAMARTEC na TEMDO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunataka kufanikiwa katika kuendeleza viwanda, hatuna budi tutambue kama maendeleo hayatokani na dhamira njema, sera nzuri na taasisi bila kuwekeza katika viwango inavyostahili. Mtaji wa kutosha ni muhimu, siyo tu katika shughuli za kuzalisha mali, bali pia huduma muhimu. Huduma za utafiti na uendelezaji uzalishaji na masoko ni ghali, lakini ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira yetu ya kutoachwa nyuma kwenye sheria ya utandawazi, ni sharti iende sambamba na uwekezaji unaostahili ili tupate maendeleo yanayotarajiwa. Ni jambo la kukatisha tamaa sana kwamba kati ya shilingi 741,200,000/= ambazo zimeombwa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za EPZ.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgao uliopatikana ni 50,000,000/= tu. Inaonekana kama mzaha zaidi kwamba hakuna hata senti moja iliyopatikana kati ya shilingi 18,344,798,045/= kwa ajili ya kuendeshea shughuli za maendeleo zinazoongezwa na Wizara hii (*NDC, TIRDO, CAMARTEC, TEMDO, TBS, BET na CBE*). Kwa upande mwingine, kwa mfano nchi jirani ya Kenya inatenga Dola za Marekani bilioni moja (*US \$ 1bn.*) kwa mwaka kwa ajili ya kuendeleza utalii pekee. Tusipojizatiti inavyostahili, tutabakia kuimba tu bila maendeleo yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo uwezo wa Serikali ni mdogo, kwa nini mapendekezo yaliyopitishwa zamani kama vile kuwa na Mfuko wa Kuendeleza Mauzo Nje (*Export Development Fund*) usizinguliwe? Suala lingine ambalo lipendekezwa na kuafikiwa kimsingi ni kwamba wadau mbalimbali waichangie *London Trade Centre*. Ipo haja ya kufufua haya na kuhakikisha yanapata mafanikio. Vinginevyo, pendekezo la kupungua vituo vyta biashara kwenye Balozi zetu mbalimbali na zera nzima ya diplomasia ya kiuchumi, zitakuwa ndoto tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Mkinga na Wilaya ya Muheza kwa jumla, ina nafasi nzuri ya kuchangia katika maendeleo ya viwanda na biashara. Jimbo la Mkinga linazalisha na lina nafasi nzuri ya kuendelea kuzalisha na kuboresha mazao mbalimbali yakiwemo katani, mpira, korosho, kakao (*cocoa*), mifugo, mazao mbalimbali ya chakula, matunda, viungo, mazao ya baharini, mazao ya misituni, madini na vito pamoja na bidhaa za utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote haya, Jimbo la Mkinga na Wilaya ya Muheza kwa jumla ni mionganoni mwa maeneo yenye hali duni kiuchumi. Bado wananchi wenyewe au Halmashauri ya Wilaya haijawa na uwezo wa kuvutia uwekezaji wa kuongeza uzalishaji pamoja na uboreshaji mazao, usindikaji na ufungashaji, ili ubora wa

bidhaa na huduma, uwe wa viwango vinavyokubalika na kuwavutia wanunuzi katika soko la ndani na la dunia kwa jumla. Haya ni baadhi ya maeneo ambayo huduma za Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Taasisi zake, ni muhimu sana katika kuendeleza bidhaa na masoko kutoka Jimboni Mkingi na Tanzania kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la faraja kubwa kufahamu kwamba hivi sasa Serikali inafikiriwa kuipa Sekta ya Viwanda na Biashara, kipaumbele kinachostahili na kuongezewa mgao wa bajeti kwa miaka ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa 100%, nikiwa na matumaini makubwa kwamba Wizara hii na taasisi inazoziongoza, itapewa kipaumbele kinachostahili mwakani na miaka inayofuata.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja hoja iliyopo mbele yetu ya kuidhinishiwa fedha za matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu katika kuunga mkono hoja hii ni huu mpango mahsus wa *EPZ*. Naomba zoezi hili liende kwa kasi kadri ya uwezo wa Wizara unavyoruhusu. Lakini naomba nipongeze kwa hatua iliyofikiwa pale Ubungo. Lakini nashauri Kiwanda cha Kubangua Korosho Vingunguti, kipewe usajili katika *EPZ*, hatimaye kifunguliwe ili kiendeleze kuchangia Pato la Taifa. Lakini zaidi ni kuwapatia ajira zaidi ya watu 3,000 walioajiriwa pale na hivi sasa hawana kazi.

Mheshikiwa Naibu Spika, lakini pia Wizara hii inapaswa ihamasishe wananchi wake kwa programu maalum ya kuanzisha biashara ya Soko la *AGO4*. Mpango huu umeletwa maalum katika Bara la Afrika ili kusaidia Waafrika kuondokana na umaskini. Lakini kwa bahati mbaya, hatukuwahi kuandaliwa kibiashara, vinginevyo, biashara hii itarudi kule kule katika nchi zinazoendelea na sisi tukaingizwa kama watumwa. Lakini bado Watanzania tunayo nafasi katika zoezi hili na tukafaidika na azma ya soko, ukizingatia Watanzania ni watundu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imebahatika kuwa ni nchi ya uzalishaji wa matunda na viingo, lakini bado hatujaweza kutumia baraka hiyo kibiashara. Hivyo, ni kuharibika mazao hayo bure. Nadhani huu ni wakati muafaka kwa Wizara hii kwa kushirikiana na wataalam kutoa msukumo maalum wa kuanzisha viwanda vidogo vidogo vyaa usindikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakiri kabisa kwamba nchi yetu ina wataalam wa kila namna katika ubunifu wa mambo, lakini sielezi kwa nini unakuja uzito wa matumizi ya mipango hiyo iliyobuniwa. Mfano, Tanzania inavyo Vyuo vya Biashara, lakini matokeo ya vijana wote wanaopitia katika vyuo hivyo hutegemea ajira Serikalini au katika sekta binafsi.

Mimi nashauri vijana hawa waandaliwe pia kuanzisha biashara zao binafsi, ikiwemo viwanda vidogo vidogo kwa kupewa mikopo ya udhamini kwa maslahi ya Taifa.

Naipongeza Wizara kwa ufanisi wake katika kufanikisha Maonyesho ya Sabasaba ya mwaka 2004, ila naomba yale yote yaliyojitekeza kwa mapungufu yatatuliwe katika maonyesho yanayofuata.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa, Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa hotuba na mipango mizuri ya Wizara yake kwa kipindi cha mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaelewa kuwa mipango hii mizuri ni matokeo ya kazi nzuri ya timu mahiri ya Wizara ambayo inaongozwa na Waziri, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Rita Mlaki, Katibu Mkuu, Bwana Ahmad Ngemera na watumishi waandamizi wa Wizara hii na Taasisi zilizoko chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa napenda nimpongeze Mkurugenzi Mkuu wa *SIDO*, Bwana Laizer na wafanyakazi waandamizi wa Shirika la Taifa la Viwanda Vidogo Vidogo. Taasisi hii imekomaa na viongozi wake wameonyesha uwezo mkubwa wa kuyaelewa mahitaji ya wananchi wetu na mazingira wanayofanyia kazi. Ni Mashirika machache ya nchi yetu ambayo yameonyesha kuwa *down to earth and ears to the people* kama *SIDO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO* imeonyesha kuwa wafanyabiashara wadogo wadogo wanakopesheka kama mipango mizuri ya kuwatayarisha na kuwafuatilia wakopaji inawekwa. Haya ni maendeleo makubwa na kuwa maendeleo haya yamefikiwa na Shirika letu wenyewe, ni kitu cha kujivunia. Naomba Wizara iendelee kulisiaidia Shirika hili ili hatua iliyofikiwa iendelee kukua. Tunaomba sasa Shirika liongezewe uwezo na mtaji wa kukopesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vikundi vitano vya wakulima na akinamama wa Jimbo langu, vimetengeneza miradi yao mitano ya kusaga na kusambaza nafaka. Kupitia mchango huu, naomba Wizara ya Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, kupokea miradi ya akinamama na wakulima hawa ambao wametengeneza michanganuo ya biashara zao na mapendekezo ya kulipa deni. Nitawasilisha maombi haya rasmi baada ya hoja hii kupita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ponjezi kwa Waziri, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Rita Mlaki, Katibu Mkuu, Wakuu wa Taasisi zilizoko chini ya Wizara na Watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri yenye kueleweka, lakini yenye malengo ambayo

utekelezaji wake nina wasiwasi nao kutokana na fedha kidogo zilizotengwa kwa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba imeonyesha wazi kuwa fedha za maendeleo, tena zote zinatoka nje. Je, wafadhili wakisitisha kuleta fedha hizo kwa sababu moja au nyininge, itakuwaje kwa miradi hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ieleweke kuwa wageni hasa Mataifa ya nje, hawatafurahia kuona Tanzania ikiendelea katika sekta ya viwanda hasa viwanda mama. Hivyo, wakati umefika sasa wa Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya utafiti utakaotupeleka kwenye sekta ya ukuaji wa viwanda mama kama chuma, madini ambayo yapo tele huko Mchuchuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba imeelezea kuwa itatoa miongozo kuhusu leseni na jinsi ya kuendesha biashara katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Naomba ufanuzi ni lini miongozo hiyo itakuwa tayari na kusambazwa sehemu husika? Yafaa miongozo hiyo iharakishwe kukamilishwa na kusambazwa ili wafanyabiashara wafaidike, la sivyo taratibu za zamani bado zitaendelezwa licha ya kwamba ni za usumbufu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali kuwa kwa vile sekta ya biashara sasa inapaswa kuendelezwa na kuendeshwa kwa mbinu za kibiashara za kisasa, elimu ni muhimu sana kwa wananchi. Hivyo, Wizara na wadau wengine wanapaswa kutoa elimu hiyo bila kuchoka kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa biashara zinazoendeshwa na akinamama mwaka hadi mwaka, ni za aina moja. Kwa mfano, biashara ya vyakula vya kusindika, vikapu na kadhalika. Je, Serikali inasaidiaje akinamama hao ili waweze kutengeneza bidhaa zinazotofautiana, lakini zenye *quality* nzuri ya kuweza kuuzika nje?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusisitiza haya, naunga mkono hoja na kumwomba Waziri ajitahidi kuhakikisha kuwa bajeti ijayo Wizara inaongezewa fedha.

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii naiunga mkono bila matatizo yoyote. Napenda kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji Wakuu wa Wizara na Mashirika mbalimbali kwa uongozi na utekelezaji wenye mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimekuwa napigania huko nyuma, ni maoni yangu ya dhati kuwa Wizara hii ikifanikisha kuwapata wawekezaji wa viwanda vya usindikaji wa vyakula (*food processing*) katika Wilaya ya Iringa, ikiwa ni pamoja na Jimbo langu la Kalenga na Mkoa mzima wa Iringa, maendeleo makubwa ya kilimo yatakuwa yamepata msukumo mkubwa sana kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mazao mengi sana yanayoweza kuwa *processed*, kwa mfano matunda, mboga, viazi, maziwa, nyama na kadhalika. Eneo hili la *Southern Highlands* lina *potential* kubwa sana ya uwekezaji. Naomba njue Wizara ya Viwanda na

Biashara ina mipango gani ya uwekezaji katika *Food Processing Industry* kwa eneo hili la Iringa?

Mheshimiwa Naibu Spika, siku za karibuni, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliweka jiwe la msingi Kibaigwa kujenga Soko la Kimataifa kwa mazao ya chakula kama mahindi. Hili ni jambo la kupongezwa sana. Kwa msingi huo, naomba nijenge hoja yenye nguvu kuwa ni muhimu sana Wizara hii ihamasishe wawekezaji na kujenga masoko ya Kimataifa ya aina ya hili la Kibaigwa katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Soko la Kimataifa lijengwe aidha, Tanangozi au Ifunda, katika Jimbo langu la Kalenga. Hizi ni *centers* zilizo katika Barabara Kuu kuelekea Kusini mwa Afrika. Soko kama hilo litatumika kupeleka mazao ya chakula kama mahindi, mchele, maharage, viazi na kadhalika katika Nchi za *SADC*. Hali hiyo itahamasisha sana kilimo cha mazao ya chakula na kurejesha kweli sifa ya *The Big Four*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo sisi wawakilishi litupasa kupigania *relentlessly* mpaka kutokee mafanikio, ni uchimbaji wa Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na chuma kule Liganga. Tukifanikiwa katika *exercise* hiyo, basi eneo hili la Kusini mwa Tanzania litakuwa *engine* ya maendeleo makubwa ya umeme na viwanda mama kwa Tanzania, Afrika Mashariki na Nchi za *SADC*. Kwa heshima naiomba Wizara iongeze jitihada kufanikisha mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko mbele ni vema tuweke sera inayotambua kuwa *source* kuu ya umeme iwe ni Makaa ya Mawe na Gesi. Maji yatumike kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, mifugo na kilimo cha umwagiliaji. Kama kuna maji ya ziada, yaongeze nguvu ya umeme.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Naibu Wake, Mheshimiwa Rita Mlaki, Katibu Mkuu wake, Ndugu Ahmada Ngemera ambaye kwa kusaidiwa na watumishi wake, wameweza kutekeleza majukumu yao vizuri. Pia nawapongeza kwa kuandaa sera mbili ambazo ndiyo msingi wa viwanda vyetu na biashara. Naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo ambayo ningependa yazingatiwe katika kuandaa mkakati wa utekelezaji wa sera husika. Pamoja na nia ya mfumo wa utandawazi kutoa fursa kwa viwanda vya ndani kupata mitaji toka nje ya nchi kunaashiria kuandaa na kujenga uwezo wa ushindani na hivyo wawekezaji wa Tanzania ni budi wawezeshwe kwa makusudi ili watoe bidhaa zenye ubora wa hali ya juu na kwa bei nafuu. Bila hilo, tutaimba tu usemi na maagizo ya Rais wetu kuhusu kununua mali ya Tanzania. Mfuko maalum wa kusaidia jitihada hizi, uwepo na usimamiwe vizuri kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwombwa Mheshimiwa Waziri kwa kutumia Kitengo cha *TBS*, kipewe watumishi wenye usoefu wa fani mbalimbali ili kudhibiti uozo na udanganyifu wa baadhi ya wafanyakishara kuingiza bidhaa ambazo ziko chini ya ubora

wa viwango vinavyotakiwa. Nafahamu kuwa mara nyingi tumekuwa tukipokea mbolea na dawa ambazo ziko chini ya viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano upo wakati fulani, mbolea ya *Urea* ambayo inatakiwa iwe na *Nitrogen* kwa 46%, lakini mbolea hiyo iligunduliwa ikiwa na 20% tu, huu ni ugaidi wa kiuchumi. Wataalam wasikubali kupelekewa *samples* na wafanya biashara, bali wasambae nchini wakajichukulie *samples* hizo wenyewe, watajionea hali halisi ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kuanzishwe Kanda ya Kusini kwa ajili ya kuendeleza kazi za *CAMARTEC* na viwanda vidogo vidogo. Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, ndiyo watumiaji wakuu wa zana za kilimo. Ni kwa msingi huyo, *CAMARTEC* wakisaidiana na *SIDO*, *TEMDO* watumie nafasi ya majengo ya Kiwanda cha Zana za Kilimo Mbeya, ili kuendeleza utafiti unaoambatana na uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi nini hatua ya Kiwanda cha Zana za Kilimo Mbeya? Kwa nini kiwanda hiki kisipewe taasisi zetu hizo nilizozitaja, ili na wao wakishirikiana na wawekezaji wa ndani na nje, wakifufue kiwanda hicho ili tuimarishe azma ya Rais wetu, kwa kuendelea kununua bidhaa zetu wenyewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni moja kubwa ya Zimbabwe (*ZIMPLOUGH*) ilionyesha nia ya kuingia kwenye biashara hiyo ya kutengeneza bidhaa kama hizo. Sijui hili limefikia wapi. Ukombozi wa mkulima wa Kanda hiyo ya Nyanda za Juu Kusini ni kufufua kiwanda hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aone namna ya kupanga taratibu za biashara ya Machinga ili isije baadaye ikwa ni kero kwa wananchi. Biashara zote zisizo rasmi kama zikiandaliwa vizuri, watasaidia sana uchumi wa nchi, lakini pia kupunguza kasi ya umaskini. Washirikishwe katika maandalizi ya njia nzuri ya kufanya biashara zao vizuri. Sekta binafsi iendelee kupewa motisha ili mchango wao utambulike rasmi katika uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ione uwezekano wa kuimarisha viwanda vidogo katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ili majengo ya *SIDO* yaliyoko Sumbawanga, yatumike kikamilifu. Namshukuru Mkurugenzi Mkuu wa *SIDO*, Ndugu Laizer, kwa kazi anayoifanya kuifufua *SIDO* na kuelekeza ili ifanye majukumu yake kama sera inavyoolekeza. Tuwape kila aina ya msaada ili watekeleze majukumu hayo kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa kila hali.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza *SIDO* kwa ku-promote wafanyabiashara wadodo wadogo hasa wanawake Mkoani Ruvuma, kwani ukurasa mpya wa maendeleo umeonekana. Nawapongeza na kuwashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara/Serikali ione uwezekano sasa wa kutumia *SIDO* kusaidia wanawake wa vijiji katika suala zima la hifadhi ya chakula, mfano kwa kushirikisha vijana. *SIDO* isaidie utengenezaji wa *solar* rahisi za mbao za kukaushia mboga, vyakula na hivyo teknolojia hiyo inaweza kutumika kuokoa usindikaji wa vyakula katika maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuamua kuiwezesha *SIDO* kwa kuipatia vitendea kazi. Nashauri kwamba kwa kuwa kwa muda mrefu sana *SIDO* ilikuwa na vikundi nya mijini tu kwa kupatiwa usafiri na nyenzo, tunategemea sasa *SIDO* ijipanue mpaka vijiji angalau hata Makao Makuu ya Wilaya kama vile Namtumbo, Mbinga, Tunduru, maeneo ya Madaba, Peramiho na Kigonsera.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwekezaji, sera ya uwekezaji na uvezeshaji ni nzuri na inahitajika sana. Lakini yako maeneo ambayo uwekezaji wala ubinafsishaji hauwezekani katika kuanzisha au kukuza suala zima la viwanda, nashauri basi kwamba ni bora maeneo yasiyo na umeme yakaanza kuwezesha katika kuanzisha viwanda vidogo vidogo, mfano, nya kusindika mazao, matunda na kadhalika. Upo uwezekano hata wa kusaidia viwanda nya kubangua korosho, kusindika mpunga, mahindi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tofauti kati ya watafiti na wazalishaji na watumiaji. Kwa muda mrefu sana kumekuwa na tafiti nyingi za kukuza viwanda na kuongeza tija katika kukuza kilimo. Bado tafiti za wataalam za kukuza kilimo na shughuli nyingi za uongezaji tija, hazijaweza kujikita katika utaratibu wa kimtiririko. Nashauri sasa kuwepo na mpango maalum wa Wizara kuunganisha tafiti na uzalishaji katika viwanda, ili kukuza teknolojia rahisi zitakazoweza kuongeza tija. Wizara zishirikiane kuondoa mianya hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu wao wote kwa kushirikiana na kuweza kuwasilisha hotuba yao ya Bajeti kwenye Bunge lako Tukufu, tena kwa ufasaha zaidi na kuonyesha nia ya kuthibitisha kuwa wao ni askari wa miamvuli na wana uwezo wa kuwatumikia walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ni kiungo muhimu sana katika nchi kiasi ambacho uwezo wake ni mkubwa sana wa kuleta uhusiano mzuri kati ya nchi na nchi kwa kutumia njia hii ya biashara na kupata kubadilishana biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, la muhimu ambalo linafaa kuzingatiwa ni ubora wa bidhaa kwani unapokuwa na bidhaa dhaifu ujue wewe utakuwa ni msindikizaji tu katika eneo la biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia nafasi hii, sasa ni wakati muafaka wa kuanzisha biashara ndani kati ya Tanzania Visiwani na Tanzania Bara kwa kueneza utaalam kwa kupitia *SIDO*, *TEMDO*, *CAMARTEC* na vinginevyo ambavyo viko Tanzania Bara na Tanzania Visiwani haviko, ningemshauri Mheshimiwa Waziri kufanya kwa makusudi mazungumzo na Waziri mwenzie wa Zanzibar wakaweza kuwasaidia wananchi kwa kuwapa elimu ya Biashara na namna ya kuzidisha ubora wa biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yetu kuna mazao na matunda mengi ambayo yanaharibika kwa kukosa elimu ya kuhifadhi na kukosa soko la uhakika ambalo kwa kiasi wananchi wengi wangeondokana na ukali wa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuangalia kwa karibu tu kuanzia Chalinze hadi Tanga basi utaona matunda mengi ambayo wananchi hawajui nini la kufanya zaidi ya kula tu, kama vile machungwa, maembe, mananasi na matunda mengine mengi ambayo wakikosa wateja matokeo yake ni kuharibika tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningombaa Wizara kwa kutumia wataalam wao wakaweza kuwa wabunifu zaidi ili waweze kuwasaidia wananchi wetu amabo wako kizani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache napenda kuunga mkono hoja hii 100%.

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naiunga mkono hoja hii na nampongeza sana Waziri na timu yake kwa kazi nzuri wanayofanya. Pamoja na hayo napenda kuchangia machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana kuwa baada ya maneno na kelele nyingi za Waheshimiwa Wabunge kuhusu kuongeza fedha kwa asasi zetu za *R & D* kwa mfano *CAMARTEC*, *TIRDO*, *SIDO* na kadhalika bado wamepewa fedha kidogo sana. Nashauri Wizara ya Fedha isaidie kuleta *Supplementary Budget* ili asasi hizi zifanye kazi zake vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *concept* za *EPZ development strategy* lazima zibadilike ili tuweze kutumia vizuri vyanzo vyetu vyaa maliasili na mazingira tuliojaaliwa na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo bandari nne Tanzania, ambazo ni Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na Zanzibar, bahati nzuri kuna nchi nyingi zimetuzunguka ambazo hazijajaaliwa bandari kama zetu. Hivyo nashauri tutumie milango hii kwa kuendeleza maeneo huru ya kiuchumi (*EPZ*) *development*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiweza kuimarisha reli na barabara zinazoanzia bandari hizi na miundombinu ya maji, umeme na kadhalika, basi kuna uwezekano mkubwa wa kuweka viwanda maalum kwa kila eneo kutegemea na mazao nafuu malighafi kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti yakinifu zitabainisha viwanda gani viwekwe wapi na mambo yawe wazi ili Watanzania na wawekezaji wengine wajue *what's what - where* na Zanzibar iamuliwe mambo yanayoweza kuwekezwa bila kuonekana kuwepo na ushindani usio na maana baina ya viwanda vyetu vya ndani, ushindani uwe katika kuuza nje na sio kuuana wenyewe kwa wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana utafiti huu mpana ufanyike ili maendeleo ya nchi yetu yaweze kwenda kwa haraka zaidi.

**MHE. DR. IBRAHIM S. R. MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuunga mkono hoja yako na kukupongeza wewe, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu wako na watumishi wa Wizara yako kwa kazi nzuri mnayoifanya.

Pili, naomba kukumbusha suala la mikopo ya mashine ndogo ndogo za kubangulia korosho kwa ajili ya wananchi wa Jimbo langu la Kibaha. Baada ya mazungumzo yangu na Mheshimiwa Naibu Waziri na wewe mwenyewe juu ya suala hili niliviarifu vikundi mbali mbali Wilayani kwangu kuwa vingefaidika na mashine hizo ili kuongeza thamani ya zao la korosho, kipato cha wananchi na kupiga vita umaskini. Mimi niko tayari kuchukua mkopo huo na niko tayari kulipa ili mradi wananchi wangu wapate mashine hizo muhimu za kutenda kazi.

Tatu, juu ya suala hilo hilo la korosho, nafahamu kuwa Kiwanda cha korosho kilichopo Kibaha kilikuwa kiuzwe kwa mwekezaji kwa masharti kuwa kiendelee kubangua korosho. Je, Serikali sasa inaweza kutamka kama mwekezaji ameshapatikana na ni nani huyo? Aidha, katika kiwanda hicho cha korosho bado kuna madai ya malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi hasa ya walinzi, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa wananchi hao wanapata haki zao kabla kiwanda hakijakabidhiwa kwa mwekezaji mpya?

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, *EPZ* kuna umuhimu kwa Serikali kwa ujumla wake kushughulikia suala la miundombinu kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya *EPZ* yakiwemo yale ya Kibaha ili wawekezaji waweze kuwekeza. Miundombinu hiyo ni pamoa na umeme. *TANESCO* pekee haina uwezo wa kushughulikia suala hili hasa pale unapohitajika umeme mkubwa, kama ilivyotokea Kibaha mwaka 2003, iliposhindikana kumpata mwekezaji kutoka Kenya kuja kujenga Kiwanda cha Chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika aidha, ningependa kufahamu hatua zilizofikiwa katika kugeuza eneo la Kiwanda cha *TAMCO* kuwa eneo la *EPZ*. Kuna mipango yoyote ya kufufua kiwanda cha *TAMCO*? Kuendelea kufungwa kwa kiwanda hicho kunadumaza uchumi wa Kibaha na Taifa kwa jumla.

Tano, kuhusu Nyumbu, pamoja na kwamba Nyumbu ni taasisi ya JWTZ, kuna umuhimu wa kushirikiana kuhakikisha kuwa Taasisi hiyo inaendeleza utafiti, ugunduzi na uzalishaji kufikia *commercial production*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita ni kuhusu *Mkuza Chicks*. Kwa kuwa wazalishaji wa vifaranga vya kuku wa *Mkuza Chicks*, waliopo Wilayani Kibaha sasa wamejenga kiwanda cha kusindika nyama ya kuku huko Kwala Wilayani Kibaha na kwa kuwa eneo hilo (Kiwanda hicho) kinategemea kupata umeme katika kipindi kifupi kijacho, Wizara iko tayari kushirikiana nami kuwashawishi wawekezaji wengine waende kwenye eneo hilo na kulifanya la EPZ kutokana na ukweli kuwa kuna eneo kubwa huko?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumkaribisha Mheshimiwa Waziri kutembelea eneo hilo na kiwanda hicho cha pekee baada ya Bunge la Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kila la kheri na kwa mara nyingine naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *SIDO*, nashauri kuwa *SIDO* sasa iwe na mpango kamambe wa kuanzisha, kueneza na kudumisha viwanda vidogo vidogo vijijini (*Cottage Industries*) katika mtindo ule wenzetu wa India au Japan walivyofanya. *SIDO* iwe na *strategic plan* hivi sasa ya kuona kuwa viwanda vidogo vidogo vienee nchi nzima ili kuongeza thamani ya mazao yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingefaa kuwa katika kila eneo la zao fulani kama vile pamba, basi viwanda vya kuchambua pamba na kusokota nyuzi viwepo. Hivyo hivyo kwa mazao mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu biashara, kwa nini *Mtware Corridor* mpaka hivi sasa haijaanzishwa rasmi? Kwa maana viongozi wa nchi zetu tatu Tanzania, Msumbiji na Malawi bado hawajasaini mkataba wa ushirikiano katika *venture* hiyo. Pia imekuwa vigumu kutekeleza miradi ya *corridor* hiyo kwa ukosefu wa *legal attainment*. Je, Wizara inasema nini kuhusu EPZ ya *Corridor* hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utandawazi, Tanzania imejitayarisha vipi katika biashara ya kikanda (*Regional East African Market, SADC*) na ile biashara ya Kimataifa (*global*). Kwa nini Wizara ya Viwanda na Biashara isifanye mpango wa makusudi kwa kuwa-coach wafanyabiashara wakubwa ili kuwa *vigorous* na *aggressive* katika biashara ya Kimataifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri kwanza, Wizara iwe na programu ya kuwasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo na wakubwa katika kufanya biashara ambayo italeta tija kubwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia iwe na mpango wa kuwapeleka wataalam wa biashara vijiji ni pia isaidie katika suala la ujasiriamali na uanzishaji vitega uchumi.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na wataalamu wote kwa kazi nzuri ya kuandaa hotuba hii inayoleta matumaini mapya ya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutoa pongezi nyingi kwa *SIDO*. Naomba sana Wizara hii iwasaidie *SIDO* kuimarisha ili iweze kusaidia walengwa na hasa wale wa vijiji ni isipokua tungeomba waongezewe fungu ili maonyesho yao yafanyike mara kwa mara. Pia suala la bei ya vifaa iangaliwe vizuri ili wananchi wa vijiji kama wa kule Ilula, Mahenge, Dabaga, na Wilaya nzima ya Kilolo waweze kununua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa pendekeso kuhusu *CAMARTEC* ili waweze kufanya kazi hii vizuri ingekua bora kitengo hiki kirudishwe Wizara ya Kilimo na Chakula ili kitengewe fungu vizuri, kwani ni kitengo muhimu kisichokuwa na fungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuipongeza Wizara sana tena sana katika kitengo cha usajili wa Makampuni, zamani ilikuwa inakuchukua zaidi ya miezi miwili kusajili kampuni, lakini leo inakuchukua siku moja tena masaa, naomba Wizara hii iangalie na kuhoji ni uchawi gani uliotumika ili uwe mfano hata kwa sekta nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa *BRELA* sasa hivi hata rushwa hakuna kwani wameimarisha vizuri sehemu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara hii ni muhimu katika maendeleo ya nchi yetu hasa wakati huu wa utandawazi na soko huria, ningeomba kwa dhati kabisa tujiimarishe zaidi ili tuache ubabaishaji ili kazi ifanyike vizuri kama wenzetu wa *BRELA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni nzuri, ina taarifa zote muhimu na zinaeleweka, hivyo mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbinga Magharibi, naunga mkono hotuba hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya *Mtware Development Corridor* imebaki kwenye maandishi tu kama Mheshimiwa Waziri alivyoandika ndani ya hotuba yake ukurasa 53 na miaka yote inayokuja itabaki hivyo hivyo bila utekelezaji. Miradi ya *Mtware Development Corridor* ni miradi muhimu sana kwa maendeleo ya nchi hii kama Mradi wa umeme wa mkaa wa mawe Mchuchuma, mradi wa chuma Liganga, mradi wa barabara Mtware hadi *Mbamba Bay*, mradi wa daraja la Muungano kati ya nchi ya Msumbiji na Tanzania na miradi mingine kama upanuzi wa bandari Mtware na *Mbamba Bay*, utalii na maji ya uhakika Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingefaa sana Serikali ingetoa upendeleo maalumu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya *Mtwara Development Corridor*. Miradi hii kama itatekelezwa italeta mapinduzi makubwa ya maendeleo katika Mikoa ya Kusini, kwa sasa Mikoa hii haina sekta ya viwanda, utalii wala haina mashamba makubwa ya kilimo. Ufumbuzi wa haya yote kama miradi ya *Mtwara Development Corridor* ikikamilika itasaidia kuleta maendeleo katika Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Mheshimiwa Waziri angeelezea kwa undani sana kwa nini miradi ya *Mtwara Development Corridor* haitekelezeki?

Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Naibu Waziri Mheshimiwa Rita Mlaki, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii walioshiriki kuandaa mpango wa Bajeti hii wenye mwelekeo wa kuleta maendeleo kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie pia nafasi hii kuendelea kuwapongeza Waziri na Naibu wake kwa mshikamano mzuri walionao katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kuwa mshikamano huu watauendeleza na Mungu awajalie. Baada ya pongezi hizi, kabla sijaanza kuchangia nitamke rasmi kuwa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mwelekeo mzuri wa Bajeti hii, napenda uchangia juu ya uingizaji wa bidhaa nchini. Naipongeza Serikali kwani mara nyingi imekuwa ikizingatia ushauri wa Bunge hili, mfano ilipobainika kwamba kuna bidhaa feki ambazo zilikuwa zinaingizwa nchini Bunge likashauri kwamba iletwe Sheria Bungeni ya Kudhibiti Uingizaji wa bidhaa zisizofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na sheria hii kuitishwa na Bunge, bado inaonyesha kwamba Sheria hii haina neno kwani bado kumekuwepo na uingizaji wa bidhaa zisizokuwa na ubora unaostahili mfano, simu za mikononi na kuifanya nchi yetu iendelee kuwa dampo (*dumping place*).

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niitumie nafasi hii kuipongeza Serikali katika suala zima la kuimarisha viwanda vyetu nchini. Pamoja na pongezi hii ningependa kuishauri Serikali katika suala zima la ujenzi wa viwanda nchini kuwa kabla ya kujenga ni bora ingekuwa inazingatia mambo muhimu likiwemo suala la upatikanaji wa malighafi mfano, pamba, alizeti, myonyo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtazamo huu, ni bora basi Serikali ingejenga viwanda mahali malighafi hizi zilipo ili kupunguza gharama za uendeshaji na usafirishaji

mfano; Kiwanda cha tumbaku kujengwa Morogoro wakati tumbaku hailimwi huko, kwani inalimwa Tabora, Singida na kwingineko.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kutoa kwa wananchi wa kawaida, lakini kwa bahati mbaya sana kumekuwa na mfumuko wa bei za bidhaa mbalimbali mfano *cement*, mabati na kadhalika hali ambayo humfanya mwananchi wa kawaida kushindwa kumudu bei hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itazame upya upandaji holela wa bei za bidhaa hizi kama nilivyotoa mfano hapa juu mfano bei ya mfuko wa *cement* Singida ni shilingi 11,000/= na Kigoma shilingi 15,000/= je, kwa utaratibu huu wananchi wetu wataondoka kwenye matembe? Kama si utapeli wa wafanya biashara kuwe na udhibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena naomba nihitimishe kwa kurudia pongezi zangu na kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na Mungu awatangulie katika kusimamia utekelezaji wa mpango.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia Wizara na Mashirika yote yaliyo chini ya Wizara hii utekelezaji mwema wa malengo waliojiwekea katika mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri kama ifuatavyo:-

Kwanza, naomba Wizara ifanye utafiti kwa nini viwanda vingi hapa nchini havukui kama inavyotakiwa hasa viwanda vya mafuta ambayo husababishwa na *tariff* za umeme na mfumo wa kodi kushindwa kushamiri. Viwanda vinapokwama, ajira ya Watanzania hukosekana. Viwanda kama *Rajani Oilmills/Shirecu (1984) Ltd Oilmills* na kadhalika. Tunapouliza wanadai gharama za umeme na gharama zingine ni kubwa kiasi cha kushindwa kuendelea. Ni vyema kwa sasa *tariff* za umeme ziainishwe na nchi za *East African Community* kuhusu Viwanda vidogo (*SME*) napenda sana kuipongeza Wizara ya Fedha na Wizara ya Viwanda na Biashara kwa msaada wa Wizara hizi kwa shughuli za Viwanda vidogo vidogo *SIDO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kama *SIDO* itapewa nguvu naamini Watanzania wataendelea. Maendeleo ya viwanda vidogo ndiyo msingi wa viwanda vikubwa. Nchi ya India ilianza na viwanda vidogo na leo viwanda hivyo ni vikubwa sana vya Kimataifa. Naiomba Wizara ya Fedha na Viwanda *SIDO* ipewe nguvu za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba *SIDO* ipewe wafadhili wanaoweza kufanya shughuli na *SIDO* hasa kuhusu kuwaendeleza Watanzania katika swala la viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupanda kwa bei ya mafuta ni vyema ukapatikana utaratibu wa kuona gharama halisi za uendeshaji wa biashara ya mafuta ili

asilimia ya kupandisha mafuta bei iwe halali siyo ya unyonyaji. Maana mafuta yakinanda kiholela yatakwamisha maendeleo ya Uchumi na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu shughuli za utafiti teknolojia ushauri na mafunzo Serikali itowe fedha za kutosha kufanya utafiti na ambayo ndiyo msingi wa maendeleo yetu. Bila utafiti wa kutosha hatuwezi kujinasua na matatizo na maendeleo yetu. Wakati wa semina ya *CAMARTEC* mimi nimeshangaa kwa Serikali kutotilia maanani na utafiti. Serikali sasa ibadilike, watowe fedha na vifaa vyta kisasa kwa mashirika ya utafiti na pia na hata watafiti binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO* katika swala la kutoa mikopo ni muhimu sana maana huwezi kusema utoaji mikopo siyo muhimu *SIDO* na upatikanaji fedha ni muhimu sana. Viwanda pamoja na biashara sharti na pesa iwepo kama ndiyo vilainisho vyta Viwanda na Biashara. Nashauri mfuko wa fedha za kukopessa washiriki wa *SIDO* ziongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza *SIDO* kwa mfano pesa shilingi 800,000,000/= zilizotolewa miaka zaidi ya kumi iliyopita bado zipo na zimeongezeka. Kutokana na mahitaji makubwa ya fedha ni vyema fedha hizi zikaongezwa. *SIDO* inao mtandao mzuri na watalaamu walio mahili wenye uwezo na ujuzi wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imeomba juzi katika swala la kufanya biashara (*socialism*) kwa maana hiyo Watanzania wengi hawana ujuzi wa biashara ni vyema fedha za kutosha ziongezwe hasa katika swala la mafunzo kwa Watanzania hasa katika swala la mafunzo ni muhimu sana fedha za kutosha zitolewe hasa kwa *SIDO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho tena napenda kuwatachia mafanikio katika kutekeleza malengo mloliojiwekea katika mwaka wa fedha wa 2004/2005.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote naomba kukiri na kujieleza kuwa nimekuwa Ofisa mwanzilishi wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo. Nchi yetu inaendelea kujigamba kuwa kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchimi wa nchi yetu. Ni kweli nchi ipi duniani imepiga hatua za kimaendeleo kwa kutegemea Kilimo? Ulaya imepiga maendeleo yake baada ya mapinduzi ya viwanda. Marekani ilijikongoja kimaendeleo kwa kutegemea kupinga maendeleo ya kiuchumi kwa kuwatumia wakulima mithili ya watumwa? Jembe la mkono kweli lilete maendeleo? Muujiza mtupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipoanzisha *SIDO* tulikuwa wadogo wa kutengeneza koroboi kwa msaada wa Baba wa Taifa tulipiga hatua polepole hadi tukaanzisha *Industrial Estates* zingine kama vile za Arusha, Moshi, Dar es Salaam zikiunganishwa na *Sister Industries* zake katika nchi za Sweden ziliweza kuzalisha mali iliyojulikana kimataifa sasa ziko wapi na mnategemea ziweje.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Estate* kama ile ya Lindi imegeuzwa kuwa ghala la korosho. Wizara inajua Mkoani Tabora tulienda mbele na kujenga *Village Estates*,

Tabora mjini Kiloleni na Kachoma, Ussoke kule Urambo, Igunga, Choma, Nata na Magili zote zimegeuka ofisi za vijiji badala ya kuzalisha mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kugwaya viwanda nchini mwetu ni umeme. Je, ipo Kamati inayoshughulikia tatizo hili kati ya Wizara ya Viwanda na Biashara na ile ya Nishati na Madini? Ipo? Kama ipo inafanyaje kazi na imefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti unaovumbua mashine *Proto Type* unawianishwaje na uwekezaji? Kuna Kamati kati ya Wizara ya Viwanda na Biashara ile ya ubinafsishaji na uwekezaji? Kama haupo uhusiano wowote basi tutaendelea kuonyesha *Proto Type machines*. Tutapiga hatua? Sidhani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na Mheshimiwa Rita Mlaki, Naibu Waziri Viwanda na Biashara kwa hotuba nzuri walioiwasilisha Bungeni. Hakika mshikamano wa kikazi uliopo kwenye Wizara hii kati ya Waziri, Naibu Waziri na watendaji wao unaleta maendeleo ya kiuchumi kwa wananchi. Hivyo naunga mkono hotuba hii nia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri, kwanza utaratibu wa viwanda vya Samaki Mwanza kupeleka na kuza nchi za nje ni mzuri na uendelee lakini kuwepo na kitengo cha kuza samaki nchini kwa kuweka kwenye makopo. Samaki wetu Watanzania wana mafuta yenye Vitaminini A ambayo yanawafaa sana watoto wachanga. Naomba Waziri ulifuatilie na kuanzisha kitengo mara moja.

Pili, vifaa vinavyotengenezwa na *SIDO*, hakika ni vifaa imara na bora kwa matumizi ya jamii yetu Tanzania. Tatizo ni bei kubwa kwa mwanakijiji wa kawaida hawezি kununua. Kwa hiyo, kama Waziri ungetoa maagizo kwa shule zetu kununua vifaa hivyo kuititia Waziri mwenzako wa Elimu na Utamaduni ili kukuza soko la vifaa vya *SIDO*.

Tatu, mikopo, nawapongeza kwa utaratibu wa utoaji wa mikopo kwa akina mama na kwa akina baba, lakini kima kiongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono tena hotuba hii mia kwa mia.

**MHE. MAJAOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia japo kwa maandishi hotuba hii nzuri mno ya Waziri wa Viwanda na Biashara inayoonyesha dira na mwelekeo wa Wizara hii katika kukuza biashara na Viwanda vyetu kwa manufaa ya ustawi wa uchumi wa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Rita Mlaki, Naibu Waziri wake na Wataalamu wa Wizara hii nyeti kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yangu kwanza, napendekeza kwa moyo wangu wote, Mheshimiwa Waziri atafute kila mbinu za kuwapata wawekezaji wa kuja kuwekeza kwenye *Open Industrial Area* ya Himo yenye zaidi ya ekari 110. Miundombinu zote zipo. Kama vile barabara, umeme, maji na kadhalika.

Pili, wapatikane wawekezaji wa kujenga Benki na Posta za kisasa, kwani maeneo ya kujenga yapo ni suala la kufika na kumuona Afisa Ardhi wa Wilaya ya Moshi na kuonyeshwa maeneo. Wakati ni huu ambao upimaji wa viwanja unaendelea.

Tatu, Mheshimiwa Waziri na wataalam wake watembelee kiwanda cha Ngozi cha Himo waone namna gani ya kukiendeleza kwani kiko katika hali mbaya sana na ngozi ziko nyingi mno Jimbo la Vunjo kwani kila siku ni ng'ombe, mbuzi na kondoo wengi mno wanaochinjwa kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri na wataalamu wake wakizingatia maoni na mapendekezo ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara pamoja na maoni ya Msemaji Mkuu kambi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Biashara na Viwanda. Hakika, kwa miaka michache ijayo itakuwa nyota ya Afrika kwa viwanda na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Rita Mlaki, Katibu Mkuu na Wataalam waliohusika na maandalizi ya hotuba hii nzuri ambayo naiunga mkono asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii ya Viwanda na Biashara, nashauri ifuatilie kwa karibu Viwanda na Makampuni yaliyo binafishwa kama yanaendelezwa kwa mujibu wa mikataba kwani kuna viwanda na makampuni kadha ambayo shughuli zake zimesitishwa na wawekezaji na badala yake majengo yamegeuzwa kuwa ma-godown.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu, Waziri Mheshimiwa Rita Mlaki, mara baada ya kuwa Naibu Waziri alijaribu kufuatilia kwa karibu sana baadhi ya viwanda na makampuni yaliyobinafsishwa aligundua ujanja uliokuwa ukitumika na wawekezaji wa kutozalisha bidhaa zilizokuwa zikitengenezwa na makampuni hayo, ziara za Mheshimiwa Naibu Waziri katika viwanda na makampuni zilipungua kasi yake hadi hivi leo. Mwanza ulikuwa mzuri na kasoro zote zilikuwa zikitangazwa kwenye vyombo vyahabari, *television*, magazeti na kadhalika. Kwa nini ufuatiliaji huo umepungua nguvu? Kuna sababu zozote?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara ya Viwanda na Biashara kuweka mikakati itakayoinua Elimu ya watendaji wake hasa katika ngazi za Wilaya. Kwa mfano Afisa Biashara wa Wilaya Liwale, Jimboni kwangu amekuwa akikaimu nafasi hiyo kwa muda wa miaka zaidi ya nane ameomba nafasi mbalimbali za mafunzo bado kufanikiwa. Kazi zake ni nzuri na amekuwa akifuatilia kazi zake vizuri lakini Wizara haifuatilia watendaji wake kwa karibu hasa walioko pembezoni kama ilivyo Liwale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama watendaji, Maafisa Biashara Wilaya hawatapewa mafunzo yatakayokwenda na wakati wa ushindani wa kibashara, lengo la Wizara la kuandaa mfumo utakaotumika katika kuhamasisha ukuaji wa Sekta ya Biashara hadi ngazi za Wilaya hautanufaisha Wilaya zote. Hivyo ni muhimu sana kutoa mafunzo ya kina kwa Maafisa Biashara Wilaya ili wafikie daraja la Kiwilaya kulingana na shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha biashara, nashauri Wizara iandae kijitabu *Business Directory*, namna ya kufanya biashara na Tanzania. Vijitabu hivyo vitatoa *contacts* za wafanyabiashara na viwanda mbalimbali wa bidhaa zinazotengenezwa, pia vitoe au vielezee masharti kwa ufupi yahusuyo biashara hizo. Vijitabu hivyo vipelekwe kwenye Balozi zetu na kusambazwa kwa wafanya biashara wa nchi za nje. Nchi nyingi zinafanya hivyo zikiwemo *Gulf countries* kama Saudi Arabia, Qatar, *UAE* na kadhalika. Hatua hii itawafanya wafanyabiashara wa nje wawe na jazba ya kufuatilia kwa karibu biashara za Tanzania kwa kutumia *Internet*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kufuatilia biashara ya chuma chakavu. Hatua hii itanusuru kuibiwa mataruma ya reli, daraja na kadhalika, hali ambayo ilijitokeza kwa kasi hadi Wilayani kwani wezi walikuwa wakivunja madaraja na visima vyta maji na kuviuza vyuma na hivyo kukwamisha maendeleo. Naomba ufuatiliaji uimarishwe katika biashara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri viwanda bunifu kama *CAMARTEC* na kadhalika wajaribu kufuatilia vifaa vinavyoagizwa nje kwa kilimo cha mazao yetu mbalimbali kwa mfano wakulima wa korosho hasa Mikoa ya Kusini Mtwara na Lindi zao hili kinahitaji kupuliziwa *sulphur* kwa kutumia blower kutoka Japan. Bei yake ni zaidi ya shilingi 500,000/= kwa moja wakulima wa zao hilo hawawezi kumudu bei hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wabunifu wetu wangejaribu kubuni chombo cha aina hiyo nina uhakika bei ingekuwa nafuu na soko lake likawa kubwa kwani kila mlima korosho lazima atumie chombo hicho ambacho hivi sasa wachache wenye uwezo wanatumia na wakati mwingine kwa kukodisha. Kama kila mkulima wa korosho atawenza kununua kwa bei nafuu kutoka kwa Wabunifu wetu tutaendeleza kilimo hicho na kuinua kiwango cha korosho kitakachouzwa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono tena asilimia mia moja.

**MHE. DR. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, chonde chonde EPZ ijengwe ili ku-process vito vya *Tanzanite*. Mawazo ya *Kilimanjaro Airport* na pengine hayatajenga Mererani, bali yatabakiza mashimo tu Simanjiro na Manyara.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mungu kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili ili niweze kuchangia hoja ya Waziri wa Viwanda na Biashara na pia kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge katika Bajeti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijazungumza naunga hoja hii mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii vile vile kuwapa pole wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijiini kwa kumpoteza Mbunge wao aliyefariki hapa juzi. Aidha, nawapa pole wote waliopatwa na mikasa mbalimbali. Vile vile nawapa hongera wale wote waliochaguliwa kwa nyadhifa mbalimbali katika nchi yetu na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kawe kwa ushirikiano mzuri walionipa kwa kipindi cha miaka minne na natumaini wataendelea kushirikiana nami kwa kipindi cha mwaka mmoja uliobaki.

Sasa naomba nianze kuchangia kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge ambazo nitazijibui kwa mafungu maalum kutoptaka na sekta au sehemu inayozungumziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na hoja ya *SIDO* ambayo asilimia 40 ya waliochangia wameiongelea hapa Bungeni. Nitawataja ninavyoendelea kujibu hoja zao. Kwanza nashukuru sana kwa pongezi nyingi nilizopewa kwa Shirika la *SIDO* na Wizara kwa ujumla na nasema sasa tunaahidi kwamba tutafanya kazi mara mbili ya ile tuliyokuwa tunafanya. Natumaini Mkurugenzi wa *SIDO*, Ndugu Laizer yuko pale anasikia na ataungana na sisi katika kuendeleza kasi ya *SIDO*. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kuwa kusema kweli *SIDO* imerudi kwa kasi mpya kabisa na mikakati mizuri sana. Naona kumetokea na kutopteka vizuri wengine wanalaumu kwa nini mwanzo ilikuwa hivi sasa tumekwenda hivi na wangependa wajue tuna mpango gani na wametoa msukumo mkubwa sana kwamba tuhakikishe tunaiiongezea fedha na kuikarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo awali mwaka 1973, *SIDO* ilipoanza ilianzishwa na Serikali na msaada kutoka nje ikiwemo Sweden. Tukajenga Estate katika Mikoa 17 na tukawa na fedha zile za mzunguko na tukatoa vifaa mbalimbali kwa njia ya *hire purchase*. Nadhani mtakumbuka au malalamiko mengi yamekuja kwa nini ilikufa na ilikuwaje? Ilikufa kwa sababu mbalimbali zingine zilikuwa ufuatiliaji wa mikopo ile mingine ilikufa kwani utaalamu ulipitwa na wakati, mingine ilikufa ni uhaba wa masoko na hali kadhalika.

Kwa hiyo, tukapoteza zaidi ya shilingi bilioni 2 zilibaki kule kwa wale watu waliokopa na tukifuatilia, tulikuta wengine walikufa. Serikali ikalitambua hili na mwaka 1994 ukaanzishwa Mfuko wa *NEDF* ambao ni mfuko uliowekwa fedha kwa wingi ambazo zilitusaidia katika kukopesha wananchi au wafanyabiashara ndogo ndogo kwa nchi nzima.

Mfuko huo ulifikia shilingi milioni 800 na fedha hizi zimekuwa zikikopeshwa kwa watu na kiasi cha juu kilikuwa shilingi laki tano. Sasa hivi tunavyoongea mfuko huu una kiasi cha shilingi 1,400,000,000. Lakini mzunguko wa fedha mpaka sasa hivi watu wamekwishapewa zaidi ya shilingi bilioni tano kwa sababu akirudisha anachukua mwingine na hali kadhalika tunazidi kuongeza mgao wa fedha. Bado Serikali ikaona hii haitoshi, tukaanza mikakati mipyä ambayo ndiyo naisema sasa hivi hapa ya *SIDO* na nitawaomba sana Waheshimiwa Wabunge mnisikilize kwa sababu wengi tukishaongea wanakuja kuniuliza imekuwaje au tutakwenda namna gani tuweze kufanikisha biashara ndogo ndogo katika Majimbo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati ambao ulifuata huu wa sasa hivi ambao umeanza mwaka 2000 mpaka 2005 halafu tunafanya 2005 kuendelea. Tulipitisha kwanza sera ambayo tumewagawia Bunge zima na ndani ya sera mtaona kwamba tumeainisha mambo mengi ambayo tungepaswa kufanya au tutafanya kuhakikisha kwamba tumewezesha *SIDO* kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitasoma majina ya hao wanaotaka kufahamu ili kusaidia na wengine wanaochangia katika hoja hii ya Waziri. Tunaye Mheshimiwa Professa Juma Mikidadi, Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Professa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Edson Halinga aliyeongea sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wote wametaka *SIDO* iongezewe fedha, wametaka *SIDO* iwe na mikakati maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO* imeweka mikakati maalum tunaita *Strategic Plan* na huu ni mpango wa kusambaza viwanda vidogo vidogo na biashara nchi nzima. Mpango huu umeanza 2003/2004 na umefiandaa kufanya yafuatayo:-

Kutafanyika tafiti ili kubaini hali halisi ya kilichopo na mahitaji katika maeneo yenu, kutoa mafunzo ya ujasiriamali katika haja ya kuanzisha viwanda, kutoa huduma za ushauri wa kiufundi na kiuchumi kwa wajasiriamali kabla na baada ya kuanzisha miradi, kusaidia kaitika uchaguzi wa teknolojia na mashine za viwanda, kuwezesha utoaji wa mafunzo, uendeshaji na matengenezo ya mitambo ya viwanda. Hata kushauri wajasiriamali na wananchi kwa ujumla kuhusu miradi inayofaa kuanzisha, vile vile hata kuandikia mchanganuo. Narudia hapo hata kuandikia mchanganuo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO* katika mikakati yake imewafundisha wataalamu kila mkoa kama kuna mkoa ambao hauna mtaalamu tumeomba kwamba leo leo ili tukuletee mtaalamu. Huyo mtaalamu wengi tumewapa magari kila mkoa wamepata gari moja la *SIDO*, sasa hivi tumeshatoa magari mikoa 12, magari 5 yanakuja kwa mikoa mingine inasemekana yatakuwa 17 bado mikoa 3 ambayo tutawapatia vile vile. Magari haya ni kusaidia kupeleka huduma za *SIDO* mpaka Vijijini, kuwafundisha watu, kuwasaidia michanganuo na hatimaye kuweza kupata fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Stephen Kahumbi, alisikitika sana kuhusiana na *SIDO Estates* ambazo ziko kule Lindi, alitaja hasa Lindi.

Binafsi nilikwenda mpaka Lindi na niliziona zile *SIDO Estates* ambazo ziko katika mikoa 17. Mikoa mingine imeshafufuliwa kwa mfano Kilimanjaro, Iringa na hapo hapo Lindi, Arusha na Mbeya. Dar es Salaam pia zinatumika zile *estates*. *Estates* nyingi wanapangisha wafanyabiashara ndogo ndogo na wanafanya biashara ndogo ndogo na wanawalipa *SIDO*. Zamani ilikuwa *SIDO* inaweza zana pale halafu watu wanakwenda wanajifunza pale. Siku hizi tunazikodisha. Pamoja na hayo tuko tayari bado kuzifufua kwa mpango ambao tutaona unaweza ukamsaidia mwananchi wa eneo lile.

Kwa mfano pale Lindi, niliongea na Waheshimiwa wa Lindi na kujaribu kuwaelekeza kwamba yale ma-godown ama zile *estates* ndogo ndogo zilizoko pale zinaffaa kuanza kuwa Viwanda Vidogo vya Kubangua Korosho na nikawaelekeza kuwa pamoja na hayo, nendeni *Cashewnut Board* muandikiwe mchanganuo mdogo, mkishaandikiwa njooni tuwape fedha. Siyo Wizara ya Viwanda na Biashara ndiyo inafanya hivyo, isipokuwa umepangwa utaratibu kuitia Mkoaa wako uchukue fedha uenze Kiwanda Kidogo cha Kubangua Korosho. Kwa mfano, Mikoa ya Kusini mnaweza mkaanza viwanda vidogo katika zile *estates* kwa shilingi milioni 17 ambazo *SIDO* tuna uwezo wa kuwapa hiyo fedha.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwaombe tena sana kwamba Mfuko wa *SIDO* tulioanzisha wa kudhamini mikopo tuutumie vizuri. Katika mkakati huu mpya ambao nimeutaja sasa hivi tumeanzisha Mfuko wa Dhamana ambao sasa hivi unafikia shilingi 1,000,500,000/=. Mpango wake nitauseleza baadaye nitakapokuwa najibu hoja ya Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, ameomba pia *SIDO* isogee mpaka Zanzibar. Hilo ni wazo zuri, tumelisikia na tumelijibu mara nyingi hapa Bungeni. *SIDO* ilipoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 28 ya mwaka 1973 ililenga huduma za *SIDO* kwa ajili ya Tanzania Bara, lakini tumeshawasiliana na Waziri Mohamed Aboud, kwamba watazame mfumo huu huu tuweze kuhakikisha tunawasaaidia *SIDO* na huku Bara watakuwa tayari kabisa kuleta wataalam Zanzibar kuwaelekeza kwa sababu pia ni Mikoa michache ili tuweze kuanzisha kitu kama hiki kwa kina manufaa makubwa kwa wananchi wa kipato cha chini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Halima Kimbau, ameonyesha ushirikiano mzuri wa *SIDO* na amefurahi, isipokuwa aliomba tuendeleze katika kusindika

mazao ya nazi. Namuhidi kwamba tutajitahidi, tutawasiliana na Mkoa wa Pwani tuhakikishe tumekuja mpaka Mafia kwa kutumia boti ili tuweze kukusaidia katika hayo masuala. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, ametaka kujua utaratibu wa hii mikopo na vile vile masharti ya mikopo ya *SIDO*. Naomba hili kila mtu alisikilize ili tusiwe na utata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila Mkoa una Ofisi ya *SIDO* na kuna *Regional Manager* wa *SIDO*. Huyu ana washauri wake, nendeni pale sasa. Hawa tumeshawaita Dar es Salaam, tumeshawafundisha na pesa zimetengwa na Hazina na za dhamana kupitia Benki Kuu. Nawaomba na nawasihi sana, tutaumia sana kama mwaka huu utakwisha tena bika kutumia shilingi 1,000,500,000/= zilizotengwa.

Waheshimiwa Wabunge, nawaomba nyie mjaribu kuwasaidia Wananchi kwa sababu hawaelewii. Kwa mfano, katika Mkoa wangu wa Dar es Salaam, nimeutangaza mkopo, lakini wameniletea mchanganuo wa karatasi moja. Mfano mtu anaandika: "Mimi nataka kuanzisha duka, nitaiza *stationery*, naomba mkopo, wako fulani, anataja jina lake." Barua inaandikwa kwa Mheshimiwa Rita Mlaki. Huo siyo mchanganuo!

Naomba muwafuate wale Maofisa wetu wa *SIDO* wawafundishe kuandika michanganuo ya watu wenu, muainishe biashara mnazoona zinafa, mpeleke *SIDO* na zitateuliwa Benki maalum ambazo zitakuwa zinatoa hizo fedha na Serikali itatoa hiyo dhamana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mohamed Missanga ametoa hoja kubwa na nzito sana kuhusiana na viwanda. Ameshangazwa sana kwa nini viwanda vingi viko Dar es Salaam! Pia, amesikitika na amejaribu kutukumbusha Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, alivyoanzisha viwanda nchi nzima na sasa hivi vimerudi Dar es Salaam na vingine vimekufa, ina maana watu wanaokaa Mikoani hawawezi kupata huduma?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kwanza nijaribu kukumbusha Sheria ya Viwanda Na. 10 ya mwaka 1967 ambayo ilikuwa inasambaza viwanda Kikanda. Lakini baada ya soko huria hatuwezi tena kurudia hapo, inabidi mwekezaji achague anakotaka na mara nyingi viwanda vinawekwa kufuatana na malighafi iliyoko pale, kufuatana na miundombinu ambayo inapatikana katika eneo hilo na kadhalika.

Kwa hiyo basi, tutakachojitahidi ni kuwashauri wawekezaji waweze kuja kuwekeza katika Mikoa kutoptaka na malighafi zilizopo katika Mikoa husika. Viwanda vingi vinaidhinishwa na *Tanzania Investment Center* na wao wanaridhia wanapotaka kuweka hivyo viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mohamed Missanga, ameendelea kuuliza na akasikitishwa sana kwa ajili ya *cement* na mabati. Ni kweli, ukitazama kuna ukweli ndani yake. Pia, ameuliza kwa nini Kiwanda cha *Cement* kisijengwe Manyoni wakati

tunapata *gypsum*. Lakini ningependa nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kuwa, *cement* inatengenezwa na *limestone* asilimia 92, *gypsum* ni asilimia 5 tu na ule udongo mwekundu (*red clay*) asilimia tatu. Hiyo asilimia 5 haiwezi kutengeneza *cement*. Kwa hiyo, bado ni tatizo kubwa kwa malighafi ili kuweza kuweka kiwanda cha *cement*. Sasa hivi viko Dar es Salaam, Tanga na Mbeya kwa sababu kule kuna *limestone* nyngi na imepimwa na inayofaa. Kuna maeneo kadhaa tumetafuta *limestone*, kwa mfano, Mtwara na Lindi, tumekuta *limestone* imechanganyika na *gypsum* ambayo nilikwishawaeleza athari yake ya kuyeyuka na kuweza kuua watu ama kuunguza watu kwa kiwango kibaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kigoma pia tunayo *limestone*, lakini imechanganyika na kitu kinaitwa *magnesium*. Kwa hiyo, *cement* ya pale tukii-test inapasuka haiwezi kufaa. Kuna mahali pengine Bunda, Seronera, *Port Ikoma* nako kuna *limestone*, lakini ni ya *grade* ya chini ambayo kitaalam haitafaa kutengeneza hiyo saruji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwambia Mheshimiwa Mohamed Missanga, kuwa tutajitahidi kuwavutia wawekezaji waje katika Mikoa mingine kufuatana na malighafi inayopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa ameuliza kwa nini Kibaigwa pasiwekwe *EPZ* ya kusindika unga? Lakini kweli, hilo swalii ni zuri kabisa, lakini siyo Serikali inayoweka kiwanda mahali. Tunaweka vivutio halafu tunawashawishi wawekezaji waweke viwanda hapo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Job Ndugai, tutaongea na *Ben Es-haaq* wale wa Scandinavia, tutaongea na Bakhresa ambao ndio wanasaga unga kupeleka nje, tuwaambie pale Kibaigwa kuna mahindi mengi sana ili tuone kama wanaweza kuja kuwekeza pale na pia tupate ajira kwa watu wa Kongwa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Joel Bendera, ameongelea kwa uchungu kabisa kuhusu matunda yanayooza kule maeneo ya Korogwe na akauliza ni kwa nini kile Kiwanda cha *TANGOLD* mwekezaji ameshindwa kukifufua?

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki kiwanda kilibinafsishwa na PSRC kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, lakini mwekezaji huyu ambaye alikichukua ambaye ni *Azania Industries* akakuta mashine ni mbovu sana. Lakini baadaye tumekuta kuna mikataba, alikuwa kama ana mpango wa kukiiza kwa mwenzake na sasa hivi kesi iko Mahakamani. Nilifika Korogwe kukifuatilia baada ya kupata swalii hapa Bungeni na nikakuta bado kiko katika ngazi ya Mahakama. Pindi kesi itakapoisha, tutajitahidi zaidi kuhakikisha kwamba kinafufuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Beatus Magayane, naye amelalamika sana na kuuliza kwamba kwa nini viwanda vya EPZ havipelekwi Kigoma? Tumesema kwamba miundombinu itakapokamilika Kigoma tutafanya mawasiliano zaidi ya kuhakikisha kwamba EPZ inapelekwa kule. Lakini nadhani Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, alieleza vizuri sana wakati wa kuwasilisha hoja yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu *TBS*. Wanasema ni vigumu kupata nembo ya ubora wa *TBS* na hivyo *TBS* ivisaidie viwanda kufika ubora unaotakiwa. Siyo vigumu kabisa, *TBS* imejitahidi kwa kila njia, imesaribu kuweka vifaa vya kisasa, isipokuwa watu wanashindwa kukidhi yale masharti. Kwa mfano, kabla kiwanda hakijapewa idhini ya kutumia nembo ya *TBS* kuna taratibu ambazo ni lazima zifuatwe, kiwanda kiwe na hali ya uzalishaji. Siyo unapeleka *sample* halafu unataka upewe nembo, ni lazima waone kwamba unaweza ukazalisha. Vile vile, wakaguzi ni lazima washughulikie hiyo sampuli yako kwenye maabara na pia walinganishe na viwango vya Kimataifa. Kwa hiyo, tutazingatia hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, niongee kuhusu masuala aliyoulizia Mheshimiwa Salome Mbatia, kwamba kwa nini wenye daladala walipandisha nauli Dar es Salaam, wizi wa *design* za khanga na *Kibo Breweries* kununuliwa na *TBL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume kweli iliingilia mambo walivyopandisha nauli za daladala pale. Lakini naomba tukumbushe kwamba, ingawa kazi ya *fair competition* ya hii Tume yetu ni kumlinda mlaji. Kwa hiyo, wanatazama kweli kama daladala wameongeza nauli ili waweze kutoa huduma bora zaidi basi wanaruhusiwa na mfano mzuri ni ule wa mabasi ya Scandinavia ambao walipandisha nauli na huduma zake ni nzuri zaidi na watu wanazidi kupanda hayo mabasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la michoro ya khanga, kusema kweli hili linategemea na wale watu wenyewe. Kama mtu ametoa khanga yenye majani ama michoro ya tausi na kiwanda cha *Mutex* wakatoa, Urafiki wakatoa na Karibu wakatoa, wao wenyewe kama mtu anaona anaharibiwa biashara, anatakiwa aende Mahakamani kwa kutumia sheria ya *Trademark*, tusichanganye kati ya *trademark* na *fair competition*. Kwa hiyo, tunawaruhusu wao wenyewe waende kule kutazama kwa nini mwenzangu ameiga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la *Breweries*, kusema kweli Tume ilikataa kabisa mwanzo kwamba tutakuwa tumeweka ukiritimba kwa *TBL*. Lakini tukafanya utafiti kutazama kwamba, je, hata tukiachia, *Kibo Breweries* itanunuliwa au itakufa? Mwishowe baada ya uchambuzi mkubwa wa miezi miwili tukatazama taratibu na baadaye tukaweza kuwaachia *TBL* wakanunua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la kupiga filimbi, kuna masuala ambayo inafaa yatangazwe na mengine siyo vizuri kutangaza kwa sababu ya athari ya imani katika soko. Kwa mfano, kuna pombe inaitwa *Konyagi Ice* na mwagine akaanzisha ya kwake inaitwa *Nyagi Ice*. Ameanzisha kwa makusudi akijua mtu akinywa ile Konyagi atafikiria ni Nyagi, kwa hiyo, wataendelea kuinywa. Suala kama hili tunawenza tukaingilia kwamba wewe unamuungilia mwenzako na hakutakuwepo na ushindani wa halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia kwa kuongelea kuhusu soko la *AGOA*. Tanzania haijaweza kutumia kikamilifu fursa ya biashara zinazotolewa chini ya

programu maalum ya *AGOA*, *EBA*, *Canadian Initiative* na kadhalika. Suala hili liliongelewa na Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa.

Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, ni kweli Tanzania hatujaweza, Serikali tumejitahidi kuingilia kati na sasa hivi kama alivyosema Waziri katika hotuba yake kwamba Serikali pamoja na uwezo mdogo ilionao imeweka Mfuko maalum wa kuweza kusaidia biashara hii na pia tumejaribu kuleta wataalam ambao wako tayari kusaidia kama mtapendelea kuingia katika biashara ya *AGOA*.

Mwisho, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge wa Kilolo ambaye anasema maonyesho ya *SIDO* yafanyike Kikanda mara kwa mara. *SIDO* imefanya Kanda zote mara ya kwanza, tumerudia mara ya pili na sasa tunakuja mara ya tatu. Kwa hiyo, tutaendelea kufanya maonyesho kadhaa kwa Kanda zote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuhitimisha hoja ambayo niliiwasilisha leo asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao ya dhati katika hoja ambayo nimewasilisha leo asubuhi na kwa namna ya pekee ningependa kumshukuru Mheshimiwa William Shellukindo na Mheshimiwa Salome Mbatia, kwa maelezo mazuri waliyotoa leo asubuhi kuhusiana na msimamo wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kumshukuru pia Mheshimiwa Adelastela Mkilindi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani ambaye amewasilisha maoni yake kwa niaba ya Mheshimiwa Freeman Mbewe, Mbunge wa CHADEMA. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii walikuwa 46. 13 wamechangia kwa kauli na 33 wamechangia kwa maandishi. Napenda pia nimshukuru Mheshimiwa Rita Mlaki, Naibu Waziri, kwa kutoa maelezo ya baadhi ya hoja ambazo zimetolewa hapa Bungeni, lakini vile vile kwa kunisaidia katika shughuli za kuendesha Wizara ya Viwanda na Biashara. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ningependa kumshukuru Katibu Mkuu, Ndugu Ahmad Ngemera na Kaimu Katibu Mkuu Adiel Nyiti, pamoja na Wataalam wote ambao wamekuwa wakinisaidia kuendesha shughuli za Wizara. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kawaida napenda niwatambue Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa kauli hapa Bungeni. Kwanza ni Mheshimiwa Salome Mbatia, Mheshimiwa Adelastela Mkilindi, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Abdullatif Hussein Esmail, Mheshimiwa

Beatus Magayane, Mheshimiwa Ally Karavina, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi na Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud. (*Makofî*)

Vile vile, sasa naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa maandishi, nao ni Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa na Mheshimiwa Margareth Mkanga.

Wengine ni Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Samwel Chitalilo, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Hasnain Murji, Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu na Mheshimiwa Jenista Mhagama. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa michango yenu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze kupitia hoja, lakini kwa kuwa muda hautoshi nitajitahidi kupitia baadhi ya hoja. Kwa mfano, iko hoja hapa iliyotolewa kuhusu leseni za biashara ambayo imetolewa na Mheshimiwa Adelastela Mkilindi, Msemaji Mkuu wa Upinzani, pia Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Herbert Mntangi na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wengine.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa napenda kuwathibitishia kuwa, Serikali inatambua matatizo wanayopata wafanyabiashara na Wananchi katika kutimiza masharti ya kukata leseni za biashara na umuhimu wa kurahisisha utaratibu na masharti yaliyopo. Hatua hiyo itawezesha sekta isiyokuwa rasmi kukua na kujumuika na sekta rasmi na kuchangia katika kuendeleza ajira na mapato ya Wananchi pamoja na ya Serikali na hivyo kupiga vita umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hii, Serikali inakusudia kufuta kabisa utaratibu wa leseni za biashara unaotokana na Sheria ya Leseni ya Biashara Na. 25 ya mwaka 1972 na kuweka utaratibu mpya utakaotekelizwa chini ya mifumo miwili. Mfumo wa kwanza unahusu uandikishaji wa biashara zote zinazofanyika nchini. Uandikishaji huu utafanyika katika Ofisi za Serikali za Mitaa, yaani Hal mashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji. Uandikishaji huu utachukua nafasi ya leseni za biashara zinazotolewa kwa mujibu wa Sheria Na. 25 ya mwaka 1972.

Aidha, Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Kitengo cha Udhibiti Bora (*Better Regulation*) ambacho kiko katika Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji

inaandaa rasimu ya sheria ya uandikishaji wa shughuli za biashara pamoja na taratibu zitakazotumika kwa utekelezaji wake. Wadau wote watashirikishwa katika kuandaa mfumo huu mpya ili kuhakikisha kuwa mfumo mpya unakidhi mahitaji ya Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa pili unahusu utoaji wa leseni za udhibiti (*regulatory licensing*) ambazo hata hivi sasa zinatolewa kwa mujibu wa sheria mbalimbali za kisekta. Lengo la utoaji wa leseni hizi ni pamoja na sababu za kiusalamu, kulinda afya za watumiaji na hata ulinzi wa mazingira na raslimali za Taifa. Lengo ni kupitia sheria zote zilizopo ili kuziwianisha na kuzifanyia marekebisho kulingana na mahitaji halisi ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zilizotangazwa kupitia Bajeti ya Serikali ni hatua za mpito. Nataka kusisitiza hili, hatua zile ni za mpito kwa sababu jambo hili ni kubwa sana, haliwezi kuwa la mara moja. Kwa hiyo, ndiyo maana tunasema tutaleta Muswada, tutaandaa mambo vizuri halafu tunaweza tukapiga hatua nzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya *turnover* ya biashara. Nakubaliana kabisa na Waheshimiwa Wabunge kuwa ni vigumu kufahamu *turnover* ya biashara mpya kama hati ya uandikishaji wa biashara itatolewa mara moja tu kwa maisha. Hili ni mojawapo ya mambo ambayo tunataka tuyashughulikie. Ni kwa nini tunaandikisha biashara? Tunaandikisha biashara kwa sababu tunataka tufahamu biashara zinafanyikaje, lakini ya pili tunataka tuondokane na hii sekta kubwa isiyokuwa rasmi, tunataka tuipeleke kwenye rasmi. Kwa wale Waheshimiwa Wabunge ambao wamesoma kitabu cha De Soto hayo ndiyo mambo yenye tunayafanya sasa. Kwa hiyo, ni muhimu kuyazingatia haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuthibitisha leseni, mojawapo ya malengo ya uandikishaji wa biashara ni kujua ni nani anafanya shughuli za kibashara, mahali anapoendesha hiyo shughuli ya biashara na kuona kama taratibu zilizowekwa zinatekeletwa, ukaguzi wa mara kwa mara utafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu ya watendaji na umma, Wizara inatambua kuwa mabadiliko yaliyotangazwa katika Bajeti ya Serikali na ambayo yanaandaliwa ni makubwa. Aidha, mabadiliko haya makubwa yana uwezo wa kurahisisha sana taratibu za kuanzisha na kuendesha biashara hususan kwa wawekezaji na wafanyabiashara wadogo. Hata hivyo, mafanikio yatapatikana endapo tu wasimamiaji wanajua majukumu yao na wale ambao wanawajibika kuandikisha biashara zao wanafahamu wajibu na haki zao, maana hii ni muhimu. Wataalam wajue wajibu wao, lakini wale wafanyabiashara nao wajue wajibu wao, lakini na haki zao ili hawa wanaowaandikisha wasiwaonee. Kwa hiyo, hili ni jambo la muhimu na tunapenda tulifanye vizuri kwa ufanisi ili Taifa letu liweze kunufaika na mabadiliko haya ya utaratibu mpya wa leseni ndani ya jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niendelee na Waheshimiwa Wabunge wengine. Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini na Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, hawa wamezungumzia suala la kiwanda cha *Premier Cashewnut*

*Industries* ambacho kiko Vingunguti, wanahoji kwa nini kimefungwa. Kimefungwa kwa sababu waendeshaji yaani wenyе mali katika kiwanda kile wanalamika kwamba gharama za uzalishaji zimekuwa kubwa mno, kwa hiyo, ndiyo maana wakaomba waingie EPZ.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini utaratibu wa EPZ ambao unasihamiwa na NDC kama Wakala wa Serikali kwa mara ya kwanza uliwakatalia, wakaomba mara ya pili wakakataliwa. Ni kwa misingi hii ya kufuata sheria tu, hawakukataliwa kwa sababu ya ujeuri wao, walifuata taratibu za sheria wakasema: "Ninyi hamfai kuingia katika EPZ." Kwa hiyo, wakaandika barua ya ku-*appeal* kwa Waziri ambayo sasa tunaizungumza katika Serikali na nina hakika tutapata ufumbuzi.

Tatizo lao kwa kweli ni kodi nyingi, kwa sababu hizi kodi kwa kweli zinalazimisha watu wetu wapeleke korosho ghafi, sasa sisi hatupendi hili jambo, tunapenda tusindike hapa. Kwa hiyo, ni lazima tuwe na utaratibu tofauti wa kushughulikia Viwanda vya Korosho ili waweze kupenda na kunufaika na kupeleka nje korosho zilizobanguliwa. Hili ndiyo linatakiwa lifanywe na tutalifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala amesema *sulphur* ina *agent* mmoja tu Mkoani Mtwara. Ni kweli yupo mmoja, lakini jukumu letu sisi kama Serikali ni *facilitation*. Kwa hiyo, tunaendelea kuhamasisha wawekezaji wengi zaidi waingie ili waweze kushughulikia suala hili la *sulphur* wasiwe peke yao tu hao hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Maonyesho ya Biashara, suala hili limeulizwa na Waheshimiwa Wabunge wengi wakiwemo Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Joel Bendera na kadhalika. Sasa jibu lake ni kwamba, kwa maonyesho haya kwa kweli mwaka huu tumejifunza kwani hatukutarajia kwamba tutapata watu wengi namna ile. Kwa mara ya kwanza tumepata watu wengi hasa ile Siku ya Sabasaba yenyewe. Kwa hiyo, nimeelekeza BET na Kamati yake kwamba kwanza tuongeze milango, badala ya kuwa na mlango mmoja tuwe na milango miwili ya kuingilia. Lakini sehemu zile nazo ziwe nyingi isiwe moja tu hapo hapo watu wengi wanalandikana, hapana, tuwe na sehemu nyingi. Lakini la pili katika hili ni kukata tiketi, tumesema wasikate tu pale pale, mtu anaweza kukata hata Mjini, anakuja pale anaingia tu. Kwa hiyo, hili nalo linatekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo tumeshalielekeza ni lile la kutochanganya maonyesho haya. *Dar es Salaam International Trade Fair* ni maonyesho ya Kimataifa, lakini vile vile Watanzania wanapenda kukumbuka Sabasaba yao. Kwa hiyo, wanaokwenda pale wengi hasa ile siku ya Sabasaba ni *for fanfare*, siyo kwa ajili ya Maonyesho ya Kimataifa.

Kwa hiyo, lazima tuwe pale na sehemu mbili ambazo zitawezesha hawa waende, lakini sehemu kubwa ile iendelee kuwa ya Kimataifa na watu wasisongamane kama walivyosongamana mwaka huu. Kwa hiyo, hili nalo tunalijua na tutaendelea kulishughulikia ili kuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Raynald Mrope, anaulizia kuhusu kuanzishwa *EPZ* ya Mtwara. Tatizo letu ni ufinyu wa Bajeti, siyo kama nia yetu ni mbaya, hapana, nia yetu ni nzuri ila tatizo letu ni ufinyu wa Bajeti. Kwa mfano, kama kwa miaka mitatu mfululizo tumepata shilingi milioni 60 kwa ajili ya *EPZ* huwezi kupiga hatua, huwezi. Nikupe mfano wa Kenya. Kenya walipoanza walipata Dola za Kimarekani milioni 30, hata hawa wenzetu wa Uganda wamepata milioni 20 za mkopo kutoka kwa *World Bank*, sasa na wenyewe mkiongezea mnaweza mkaunda mazingira mazuri zaidi ya kuwekeza na napenda kusisitiza hili kwamba, katika mazingira ya leo ya viwanda siyo tu kuwezesha kupata umeme, barabara, simu, maji na kadhalika, lakini sasa hivi hata majengo. Majengo ya kiwanda ni moja ya miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa navyo hivyo utapata wawekezaji haraka maana tumejifunza Kenya na tumejifunza Uganda, tumejifunza kale la nchi kadogo la Lesotho kale kana viwanda vya *EPZ* zaidi ya mia mbili vya nguo (*garments*) na wanapeleka Marekani. Mwaka 2003 walipeleka dola za Kimarekani 380, mwaka huu wanasema zitafika 420 milioni. Kwa hiyo, unaweza kuona kwamba bila kuwa na miundombinu sahihi huwezi kupiga hatua katika *EPZ*, ni lazima ufanye hivyo. Kwa hiyo, hoja hapa siyo ya ujeuri lakini ni hoja ya pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa anaulizia ni kwa nini nchi yetu ina wanachama wengi? Tuna Jumuiya ya *East African Community*, tuna Jumuiya ya *SADC* na ni kwa nini tulitoka *COMESA*?

Sasa kwanza niseme kwamba kuwa na Jumuiya hizi nyingi siyo jambo bay a kwa kweli kwa sababu kwa mfano *SADC* kuna *historical background* kwa nini tuliiingia mle. Lakini kuwepo *SADC* ni jambo jema kwa sababu pale kuna Afrika Kusini ni *an economic power*. So, kuwa nao ni jambo jema, lakini vile vile kuwa na wenzetu hapa majirani zetu Uganda na Kenya ni jambo jema vile vile, kwa hiyo, ni muhimu kuwepo. Sasa hili la *COMESA* tulijitoa kulikuwa na sababu maalum, lakini Serikali iko katika kufikiria jambo hili upya na tutafanya uamuzi pale Serikali itakapokuwa tayari.

Kuhusu suala la Mchuchuma na Liganga limezungumzwa na Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, Mheshimiwa Ally Karavina na Wabunge wengi hata nadhani na Mheshimiwa Rainald Mrope pale na kadhalika. Sasa tatizo la hapa, hatua tuliyopiga ni nzuri na kubwa tunaendelea sasa hivi, lakini tatizo lilikuwa ni namna gani kwanza kuamua jambo hili kubwa kwa ajili ya *project tunazoziita anchor projects* za Mchuchuma na Liganga , lakini tunapiga hatua vizuri. Kwa mfano Liganga tumeshapata wawekezaji ambao wameonyesha nia kwanza Kenya, pili India, tatu China . Kwa hiyo, tatizo letu la Liganga kwa kweli sasa hivi litakuwa ni suala la usafiri wa barabara. Kama tukitengeneza barabara na reli suala la kuchimba Liganga litakuwepo na hata suala la Mchuchuma nalo tumefikia hatua nzuri sana kwamba Serikali imeshatoa kibali kwa wawekezaji binafsi ili wajiandae kuona jinsi gani wanawenza kufufua. Kwa hiyo, jambo hili tumepiga hatua tumechukua muda, siyo mbaya kuchukua muda kwa sababu tunataka tulijue vizuri, lakini sasa tumepiga hatua. Mimi mwenyewe nimeshakwenda mara mbili pale Liganga na Mchuchuma kwa hiyo, napajua kabisa kwamba sisemi kwa sababu sijui, hapana napajua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Semindu Pawa, anakumbusha kwamba *TBS* ipime bidhaa zilizoko kwenye *supermarket* mara kwa mara na *TBS* vile vile ifanye *surprise check up* hasa kwenye *supermarkets* na viwanda vilivyobinafsishwa na ambavyo havizalishi vichukuliwe na kupewa wawekezaji wengine. Pia Viwanda vyā Magunia vifufuliwe.

Hoja hizi zote tunaziafiki, lakini napenda kusisitiza tu kwamba *TBS* inafanyakazi hii mara kwa mara, isipokuwa *constrain* yao ni *manpower* lakini wanajitahidi kwenda kukagua kule na siyo wao tu hata Mamlaka ya Madawa na Vyakula ambayo iko chini ya Wizara ya Afya na yenyewe inafanya kazi. Ile *TUKUTA* tuliiua kwa sababu ilikuwa imepitwa na wakati kwa hiyo, tuna mamlaka mpya ambayo inashughulikia kazi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda ambavyo vimebinafsishwa lakini havifanyikazi katika Wizara yangu nadhani sasa hivi viko viwili ama vitatu. Kwa sababu kilikuwa kimoja cha *Polytex* cha Morogoro tulikinyang'anya lakini yule bwana tukatangaza upya akachukua tena yule yule. Lakini sasa hivi sehemu kubwa amekikarabati. Hivi ninavyosema kuna wafanyakazi karibu 200 na tatizo sasa hivi anangoja pamba.

Kwa hiyo, kiwanda kile tunaweza kusema kimefufuka. Viwanda vyā ngozi vyā Morogoro na Mwanza ambavyo unaweza kusema ndiyo vimebakia, hivi wawekezaji wana sababu maalum ambayo sisi Serikali tunaishughulikia. Kwa hiyo, mimi nina hakika tukikamilisha sisi Serikali mambo yale ambayo wametutaka tufanye, viwanda pia vitafufuka. Kwa hiyo, kazi inakwenda vizuri. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na swali la *EPZ* ya Kibaha. Mimi nataka kusema hivi pale Kibaha *TAMCO*, Serikali ilishaamua kwamba pawe *EPZ* na tunaendelea kupaendeleza kama *EPZ*. Shabaha yetu pale ni kuwa tuwe na kiwanda cha kwanza cha kuunganisha matrekta na tunafanya mjadala huu mzuri tunataka tuwe na kiwanda cha trekta pale. Tulishawaomba Wahindi, Mahendra Mahendra wamechukua muda, sasa tunawaomba wengine. Kwa hiyo, tunaendelea kuwaomba na tukifanikiwa tutawaleta pale. (*Makofit*)

Lakini vile vile wenzetu wa Nyumbu tunashirikiana nao, nao wanataka ule mradi wa *Nyumbu commercialize* na mahali pake ni pale, pana *facilities* tayari. Kwa hiyo, ni muhimu viongozi wakatambua kwamba uamuzi huu wa kuweka viwanda pale ni uamuzi mzuri. Mimi nimetembelea Bangladesh, viwanda vyā nguo haviko mbali na mji, viko katika mitaa mle mle. Unaweza kuona jengo la ghorofa tatu, nne, mle ndani ndiyo kiwanda cha *garment*, kwa hiyo, jambo hili tusishangae. (*Makofit*)

Mimi nafikiri kwa watu wa Pwani kuwa na viwanda vingi pale Kibaha, itasaidia kwanza ajira, lakini vile vile itasaidia hali bora ya hawa watakaoajiriwa. Kwa hiyo, ni jambo zuri kwao kutenga eneo hilo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Remidius Kissassi, ameuliza suala la Bandari ya Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na Zanzibar ambalo hili ni jambo la *Special Economic Zones*. Dhana hii inakubalika leo katika shughuli za kiuchumi kwa sababu ya ku-*fast track economic activities*. Kwa hiyo, jambo hili linachunguzwa na nina hakika tutakapopata uamuzi mzuri tutaweza kufanya uamuzi. Lakini lina mambo yake, mambo haya hayataki kufanya haraka, yanatakiwa kufanya taratibu na vizuri. (*Makofî*)

Pia Mheshimiwa Salome Mbatia, amezungumzia suala la *internet* Wilayani, hili ni jambo zuri. Lakini ni muhimu vile vile kujua kwamba namna gani hawa wananchi watawezeshwa kutumia *internet* na kuzianzisha *internet* kwa hiyo, hili si jambo rahisi lakini ni jambo zuri. (*Makofî*)

Kuna suala la maendeleo ya shughuli za *CAMARTEC* ambalo pia ameliuza Mheshimiwa Raynald Mrope, vile vile Mheshimiwa Edson Halinga amelitaja hapa. Hili napenda kusema ya kwamba hili tunalipokea na tutaendelea kulishughulikia kwa nguvu zetu zote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mafuta la *TIPER* ambalo limeulizwa hapa kwa nini *TIPER* imefungwa? *TIPER* kwa kweli ni kiwanda lakini hakiko moja kwa moja chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Lakini napenda kusema kwa sababu najua kwamba kiwanda kile kwa kweli kimechoka ni cha siku nyingi sana. *Machine* zake ni *obsolete*. Kwa hiyo, kuendelea kukiendesha ni hasara kubwa. Wenzetu wa Kenya ambacho ni nafuu kidogo kilifanyiwa ukarabati na chenyewe kinawapa matatizo kweli.

Kwa hiyo, hoja hapa kama alivyosema Waziri wa Nishati na Madini kwamba tunatafuta mwekezaji, tukipata mwekezaji, tukimpa ili yeye aweke *machine* mpya ambazo zinaweza kufanya kazi vizuri zaidi kuliko ilivyo sasa hivi na kwa faida. Vinginevyo mnaweza mkawa na ndiyo ikaongeza gharama zaidi. (*Makofî*)

Liko pia suala la Mheshimiwa Dr. Mary Nagu alisema vipi *EPZ* ya Mererani? Hili tunatalifikiria hatujalisahau tunaendelea kulishughulikia lakini tatizo letu ni fedha. Kwa kweli ufumbuzi kwa maoni yangu matatizo ya Mererani pale ni kupafanya *EPZ*. Kwa maana hiyo, kila kitu kinakuwa mle mle, *auction flow* inakuwa mle mle, *bank* inakuwa humo humo, maduka yanakuwa humo, *everything within those premises*. Hapa unaweza kupiga hatua vizuri. (*Makofî*)

Pia Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud pia alizungumzia *TIPER* lakini pia na *UFI*. *UFI* imebinafsishwa, kiwanda kile kipyä sasa kitakuwa kinatengeneza mabomba pale ambayo yatatumika kwa Mradi wa Maji wa Shinyanga, yale mabomba mapana na itakuwa ya kwanza katika nchi yetu kutengeneza mabomba makubwa namna ile. (*Makofî*)

Kwa hiyo, kazi ile ni nzuri na inaendelea vizuri pale kama umepita karibuni pale Dar es Salaam utakuta kiwanda kile kinaanza kukarabatiwa na matumaini yangu kitaanza uzalishaji mapema zaidi. Kwa hiyo, jambo hili ni zuri. (*Makofî*)

Halafu Mheshimiwa Ally Karavina amezungumzia suala la *AGRO Processing Industries*, suala la uchumi wa jiografia, suala la Kiwanda cha Zana za Kilimo cha Mbeya na Kiwanda cha Mbolea. Mambo yote haya ni mazuri na mimi ni matumaini yangu kwamba baada ya kuanza kutumika kwa gesi ya Songsongo hatua ya pili itakayofuata ni kuwa na Kiwanda cha Mbolea, kutokana na gesi ile kwa sababu mpango huo ulikuwepo tangu zamani. Kwa hiyo, huu utaweza ku-*take off* baadaye. (*Makofi*)

Suala la Kiwanda cha Zana za Kilimo cha Mbeya tunatafuta mwekezaji, tukimpata ataendelea na kazi ile ambayo sisi tulishindwa kwa sababu hatukuweza kuendesha vizuri kiwanda kile. Uchumi wa jiografia hili ndiyo muhimu sana kwa sababu Tanzania ilivyo kijiografia ni mahali pazuri sana kuendesha *transit trade*, ndiyo, *transit trade* ni *very ideal* kwa sababu tunapakana na Burundi, Rwanda na Uganda ambao hawawezi kufika baharini bila kupitia Tanzania. Tuna *Eastern Congo*, hata Zambia na Malawi.

Kwa hiyo, suala hili la uchumi wa jiografia mimi nakuunga mkono na tutaendelea kulifuatilia na ndiyo maana sera yote ya *special development initiative* msingi wake ni huo kutumia jiografia katika kuleta maendeleo ya nchi ndiyo maana kuna *Mtware Development Corridor* na *Central Corridor*. Tena sasa hivi hapa mameneja wake tayari wameshateuliwa wapo pale *NBC*. Kwa hiyo, tunapiga hatua tunakwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni suala la Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, ametuambia pia ni sawa sawa kwamba bila kuwa na umeme, hamuwezi kupiga maendeleo ya viwanda. Ni kweli kabisa, umeme, maji na kadhalika ni vitu muhimu. Kwa hiyo, hili lote tunalitambua na tunaendelea kushirikiana na Serikali, kwa ujumla yote ili kuweza kufanikisha suala la umeme, maji, barabara, miundombinu na suala la simu. Katika mazingira ya leo masuala kama *internet* na kadhalika. Yote haya ni muhimu sana katika ujenzi wa viwanda na ujenzi wa biashara katika mazingira haya mapya ya uchumi wa soko na utandawazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge na naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

## **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **Fungu 44 - Wizara ya Viwanda na Biashara**

Kifungu 1001 - *Administration and General* .... .... .... .... .... 2,152,858,500/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, msimame hivyo hivyo. Mheshimiwa George Mlawa kaa, Mheshimiwa Maria Watondaha kaa, Mheshimiwa Philip Magani, Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Hasnain Mohamed Murji, Mheshimiwa Thomas

Ngawaiya, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, mkae. Mkae wote. Haya Mheshimiwa George Mlawa.

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Mheshimiwa Waziri, anipe ufanuzi *Sub vote 1001*. Katika mchango wangu wa maandishi pamoja na mambo mengine nilielezea au nilipongeza kitendo cha Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuweka jiwe la msingi la Soko la Kimataifa Kibaigwa na nikapendekeza vile vile kwamba sehemu nyingine ambazo zinazalisha sana chakula kama Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini, kunaweza kukawa na Masoko ya Kimataifa ya aina hiyo ili kupeleka chakula na mazao mengine katika soko la *SADC* na nikapendekeza vile vile kwamba hilo linawezekana hata katika jimbo langu kama tunaweza kuwa na soko la Kimataifa kule Tanangozi au Ifunda ambayo ni *along the main road*.

Sasa niliomba Mheshimiwa Waziri, atusaidie ku-*facilitate* wawekezaji watujengee masoko ya namna hiyo. Sasa Mheshimiwa Waziri, ningemba atoe *comment* yake je, jambo hilo linawezekana? Ahsante. (*Makofii*)

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo kuhusu hoja aliyoelezea Mheshimiwa George Mlawa. Kazi ya kuhamasisha wawekezaji ni kazi ambayo naifanya siku zote na mimi niko tayari kuhamasisha lakini siwezi kutoa ahadi kwamba nitamleta mwekezaji fulani aje akajenge soko katika Jimbo la Kalenga au Iringa. Kitu ninachowea kusema kwamba sisi kama Serikali, mimi kama Waziri nitaendelea kuhamasisha wawekezaji. Tumehamasisha wengi sana. Pale Ubungo tuna wawekezaji karibu 8 kwa ajili ya *Export Processing Zone* ya *garments*, lakini bahati mbaya hatuna mahali pa kuendesha shughuli hizo. Kwa hiyo, tuna matatizo hayo. Lakini kwa kuhamasisha tutahamasisha lakini siwezi kusema kesho nitawatafuta mmoja aje, nitakuwa nadanganya Bunge hili na mimi naogopa. Ahsante sana. (*Makofii*)

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuongeza maelezo ya ziada kwa yale ambayo ameyatoa mwenzangu Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, kwamba kama Mheshimiwa George Mlawa, atakubali nadhani angesubiri mpaka tarehe 29 Julai, 2004 wakati nitakapotoa hotuba yangu nitakuwa na maelezo makubwa ya kueleza juu ya uendelezaji wa masoko katika Taifa letu. (*Makofii*)

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Sub vote* ya 1001 mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa katika maelezo yake Mheshimiwa Waziri ameeleza kiwanda cha *UFI* kimebinafsishwa na sasa kitakuwa kinatengeneza mabomba na kwa kuwa Kiwanda cha Zana za Kilimo cha Mbeya bado wanatafuta mwekezaji. Lakini kwa kuwa zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima na wanategemea majembe madogo madogo hasa sisi wa Mkoa wa Lindi ambao matrekta ni machache sana. Je, tutapata wapi zana za kilimo kama *UFI* inatengeneza mabomba tena na siyo zana za kilimo? Naomba ufanuzi. (*Makofii*)

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo kuhusu maelezo aliyotoa Mheshimiwa Maria Watondoha, kwamba ni

kweli Kiwanda cha *UFI* kimebinafsishwa na sasa kinafanya kazi nzuri zaidi *output* na *turnover* yake itakuwa kubwa zaidi na Taifa litanufaika zaidi kwa namna ya kwamba kwanza *tuta-serve foreign exchange*, haya mabomba tungeagiza nje kwa ajili ya mradi mkubwa huo wa Maji wa Shinyanga. Lakini sasa tunatengeneza wenyewe tutakuwa tunapata. Kwa hiyo, *self-reliance* hii mimi nafikiri tungeipigia makofi, ni nzuri. (*Makofî*)

Sasa kuhusu majembe, majembe yanapatikana katika nchi na sisi tutaendelea kuyaagiza majembe. Lakini ndiyo maana nimesema Kiwanda cha Zana za Kilimo Mbeya tutaendelea kumtafuta mwekezaji ili aweze kukinunua na aendelee kutengeneza majembo na *ma-plough* ya kukokotwa na wanyama. Kwa hiyo, hili tunalifanya lakini nataka kusema kwamba mambo haya ya kumtafuta mwekezaji ni magumu kweli, yanachukua muda kweli kweli na yanatokana na mazingira mliyomwekeea. Kwa mfano Kiwanda cha *SPM* kama mnakumbuka imechukua miaka 10 kumtafuta mwekezaji mpaka tukawa hatuelewani wakati fulani hapa ndiyo tukampata. Sasa kwa hiyo, jambo hili la kutafuta mwekezaji siyo rahisi. Mwekezaji hanunuliwi kwa pesa, anaomba, anabembelezwa, halafu anawekewa mazingira muafaka. Ahsante. (*Makofî*)

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Lakini swalilangu lilikuwa ni je, zana za kilimo zitakuwa zinatengenezwa wapi? Au anachotuambia kwamba sasa majembe ya mkono tutakuwa tunaagiza kutoka nje na hatutegemei kuzalisha humu nchini? Nilikuwa nataka ufanuzi huo tu, ili na sisi tufahamu hasa sisi wakulima wadogo wadogo tunaotegemea majembe zaidi. Nakushukuru.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanuzi ni kwamba nimesema pale mwanzo kwamba majembe yanaendelea kuagizwa kutoka nje. Hivi ndani ya nchi tuna majembe na yanaagizwa kutoka nje kutoka China na Kenya. Kwa hiyo, majembe yataendelea kuagiza hilo la kwanza.

Lakini la pili, nimesema vile vile kwamba Kiwanda cha Zana za Kilimo cha Mbeya tunamtafuta mwekezaji, akipatikana ataendelea kutengeneza majembe ndani ya nchi. (*Makofî*)

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kuhusu kifungu 1001 Mshahara wa Waziri. Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu suala la *sulphur* mimi nadhani hakulenga hoja ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Abdillahi Namkulala.

Swali lilikuwa ni kwamba pamoja na kuwa aliyepewa kibali cha kuleta *sulphur*, mfanyakabiashara huyo alihodhi ile *sulphur* hakuiuza wakati muafaka, wakati wananchi wanatangaziwa kuwa bei ya *sulphur* itakuwa shilingi 8,500/= kwa mfuko kwa kilo 50. Lakini kilichotokea ni kwamba wakati ambapo hakuna mtu mwininge aliyeagiza ile *sulphur* kwa sababu wakati wa kutumia *sulphur* umeshafika yeye akawa anafanya utaratibu wa kugawa ile *sulphur* kupitia wafanyakabiashara ndugu zake na akaongeza bei ya *sulphur* kuwa mfuko mmoja shilingi 15,000=/. Sasa je, hii si ukiukaji wa haki ya biashara (*fair trade*)? Je, mtu huyu atachukuliwa hatua gani? Hiyo ndiyo hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Naomba nimjibu Mheshimiwa Philip Magani, kwa swali ambalo amelileta sasa. Pale mwanzo tulivyodhani sisi na tulivyopata maelezo ya Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, ilikuwa tatizo alikuwa mfanyakiareshara mmoja ambaye ana ukiritimba. Kwa kweli katika mazingira ya mahali popote pale katika uchumi wa leo kama unakuwa na mfanyakiareshara mmoja lazima atafanya ukiritimba. Lakini hilo la kuhodhi haliwezi kumngoja Waziri wa Viwanda na Biashara kwa sababu pale Lindi pana viongozi wa Serikali. Huyu mnashtaki tu, anapata msukosuko halafu anatengeneza mambo yake vizuri.

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijatosheka na maelezo aliyotoa Mheshimiwa Waziri. Mimi nilidhani kwamba Wizara yake ndiyo inasimamia biashara kwa kupitia kwa ma-*Regional Commissioner* na kadhalika. Je, alitoa *instructions* zipo kwa ma-*Regional Commissioner* hao?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ndiyo napata sasa hivi hapa kwenye hoja hii. Sasa nitatoaje *instruction*? Hili kama ni tatizo linatakiwa liandikiwe barua kwa *Commissioner* wa *fair competition*, analalamika kwamba kuna mtu hapa anahodhi bidhaa kama alivyofanya mtu wa *Mabibo Beer and Wines* ameandika barua yake, tena huyu Bwana *Commissioner* wa *Fair Competition* yupo pale anafanya mambo kisheria kabisa, anachunguza na kadhalika. Unajua uchumi mpya huu hatutakiwa Serikali tuingilie mara kwa mara.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Ndiyo! (*Makofî/Kicheko*)

Uchumi mpya huu, hili naomba nilieleze vizuri na nimelieleza kwenye hotuba yangu pale kwamba katika utaratibu huu wa uchumi mpya *Commissioner* ana vitu viwili pale, ye ye mwenyewe kama ya Tume ya *Fair Competition* lakini ana pia *Fair Competition Tribunal* ambayo ina ma-*commissioners*. Kwa hiyo, lazima mshtaki tena muandike na *evidence* kwanza kwamba kwa nini mafikiri huyu mtu anafanya vibaya?

Sasa wao wenyewe ndiyo wanafanya *investigation*. Ule uchumi wa zamani wa kutumia mabavu tuuache. Ndiyo! (*Kicheko/Makofî*)

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kuhusu kifungu 1001 Mshahara wa Waziri, nina mambo mawili madogo. La kwanza kwa vile viwanda ndivyo vinasaidia uzalishaji mali yaani uchumi unaongezeka katika nchi na kwa maana ya Mkoa wa Mtwara, kuna viwanda ambavyo bado havifanyi kazi kwa muda mrefu na wananchi wake kukosa kuzalisha kwa maana korosho zinazobanguliwa kuuzwa nchi za nje. Ningependa Waziri anisaidie kwa sababu sikusikia alipokuwa anahitimisha. Pamoja na mipango ambayo iko humo lakini mipango nimechoka nayo kusikia mipango, mipango, tunataka utekelezaji. (*Makofî/Kicheko*)

La pili, ni kuhusu *Mtwara Corridor*. *Mtwara Corridor* tangu imeanza sasa ina muda mrefu lakini utekelezaji wake unasuasua. Mimi nilitegemea leo Waziri atafafanua zaidi kwa sababu umekusanya mipango ndani yake katika *Mtwara Corridor*. Kama hafafanui hapa na hii ndiyo Bajeti leo tunaipitisha atafafanua lini? Naomba anipe maelezo. (*Makofî*)

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Lydia Boma, kwa maswali yake yote mawili. Kwanza kuhusu viwanda vya korosho, unajua sasa hivi katika mazingira ya leo viwanda vya korosho ambavyo vilikuwa vinatumia mashine ya zamani haviwezi tena ku- *meet export requirements* kwa sababu korosho ikipita kwenye mashine zile inapondekapondeka kwa hiyo, unakosa ile *grade one* ambayo inatakiwa. Korosho ina *grade* kama 32.

Kwa hiyo, ndiyo maana pale Vingunguti wana ile *Premier Cashew-nut Company*. Sehemu kubwa ya kazi ile inafanywa kwa mkono ndiyo unapata *better quality*. Kwa hiyo, basi inauzika vizuri. Kwa hiyo, viwanda vile lazima tuvibadilishe. Kule Mtwara, kiwanda kizuri ni kile cha *OLAM* na tunaendelea kumhamasisha yule akipanue ili aongeze *capacity*. Lakini kuna matatizo mengine niliyosema pale mwanzo ambayo lazima tuya-solve kupunguza gharama ya uzalishaji wa ubaguaji wa korosho ili awe *competitive* katika *International Market*. Lakini hilo ni muhimu kulizingatia.

Lakini la pili lile la miradi kwanza *coordinator* wa *Mtwara Corridor* siyo mimi, ni Wizara ya Ujenzi ambayo imeshapitisha bajeti yake hapa. Lakini kwa sababu ni Serikali hiyo moja ndiyo najitahidi kujibu hapa na najibu hivi pale katika *Mtwara Corridor* kuna vitu viwili vilikuwa *identified*, kuna zile *anchor projects* na *projects* ambazo kama ni *follow up*. *Anchor projects* kwa kweli ni tatu, *Liganga Iron core*, *Mchuchuma coal* na ule unaitwa *Mchuchuma coal to electricity project* na barabara ya Mtwara - *Mbamba Bay* ya lami. Barabara ya Mtwara - *Mbamba Bay* imeshafanyiwa tayari *feasibility study* na mambo yake yanakwenda vizuri, iko kwenye *design*. Sasa imeongezeka, sasa imepanda *grade* kutoka *feasibility study* kwenda kwenye *design*. Kwa hiyo, *progress* ndiyo inakwenda kwa sababu katika miradi hii ya barabara huwezi ukaleta ma-buldozer ukafyeta lazima ufanye *feasibility study to determine economic viability*, lakini *to under take design which will be able to determine the quality of the road*. (*Makofî*)

Kwa hiyo, vyote hivyo vinafanyika. Kwa hiyo, mimi nafikiri tuipongeze Serikali kwa kufanya kazi nzuri ambayo imepiga maendeleo. (*Makofî*)

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongezee kidogo maelezo mazuri sana ya Waziri wa Viwanda na Biashara juu ya viwanda vya korosho. Uuzaji wa viwanda hivi umeshatangazwa kuitia kwenye magazeti ya nchi hii. Kama Waheshimiwa Wabunge walisoma magazeti yale, wangeona haya aliyoeleza Mheshimiwa Waziri kwamba kutokana na hii teknolojia ya kutumia mashine kuvunja vunja sana korosho katika tangazo lile tunasema si lazima uendelee na teknolojia ile, nunua hiki kiwanda *install teknolojia unayona appropriate*, halafu uendelee.

Kwa hiyo, hiyo ndiyo hali iliyopo na *feedback* tunayopata ni kwamba kuna wananchi ambao wamejitolea kununua viwanda hivi na tunaomba mu-*encourage* sana wananchi wa Tanzania wanunue viwanda hivi kwa sababu teknoloji inayotumika kutengeneza korosho sasa hivi siyo *complicated* kiasi cha kushindikana kukua *installed* katika viwanda hivi. Wakati huo huo tunajitahidi sana kueneza hii teknoloji ya mashine za mikono za kukata korosho ili kadri itakavyo wezekana korosho ziweze kuanza kuwa *processed* kuanzia kijijini halafu baadaye zipelekwe kwenye *central place* ambapo sasa zitamaliziwa tayari kwa ajili ya kuuzwa nje. Kwa hiyo, nilikuwa naona niongezee hayo majibu. (*Makofi*)

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. *Sub vote 1001*, Mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sikuridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri kuhusu kile kiwanda cha *Premier Cashewnut*. Kwa masikitiko makubwa sana Mheshimiwa Waziri kabla hajateuliwa kuwa Waziri alikuwa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mipango na Fedha. Yeye pamoja na Kamati nzima ilitembelea kile Kiwanda cha *Premier Cashewnut*, aliona kazi inayofanywa pale.

Kile kiwanda kimetoa ajira ya akinamama 2,500 na hata hotuba mojawapo ya Mheshimiwa Rais anayotoa kila mwisho wa mwezi alikipongeza kile kiwanda kwa kutoa ajira kubwa kwa akinamama. Pia kimejenga kiwanda kingine jirani pale ya kiwanda kile kipo tayari kutoa ajira ya akinamama 2,000 tena. Kwa hiyo sasa hivi kinakosesha ajira ya akinamama 4,500. Sasa kuna sababu gani ya msingi inachokifanya kiwanda kile kisiingizwe katika EPZ? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namtaka Mheshimiwa Waziri atamke rasmi sasa hivi kwamba *NDC* wana matatizo yao na ndio maana wame-*appeal* kwa Waziri, atamke mara moja kwamba kile kiwanda kinaingia kwenye EPZ ili akinamama 4,500 wawzeze kupata hiyo ajira. Hakuna hata kiwanda kimoja Tanzania kinachowezza kutoa ajira ya watu 4,500. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri tulimwuliza swalii kwamba sisi tuna akinamama wanaobangua korosho ambao leo wanadhalilika sana Mtwara. Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge mmefika pale Mtwara mmeona wale akinamama wanavyojianika barabarani. Lakini Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kwamba tatizo sio *quality*, tatizo ni *packing*. Sasa hivi ni shilingi ngapi zinazohitajika kuwasaidia kuwapa *packing machine* ya *vacuum* jamani? Misaada mingapi tunatoa? Na Mheshimiwa nimemletea zawadi ya korosho za akinamama hizo ili a-test *quality* yake na *quality* ya viwandani inayotengenezwa. Haiwezi kulingana. *Quality* ya akinamama ni *quality* ya hali ya juu sana kupita hata korosho zinazotengenezwa viwandani. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuliulizwa swalii Na.77, hilo swalii liliulizwa katika Kikao cha Sita cha tarehe 11 Februari, 2003 na hilo swalii liliulizwa na Mheshimiwa Edson Halinga. Alipouliza swalii kuhusu hiki kiwanda cha *Premier*

*Cashewnut* kutoingizwa katika EPZ, kuna majibu ya Serikali yapo hapa yanasema kwamba hakuna *objection* yoyote kile kiwanda kuingizwa katika EPZ. Sasa tangu tarehe 11 Februari, 2003 mpaka leo kile kiwanda hakijapewa nafasi ya EPZ. Sasa tunataka majibu yake. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mbunge katika maelezo yake alisema *quality* ya akinamama, alikuwa na maana *quality* ya korosho wanazobangua akinamama. (*Kicheko/Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Murji. Kwanza nianze na lile la *quality* ya korosho zinazobanguliwa na akinamama. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nilitembelea Mkoa wa Mtwara na Mkoa wa Lindi na kwa masikitiko makubwa sana nilikuta akinamama wanabangua korosho nzuri kabisa bila kuzivunja, wako chini ya miti, wana-*pack* kwa kutumia mishumaa kwa hali ambayo hairidhishi kabisa. Serikali tumeliona hilo, nimewasiliana na Wabunge wa Mikoa yote inayozalisha korosho na nikawaeleza mikakati ya Serikali ili tuweze kuwasaidia hawa akinamama ambao ni wengi na korosho ni nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema tena na nitasema tena kwamba Serikali imejiandaa na iko tayari. Tumeandika mpaka mchanganuo nimeugawa kwa Wabunge wote, ulioandikwa na *Cashewnut Board*, ile Bodi ya Korosho ambayo iko Mtwara na Ndugu Mhagama, Meneja Mkuu yuko tayari kusaidia Mikoa yote. Tukawaeleza utaratibu wa kupata mashine 1,000 na kila mashine ni shilingi 50,000/= tu na *SIDO* iko tayari na imeanza kuzitengeneza. Lakini linalohitajika, tukianza viwanda kwa mfano wanawake 1,000 wawe wa Mtwara au Lindi tuwapange katika eneo ambalo tungewapa *godown* mojawapo la *cashewnut* tulikuwa tayari. Mkishaweza kupata wanawake, tutengeneze kiwanda cha kati cha milioni 17, nimekitaja hapa leo, viwili vitatu kama vile vya Naliendele, baada ya hapo tupate *outlet* ya kiwanda kikubwa kama cha *OLAM* ambacho kingegharimu kama milioni 200 au 300 tulikuwa tuko tayari, hatimaye tununue mashine za ku-*pack* ambayo ni Dola 25, yote tunajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana, sikuona yejote aliyejitokeza kuja kufanya biashara hii. Serikali hatuendi kuifanya hii biashara. Sasa naomba tuanze kazi. Tutautumia pesa za *SIDO* na tuko tayari. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunawapongeza sana *Premier Cashewnut* kwa kutuonyesha njia maana ndio wa kwanza walioanza. Kwa hiyo, tunawapongeza sana. Katika hiki kipindi ambacho tumekuwa hapa Bungeni tumekuwa tukishughulikia sana hili suala la usindikaji na ubanguaji wa korosho. Tatizo kubwa la kile kiwanda kwanza ni upatikanaji wa korosho za kutosha na pili ni kodi nyingi zinazotozwa ambazo zinawakwamisha. Sasa tumekubaliana na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Waziri wa Fedha, Ushirika na Masoko, tutakutana chini ya Waziri Mkuu kuzungumzia suala hili kwamba ni *incentives* gani

tuweke ili kuwawezesha watu kutengeneza korosho humu humu ndani na ni *incentives* gani tuweke ili kuwafanya watu wasiuze korosho *raw* nje ya nchi.

Hatua ya kwanza imeshachukuliwa, ubinafsishaji wa viwanda nya korosho na vitabinafsishwa vyote 12. Hatua ya pili ni hii sasa ya kutoa *incentives* kwa hawa watakaobangua korosho humu ndani wakiwemo *Premier Cashewnut, Mohamed Enterprises* na yule mwingine ambaye yuko Mtwara, *OLAM*. Kwa hiyo, tukipewa muda kidogo wakati tukiwa hapa hapa Bungeni tutakuwa tumelifanyia uamuzi hili jambo. (*Makofi*)

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama tena kwa masikitiko makubwa. Namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake. Lakini mimi ni Mbunge ninayetoka Mikoa inayozalisha korosho. Hiyo barua anayoisema mimi sijaipata bado. Sasa ninachosema, mimi nimesimama kumwomba Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba sisi hatutaki mashine za kubangua korosho, wale akinamama wanazo njiana mbinu zote za kubangua korosho wanazo, walichokwama ni *packing machine*.

Kwa hiyo, tunaomba msaada kutoka kwake wa *packing machine* ya dola 25,000. Hiyo *packing machine* ikipatikana tutaweka *one centre* hata tukikubaliana kuweka Mtwara, basi watu kutoka Masasi, Newala, Tandahimba, tutakuja *ku-pack* pale. Tena kwa masikitiko mengine sijajibwa swali langu na Mheshimiwa Waziri ambaye alikuwa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mipango na Fedha, alitembelea kile kiwanda akaona kazi inayofanywa kuhusu suala la kuingizwa kwenye *EPZ*. Tunaomba jibu lake. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona Mheshimiwa Mbunge anaelewa kabisa anachokisema kwa sababu nimekwenda Mtwara, *mobile phones* zipo, niko Mtwara nimelala nampigia simu usiku Murji uko wapi? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, akanijibu niko Dar es Salaam. Nikamwambia sawa, utaondoka lini? Akaniambia nakuja kesho. Nikaahirisha safari, hakuja, siku ya tatu niko Dar es Salaam, nimelala ananipigia simu mimi niko Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema, tupo tayari pesa ipo. Isipokuwa pesa hazitolewi bila utaratibu, huwezi kuzichukua umpe mtu. Tunataka, kama Mheshimiwa Murji anataka, atuandikie mchanganuo alete tutampa yeye Murji dola 25,000 alipe kama mkopo lakini awape akinamama *a-pack* pale kwenye kile kiwanda kimoja na jengo nimeliona, *a-pack* korosho, akusanye awe kama *collection centre* awasaidie *ku-pack* na *ku-export*. Tuko tayari Mheshimiwa Murji. Karibu sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu alilotoa Waziri wa Kilimo na Chakula ndio jibu zuri. Kwa nini? Kwa sababu sheria ya *EPZ* imekuja baada ya hawa jamaa wa Viwanda nya Korosho kuwepo. Kwa hiyo, masharti ya *EPZ* kwa kweli tunataka kiwanda ambacho kwanza kiwe kipyaa ambacho kinatengeneza bidhaa mpya na kwa masoko maalum. Kwa hiyo, sio rahisi kumuingiza *Premier Cashewnut* kwenye *EPZ* kirahisi kwa sababu tukifanya hivyo, je, akituumba *Sun*

*flag, wana-A to Z* wote hawa wataingia humo na itakuwa EPZ ya fujo. Ndiyo! Tuna ushahidi wa kutosha duniani kote walikofanya EPZ ambako walikiuka misingi hii ya *fast truck* na *special product for special market*. Maana hii ni muhimu, mfano ni Ghana. Wameondokana na EPZ sasa wana *Presidential Initiatives*.

Kwa hiyo, ni muhimu tufanye vizuri jambo hili ili tufikie zile shabaha zake. Kwa hiyo, tatizo la *Premier Cashewnut* siyo *incentives*, hawa jamaa wa kilimo tukikutana pamoja na Waziri wa Fedha na mimi chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tatizo lao pale ni kodi nyingi ambazo nyingine ni za ovyo, zinaongeza *costs*. India kwa mfano leo ukipelekea *raw cashew* unapata *zero custom duty*. Lakini ukipeleka *processed* kesho unalipa 400%. India marafiki zetu hawa lakini wanatufanyia hivyo. Kwa hiyo, ni muhimu na sisi tuwe na *system* yetu ya kuwawezesha hawa jamaa wa-*process cashew at a team upraise so that they become internationally competitive*. Ndio sheria yake! (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nadhani inatosha Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Murji bado hujaridhika? (*Makofi*)

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Ndiyo Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bado sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Kwa sababu gani? Mheshimiwa Murji, umesimama mara ya kwanza umejaribu, umeeleza na Naibu Waziri amejibu, umesimama tena, umeeleza, amejibu, sasa pengine ama utoe shilingi ama unyamaze. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, nia ni kumaliza mapema lakini wakati huo huo tukilinda haki ya kila Mbunge kufanya mambo yake. Sasa unayo haki kabisa, kama unaona huridhiki, unaondoa shilingi halafu tunapiga kura. Kama umeridhika, naomba tuendele. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mshahara wa Waziri kifungu 1001. Tatizo langu kubwa linataka ufanuzi kuhusu *Kibo Breweries* ya Moshi. Maamuzi ya kuuza *Kibo Breweries* ya Moshi kama vilivyouzwa viwanda vingine, mwanzo wale wafanyakazi wote walifukuzwa tena saa hiyo hiyo bila *notice* na milango ikafungwa tuliona kama ni kitu cha kawaida. Lakini baada ya yule mnunuzi kununua na yule mnunuzi aliondoka na usfunguo, *Dar es Salaam Kibo Tanzania Breweries*. Niliwahi kuhoji hapa Bungeni kwamba mpaka leo kile kiwanda kimefungwa wale wafanyakazi hawana kazi, ajira hamna. Tulipojaribu kuuliza, yule mnunuzi alisema kwani bia hampati? Sasa hiyo naona ni *monopoly* na sisi sera yetu tulikubaliana kwamba sio suala la *monopoly* ni suala la *competition*. Sasa tatizo hilo ni kubwa sana Moshi kwa sababu viwanda vilivyouzwa Moshi hata vya mbao vyote hakuna na ajira inakuwa hakuna. Nilitaka ufanuzi wa Waziri wa Viwanda na Biashara anifahamishe kwamba ni lini kile kiwanda cha *Kibo Breweries* kitakapofunguliwa kwa

sababu shida ni watu hawana ajira na kama ndio hivyo, je, tunaruhusu ku-*monopolize* kwa sababu *competition* inakuwa hakuna? Nataka ufanuzi wa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi kuhusu swali la Mheshimiwa Thomas Ngawaiya kama ifuatavyo;-

Kiwanda cha Kibo kiliuzwa na mwenye Kiwanda kile ambaye ni *East African Breweries* aliyeo Kenya. Aliamua kumuuzia *Tanzania Breweries*. *Tanzania Breweries* walikuwa na kiwanda vile vile Kenya ambacho kilikuwa kinapata hasara kama kilivyokuwa kinapata hasara Kibo na chenyewe wakamuuzia *East African Breweries*. Sasa mwenye kiwanda anaweza akakinunua halafu akakifunga na huwezi kumchapa viboko. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hapa sio kiwanda kufungwa, hoja ni je, bia zipo? Bia zile ambazo zilikuwa zinatengenezwa na *Kibo Breweries* na kwa ubora ule ule! Huu ndio uchumi wa leo. Jamani hivi nyie hamjasikia huko Uingereza na Marekani viwanda vinakuwa *merged*? Juzi tu hapa kulikuwa na yule *Mackses Feza* kama umefika London, yule bwana anataka kununuliwa anakataa, anasema msininunue. Lakini anataka kununuliwa tena usipotaka mwenyewe kwa hiari yako unaweza kununuliwa hata kwa nguvu. Huo ndio uchumi wa sasa. Ahsante. (*Kicheko*)

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mmoja ni sawa alivyoleza Mheshimiwa Waziri kwamba mtu anaweza akanunua kiwanda na akafunga tu. Lakini kama Serikali, maana Wizara ni Serikali na Waziri ni Serikali na ninayo taarifa kamili kwamba kile kiwanda kilikuwa hakiingizi hasira, sasa Waziri atakuwa tayari kusema kama ni kweli kilikuwa kinaingiza hasara ndiyo maana kikauzwa? Je, Serikali haiwezi ikaingilia mahali ambapo inaona kwamba sera ya nchi inapotoshwa makusudi kwa sababu watakuja akina Ngawaiya watanunua viwanda vingi, watafunga na kila mtu. Hiyo ni sera yetu inapotoshwa. Hakuna upotoshaji hapo?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya akitaka aje Ofisini Dar es Salaam, nitampa *data* zote zinazohusiana na Kiwanda cha Kibo kwamba kilikuwa kinapata hasara. Hilo la kwanza.

Lakini la pili, Sera ya Serikali ni kuhamasisha viwanda, ni kweli, lakini kiwanda kikishamilikiwa na mtu, Serikali tena haiwezi kusema bwana kiwanda hiki kiendelee kuendeshwa. Serikali ya namna hiyo sio hii tena ni zile Serikali zilizokwa zinatumia *command economy* ndiyo maana viwanda vyetu vimekufa kwa sababu tulikuwa tunavilazimisha vifanye kazi wakati haviwezi ku-*sustain*.

Sasa lazima tukubaliane na ukweli huo wa sasa kwamba *if you make profit you survive, if you don't you perish*. Ndiyo mambo yenye katika uchumi wa leo. Sasa akisema sawa Serikali wewe unataka kiwanda hiki kisifungwe, basi kuanzisa leo mtakuwa mnalipa mishahara ya wafanyakazi. Ninyi Bunge mtatupa pesa tukalipiwe mishahara hiyo, mikopo ya kujenga *infrastructure* ya EPZ, nanyimwa pesa kwa sababu

haziko, sio kama zipo. Sasa zitakuwepo za kulipa mishahara ya watu wengine? Haiwezekani bwana! Ahsante.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye *Sub Vote* hiyo hiyo Mshahara wa Waziri, 1001. Nina jambo moja tu ambalo nina nia ya kupata ufanuzi, sina shida kabisa na mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

Katika hotuba ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba hapa Bungeni ambayo ililenga kuondoa usumbufu mkubwa kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na kuwasaidia wenyе kipato kidogo, alifanya mabadiliko katika sheria ya *Stamp Duty* na malipo yake yatakuwaje na mabadiliko kwenye masuala ya malipo ya leseni. Alisema kwamba leseni hazitatolewa tena, zinafutwa kuanzia tarehe 1 Julai, 2004. Leo ni tarehe 20 Julai, 2004. Hakutakuwa na leseni ila kwa wafanyabiashara wakubwa kama nakosea atanisahihisha. Kwa wafanyabiashara wakubwa zitatolewa bure na zinatolewa mara moja tu, sio kila mwaka kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake, ninanukuu ukurasa wa 30 pale kwa kifupi sana, kasema: "Hatua hizo alizozitaja Mheshimiwa Basil Mramba na kama ziliviotangazwa hapa Bungeni zitatekelezwa baada ya kufuta sheria ya sasa ya biashara." Sasa leo ni tarehe 20 Julai, 2004, Bunge lilimuunga mkono Mheshimiwa Basil Mramba na Watanzania wamemuunga mkono katika hili.

Sasa nimesimama hapa kumwomba Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na yeze amuunge mkono kwamba kuanzia tarehe 1 Julai, 2004 leseni hizi zimefutwa kwa sababu kinachotokea ni kwamba mkanganyiko huko nje ni mkubwa sana. Wafanyabiashara wanakwenda pale, wanakusanya leseni za biashara wakati Bunge limetangaziwa hapa tarehe 1 Julai, 2004 hiki kitu kitakuwa hakuna. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ni moja. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri amuunge mkono mwenzake. Ni hilo tu. (*Makofî*)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna lililoharibika kwa sababu kabla ya mwisho wa Bunge hili, mimi naleta *Finance Bill*, Muswada wa Sheria ya Fedha ambao ni desturi kila mara baada ya Bajeti unakuja Muswada wa Sheria Fedha. Muswada huu utasema yale niliyosema na nyie mtapitisha. Sasa mkijaribisha mengine baadaye nyie wenywewe ndio mnajua. Kwa hiyo, hakuna lililoharibika kwa sababu sheria hiyo mpya inazungumzia Waziri, haitakiuka huo Muswada wa fedha ambao nyie mtakuwa mmeshapitisha. Ila itaunganisha na kuboresha, basi. (*Makofî*)

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kifungu 1001, Mshahara wa Waziri. Katika mchango wangu wa maandishi nilieleza jinsi nilivyokuwa nimefurahia wakati Naibu Waziri alipopata nafasi hiyo akafanya ziara kwa kutumia mwavuli wake katika Makampuni mbalimbali yaliyobinafsishwa na viwanda mbalimbali kitu ambacho kilituletea wananchi kujua nini kilichokwuwa kinafanyika na dosari zilikuwa zinaonekana katika vyombo vya habari

pamoja na *television*. Lakini imeshangaza muda sio mrefu baada ya hapo moto huo ulizimika. Mwavuli ulishindwa kukunjuka tena au vipi?

Pili, inashangaza kuona kwamba wakati wakulima wa korosho wanahangaika na bei kubwa ambayo hivi sasa imepanda, mfuko mmoja wa *sulphur* umefikia mpaka shilingi 15,000/= badala ya shilingi 9,000/= au shilingi 8,000/=, Serikali inasema biashara hiyo haiingiliwi, mbona sasa hivi Serikali inaingilia biashara ya magogo, chuma chakavu na biashara ya sukari? Je, Serikali ni tofauti kwa wakulima wa korosho au ni hii hii moja? Naomba jibu. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, kama ifuatavyo:-

Naomba kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba mwavuli bado umefunguka na bado uko angani, haujatua. (*Kicheko/Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Tua bwana, hujatua! (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Umetua! Umetua salama. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli hili suala la viwanda ambavyo vimebinafsishwa na vikatekelezwa, vimewagusa Waheshimiwa Wabunge wengi na Watanzania wote kwa ujumla. Kweli tulitangaza, ilikuwa kauli ya Serikali na sio yangu mwenyewe na suala limeongelewa katika Kamati mbalimbali za Serikali ikiwemo *IMTC* na baadaye inangojewa kuamuliwa na Baraza la Mawaziri, lakini kabla hatujachukua kiwanda ambacho tulikwishakibinafsisha, lazima kuna mambo kadhaa ambayo tunafuutilia.

Ya kwanza ambayo Wizara hii tumefanya, tumekusanya mikataba yote kabisa ambayo *PSRC* iliandikiana na walionunua viwanda. Mikataba ilionyesha wazi kwamba aendeleze investment, afanye kadha wa kadha. Kipengele ambacho tulikuwa tunakitafuta asipofanya, tutafanya nini ili sheria isije ikatuzunguka tuiweke Serikali katika matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, tumeprata kipengele ambacho kinaonyesha kwamba tunaweza tukachukua na Mheshimiwa Rais alihutubia Bunge hapa nakumbuka Janiuri, 2003 na akasema hatutasita kuvichukua kwa manufaa ya Watanzania walio wengi.

Mpaka sasa hivi tumekwishachukua viwanda zaidi ya vinne na kama alivyoongea Mheshimiwa Waziri hapa, tumeichukua *Morogoro Polyester*, tumechukua *TABOTEX*, *Tegry Plastics*, sasa hivi tunaangalia tena Wawekezaji wazuri na tunawapa mikakati au tunasaini nao mikataba maalum kwamba inaitwa, anaandika *undertaking* ambayo anaeleza kwamba nisipofanya hivyo kwa miezi tisa au mwaka mninyang'anyo.

Kwa hiyo Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, zoezi linaendelea, ni gumu sana, sio rahisi kama watu walivyodhani, lakini kusema ule ukweli Serikali bado ina nia hiyo na tutaendelea kwa nguvu kubwa kabisa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Yalikuwa maswali mawili. Kuna lile la *sulphur* anasema gogo mnaingilia, nini mnaingilia, *sulphur* vipi?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya *sulphur* inaweza ikaingiliwa kama tunapewa maandishi kwamba bei hii inakiuka utaratibu wa ushindani wa biashara. Serikali haiwezi kuingia tu, lazima tupate haya malalamiko na mimi ningependa sana nipate haya malalamiko. Malalamiko haya mimi nayapata leo hapa. Sasa hapa ni vigumu sana kuyatazama vizuri kwamba yana mambo ambayo yanapaswa kufanyika.

Kwa hiyo Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, tuletee maandishi hayo, tutalichunguza hili jambo maana hii hatuwezi kusema, kwa sababu tumeletewa, tutalifanya uamuzi hapo hapo. Haiwezekani! Tutawa-*commission* wataalam, watachunguza halafu tutatoa jibu. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nisimame na kusema kwamba Serikali haiingilii biashara ya magogo. Lakini Serikali kazi yake ni kusimamia sheria na taratibu. Sheria ambayo tumeipitisha ni kwamba kuanzia tarehe 1 Julai, 2004 magogo hayatasafirishwa nje ya nchi. Kwa hiyo, Serikali inasimamia sheria na taratibu ambayo ndiyo kazi ya Serikali. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan Kigwalilo bado umesimama?

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Ehe!

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Labda sijaelewaka. Ni hivi, hili Bunge kazi yake sisi ni kulalamikia yale ambayo wananchi wetu wanatarifu tuje tuyaseme hapa. Ninaamini mchango wa Wabunge ndio unaoipelekea Serikali kufuatilia suala la magogo, sukari na mengineyo. Sasa na hili pia ni suala ambalo linatakiwa kufuatiliwa na Waziri mhusika bila ya kukwepakwepa. Hayo ndiyo tunayokwambia na ndivyo inavyotokea. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri anachosema, hahitaji kukupa barua nyingine. Alichosema hapa ndio hicho ufuatilie. Una jibu?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa! Sasa aruhusu hela yangu basi! (*Kicheko*)

**MHE. ABDULKARIM H.E. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi niko katika Kifungu hicho hicho cha *Sub Vote 1001*, Mshahara wa Waziri, lakini

sikusudii kuzuia, isipokuwa nilikuwa nataka nipate ufanuzi kwa sababu juzi katika kuuliza swali langu la nyongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri, alijibu kwamba Serikali au Wizara yake imetayarisha magari ya *Foeu Wheel* kwa ajili ya kuwapa Mameneja wa Mikoa wa *SIDO* Tanzania nzima upande wa Bara.

Lakini Mafia hatuweza kununua boti kupeleka kule na leo katika majibu yake amesema kwamba atatafuta boti kwa ajili ya kuendea Mafia. Mimi nilikuwa nauliza hivi, sisi shida yetu siyo boti kwa ajili ya kupanda Meneja yule kwenda Mafia, shida yetu watu wa Mafia kwamba miradi mingi inayokuja Mkao wa Pwani, Mafia imekuwa tunaisikia tu hasa inayohusiana na pesa na ambayo inaleta maendeleo, lakini kuna Mawaziri ambao tayari wameshafika Mafia na kujionea hali halisi ya Mafia jinsi tulivyokuwa nyuma kimaendeleo. (*Makofit*)

Tunaomba hii Wizara Mheshimiwa Waziri na Naibu wake hebu waje Mafia waone jinsi wananchi wanavyotaka maendeleo. Kwa sababu kumsaidia mfanyakishara ndogo ndogo siyo lazima korosho. Sisi kwetu tuna nazi na kila siku tunasikia faida ya mnazi mmoja nini taratibu zake. Tuna bahari, tuna akinamama, Mheshimiwa Asha-Rose Migiro alifika Jibondo akaona akinamama wanaokwenda baharini na kuweza hata kusindika mazao ya samaki.

Tunasema hivi, namwomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri safari hii basi ajaribu kuongeza fungu na amwelekeze Meneja wa Mkao, Mama Balozi aje Mafia na atoe mikopo kwa akinamama na vijana na wananchi wa Mafia na kama hakuna na kama kuna sababu ya watu wengine ambao labda viongozi, wananchi walichukua mikopo zamani, ambayo hawataki kurejesha au hawajarejesha basi sheria zipo, ziko vyombo vya kuweza kukaa nao na kuelewana nao ama kusameheana au kupeleka Mahakamani yaishe. Lakini tunaomba safari hii Mafia *SIDO* ifike na wananchi wapate kufaidika na Wizara hii. Ahsante sana. (*Makofit*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa hoja ya Mheshimiwa Mbunge wa Mafia. Kwanza naomba nitoe ufanuzi. Nilipojibu swali tarehe 17 Julai, 2004 nilisema kwamba kila Mkao utapata gari na Mkao wa Pwani utapata gari la *Four Wheel Drive* na nilielekeza kwamba Mafia ni Kisiwani. Nikasema sawa, hatuwezi kuwanunulia boti ili Mameneja waje kule kukagua lakini tutahakikisha kwamba tumefika Mafia.

Kwa hiyo, hatukusema tutanunua boti. Lakini naomba kusema kwamba maendeleo yanaletwa na wale watu waliopo katika lile eneo nikiwa nina maana wananchi wa Mafia tunawaeleza kwamba kuna fedha za mikopo, kuna vitendea kazi mbalimbali, kuna ushauri unatolewa. Kwa hiyo, ni jukumu lenu kusema mnataka tuwafanyie nini. Kwa maana hiyo basi, kabla hujawasha tena hiyo *microphone* Mheshimiwa Mbunge, nakuahidi kwamba mimi binafsi na Meneja wa *SIDO* wa Mkao wa Pwani, tutakuja Mafia kutoa ushauri na kutazama nini kifanyike pale Mafia kwa kutumia fedha za *SIDO*. (*Makofit*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, bado dakika moja kufikia ile hatua yetu ya *guillotine*. Sasa hiyo dakika moja tutahoji kifungu kimoja lakini sasa itabidi jumla. Haya muda umefika.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 44 - Wizara ya Viwanda na Biashara**

Kifungu 1001 - <i>Administrative and General</i> .....	2,152,858,500/=
Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts</i> .....	145, 151,500/=
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning</i> .....	716,962,800/=
Kifungu 2001 - <i>Industry</i> .....	2,348,371,200/=
Kifungu 3001 - <i>Commerce</i> .....	1,776,855,400/=
Kifungu 3002 - <i>SADC</i> .....	-
Kifungu 3003 - <i>Weights and Measures</i> .....	-
Kifungu 3004 - <i>Trade Practices Bureau Agency</i> .....	171,000,200/=
Kifungu 3005 - <i>Trade Practices Tribunal</i> .....	41,670,800/=

(*Vifungu viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

#### **MIPANGO YA MAENDELEO**

#### **Fungu 44 - Wizara ya Viwanda na Biashara**

Kifungu 1001 - <i>Administration and General</i> .....	102,000,000/=
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning</i> .....	1,460,649,000/=

(*Vifungu viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu likiwa limekaa kama Kamati ya Matumizi, limepitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2004/2005 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba taarifa ya Kamati hii sasa ipokelewe na Makisio haya yapitishwe. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2004/2005  
yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 01.36 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatano  
tarehe 21 Julai, 2004 saa tatu asubuhi)*